JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

ISO 9001:2015 Certified

# RIPOTI KUU YA MWAKA YA UKAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23




MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU
WA HESABU ZA SERIKALI
MACHI 2024

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT
ISO 9001:2015 CERTIFIED

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Audit House, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu ya upepo "Ukaguzi" Simu: +255 (026) 2161200 Nukushi: +255 (026) 2117527; Barua pepe: ocag@nao.go.tz Tovuti: www.nao.go.tz.

**Kumb. Na. No.CGA.319/421/01B** **28 Machi 2024**

Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
11400 Chamwino
**40400 DODOMA.**

**YAH: RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti yangu ya mwaka ya ukaguzi wa Tawala za Miko ana Setikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Ripoti hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi na mapendekezo ya hatua za kuchukua ambazo zinalenga kukuza uwajibikaji katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma.

Nawasilisha kwa unyenyekevu.

**Charles E. Kichere**
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



# SALAMU KUTOKA KWA MKAGUZI NA MDHIBITI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Wajibu wa kikatiba na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

**NAOT Dira, Dhima na Kauli mbiu**

**01 — Dira Yetu**
Kuwa Taasisi yenye Kuaminika na ya Kisasa katika Ukaguzi wa Umma inayotoa Huduma za Ukaguzi za Viwango vya Juu Vinavyoimarisha Imani kwa Umma.

**02 — Dhima Yetu**
Kutoa Huduma za Ukaguzi zenye Kiwango cha Juu kwa Njia za Kisasa zenye Kuimarisha Uwajibikaji na Uwazi katika Usimamizi wa Rasilimali za umma

**03 — Kauli Mbiu Yetu**
Kuwa Taasisi yenye Kuaminika na ya Kisasa katika ukaguzi wa umma

### Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo

Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo.

### Kufanya kazi kwa ushirikiano

Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

### Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo

Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi stahiki.




### Kufanya kazi kwa utaalam

Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora.

### Kufanya kazi kwa uadilifu

Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadili na sheria katika utoaji wa huduma za ukaguzi.

### Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi

Tunahimiza, kuvumbua, na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwa ajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

# YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI ........................................................vi
ORODHA YA VIAMBATISHO ........................................................ xi
VIELELEZO ........................................................ xiv
VIFUPISHO ........................................................ xv
MUHTASARI ........................................................xviii
SURA YA KWANZA ........................................................ 1
MAELEZO YA AWALI ........................................................ 1
SURA YA PILI ........................................................ 3
HATI ZA UKAGUZI........................................................ 3
SURA YA TATU ........................................................ 6
UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MIAKA ILIYOPITA........... 6
SURA YA NNE ........................................................ 9
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI ........................................................ 9
SURA YA TANO ........................................................23
USIMAMIZI WA UNUNUZI NA MIKATABA........................................................23
SURA YA SITA........................................................55
USIMAMIZI WA MAPATO ........................................................55
SURA YA SABA........................................................70
USIMAMIZI WA MATUMIZI ........................................................70
SURA YA NANE ........................................................82
USIMAMIZI WA RASILIMALIWATU NA MISHAHARA........................................................82
SURA YA TISA........................................................87
TATHMINI YA UTAWALA BORA, MIFUMO YA NDANI NA USIMAMIZI WA VIHATARISHI........................................................87
SURA YA KUMI........................................................ 101
MFUKO WA WANAWAKE, VIJANA, NA WATU WENYE ULEMAVU .............. 101
SURA YA KUMI NA MOJA ........................................................ 114
TAMTHMINI YA MIRADI YA MAENDELEO........................................................ 114
SURA YA KUMI NA MBILI ........................................................ 127

UFANISI WA KIUTENDAJI KATIKA SEKTA YA ELIMU ............................ 127
SURA YA KUMI NA TATU ........................................................ 134
UFANISI WA UENDESHAJI KATIKA SEKTA YA AFYA ............................ 134
SURA YA KUMI NA NNE ......................................................... 149
MAPITIO YA UTENDAJI WA UWEKEZAJI KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA ...................................................................... 149
SURA YA KUMI NA TANO ........................................................ 168
UFANISI KATIKA UDHIBITI WA TAKA............................................ 168
SURA YA KUMI NA SITA......................................................... 181
MAPITIO YA USIMAMIZI WA ARDHI .............................................. 181
SURA YA KUMI NA SABA......................................................... 190
TATHIMINI YA KUKABILIANA NA MAAFA......................................... 190
SURA YA KUMI NA NANE ........................................................ 196
KAGUZI MAALUM ................................................................. 196
SURA YA KUMI NA TISA......................................................... 200
MAPITIO YA UFANISI WA SEKRETARIETI ZA MIKOA ............................ 200
SURA YA ISHIRINI ............................................................... 218
OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA .................. 218

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Mwenendo wa hati za ukaguzi ............................................ 4
Jedwali Na. 2: Utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi mwaka 2022/23 ............ 6
Jedwali Na. 3: Utekelezaji wa maagizo ya kamati ya LAAC .............................. 7
Jedwali Na. 4: Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi kilichotolewa ............................ 10
Jedwali Na. 5: Mwenendo wa makusanyo halisi ikilinganishwa na bajeti ............ 11
Jedwali Na. 6: Ziada ya makusanyo ukilinganisha na bajeti ............................ 12
Jedwali Na. 7: Halmashauri zilizokusanya pungufu ya bajeti ........................... 12
Jedwali Na. 8: Ruzuku ya matumizi ya kawaida ikilinganishwa na bajeti ............ 13
Jedwali Na. 9: Ruzuku za maendeleo ikilinganishwa na bajeti ........................ 14
Jedwali Na. 10: Bajeti pungufu kwa ajili ya kulipa madeni .............................. 14
Jedwali Na. 11: Fedha za bakaa ambazo hazikutumika kwa wakati ................... 18
Jedwali Na. 12: Kutorejeshwa kwa fedha zilizochukuliwa na Hazina................. 18
Jedwali Na. 13: Kubadili matumizi ya fedha bila kibali ................................. 22
Jedwali Na. 14: Upungufu ya utendaji bodi za zabuni ................................... 24
Jedwali Na. 15: Ununuzi kwa njia ya waraka ambayo haujaripotiwa ................. 24
Jedwali Na. 16: Uamuzi ya wajumbe wa bodi ya zabuni pungufu ya akidi........... 25
Jedwali Na. 17: Ununuzi nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka ..................... 25
Jedwali Na. 18: Ununuzi usioidhinishwa na bodi za zabuni............................. 26
Jedwali Na. 19: Ununuzi mdogo bila taarifa kwa bodi ya zabuni ....................... 27
Jedwali Na. 20: Ununuzi uliofanyika nje ya mfumo wa kieletroniki ................... 28
Jedwali Na. 21: Mapungufu katika ununuzi kupitia mfumo wa kielektroni........... 28
Jedwali Na. 22: Ununuzi kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa....................... 29
Jedwali Na. 23: Ununuzi uliofanyika bila ushindanishi wa bei .......................... 30
Jedwali Na. 24: Ununuzi wa bidhaa bila kuanisha viwango/vipimo .................... 31
Jedwali Na. 25: Taasisi zilizotumia njia ya ununuzi wa mzabuni mmoja au wachache ............................................................................................ 33
Jedwali Na. 26: Ujenzi wa miradi bila tathmini ya athari za mazingira ............... 34
Jedwali Na. 27: Mikataba ambayo haikuhakikiwa na mwanasheria .................... 36
Jedwali Na. 28: Mikataba isiyozingatia maoni ya wanasheria ........................... 36
Jedwali Na. 29: Malipo yaliyofanyika kabla ya bidhaa kupokelewa.................... 37
Jedwali Na. 30: Mapokezi ya vifaa/bidhaa bila ukaguzi.................................. 38

Jedwali Na. 31: Vifaa vya ujenzi ambavyo havikupimwa ubora wake ................ 39
Jedwali Na. 32: Halmashauri zenye nyaraka za zabuni zisizoidhinishwa ............ 40
Jedwali Na. 33: Malipo kwa kazi ambazo hazijapimwa/hazijatekelezwa ............ 41
Jedwali Na. 34: Malipo kwa kazi ambazo hazijatekelezwa............................. 42
Jedwali Na. 35: Upungufu katika uandaaji wa sanifu za miradi........................ 43
Jedwali Na. 36: Upungufu katika usanifu za miradi ..................................... 44
Jedwali Na. 37: Kucheleweshwa kwa malipo ya Wakandarasi.......................... 45
Jedwali Na. 38: Mabadiliko ya kazi yaliyofanyika bila kibali............................ 46
Jedwali Na. 39: Malimbikizo ya riba kwa kuchelewesha malipo ........................ 47
Jedwali Na. 40: Miradi iliyotekelezwa pasipo kukasimu majukumu ya afisa masuuli ........................................................................................... 49
Jedwali Na. 41: Vifaa vya ujenzi ambavyo havijatumika ................................. 50
Jedwali Na. 42: Vifaa vya ujenzi ambavyo havikununuliwa viwandani ............... 51
Jedwali Na. 43: Mabati yaliyonunuliwa bila ushahidi viwango vya ubora ............ 51
Jedwali Na. 44: Kutojumuishwa kwa ununuzi wa ngazi ya chini katika ripoti ya manunuzi ........................................................................................... 53
Jedwali Na. 45: Ununuzi pasipo kushirikisha kitengo cha ununuzi.................... 54
Jedwali Na. 46: Vyanzo vya mapato visivyokusanywa.................................... 58
Jedwali Na. 47: Ushuru wa huduma usiokusanywa ....................................... 60
Jedwali Na. 48: Makusanyo ya ushuru wa huduma bila uthibitisho .................... 62
Jedwali Na. 49: Ukusanyaji usioridhisha katika vyanzo vikubwa vya mapato........ 63
Jedwali Na. 50: Taarifa ya makusanyo ya mawakala ..................................... 65
Jedwali Na. 51: Ushuru wa mazao usiokusanywa ......................................... 66
Jedwali Na. 52: Mawasilisho ya dhamana ya kazi pungufu .............................. 68
Jedwali Na. 53: Ankara zilizorekebishwa bila viambatisho toshelevu ................. 69
Jedwali Na. 54: Salio pungufu la benki kufidia madai ya waweka Amana............ 72
Jedwali Na. 55: Malipo zaidi ya kiasi kilichowekwa akaunti ya Amana ................ 72
Jedwali Na. 56: Uhamisho wa mapato ya ndani kwenda akaunti ya Amana .......... 73
Jedwali Na. 57: Malipo bila ya fedha kupokelewa akaunti ya Amana .................. 73
Jedwali Na. 58: Malipo yasiyo na stakabadhi za kielektroni ............................ 75
Jedwali Na. 59: Matumizi yasiyo na tija.................................................... 76
Jedwali Na. 60: Mwenendo wa matumizi yasiyo na tija.................................. 77
Jedwali Na. 61: Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslimu ................................ 78
Jedwali Na. 62: Kodi ya zuio isiyowasilishwa TRA ........................................ 79
Jedwali Na. 63: Madai ya watumishi yasiyolipwa.......................................... 83

Jedwali Na. 64: Makato kutowasilishwa katika taasisi husika 84
Jedwali Na. 65: Upungufu katika utendaji wa kamati za ukaguzi 90
Jedwali Na. 66: Upungufu katika udhibiti wa mifumo na viashiria vya hatari 94
Jedwali Na. 67: Upungufu katika mifumo ya TEHAMA na uhasibu 96
Jedwali Na. 68: Magari ambayo hayajafanyiwa matengenezo au kuuzwa 100
Jedwali Na. 69: Michango isiyowasilishwa kwenye Mfuko wa Vikundi 102
Jedwali Na. 70: Mwenendo wa michango ambayo haikuwasilishwa 103
Jedwali Na. 71: Mikopo isiyorejeshwa na vikundi vilivyositisha biashara 105
Jedwali Na. 72: Mabadiliko ya miradi ya vikundi bila idhini ya Kamati 106
Jedwali Na. 73: Fedha za Mfuko wa Vikundi katika akaunti ya Amana 108
Jedwali Na. 74: Mikopo iliyotolewa kabla ya kusainiwa kwa mikataba 108
Jedwali Na. 75: Mikataba isiyo hakikiwa na Mwanasheria 109
Jedwali Na. 76: Mikopo iliyotolewa zaidi ya kiasi kilichoombwa 109
Jedwali Na. 77: Upungufu katika matumizi ya mfumo wa TPLMIS 110
Jedwali Na. 78: Kutosajiliwa kwa mikopo ya vikundi kwenye TPLMIS 112
Jedwali Na. 79: Kutothibitishwa uwepo wa vikundi vilivyopewa mikopo 113
Jedwali Na. 80: Upungufu katika utekelezaji wa miradi ya CSR 114
Jedwali Na. 81: Upungufu katika utekelezaji wa miradi ya CSR 116
Jedwali Na. 82: Miradi ya Mfuko wa Jimbo isiyoibuliwa na jamii 117
Jedwali Na. 83: Fedha za Miradi zilizobadilishwa matumizi 119
Jedwali Na. 84: Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi 122
Jedwali Na. 85: Upungufu wa miundombinu 129
Jedwali Na. 86: Upungufu wa walimu 130
Jedwali Na. 87: Upungufu wa vitabu vya kiada katika shule za msingi 132
Jedwali Na. 88: Uhaba wa vifaa-tiba katika sehemu za kutolea huduma za afya 137
Jedwali Na. 89: Vifaa tiba vilivyonunuliwa lakini havitumiki 137
Jedwali Na. 90: Miundombinu ya afya ambayo haitumiki ipasavyo 138
Jedwali Na. 91: Uhaba wa wahudumu wa afya 139
Jedwali Na. 92: Vifaa-tiba ambavyo havikupokelewa kutoka MSD 140
Jedwali Na. 93: Bidhaa za afya ambazo hazikupokelewa kutoka MSD 141
Jedwali Na. 94: Ufanisi wa kifedha wa mfuko wa iCHF 142
Jedwali Na. 95: Uandikishaji katika ngazi ya Sekretarieti ya Mkoa 143
Jedwali Na. 96: Ruzuku ya makusanyo ambayo haijatolewa 144
Jedwali Na. 97: Madai yaliyokataliwa na NHIF 145

**Jedwali Na. 98: Ununuzi bila kibali cha kukosekana vifaa kutoka MSD** .............. 146
**Jedwali Na. 99: Hasara itokanayo na ununuzi bila kibali cha MSD** .................... 146
**Jedwali Na. 100: Fedha za vifaa-tiba zilizochepushwa** ................................ 147
**Jedwali Na. 101: Uwekezaji wa taasisi** ................................................... 150
Jedwali Na. 102: Hasara inayotokana na uwekezaji katika hisa .......................... 151
**Jedwali Na. 103: Makampuni yenye mwenendo usioridhisha** .......................... 151
**Jedwali Na. 104: Upotevu wa mapato kwa kutumia viwango visivyoidhinishwa** ... 152
**Jedwali Na. 105: Kodi zisizokusanywa kwenye vituo vya mabasi** ..................... 155
**Jedwali Na. 106: Upotevu wa mapato ya masoko kwa kukosekana ufanisi** ......... 155
**Jedwali Na. 107: Bajeti ikilinganishwa na michango halisi** ............................ 165
**Jedwali Na. 108: Upungufu wa miondombinu ya taka** .................................. 169
**Jedwali Na. 109: Uzalishaji wa taka katika Halmashauri kwa miaka mitatu** ........ 170
**Jedwali Na. 110: Mapato na matumizi ya ukusanyaji taka** ............................ 172
**Jedwali Na. 111: Mawakala wakusanya ushuru wa taka wasio na dhamana** ........ 174
**Jedwali Na. 112: Ukusanyaji wa ushuru wa taka bila ya mikataba halisi** ............ 175
**Jedwali Na. 113: Mawakala waliowasilisha benki kiwango pungufu** .................. 176
**Jedwali Na. 114: Makusanyo ya ada ya taka chini ya kiwango cha mikataba** ....... 178
**Jedwali Na. 115: Ufanisi wa kifedha wa programu ya KKK** ............................ 181
**Jedwali Na. 116: Halmashauri zisizokamilisha urejeshaji wa Mkopo** ................ 184
**Jedwali Na. 117: Miradi mipya iliyojengwa kabla ya kupata hatimiliki** .............. 188
**Jedwali Na. 118: Hasara iliyosababishwa na moto** ...................................... 191
**Jedwali Na. 119: Kutoidhinishwa kwa usanifu wa majengo na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji** .............................................................................. 194
**Jedwali Na. 120: Utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi** ........................... 201
**Jedwali Na. 121: Utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya PAC** .......................... 201
**Jedwali Na. 122: Taarifa ya utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya PAC** ............. 202
**Jedwali Na. 123: Malipo kwa shughuli zisizokusudiwa** ................................. 203
**Jedwali Na. 124: Malipo bila stakabadhi sambamba** .................................... 203
**Jedwali Na. 125: Malipo yasiyokuwa na stakabadhi za kielektroniki** ................. 204
**Jedwali Na. 126: Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslimu** ............................. 205
**Jedwali Na. 127: Kutorejeshwa kwa masurufu** ........................................... 206
**Jedwali Na. 128: Adhabu ya malimbikizo ya makato ya watumishi** .................. 206
**Jedwali Na. 129: Manunuzi bila idhini ya bodi** ........................................... 207
**Jedwali Na. 130: Manunuzi nje ya mfumo wa ununuzi wa kielektroniki** ............ 208
**Jedwali Na. 131: Manunuzi yaliyofanywa bila ushindanishi** ........................... 208

**Jedwali Na. 132: Mapungufu katika mchakato wa ununuzi** ............................ 210
**Jedwali Na. 133: Sekretarieti za Mikoa zenye miradi yenye mapungufu** ........... 212
**Jedwali Na. 134: Miradi ambayo haijakamilka** ............................................ 213
**Jedwali Na. 135: Miradi kutokamilika licha ya muda kuisha** ........................... 213
**Jedwali Na. 136: Madeni na madai yasiyolipwa** .......................................... 214
**Jedwali Na. 137: Uhamishaji wa fedha bila kibali** ....................................... 215
**Jedwali Na. 138: Ucheleweshwaji ugawaji wa bakaa** .................................. 216
**Jedwali Na. 139: Ushuru wa maegesho ambao haukukusanywa** ...................... 220
**Jedwali Na. 140: Maombi ya maegesho maalumu yaliyocheleshwa** .................. 221
**Jedwali Na. 141: Kutowiana kwa bajeti ya miradi na MTEF** ............................ 222
**Jedwali Na. 142: Matengezo ya barabara ya Ngerengere - Kidunda** .................. 226
**Jedwali Na. 143: Zabuni ambazo hazikukidhi vigezo** .................................... 231
**Jedwali Na. 144: Malipo kwa kazi ambazo hazikufanyika** .............................. 235
**Jedwali Na. 145: Halmashauri zilizochelewesha marejesho** ........................... 242
**Jedwali Na. 146: Ununuzi bila ya idhini ya Bodi ya Zabuni** ............................ 244

# ORODHA YA VIAMBATISHO


Kiambatisho 1: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi ............................................. 249

Kiambatisho 2: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka 2022/23 ............................................................ 256

Kiambatisho Na. 3: Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za serikali za mitaa ....................................................................................... 262

Kiambatisho Na. 4: Jumla ya bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo dhidi ya jumla ya fedha zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2022/23 ...................................... 267

Kiambatisho Na. 5: Makadirio ya mapato ya ndani na makusanyo halisi kwa mwaka 2022/23 ....................................................................................... 269

Kiambatisho Na. 6: Mamlaka za serikali za mitaa zilizokusanya mapato ya ndani zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa ........................................................................ 275

Kiambatisho Na. 7: Mamlaka za serikali za mitaa zenye makusanyo pungufu ya makadirio ya bajeti ..................................................................................... 278

Kiambatisho Na. 8: Ruzuku za matumizi ya kawaida zilizotolewa ikilinganishwa na makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa .......................................................... 281

Kiambatisho Na. 9: Ruzuku za maendeleo zilizotolewa ikilinganishwa na makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa ........................................................................ 282

Kiambatisho Na. 11: Fedha za miradi zilizochepushwa kutumika kwenye miradi mingine pamoja na shughuli za kawaida ambazo hazikukusudiwa ................................. 285

Kiambatisho 12: Jumla ya makusanyo ya mamlaka za serikali za mitaa ................ 288

Kiambatisho Na. 13: Orodha ya Madeni Katika mfumo wa Mapato wa LGRCIS ......... 291

Kiambatisho Na. 14: Vyanzo vya Mapato Visivyokusanywa ............................... 293

Kiambatisho 15: Makusanyo Ambayo Hayakupelekwa Benki .............................. 296

Kiambatisho 16: Matumizi ya Fedha za Akaunti ya Amana kwa shughuli zisizokusudiwa ....................................................................................... 298

Kiambatisho 17: Madeni Yasiyolipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023 .................. 300

Kiambatisho Na. 18: Madai ya mishahara na yasiyo ya mishahara ya watumishi ambayo hayajalipwa ....................................................................................... 302

Kiambatisho 19: Makato ya mishahara kutowasilishwa katika Taasisi husika ........... 304

Kiambatisho Na. 20: Watumishi wenye tarehe za kuzaliwa zinazotofautiana kati ya taarifa za Mishahara na Mamlaka ya Kitambulisho cha Taifa "NIDA" .................... 306

Kiambatisho Na. 21: Upungufu Katika Utendaji na Ukosefu wa Vitendea kazi katika kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ............................................................... 309

Kiambatisho 22: Mifumo ya Udhibiti wa Ndani Kushindwa Kugundua Vihatarishi vya Ubadhirifu Vilivyoonekana Katika Malipo ................................................... 311

Kiambatisho 23: Thamani ya Mfuko wa Wanawake Vijana na watu wenye Ulemavu .. 318

Kiambatisho Na. 24: Michango ya Halmashauri kwenye Mfuko wa Wanawake Vijana na watu wenye Ulemavu ........ 321

Kiambatisho Na. 25: Mikopo iliyotolewa ........ 323

Kiambatisho Na. 26: Halmashauri zilizotoa mikopo kinyume na uwiano ........ 327

Kiambatisho Na. 27: Mikopo isiyorejeshwa kwa muda mrefu ........ 330

Kiambatisho Na. 28: Miradi Iliyotelekezwa ........ 332

Kiambatisho Na. 29: Miradi Iliyokamilika lakini Haitumiki ........ 333

Kiambatisho Na. 31: Kasoro zilizobainika katika utekelezaji wa miradi ........ 337

Kiambatisho Na. 32: Miradi Isiyokamilika kwenye mamlaka za serikali za mitaa ........ 339

Kiambatisho Na. 33: Kuchelewa kukamilika kwa miradi ya maendeleo katika mamlaka za serikali za mitaa ........ 342

Kiambatisho 34: Kiasi pungufu cha fedha kilichotolewa kutekeleza miradi ........ 344

Kiambatisho 35: Fedha pungufu zilizotolewa kwa ajili ya Elimu bila malipo ........ 347

Kiambatisho Na. 36: Upungufu wa miundombinu katika shule za Msingi ........ 349

Kiambatisho Na. 37: Upungufu wa Miundombinu katika shule za Sekondari ........ 350

Kiambatisho 38: Upungufu wa walimu katika shule za Msingi na Sekondari ........ 351

Kiambatisho 39: Bajeti Pungufu ya Ruzuku ya uendeshaji wa shule na chakula katika shule za msingi na sekondari ........ 351

Kiambatisho Na. 40: Kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya ........ 354

Kiambatisho Na. 41: Upungufu wa magari ya kubebea wagonjwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ........ 356

Kiambatisho 43: Upungufu wa Vifaatiba ........ 362

Kiambatisho Na. 45: Hali ya uandikishaji katika ngazi ya Sekretarieti ya Mkoa ........ 393

Kiambatisho 46: Makusanyo yatokanayo na taka katika Halmashauri kwa mwaka 2022/23 ........ 395

Kiambatisho 47: Upungufu uliobainika katika usimamizi wa taka katika Halmashauri 397

Kiambatisho Na. 48: Ufanisi katika Matumizi ya fedha za Programu ya KKK ........ 400

Kiambatisho 49: Mashauri ya ardhi dhidi ya mamlaka za serikali za mitaa ........ 402

Kiambatisho 50: Taasisi zisizozingatia maagizo ya Jeshi la Zimamoto na uokoaji katika ujenzi ........ 405

Kiambatisho Na. 51: Hali ya Utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa Sekretarieti za Mikoa ........ 406

Kiambatisho Na. 52: Fedha za maendeleo ambazo hazikupokelewa kutoka Hazina... 408

Kiambatisho 53: Halmashauri zilizopokea fedha za maendeleo kidogo ikilinganishwa na zilizotolewa na Hazina ........ 409

Kiambatisho 54: Fedha za maendeleo zilizopelekwa zaidi kwenye Halmashauri ikilinganishwa na fedha zilizopokelewa kutoka Hazina ........ 410

Kiambatisho 55: Fedha za maendeleo zilizopelekwa Halmashauri pungufu ya zilizoombwa Hazina........ 410
Kiambatisho 56: Fedha za maendeleo zilizopelekwa Halmashuri zaidi ya fedha zilizoombwa Hazina........ 411
Kiambatisho Na. 57: Halmashauri zenye miradi ambayo utekelezaji wake umecheleweshwa ........ 413
Kiambatisho Na.58: Halmashauri zenye miradi yenye kasi ndogo ya utekelezaji...... 414
Kiambatisho 59: Upungufu katika usanifu wa miradi........ 415
Kiambatisho 60: Ununuzi uliofanyika bila kutumia njia ya ushindani wa bei........... 417

# ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa makusanyo ya Mapato .................... 55

Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa makusanyo yasiyowalishwa benki ..... 59

Kielelezo Na. 3: Masoko yaliyoteketea kwa moto katika Halmashauri kwa miaka iliyopita ........................................................ 192

Kielelezo Na. 4: Baadhi ya maeneo yaliyoathirika na mafuriko ....... 194

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ALAT | Jumuiya ya Tawala za Serikali za Mitaa Tanzania |
| AMCOS | Vyama vya Ushirika |
| CDCF | Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo |
| CHF | Mfuko wa Afya ya Jamii |
| CSR | Uwajibikaji wa Taasisi kwa Jamii |
| DART | Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka |
| EFD | Kifaa cha Stakabadhi za kieletroniki |
| EIA | Tathmini ya Athari ya Kimazingira |
| ESDP | Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu |
| FFARS | Mfumo wa Taarifa za Kifedha Unaotumiwa katika Ngazi za Chini za Serikali |
| GCC | Masharti ya Jumla ya Mikataba |
| GoT-HoMIS | Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Hospitali Tanzania |
| GPSA | Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini |
| H/Jiji | Halmashauri ya Jiji |
| H/M | Halmashauri ya Manispaa |
| H/Mji | Halmashauri ya Mji |
| H/W | Halmashauri ya Wilaya |
| HCMIS | Mfumo wa Pamoja wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara |
| iCHF | Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa |
| ISSAI | Viwango vya Kimataifa kwa Taasisi Kuu za Ukaguzi |
| LAAC | Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa |
| LARAM | Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato wa Serikali za Mitaa |
| LGA | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| LGLB | Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa |
| LGRCIS | Mfumo wa taarifa za ukusanyaji mapato katika Mamlaka za serikali za Mitaa |
| MSD | Bohari Kuu ya Dawa |
| MUSE | Mfumo wa Ulipaji Serikalini |
| Na. | Namba |
| NHIF | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| OR TAMISEMI | Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PAC | Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali |
| PPRA | Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma |
| Sh. | Shilingi |
| TAA | Mamlaka ya Viwanja wa Ndege |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TANePS | Mfumo wa Kielektroni wa Ununuzi Tanzania |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |
| TARURA | Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini |
| TEA | Mamlaka ya Elimu Tanzania |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |



# SALAMU KUTOKA KWA MKAGUZI NA MDHIBITI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023 ambayo inajumuisha Ofisi ya Rais – Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa Pamoja na taasisi zilizopo chini yake, Sekretariati za Mikoa Pamoja na Mamlaka za Serikali za mitaa.

Napenda kutambua juhudi za Serikali inayoongozwa na Mh. Dkt.Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Pia nashukuru ushirikiano wa menejimenti za taasisi katika kutoa taarifa na ufafanuzi muhimu kwa ajili ya kuandaa ripoti ya ukaguzi.

Matokeo ya ukaguzi yanadhihirisha nyanja mbalimbali za usimamizi wa fedha katika Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa. Ingawa baadhi wameonesha usimamizi mzuri wa fedha, wengine wamekabiliwa na changamoto katika kudumisha utulivu wa kifedha na utendaji. Ni muhimu kwa serikali kuingilia kati na kuhakikisha taasisi zinafanya kazi kwa ufanisi, kuchangia uchumi, na kutoa huduma za hali ya juu kwa wananchi.

Ripoti hii imepangwa katika sura 20, kila moja ikizingatia vipengele tofauti, ikiwa ni pamoja hati za ukaguzi, hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita, mapitio ya utekelezaji wa bajeti, ununuzi na usimamizi wa mikataba, usimamizi wa mapato na fedha, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa rasilimali watu, mifumo ya uongozi na udhibiti wa ndani, Pamoja na mfuko wa kina mama, vijana na watu wenye ulemavu.

Pia ripoti hii imeangazia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ufanisi wa utendaji katika sekta ya elimu, afya, uwekezaji, taka, ardhi, majanga mbalimbali, pamoja na utendaji wa jumla wa sekretariati za mikoa pamoja na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ripoti hii pia inabainisha maeneo ambayo taasisi hizi zinahitaji kuboresha utendaji kazi na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Katika ripoti hii, nimetoa mapendekezo ya jinsi ya kuimarisha utendaji kazi wa taasisi zilizoripotiwa, kuongeza uwazi na uwajibikaji, na kuimarisha utawala bora. Ninaamini mapendekezo haya yatakuwa na manufaa kwa serikali, na wadau wengine katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora.

Mwisho, natoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa juhudi zao za dhati katika kufanya ukaguzi na kuandaa ripoti hii. Kujitolea kwao na bidii yao imekuwa nguzo muhimu katika utayarishaji wa ripoti hii, na ninashukuru kwa mchango wao.

**Charles E. Kichere**
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# MUHTASARI

Ibara ya 143(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 20 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, [SURA YA 418], vinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi wa kila mwaka wa hesabu za taasisi mbalimbali za Serikali. Kufuatia ukaguzi huo, CAG huwasilisha ripoti kwa Rais ambaye, kwa kuzingatia Ibara ya 143(4) ya Katiba na Kifungu cha 34(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, [SURA YA 418] huziwasilisha bungeni.

Muhtasari huu unaangazia masuala muhimu yaliyojitokeza katika ripoti hii kuhusu ukaguzi uliofanywa katika OR-TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake.

### Maoni ya ukaguzi

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, nilifanya ukaguzi na kutoa hati kwa taasisi 220. Kati ya hizo, 217 (99%) zilikuwa na hati inayoridhisha, 3 (1%) zilipata hati yenye shaka. Hakukuwa na matukio ya hati mbaya au kushindwa kutoa maoni.

### Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita

Tathmini yangu ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita inaonesha kwamba, mapendekezo ya ukaguzi yapatayo 8,238 yalitolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa 184 ambapo mapendekezo 609 (7%) hayakutekelezwa.

### Mapitio ya utekelezaji wa bajeti

Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, OR-TAMISEMI, sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa ziliidhinishiwa bajeti yenye jumla ya sh. Trilioni 8.82 kwa ajili ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Nilibaini kuwa jumla ya Sh. trilioni 7.61 zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo sawa na 86% ya makadirio yaliyoidhinishwa. Hii inaashiria kuwa Sh. trilioni 1.21 hazikutolewa. Aidha, fedha zilizotolewa katika mwaka huu wa fedha zilikua na ongezeko la Sh. bilioni 90 ikilinganishwa na Sh. trilioni 7.52 zilizotolewa katika mwaka wa fedha uliopita wa 2021/22.

Pia nilibaini kuwa makusanyo ya mapato yatokanayo na vyanzo ndani kwa mwaka wa fedha 2022/23 yalifikia Sh. bilioni 912.12, yakizidi kidogo bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. bilioni 911.86 kwa tofauti ya Sh. bilioni 0.26, sawa na asilimia 0.03. Aidha, kulikuwa na ongezeko kubwa la Sh. bilioni

20.28 ikilinganishwa na makusanyo ya mapato ya ndani ya Sh. bilioni 891.84 kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2021/22.

### Ununuzi na usimamizi wa mikataba

Katika mapitio yangu ya michakato ya ununuzi katika mamlaka 35 za serikali za mitaa, nilibaini kuwa ununuzi wa jumla ya Sh. bilioni 4.22 ulifanyika bila kuitisha nukuu za ushindanishi wa bei, na mamlaka 16 za serikali za mitaa, zenye ununuzi wa jumla ya Sh. bilioni 4.87 ziliamua kutumia njia ya mzabuni mmoja au wachache badala ya njia ya ushindanishi bila sababu za kuridhisha.

Aidha, ilibainika kuwa mamlaka 13 za serikali za mitaa zilinunua bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 1.45 ambazo hazikupokelewa licha ya malipo kufanyika.

Kuhusu usimamizi wa mikataba, ilibainika kuwa mkandarasi na mkandarasi mshauri waliohusika na usimamizi wa ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Halmashauri ya Jiji Dar es Salaam kilichopo Mbezi Luis walikuwa hawajalipwa ankara zao za jumla ya Sh. bilioni 8.92, hivyo kusababisha madai ya riba ya Sh. bilioni 2.23.

### Usimamizi wa mapato

Nilibaini kuwa pamoja na kuanzishwa kwa TAUSI kama mfumo wa kukusanya mapato na maelekezo mahususi kwa mamlaka za serikali za mitaa kusajili mashine za kukusanyia mapato (POS), kufanya usuluhishi wa wadaiwa kwenye mfumo wa awali wa LGRCIS, na kutumia moduli zote ndani ya TAUSI kwa ukamilifu, bado kuna Sh. bilioni 45 ambazo ni madai ya mapato yasiyokusanywa kwenye mfumo wa LGRCIS. Hali hii inaleta shaka kuhusiana na uwezekano wa upotevu wa mapato, hususani wakati huu ambapo matumizi ya mfumo yamesitishwa.

Aidha, nilibaini kuwa jumla ya Sh. bilioni 61 hazikukusanywa na mamlaka 130 za serikali za mitaa, kutoka vyanzo mbalimbali kama vile kodi ya maduka, vibanda vya soko, kodi ya nyumba, mauzo ya viwanja, ukusanyaji wa taka, leseni za biashara, leseni za vileo, maeneo ya wazi yaliyokodishwa, ada za maegesho, na vyanzo vingine vya mapato, ikiashiria kukosa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

Katika kupitia taarifa za mifumo ya LGRCIS na TAUSI, nilibaini kuwa jumla ya Sh. bilioni 6.2 ambazo ni mapato yaliyokusanywa kupitia mashine za POS katika mamlaka za serikali za mitaa 96, hazikuwa zimewasilishwa benki za mamlaka za serikali za mitaa husika.

### Usimamizi wa matumizi

Tathmini yangu ya usimamizi wa akaunti ya amana unaofanywa na mamlaka za serikali za mitaa iliibua kasoro kadhaa zenye jumla ya Sh. bilioni 10.71 katika akaunti za amana zinazomilikiwa na mamlaka za serikali za mitaa. Ukosefu wa udhibiti wa ndani ulichangia usimamizi usioridhisha na malipo yasiyodhibitiwa kutoka kwenye akaunti mbalimbali za amana.

Aidha, ukaguzi wangu katika mamlaka za serikali za mitaa 37 ulibaini kuongezeka kwa madai ya wazabuni na wafanyakazi kutoka Sh. bilioni 64.87 kwa mwaka wa fedha 2021/22 hadi Sh. bilioni 87.32 kwa mwaka wa fedha 2022/23, ikiashiria ongezeko kubwa la Sh. bilioni 22.45, sawa na 35%. Ongezeko hili la madeni linatokana na matumizi ambayo hayalingani na hali ya kifedha ya taasisi na ucheleweshaji wa malipo ya madai.

### Usimamizi wa rasilimali watu

Katika mamlaka 54 za serikali za mitaa, nilibaini madai ya watumishi yenye jumla ya Sh. bilioni 36.47 ambayo hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12. Madai haya yanajumuisha malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi, stahiki za wastaafu, na stahiki zingine kama vile posho za kisheria kwa wakuu wa idara na vitengo.

Pia, ulinganifu wa taarifa za mishahara kutoka kwenye Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Rasilimali Watu (HCMIS) na kanzidata ya mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ulibaini utofauti mkubwa. Mathalani, utofauti wa tarehe za kuzaliwa ulibainika kwa watumishi 77,286 katika takwimu za kanzidata zote mbili, na kusababisha mkanganyiko kuhusiana na tarehe sahihi za kuzaliwa kwa watumishi wa umma. Vilevile, nilibaini kuwa hapakuwa na takwimu zozote za watumishi 86 katika kanzidata ya NIDA.

### Tathmini ya utawala, udhibiti wa ndani na usimamizi wa vihatarishi

Tofauti na kwenye mashirika ya umma, ambapo bodi za wakurugenzi hunufaika na kamati huru za ukaguzi zinazojumuisha wajumbe wenye sifa za kitaaluma, mamlaka za serikali za mitaa hazina utaratibu sawa wa usimamizi. Kamati za Ukaguzi kwenye mamlaka za serikali za mitaa huripoti moja kwa moja kwa Wakurugenzi Watendaji, badala ya kuwa vyombo huru vya ushauri vinavyojikita kwenye masuala ya fedha na ukaguzi wa ndani na wa nje, na kuwajibika kwa wenye dhamana ya utawala, yaani Baraza la Madiwani. Utofauti huo unatia shaka, hususani kwa kuzingatia kwamba wajumbe wa baraza hawalazimiki kuwa na ujuzi wa masuala ya kifedha.

Aidha, tathmini yangu ya mifumo ya uhasibu na TEHAMA katika mamlaka za serikali za mitaa ilibaini upungufu katika Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) ambao umechangia katika dosari zilizobainika wakati wa ukaguzi wa miamala iliyofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe. Malipo ya jumla ya Sh. bilioni 1.23 yalifanywa kupitia akaunti ya mishahara kwa shughuli ambazo hazikufanyika.

Malipo hayo yaliwezeshwa katika akaunti ya mishahara kupitia matumizi yasiyo sahihi ya stakabadhi za mfumo wa kihasibu ambazo hutumika kutambua mishahara inayolipwa moja kwa moja na hazina kwa watumishi.

### Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

Katika kukabiliana na changamoto za awali za uendeshaji wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, tarehe 29 Machi 2023, baada ya kupokea ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2021/22, Mheshimiwa Rais aliagiza kufanyika kwa mapitio ya utaratibu wa utoaji wa mikopo hiyo. Baada ya hapo, Mh. Waziri Mkuu, aliziagiza mamlaka za serikali za mitaa nchini kusitisha utoaji wa mikopo kwa vikundi ili kuipa Serikali muda wa kuanzisha mfumo mpya wa utoaji wa mikopo utakaotatua changamoto zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Wakati mfumo mpya wa utoaji mikopo ukisubiriwa, nimebaini katika tathimini niliyoifanya katika mwaka wa fedha 2022/23 kuwa mamlaka 62 za serikali za mitaa hazikuchangia kikamilifu 10% ya mapato yake ya ndani kwenye Mfuko kama inavyotakiwa, hivyo kusababisha michango ambayo haikuwasilishwa kiasi cha Sh. bilioni 7.27.

Katika tathmini ya ufanisi wa mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu nilibaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, wanufaika wa mikopo katika mamlaka za serikali za mitaa 151 walikuwa hawajarejesha mikopo yenye jumla ya Sh. bilioni 79.70.

Vilevile, katika mapitio ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi, nilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 46 zilikuwa na mikopo isiyorejeshwa ya jumla ya Sh. bilioni 5.70 kutoka kwa vikundi 1,334 vilivyositisha kufanya shughuli zao; na vikundi 851 katika mamlaka za serikali za mitaa 19 vilivyoripotiwa kupokea mikopo ya jumla ya Sh. bilioni 2.6 havikuthibitika uwepo wake.

### Tathmini ya miradi ya maendeleo

Mamlaka za serikali za mitaa zimetekeleza miradi mingi ya maendeleo, ambayo, kimsingi, inafadhiliwa kupitia ruzuku kutoka serikali kuu,

michango kutoka kwa wadau wa maendeleo, mapato ya vyanzo vya ndani pamoja na michango ya wananchi.

Katika tathmini yangu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023, nilibaini mamlaka za serikali za mitaa 20 zenye miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 8.04 ambayo imekamilika lakini haitumiki, hivyo kutofikiwa malengo yaliyokusudiwa.

Aidha, katika tathmini ya hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo nilibaini kuwa, miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 12.92 katika mamlaka za serikali za mitaa 12 iliyokuwa katika hatua mbalimbali za ukamilishaji, ilitelekezwa kwa muda wa kati ya miaka miwili hadi 21. Vilevile, nibaini dosari mbalimbali katika miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 13.81 iliyotekelezwa na mamlaka 14 za serikali za mitaa.

### Ufanisi wa uendeshaji katika sekta ya elimu

Katika mwaka wa fedha 2022/23, kulikuwa na upungufu wa ruzuku ya elimu bila malipo iliyotolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa 15 kwa ajili ya shule za msingi na sekondari, ikiwa jumla ya Sh. bilioni 1.25 kati ya Sh. bilioni 11.83 zilizokuwa zimepangwa katika bajeti ya kipindi hicho. Fedha hizi ni muhimu kwa shule kupata rasilimali muhimu kama vile vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuwezesha ukarabati wa miundombinu na hatimaye kuchangia katika uboreshaji wa elimu.

Vilevile, OR-TAMISEMI ilitoa jumla ya Sh. bilioni 10.6 kwa Taasisi ya Elimu Tanzania kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya shule za msingi. Taasisi hiyo iliingia mkataba na kampuni nne za uchapaji na usambazaji wa vitabu milioni 2.51. Hata hivyo, ushahidi wa kuthibitisha usambazaji wa vitabu vilivyonunuliwa kwa shule za msingi haukupatikana.

### Ufanisi wa uendeshaji katika sekta ya afya

Nilibaini kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa vituo vya afya vyenye thamani ya Sh. bilioni 13.80 katika mamlaka za serikali za mitaa 17 zaidi ya muda uliopangwa. Sambamba na hilo, mamlaka za serikali za mitaa sita ziliomba nyongeza ya fedha kiasi cha Sh. bilioni 3.85 kutoka OR-TAMISEMI kwa ajili ya kukamilisha miradi ya afya.

Aidha, mamlakaza serikali za mitaa 15 zililipa Sh. bilioni 3.05 kwa bohari kuu ya dawa (MSD) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba mbalimbali. Hata hivyo, vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.78, sawa na 58% havikupokelewa. Vilevile, mamlaka za serikali za mitaa zilipokea ruzuku ya vifaa tiba ya Sh. bilioni 11.91 kutoka Wizara ya Afya kupitia MSD, lakini ni vifaatiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 3.61 pekee ndio

vilipokelewa sawa na 30%, wakati fedha za ruzuku ya Sh. bilioni 8.37 sawa na 70% hazikutumika.

Pia, nilifanya mapitio ya makusanyo ya fedha za mfuko wa iCHF ngazi ya Mkoa na kubaini kuwa, wanufaika katika mamlaka za serikali za mitaa 11 walichangia jumla ya Sh. bilioni 1.9. Hata hivyo, serikali kuu ilishindwa kurejesha ruzuku inayolingana na kiasi kilichokusanywa ili kusaidia Mfuko huo.

### Tathmini ya ufanisi wa uwekezaji

Mwaka 2001, mamlaka za serikali za mitaa za Mkoa wa Dar es Salaam kwa pamoja zilianzisha Benki ya Wananchi (DCB Bank), ambayo ilianza kufanya kazi mwaka 2002. Mamlaka hizo ni halmashauri ya jiji la Dar es Salaam, halmashauri za manispaa za Ilala, Kinondoni, Temeke, Kigamboni na Ubungo. Kwa pamoja, ziliwekeza mtaji wa Sh. bilioni 26.89 katika hisa 31,923,990.

Hata hivyo, imeonekana kuwa thamani ya hisa hizo imekuwa ikishuka mwaka hadi mwaka. Bei ya hisa moja kwa mwaka 2002 ilikuwa ni Sh. 1,000 ilipungua hadi kufikia Sh. 250 kwa mwaka 2018/19, ambapo bei ya sasa ya hisa ni Sh. 140. Kupungua huku kwa bei ya hisa kumesababisha hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 22.

Kwa upande mwingine, mamlaka za serikali za mitaa nne zimewekeza katika timu za mpira wa miguu zinazoshiriki ligi mbalimbali zikiwamo KMC FC, Geita Gold FC, Mbeya City FC, na Dodoma Jiji FC ambazo zote zimesajiliwa rasmi na shirikisho la mpira wa miguu Tanzania na kushiriki ligi mbalimbali ikiwemo ligi kuu ya Tanzania bara.

Hata hivyo, nilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa zinalipia gharama za uendeshaji wa timu hizo kutoka katika mafungu yake ya bajeti ya matumizi na kupitia fedha zinazokusanywa katika vyanzo vya ndani kila mwaka. Aidha, mapato yanayotokana na vyanzo vya nje, kama vile ada ya kiingilio, mauzo ya jezi na udhamini kutoka kwa makampuni na taasisi kama Parimatch, Geita gold mine, shirikisho la soka Tanzania na Azam broadcasting media hazijumuishwi katika mapato ya mamlaka ya serikali za mtaa.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, timu hizi zilikuwa na jumla ya makusanyo ya Sh. bilioni 7.01, ambapo Sh. bilioni 3.66 sawa na 52%, zilitolewa na mamlaka za serikali za mitaa husika. Pia, timu hizi hazijatunga sheria ndogo, hazitayarishi taarifa za fedha, na hazionekani

kuwa na uendeshaji unaojitegemea nje ya mfumo wa mamlaka za serikali za mitaa.

### Mapitio ya udhibiti wa taka

Katika mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya Sh. bilioni 19.45 zilikusanywa na mamlaka 117 za serikali za mitaa kama ada ya ukusanyaji wa taka. Hata hivyo, katika mapitio ya ukusanyaji wa mapato, nilibaini tofauti kubwa katika ukusanyaji wa ada za taka, ikilinganishwa na masharti yaliyobainishwa katika mikataba ya mawakala na mamlaka za serikali za mitaa. Utofauti huo unaonesha kuwa mawakala walishindwa kukusanya jumla ya Sh. bilioni 1.55.

Aidha, kituo cha kutengeneza mbolea cha Mabwepande kinachomilikiwa kwa ubia kati ya halmashauri ya manispaa ya Kinondoni na jiji la Hamburg kimelenga kuongeza ufanisi katika kudhibiti taka kupitia matumizi mbadala kwa kuzibadilisha kuwa mbolea isiyo na kemikali. Kituo hicho kinawakilisha uwekezaji mkubwa katika usimamizi endelevu wa taka unaolenga kunufaisha jamii na kutunza mazingira ambapo fedha kiasi cha Sh. bilioni 7.10 zimewekezwa katika mradi huo sambamba na mali zisizo hamishika zenye thamani ya Sh. bilioni 1.08.

### Mapitio ya usimamizi wa ardhi

Nimefanya tathmini ya utekelezaji wa programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, na kubaini kuwa OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ilitoa mikopo yenye jumla ya Sh. bilioni 42.28 kwa mamlaka za serikali za mitaa 58. Hata hivyo, mamlaka hizo ziliweza kurejesha kiasi cha Sh. bilioni 20.42 wakati kiasi cha Sh. bilioni 21.85, sawa na 52% ya mikopo iliyotolewa hakikurejeshwa.

Vilevile, katika kupitia mashauri ya ardhi yaliyosajiliwa katika mahakama na mabaraza mbalimbali ya ardhi katika mamlaka za serikali za mitaa 19, nilibaini uwepo wa mashauri 61 ambayo yalikuwa yanaendelea, yakiwa na madai dhidi ya mamlaka hizo ya jumla ya Sh. bilioni 4.18. Aidha, kulikuwa na mashauri ya ardhi 33 ambayo hayakuhusisha madai ya fedha. Napata wasiwasi kutokana na idadi kubwa ya mashauri ya ardhi dhidi ya mamlaka za serikali za mitaa.

### Ukaguzi maalumu

Katika mwaka wa fedha 2022/23, nilifanya kaguzi maalumu tano katika mamlaka tano za serikali za mitaa zilizoombwa na taasisi na wadau

mbalimbali. Matokeo ya kina ya kaguzi hizo yamewasilishwa kwa mamlaka zinazohusika kwa ufuatiliaji na kuchukua hatua zinazofaa.

### Mapitio ya sekretarieti za mikoa

Kufuatia kuvunjwa kwa iliyokuwa halmashauri ya jiji la Dar es Salaam, mnamo tarehe 25 Februari 2021, sekretarieti ya mkoa wa Dar es Salaam ilipewa jukumu la kusimamia na kuratibu uhamisho wa mali, madeni na watumishi kwenda halmashauri mpya ya Jiji la Dar es Salaam iliyoanzishwa, halmashauri za manispaa za mkoa wa Dar es Salaam, na sekretarieti ya mkoa wa Dar es Salaam. Hata hivyo, kumekuwa na ucheleweshaji wa mgawanyo wa bakaa ya fedha kiasi cha Sh. bilioni 2.6 ambapo fedha hizo zimebaki bila kutumika.

Aidha, nilibaini kuwa sekretarieti ya mkoa wa Mwanza ilikuwa na jumla ya Sh. bilioni 3.11 kwenye akaunti ya amana. Fedha hizo zilikusudiwa kutumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika kiwanja cha ndege cha Mwanza. Licha ya maelekezo ya kukabidhi mradi huo kwa mamlaka ya viwanja vya ndege ya Tanzania yaliyotolewa tarehe 11 Agosti 2022, bado fedha hizo zimebaki bila kutumika.

Kushikilia fedha kwa muda mrefu katika akaunti za sekretarieti za mikoa kunaleta wasiwasi kutokana na uwezekano wa kutumika kinyume na utaratibu au kwa shughuli ambazo hazikupangwa.

### Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Wakati wa tathmini yangu ya mfumo wa ukusanyaji wa ada za maegesho, nilibaini kuwa kuanzia Aprili 2021 hadi Juni 2023, wamiliki wa magari yaliyoegeshwa kwenye hifadhi za barabara walishindwa kulipa ada ya maegesho ya jumla ya Sh. bilioni 9.98, ikimaanisha kuwa OR-TAMISEMI imeshindwa kutekeleza hatua madhubuti kuwezesha ukusanyaji wa kiasi kinachodaiwa.

Vilevile, katika kupitia mwenendo wa makusanyo ya ada za maegesho kufuatia uhamisho wa jukumu la ukusanyaji kutoka TARURA kwenda OR-TAMISEMI tangu mwezi Julai 2022, nilibaini kupungua kwa makusanyo. OR-TAMISEMI, kupitia mamlaka za serikali za mitaa, ilikusanya Sh. bilioni 12.78 katika mwaka wa fedha 2022/23, ikiwa ni 56% ya lengo la TARURA la Sh. bilioni 23.02. Hii inaonesha upungufu wa kiasi cha Sh. bilioni 7.73 (38%) ikilinganishwa na makusanyo ya TARURA ya Sh. bilioni 20.51 kwa mwaka wa fedha 2021/22, na upungufu wa Sh. bilioni 2.58 (17%) ikilinganishwa na makusanyo ya TARURA ya Sh. bilioni 15.37 ya mwaka 2020/21.

Pia, nilipitia mpango wa matumizi wa muda wa kati (MTEF) kwa mwaka wa fedha 2022/23, na kubaini kuwa OR-TAMISEMI ilitenga bajeti ya jumla ya Sh. bilioni 71.42 kwa ajili ya miradi sita. Hata hivyo, bajeti halisi ilitakiwa kuwa Sh. bilioni 724.93, wakati wa utekelezaji, kiasi halisi kilichotolewa ni Sh. bilioni 731.40, ambapo Sh. bilioni 590.56 zilitumika katika mwaka fedha ninaoangazia. Hii inaonesha upungufu mkubwa katika mchakato wa uandaaji wa bajeti katika OR-TAMISEMI.

Aidha, mapitio ya mchakato wa tathmini kuhusiana na mikataba 25 ambayo TARURA iliwatunuku wakandarasi 14 katika mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini wakandarasi sita wailitunukiwa mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 1.99 licha ya kutokukidhi vigezo vilivyobainishwa kwenye nyaraka za zabuni.

# SURA YA KWANZA



## MAELEZO YA AWALI

### 1.0 Utangulizi

Ripoti hii inatoa matokeo na mapendekezo yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa taasisi za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023.

Taasisi zilizokaguliwa ni pamoja na Fungu Na. 56, ambayo ni OR-TAMISEMI pamoja na taasisi saba zilizoko chini yake ambazo ni Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Chuo cha Mafunzo ya Serikali za Mitaa - Hombolo (LGTI), Mfuko wa Barabara Chini ya OR-TAMISEMI, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB), Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Jumuiya ya Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT), na Fungu Na. 2 - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Aidha, ukaguzi umejumuisha Sekretatiati 26 za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 184, na kampuni tanzu mbili ambazo ni Kampuni ya Nyama ya Arusha Pamoja na Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam, hivyo kufanya jumla ya wakaguliwa kuwa 220.

### 1.1 Malengo ya ukaguzi

Ukaguzi ulilenga kutoa hati iwapo taarifa za fedha zilitayarishwa kwa kuzingatia viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha. Aidha, ukaguzi ulilenga kupitia na kutathmini ufuataji wa sheria za ununuzi pamoja na sheria ya bajeti, kanuni, na miongozo husika.

### 1.2 Mbinu ya ukaguzi

Ukaguzi ulifanywa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi wa Serikali (ISSAI) vilivyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi wa Serikali (INTOSAI), pamoja na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA).

Mbinu za ukaguzi zilijumuisha hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kukagua nyaraka, kufanya mahojiano, kuchambua taarifa na kutembelea

maeneo husika. Ukaguzi pia ulihusisha tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani na kuangalia kama inazingatia sheria, kanuni, na sera husika.

## 1.3 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi ulijumuisha ukaguzi wa taarifa za fedha na utekelezaji wa sheria katika maeneo ya usimamizi wa mapato, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa manunuzi na mikataba, mishahara na usimamizi wa rasilimali watu, na utendaji kazi. Aidha, ukaguzi ulijumuisha tathmini ya usimamizi wa vihatarishi, udhibiti wa mifumo ya ndani na utawala katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali. Vilevile, ukaguzi ulihusisha ukaguzi wa awali wa mafao ya watumishi wa Serikali walioastaafu ambao mafao yao yanalipwa moja kwa moja kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

# SURA YA PILI

## HATI ZA UKAGUZI

### 2.0 Utangulizi

Hati ya ukaguzi hupatikana kwa kuzingatia tathmini ya hitimisho linalotokana na ushahidi wa ukaguzi uliopatikana, kwa kujiridhisha kuwa taarifa za fedha kwa ujumla wake zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu (IPSAS).

Hili linafanikiwa kwa kuandaa na kufanya ukaguzi kwa namna ambayo itamuwezesha mkaguzi kujiridhisha kutokana na tathimini ya matokeo ya Ukaguzi dhidi ya kiwango/kipimo kilichowekwa. Hati ya ukaguzi hutolewa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI) 1200.

### 2.1 Aina ya Hati za Ukaguzi

Kuna aina nne za hati za ukaguzi; hati hizo ni inayoridhisha, isiyoridhisha, mbaya, na kushindwa kutoa maoni.

**Hati Inayoridhisha** hutolewa pale taarifa za fedha zinapotayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango vilivyokubalika kimataifa katika uandaaji wa taarifa za fedha.

**Hati Isiyoridhisha** hutolewa pale taarifa za fedha zinapokuwa zimetayarishwa kwa usahihi isipokuwa kuwapo kwa dosari katika eneo moja au mambo mengine. Hii inaweza kutokea pale unapopatikana ushahidi wa kutosha kumuwezesha Mkaguzi kuhitimisha kwamba kasoro hizo zimezidi kiwango cha juu kisichohimilika ingawa hazikuathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha kwa ujumla wake.

Pia, hati isiyoridhisha inaweza kutolewa pale ambapo Mkaguzi ameshindwa kupata ushahidi wa kutosha kumwezesha kutoa maoni ya ukaguzi, lakini akahitimisha kwamba dosari zilizotokana na kukosa

ushahidi zimezidi kiwango cha juu kisichohimilika lakini haziathiri taarifa za fedha kwa ujumla wake.

**Hati mbaya** hutolewa pale ambapo mkaguzi amejiridhisha kulingana na ushahidi wa kutosha wa kikaguzi kuwa, dosari zilizobainika katika eneo moja au kwa ujumla wake, zimeathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha, hivyo kusabisha taarifa hizo kutokuwa sahihi.

**Kushindwa kutoa maoni** hutokea pale ambapo mkaguzi ameshindwa kupata ushahidi wa kutosha au taarifa muhimu zinazomuwezesha kutoa maoni katika taarifa za hesabu. Katika hali hiyo, mkaguzi anahitimisha kwamba athari zinazoweza kutokea kwa dosari zisizogundulika katika taarifa za hesabu, zinaweza kuwa zimezidi kiwango cha juu kisichohimilika na zinaathiri taarifa za fedha kwa ujumla wake.

Katika hali ya nadra sana, inayohusisha kutokuwa na uhakika wa kutosha katika eneo moja au lingine, mkaguzi anaweza kushindwa kutoa maoni ingawa amepata ushahidi wa kutosha. Hii ni kwa sababu ya uwezekano wa kukosa uhakika katika eneo moja ukawa na uhusiano katika eneo lingine hivyo kusababisha athari katika taarifa za hesabu kwa ujumla wake kiasi cha mkaguzi kushindwa kutoa maoni.

## 2.2 Maoni ya ukaguzi yaliyotolewa mwaka husika

Katika mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya hati 220 zimetolewa kwa tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa. Kati ya hizo, 217 ni hati zinazoridhisha. Hata hivyo, hati zisizoridhisha tatu zilitolewa kwa H/W Serengeti, H/W Mpimbwe, na H/W Kilindi.

Aidha, mapitio ya hati za ukaguzi kwa miaka minne mfululizo kuanzia 2019/20 hadi 2022/23 ulifanyika kwa taasisi nane zilizo chini ya OR-TAMISEMI, sekretarieti za mikoa 26 na mamlaka za serikali za mitaa 184 na kampuni tanzu mbili. Matokeo kwa kina yameoneshwa katika **Jedwali Na.1** na **Kiambatisho Na.1**.

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa hati za ukaguzi**

| Mwaka wa Fedha | Taasisi | Hati | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Mbaya | Kushindwa Kutoa Maoni | |
| | Halmashauri | 181 | 3 | 0 | 0 | **184** |
| | Kampuni tanzu | 2 | 0 | 0 | 0 | **2** |
| 2022/23 | Sekretarieti za mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | **26** |
| | OR-TAMISEMI | 8 | 0 | 0 | 0 | **8** |

| Mwaka wa Fedha | Taasisi | Hati | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Mbaya | Kushindwa Kutoa Maoni | |
| **Jumla** | | **217** | **3** | **0** | **0** | **220** |
| | | | | | | |
| 2021/22 | Halmashauri | 170 | 13 | 1 | 0 | **184** |
| | Sekretarieti za mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | **26** |
| | OR-TAMISEMI | 8 | 0 | 0 | 0 | **8** |
| **Jumla** | | **204** | **13** | **1** | **0** | **218** |
| | | | | | | |
| | Halmashauri | 176 | 8 | 1 | 0 | **185** |
| 2020/21 | Sekretarieti za mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | **26** |
| | OR-TAMISEMI | 7 | 1 | 0 | 0 | **8** |
| **Jumla** | | **209** | **9** | **1** | **0** | **219** |
| | | | | | | |
| | Halmashauri | 120 | 53 | 12 | 0 | **185** |
| 2019/20 | Sekretarieti za mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | **26** |
| | OR-TAMISEMI | 7 | 1 | 0 | 0 | **8** |
| **Jumla** | | **153** | **54** | **12** | **0** | **219** |
| | | | | | | |

# SURA YA TATU



## UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MIAKA ILIYOPITA

### 3.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi na maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Pia, inaangazia kama hatua zilizochukuliwa zimetatua dosari zilizobainishwa katika kaguzi zilizopita.

Kifungu Na. 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, [Sura ya 418] kinanipa mamlaka ya kujumuisha katika Ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi, hali ya utekelezaji wa mpangomkakati juu ya hoja na mapendekezo yangu iliyoandaliwa na maofisa masuuli na kuratibiwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita kuhusu ripoti mamlaka za serikali za mtaa pamoja na maagizo ya LAAC ni kama ifuatavyo:

### 3.1 Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka 2022/23

Mapitio yangu kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita yanaonesha kuwa mapendekezo 8,238 yalitolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa 184 ambapo kati ya hayo, mapendekezo 609 (asilimia saba) hayakutekelezwa. Maelezo yameoneshwa katika **Jedwali Na. 2** na **Kiambatisho Na.2**.

**Jedwali Na. 2: Utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi mwaka 2022/23**

| Hatua ya utekelezaji | Idadi ya mapendekezo | % |
|---|---|---|
| Yaliyotekelezwa | 3496 | 42 |
| Yanayoendelea | 2983 | 36 |
| Hayajatekelezwa | 609 | 7 |
| Yaliyojirudia | 861 | 11 |

| Hatua ya utekelezaji | Idadi ya mapendekezo | % |
|---|---|---|
| Yaliyopitwa na wakati | 289 | 4 |
| **Jumla** | **8238** | **100** |

Kwa ujumla, ufanisi utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi hauridhishi kutokana na kutokuwapo kwa juhudi za kutosha katika kushughulikia upungufu uliobainishwa kwenye ripoti zangu.

Kushindwa kufanyia kazi mapendekezo yangu kwa wakati kunaweza kusababisha udhaifu kama huo kujirudia katika miaka inayofuata, hali ambayo inaweza kuathiri ufanisi katika uendeshaji Halmashauri.

**Ninasisitiza mamlaka za serikali za mitaa zitekeleze mapendekezo yangu ili kuongeza uwajibikaji na kudhibiti kujirudia kwa udhaifu uliobainishwa.**

## 3.2 Utekelezaji wa maagizo ya kamati ya LAAC

Kifungu Na. 38 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, [Sura ya 418] kinatamka Mlipaji Mkuu wa Serikali na ofisa masuuli kuzingatia uchunguzi na mapendekezo ya kamati ya kusimamia masuala ya fedha iliyoundwa na Bunge.

Tathimini yangu ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa mwaka wa fedha 2022/23 inaonesha kuwa maagizo mengi yaliyotolewa yamebakia kwa muda mrefu bila kutekelezwa na mamlaka za serikali za mitaa.

Kati ya maagizo 1,160 yalitolewa na LAAC kwa mamlaka za selikali za mitaa 173 katika mwaka unaongaziwa, maagizo 389 (33%) yalitekelezwa, maagizo 414(36%) yapo katika utekelezaji, maagizo 352(30%) hayajatekelezwa na maagizo matano (0.043%) yamejirudia au kupitwa na wakati kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 3** na **Kiambatisho Na.3** cha ripoti hii.

**Jedwali Na. 3: Utekelezaji wa maagizo ya kamati ya LAAC**

| Hatua ya utekelezaji | Idadi ya Mapendekezo | % |
|---|---|---|
| Yaliyotekelezwa | 389 | 33 |
| Yanayoendelea | 414 | 36 |
| Hayajatekelezwa | 352 | 30 |
| Yaliyojirudia | 2 | 0.17 |
| Yaliyopitwa na wakati | 3 | 0.26 |
| **Jumla** | **1,160** | **100** |

Kushindwa kutekeleza kwa haraka maagizo ya kamati ya bunge ya hesabu za serikali za mitaa kunaonesha kuwa upungufu uliobainishwa haujashughulikiwa ipasavyo, hivyo taasisi husika kuendelea kuwa katika hatari ya ubadhirifu, ukosefu wa ufanisi, na kushindwa kufikia malengo yaliyotarajiwa.

**Ninapendekeza menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha maagizo yote ambayo hayajatekelezwa yanashughulikiwa na kuwasilishwa kwa wakati kwenye kamati na hatua zilizochukuliwa.**

### 3.3 Hatua zisizosahihi katika utekelezaji wa mapendekezo zinazochukuliwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali

Kifungu Na. 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, [Sura ya 418], kinataka taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa mwaka uliopita iingizwe kwenye ripoti inayofuata baada ya kuwasilishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Ninampongeza Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia kifungu tajwa hapo juu, kwani majibu ya serikali kuhusu ripoti kuu ya mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/22 yalipokelewa kwa njia ya barua yenye nambari ya kumbukumbu 116/47/4/01A/25 ya tarehe 05 Julai 2023.

Pamoja na kutambua juhudi za Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa kutekeleza mapendekezo yangu ya ukaguzi, nina shaka na kutokutekelezwa kwa mapendekezo kwa muda uliotakiwa. Kushindwa kuchukua hatua kwa wakati dhidi ya mapendekezo yangu kunaweza kusababisha kujirudia kwa udhaifu kama huo katika miaka inayofuata.

**Ninapendekeza Mlipaji Mkuu wa Serikali atekeleze kwa wakati mapendekezo ya ukaguzi yanayotolewa, na kuhakikisha kuwa upungufu wote uliobainishwa katika ripoti zilizotangulia unarekebishwa.**

# SURA YA NNE




## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI

**4.0 Utangulizi**

Sura hii inatoa tathmini ya kina ya utekelezaji wa bajeti kwa mamlaka za serikali za mitaa itokanayo na ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani, utoaji wa fedha kutoka serikali kuu kulingana na ruzuku iliyokadiriwa, na misaada kutoka kwa wadau wa maendeleo.

Kifungu cha 46(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuwasilisha bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi katika mwaka wa fedha husika. Vivyo hivyo, Kifungu cha 45(a) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, kinamkasimu ofisa masuuli wajibu wa kusimamia matumizi ya fedha zinazopokelewa kutoka mfuko mkuu kama ilivyobainishwa katika sheria.

Tathmini yangu ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/23 yenye lengo la kubainisha ni kwa kiasi gani mamalaka za serikali za mitaa zilizingatia sera ya bajeti ya serikali, miongozo, sheria ya matumizi na mifumo mingine muhimu ya mipango ya kitaifa.

Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 ililenga kutekeleza awamu ya tatu ya mpango maendeleo wa taifa wa miaka mitano, unaolenga kukuza uchumi shirikishi na shindani, kuimarisha maendeleo ya viwanda na kuongezea thamani kilimo, kuchochea uwekezaji na biashara, kukuza maendeleo ya watu na kukuza ujuzi.

**4.1 Mapitio ya bajeti**

OR-TAMISEMI ina jukumu la kuratibu na kusimamia tawala za mikoa ili kuwezesha mamlaka za serikali za mitaa kutekeleza majukumu yao kulingana na majukumu ya Wizara yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jumla ya makadirio ya bajeti yaliyoidhinishwa kwa OR-TAMISEMI, sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa katika mwaka wa fedha 2022/23 yalikuwa Sh. trilioni 8.82 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Mwenendo wa bajeti ni kama ulivyooneshwa katika **Jedwali Na.4.** Fedha zilizotolewa katika mwaka huu wa fedha ziliongezeka kwa kiasi cha Sh. bilioni 90 ikilinganishwa na Sh. trilioni 7.52 zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2021/22.

Mwenendo wa miaka minne mfululizo kuhusu mgao wa bajeti ya ruzuku za matumizi ya kawaida na maendeleo umeoneshwa katika **Jedwali Na.4** na **Kiambatisho Na.4.**

**Jedwali Na. 4: Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi kilichotolewa**

| Mwaka wa fedha | Jina la Taasisi | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) (A) | Kiasi kilichotolewa (Sh.) (B) | Utofauti (Sh.) C=(B-A) |
|---|---|---|---|---|
| 2022/23 | OR-TAMISEMI, RS & LGAs | 8,819,148,246,175 | 7,606,495,440,875 | (1,212,652,805,299) |
| 2021/22 | | 8,249,270,135,979 | 7,521,709,076,085 | (727,561,059,894) |
| 2020/21 | | 6,946,188,944,481 | 5,792,751,665,853 | (1,153,437,278,628) |
| 2019/20 | | 6,805,675,947,122 | 5,458,401,067,527 | (1,347,274,879,595) |

**Ingawa serikali iliweza kutoa 86% ya bajeti iliyoidhinishwa, bado ninasisitiza kuweka malengo halisi na kudumisha uwajibikaji na uwazi katika masula ya kifedha ili kuongeza ufanisi katika mipango ya matumizi ya rasilimali.**

## 4.2 Tathmini na mapitio ya mienendo ya bajeti katika mamlaka za serikali za mitaa

### 4.2.1 Mwenendo wa makusanyo halisi ya mapato kutoka vyanzo vya ndani ukilinganishwa na bajeti kwa miaka mitano

Mapato ya ndani yanajumuisha fedha zinazokusanywa kupitia vyanzo mbalimbali kama vile mazao ya kilimo, ada, tozo na adhabu, ada za leseni, vibali vya ujenzi, na vyanzo vingine vilivyotengwa kwa matumizi ya kawaida na ya maendeleo.

Pia, nilifanya uchambuzi wa taarifa za hesabu zilizowasilishwa na mamlaka serikali za mitaa 184 na kubaini kuwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2022/23 ulifikia kiasi cha Sh. bilioni 912.12 kati ya makadirio yaliyoidhinishwa ya kiasi cha Sh. bilioni 911.86, hivyo

kukusanya zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa kwa kiasi cha Sh. bilioni 0.26 sawa na asilimia 0.03.

Pia, nilibaini ongezeko la makusanyo la Sh. bilioni 20.29 kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na mapato ya Sh. bilioni 891.84 yaliyokusanywa katika mwaka wa fedha 2021/22, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 5** na **Kiambatisho Na.5.**

***Jedwali Na. 5: Mwenendo wa makusanyo halisi ikilinganishwa na bajeti***

| Mwaka wa fedha | Bajeti iliyokadiriwa (Sh.) (A) | Kiasi kilichokusanywa (Sh.) (B) | Utofauti (Sh.) C=(B-A) | Ufanisi katika utendaji (%)=C/A *100 |
|---|---|---|---|---|
| 2022/23 | 911,863,338,484 | 912,123,865,087 | 260,526,603 | 0.03 |
| 2021/22 | 873,898,493,691 | 891,836,133,308 | 17,937,639,617 | 2 |
| 2020/21 | 822,375,950,562 | 769,422,329,061 | (52,953,621,501) | (6) |
| 2019/20 | 759,907,423,938 | 709,573,567,541 | (50,333,856,397) | (7) |
| 2018/19 | 725,633,451,671 | 639,401,151,405 | (86,232,300,266) | (11) |

Licha ya mwelekeo mzuri wa ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, bado kuna ukusanyaji mdogo wa mapato ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa. Hii inaashiria kuwa si vyanzo vyote vya mapato vilikusanywa ipasavyo.

**Ninazihimiza mamlaka za serikali za mitaa kubainisha vyanzo vya mapato ambavyo havikukusanywa, kufanya upembuzi yakinifu, kuandaa bajeti zenye uhalisi ambazo zitaongeza ukusanyaji wa mapato, na kuweka mikakati madhubuti ya ukusanyaji ili kuhakikisha vyanzo vyote vya mapato vinakusanywa ipasavyo ili kufikia malengo yaliyotarajiwa.**

### 4.2.2 Tathmini ya jumla ya utendaji wa mamlaka ya serikali za mitaa

#### a) Mamlaka za serikali za mitaa zilizokusanya mapato ya ndani zaidi ya makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa

Makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mamlaka 79 za serikali za mitaa ilikuwa kiasi cha Sh. bilioni 327.99, ambapo makusanyo halisi yalikuwa Sh. bilioni 444.13, ikionesha ufanisi katika makusanyo kwa ziada ya 135% ikilinganishwa na bajeti.

Katika mwaka wa fedha uliopita mamlaka 102 za serikali za mitaa zilikusanya mapato zaidi malengo kwa 116% kama ilivyoelezwa kwenye **Jedwali Na. 6** na **Kiambatisho Na.6.**

*Jedwali Na. 6: Ziada ya makusanyo ukilinganisha na bajeti*

| Mwaka wa fedha | Bajeti iliyokadiriwa (Sh.) (A) | Mapato halisi (Sh.) (B) | Utofauti (Sh.) C=(B-A) | Ufanisi katika utendaji (%)=C/A *100 | Idadi ya Mamlaka za Serikali za mitaa |
|---|---|---|---|---|---|
| 2022/23 | 327,986,323,174 | 444,127,705,034 | 116,141,381,860 | 135 | 79 |
| 2021/22 | 413,871,167,926 | 479,401,407,535 | 65,530,239,610 | 116 | 102 |
| 2020/21 | 346,128,129,473 | 376,302,581,046 | 30,174,451,573 | 109 | 64 |
| 2019/20 | 315,579,839,663 | 363,859,170,229 | 48,279,330,566 | 115 | 62 |

**Ingawa ninatambua juhudi za mamlaka za selikali za mitaa katika ukusanyaji wa mapato, bado ninasisitiza juu ya umuhimu wa kuboresha maandalizi ya bajeti. Hii inajumuisha kuweka malengo yanayoweza kufikiwa na kurekebisha mara kwa mara vyanzo vya mapato ili kuendana na uwezo halisi wa kukusanya. Hii itasaidia katika kuhakikisha uadilifu na uwazi wa taratibu za kifedha ndani ya mamlaka za serikali za mitaa na kuongeza ufanisi wa matumizi bora ya rasilimali.**

**b) Mamlaka za serikali za mitaa zilizokusanya mapato ya ndani chini ya makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa**

Nilibaini kuwa, mamlaka 103 za serikali za mitaa ziliidhinishiwa makadirio ya makusanyo ya mapato kiasi cha Sh. bilioni 575.03 ambapo zilifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 459.15 ikionesha ufanisi wa ukusanyaji kwa 80% ikilinganishwa na makisio. Mwenendo wa ukusanyaji mapato pungufu ya makisio umeoneshwa katika **Jedwali Na.7** na kufafanuliwa katika **Kiambatisho Na.7**.

**Jedwali Na. 7: Halmashauri zilizokusanya pungufu ya bajeti**

| Mwaka wa fedha | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) (A) | Makusanyo Halisi (Sh.) (B) | Utofauti (Sh.) C=(B-A) | Ufanisi (%)=B/A *100 | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2022/23 | 575,028,005,691 | 459,147,150,434 | (115,880,855,257) | (80) | 103 |
| 2021/22 | 460,027,325,765 | 412,434,725,772 | (47,592,599,993) | (90) | 82 |
| 2020/21 | 476,247,821,089 | 393,119,748,015 | (83,128,073,074) | (83) | 121 |
| 2019/20 | 442,034,532,275 | 343,421,345,312 | (98,613,186,963) | (78) | 123 |

Ninatilia mkazo kwa mamlaka za serikali za mitaa ambazo ukusanyaji halisi wa mapato ulishuka chini ya kiwango kilichokadiriwa. Hii inaashiria kutokusanya kikamilifu kwa vyanzo vyote vya mapato vilivyopo, hali ambayo inasababisha kushindwa kutekeleza shughuli zilizopangwa kutekelezwa kupitia mapato ya ndani.

**Katika kuongeza mapato ya ndani na kuboresha ufanisi, ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa kutimiza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na kutafuta fursa ya vyanzo vipya ikijumuisha kurasimisha biashara zisizo rasmi; kukuza ushirikiano na sekta binafsi na kupitia upya kodi na ushuru uliopo ili kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari.**

### 4.2.3 Mapitio ya fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida

Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa OR-TAMIISEMI, sekretarieti za mikoa 26 na mamlaka 184 za serikali za mitaa ilikua Sh. trilioni 5.55 ambapo kiasi cha Sh. trilioni 5.21 kilitolewa kwa matumizi ya kawaida, sawa na 94% ya makadirio ikiimanisha kuwa kiasi cha Sh. bilioni 344.28 hakikutolewa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 8** na maelezo zaidi katika **Kiambatisho Na.8.**

*Jedwali Na. 8: Ruzuku ya matumizi ya kawaida ikilinganishwa na bajeti*

| Mwaka wa fedha | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) (A) | Fedha iliyotolewa (Sh.) (B) | Utofauti (Sh.) C=(B-A) | Ufanisi (%)=C/A *100 |
|---|---|---|---|---|
| 2022/23 | 5,550,172,280,648 | 5,205,891,865,384 | (344,280,415,263) | 94 |
| 2021/22 | 4,912,836,455,163 | 4,807,125,959,060 | (105,710,496,103) | 98 |
| 2020/21 | 5,349,085,836,370 | 4,760,974,162,598 | (588,111,673,772) | 89 |
| 2019/20 | 5,289,377,847,806 | 4,551,253,607,566 | (738,124,240,240) | 86 |

**Ninashauri Serikali, kupitia Wizara ya Fedha, kutoa fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa. Pia, viongozi wa mamlaka za serikali za mitaa kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato kwa kuongeza wigo wa mapato kutoka vyanzo vya ndani. Hii inaweza kufikiwa kupitia usimamizi wenye ufanisi wa katika ukusanyaji wa mapato.**

### 4.2.4 Mapitio ya fedha za ruzuku ya maendeleo

Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa OR-TAMIISEMI, sekretarieti za mikoa 26 na mamlaka za serikali za mitaa 184 ilikua kiasi cha Sh. trilioni 3.27 ambapo kiasi cha Sh. trilioni 2.40 kilitolewa na serikali sawa na 73% ya makadirio yaliyoidhinishwa. Upungufu katika utoaji wa fedha unaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Maelezo ya kina ya ruzuku ya maendeleo iilizotolewa ikilinganishwa na makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa yameoneshwa katika **Jedwali Na. 9** na **Kiambatisho Na.9.**

***Jedwali Na. 9: Ruzuku za maendeleo ikilinganishwa na bajeti***

| Mwaka wa fedha | Bajeti Iliyoidhinishwa (Sh.) (A) | Fedha Tolewa (Sh.) (B) | Utofauti (Sh.) C=(B-A) | Ufanisi (%)=C/A *100 |
|---|---|---|---|---|
| 2022/23 | 3,268,975,965,527 | 2,400,603,575,491 | (868,372,390,036) | 73 |
| 2021/22 | 3,336,433,680,816 | 2,714,583,117,025 | (621,850,563,791) | 81 |
| 2020/21 | 1,597,103,108,111 | 1,031,777,503,255 | (565,325,604,856) | 65 |
| 2019/20 | 1,516,298,099,316 | 907,147,459,961 | (609,150,639,355) | 60 |

Ruzuku za maendeleo zinapotolewa pungufu ya kiasi kilichoidhinishwa na bunge, inaathiri utoaji wa huduma muhimu kwa jamii na inakwamisha utekelezaji wa miradi muhimu kwa ajili ya ustawi na maendeleo.

**Ninaishauri serikali kutoa fedha za kutosha kwa mamlaka za serikali za mitaa ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuepusha athari katika utoaji wa huduma nchini. Pia, menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa ziongeze wigo wa ukusanyaji mapato ili kuongezea katika ruzuku inayotolewa na hazina kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo.**

### 4.2.5 Bajeti pungufu iliyotengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni pamoja na madai ya wafanyakazi Sh. bilioni 99.25

Mamlaka za serikali za mitaa zilitenga bajeti kwa ajili ya kulipa madeni katika kwa mwaka wa fedha 2022/23, lakini bajeti hiyo ilionekana kuwa haitoshi kulipa sehemu kubwa au madeni yote yaliyobainishwa katika taarifa za fedha za hesabu za mwaka 2021/22.

Hivyo, madeni ya wazabuni na madai ya wafanyakazi ya kiasi cha Sh. bilioni 99.25 katika mamlaka 42 za serikali za mitaa hayakulipwa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 10.**

**Jedwali Na. 10: Bajeti pungufu kwa ajili ya kulipa madeni**

| Na | Halmashauri | Deni/madai (Sh.) | Na | Halmashauri | Deni/madai (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jjiji Dodoma | 24,945,385,199 | 23 | H/W Kibaha | 1,523,656,567 |
| 2 | H/Jiji Dar es Salaam | 9,542,097,966 | 24 | H/M Kinondoni | 1,481,432,412 |
| 3 | H/W Bukombe | 3,607,351,174 | 25 | H/W Nkasi | 1,350,576,190 |
| 4 | H/M Sumbawanga | 3,387,777,612 | 26 | H/M Bukoba | 1,264,620,034 |
| 5 | H/W Iringa | 3,138,458,065 | 27 | H/W Urambo | 1,245,081,772 |
| 6 | H/W Kalambo | 3,014,848,000 | 28 | H/W Mpimbwe | 1,214,052,233 |

| Na | Halmashauri | Deni/madai (Sh.) | Na | Halmashauri | Deni/madai (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | H/M Kigoma Ujiji | 2,816,626,087 | 29 | H/Mji Njombe | 1,214,052,233 |
| 8 | H/W Chalinze | 2,729,490,447 | 30 | H/W Nyasa | 1,184,847,576 |
| 9 | H/W Geita | 2,640,600,238 | 31 | H/W Ngara | 1,045,657,140 |
| 10 | H/W Mpwapwa | 2,551,616,107 | 32 | H/W Bagamoyo | 1,015,449,915 |
| 11 | H/W Sumbawanga | 2,311,057,460 | 33 | H/W Misungwi | 1,011,288,385 |
| 12 | H/W Handeni | 2,308,131,747 | 34 | H/W Rufiji | 1,010,158,054 |
| 13 | H/W Kongwa | 2,145,149,621 | 35 | H/W Missenyi | 911,236,121 |
| 14 | H/W Namtumbo | 1,947,544,000 | 36 | H/Mji Mbinga | 886,752,723 |
| 15 | H/W Kyerwa | 1,892,348,447 | 37 | H/W Mkuranga | 734,923,823 |
| 16 | H/W Karagwe | 1,825,779,339 | 38 | H/Mji Mafinga | 533,885,646 |
| 17 | H/W Sikonge | 1,792,988,872 | 39 | H/W Lushoto | 478,317,867 |
| 18 | H/W Kakonko | 1,667,035,500 | 40 | H/W Kilolo | 298,959,193 |
| 19 | H/W Mafia | 1,637,556,172 | 41 | H/W Mufindi | 198,708,929 |
| 20 | H/W Njombe | 1,574,098,595 | 42 | H/W Bahi | 63,000,000 |
| 21 | H/W Newala | 1,571,530,000 | | Jumla | **99,251,228,751** |
| 22 | H/Mji Kibaha | 1,537,101,290 | | | |

Kutengwa kwa bajeti pungufu kwa ajili ya kulipa madeni inazua maswali juu ya uwezo wa kifedha pamoja kuchafua taswira ya taasisi.

Inaweza kusababisha taasisi kulimbikiza madeni kutokana na vikwazo vinavyowekwa katika bajeti ambavyo vinaiondolea taasisi uwezo kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa madeni.

**Kwa kuzingatia niliyoyabainisha, ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, wafanye tathmini kamili ya madeni yaliyosalia na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kulipa madeni, kwa kuzingatia madeni yaliyohakikiwa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa.**

### 4.2.6 Mapato ya ndani mbayo hayakutengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli za vijiji/mitaa kiasi cha Sh. bilioni 20.23

Kufuatia tathmini ya fedha zilizotengwa kwenye bajeti kutoka kwenye vyanzo vya mapato ya ndani katika mamlaka 184 za serikali za mitaa, nilibaini kuwa mamlaka 79 za serikali za mitaa hazikufuata mgao wa asilimia uliopendekezwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo, hivyo kusababisha kiasi cha Sh. bilioni 17.60 kutochangiwa.

Pia, mamlaka 10 za serikali za mitaa hazikutenga kiasi cha Sh. bilioni 0.50 kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za ofisi za vijiji/mitaa; mamlaka saba za serikali za mitaa hazikuchangia kiasi cha Sh. bilioni 0.77 kwa ajili ya shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji; na mamlaka mbili za serikali za mitaa hazikutenga kiasi cha Sh. bilioni 1.32 kwenda TARURA kwa ajili ya

kufadhili miundombinu ya barabara. Hii inafanya jumla ya kiasi cha Sh. bilioni 20.23 ambazo hazikupelekwa kwenye miradi ya maendeleo na uendeshaji kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 10.**

Hii ni kinyume na maelekezo yaliyotolewa kwenye barua ya tarehe 3 Januari 2018 iliyotolewa na OR-TAMISEMI yenye nambari ya kumbukumbu CBD.421/422/01/43. Katika barua hiyo, mamlaka za serikali za mitaa ziligawanywa katika makundi mawili, zikipewa misimbo ya "A" na "B"; ilitoa maelekezo kwa mamlaka ya serikali za mitaa ya kutenga 60% na 40% ya mapato yao ya vyanzo vyao ndani kwa miradi ya maendeleo mtawalia.

Vilevile, Aya ya 83 (iii) na iv) ya mwongozo wa maandalizi ya mipango na bajeti kwa mwaka 2022/23 wa Novemba 2021 iliwaagiza maofisa masuuli ambao mapato yao ya ndani yanazidi Sh. bilioni 5 kutenga 60% ya mapato yao ndani kwa shughuli za maendeleo na halmashauri ambazo mapato yao ya ndani yako chini ya Sh. bilioni 5 kutenga 40% ya mapato ya ndani kwa shughuli za maendeleo.

Pia, Aya ya 1.7.2A (xii) ya mwongozo wa bajeti 2022/23 inawataka wakurugenzi wa halmashauri kutenga kiasi cha Sh. 200,000 na 100,000 (kwa mamlaka za serikali za mitaa zilizo chini ya bilioni 1) kwa robo kutoka kwa mapato ya vyanzo vya ndani kama fedha za uendeshaji wa ofisi kwa kila kijiji/mitaa.

Pia, Aya ya 1.7.2 (107) (B (xi-xiii)) ya mwongozo wa maandalizi ya mipango na bajeti wa 2022/23 inazitaka mamlaka za serikali za mitaa kutenga 20% ya mapato yanayotokana na ushuru wa mazao ili kusaidia shughuli za kilimo, ikiwamo kuchochea uzalishaji mkakati wa mazao, 15% ya mapato yanayotokana na bidhaa za mifugo kuchochea ufugaji wa mifugo, na asilimia tano ya mapato yanayotokana na bidhaa za uvuvi kwa maendeleo ya shughuli za uvuvi.

Pia, waraka na. AE.35/488/01/13 uliotolewa tarehe 06 Desemba 2022 na Katibu Mkuu wa OR-TAMISEMI uliwataka wakurugenzi wa mamlaka za manispaa za Kigamboni, Temeke, Kinondoni, Ubungo, Ilemela, Morogoro, Kahama na Moshi; wakurugenzi wa mamlaka za miji ya Geita, Tunduma na Njombe; na wakurugenzi wa halmashauri za wilaya za Chalinze, Mkuranga na Mufindi kutenga bajeti ya 10% kutoka kwenye mapato ya vyanzo vya ndani kwa ajili ya kufadhili shughuli zinazohusiana na TARURA ndani ya maeneo yao ya mamlaka.

Kutozingatia mwongozo wa bajeti wakati wa maandalizi na utekelezaji unasababisha kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa, hivyo kufanya malengo yaliyokusudiwa kutofikiwa.

**Ninasisitiza mapendekezo yangu ya mwaka uliopita kwamba uongozi wa mamlaka za serikali za mitaa kuzingatia kikamilifu maelekezo ya serikali na mwongozo wa bajeti kwa kutenga fedha ama asilimia iliyokubaliwa kwenye mapato yao ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli za vijiji/mitaa.**

**Pia, kuhakikisha kuwa fedha zote zilizotengwa kwa madhumuni ya maendeleo zinatumika kwa miradi iliyokusudiwa tu, na kuepuka kuchepusha fedha hizo kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo.**

### 4.2.7 Upungufu uliobainika katika fedha za bakaa ya miradi ya maendeleo

#### (i) Fedha za miradi ya maendeleo zilizosalia mwisho wa mwaka Sh. bilioni 19.79

Kanuni Na. 21 (1) na (2) ya Kanuni za Bajeti za mwaka 2015 ambazo inawapa mamlaka maofisa masuuli kuwasilisha maombi ya fedha zilizosalia kwa kutoa taarifa kwa Mlipaji Mkuu na nakala kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu shughuli ambazo hazikutekelezwa ndani ya siku kumi na tano kabla ya tarehe 30 Juni ya kila mwaka wa fedha. Taarifa hiyo inatakiwa kuonesha sababu za kushindwa kutumia fedha; namna ambavyo fedha hizo zitatumiwa; na tathmini ya uwezo wa kutumia fedha hizo sambamba na mgawo mpya wa bajeti; na kwamba fedha zote ambazo hazikutumika mwishoni mwa mwaka wa fedha zitatumika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha unaofuata.

Ingawa, nilibaini mamlaka 27 za serikali za mitaa zilikuwa na kiasi cha Sh. bilioni 19.79 ambazo zilisalia mwisho wa mwaka kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo. Hata hivyo, fedha hizi hazikutumika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha uliofuata wa 2022/23, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 11.**

**Jedwali Na. 11: Fedha za bakaa ambazo hazikutumika kwa wakati**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Liwale | 2,100,413,935 | 15. | H/W Mtwara | 404,525,372 |
| 2. | H/Jiji Dodoma | 2,050,847,000 | 16. | H/W Karagwe | 369,040,500 |
| 3. | H/Jiji Dar es Salaam | 1,866,332,326 | 17. | H/Mji Mafinga | 360,022,654 |
| 4. | H/W Chamwino | 1,425,000,000 | 18. | H/W Rorya | 306,660,772 |
| 5. | H/W Njombe | 1,343,751,376 | 19. | H/W Arusha | 289,281,771 |
| 6. | H/W Mbozi | 1,317,438,387 | 20. | H/Mji Ifakara | 250,000,000 |
| 7. | H/W Tarime | 1,150,000,000 | 21. | H/W Nyasa | 207,766,458 |
| 8. | H/W Makete | 1,055,549,908 | 22. | H/W Shinyanga | 193,905,349 |
| 9. | H/W Mkinga | 1,039,280,028 | 23. | H/W Monduli | 168,258,006 |
| 10. | H/W Musoma | 1,000,000,000 | 24. | H/W Mkalama | 155,471,969 |
| 11. | H/Mji Newala | 915,552,827 | 25. | H/W Muheza | 95,173,906 |
| 12. | H/W Bukombe | 574,838,172 | 26. | H/W Chato | 60,005,046 |
| 13. | H/W Ludewa | 569,099,519 | 27. | H/W Kalambo | 50,291,797 |
| 14. | H/W Mufindi | 467,636,722 | **Jumla** | | **19,786,143,800** |

Kucheleweshwa kwa utoaji wa fedha na idhini au marekebisho ya vifungu katika mifumo kama vile PLANREP, FFARS, na MUSE kumesababisha kutokamilika kwa miradi iliyoidhinishwa na kuchelewesha utoaji wa huduma kwa walengwa. Hali hii inaweza kuongeza gharama za miradi kutokana na athari za mfumuko wa bei.

**(ii) Bakaa ya miradi ya maendeleo ambayo haikurejeshwa na hazina Sh. milioni 832.59**

Nilibaini kuwa mamlaka saba za serikali za mitaa zilirudisha Hazina kiasi cha Sh. milioni 832.59. Hata hivyo, fedha zilizotumwa hazikurudishwa katika mwaka wa fedha wa 2022/23 ili kuruhusu utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

**(iii) Bakaa ya miradi ya maendeleo ambayo haikuhamishwa kwenda hazina Sh. milioni 551.20**

Pia, nimebaini mamlaka mbili za serikali za mitaa zilikuwa na bakaa ya jumla ya kiasi cha Sh. milioni 551.20 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambazo hazikurudishwa Hazina. Hivyo, kufanya jumla ya kiasi cha Sh. bilioni 1.38 ambazo ama hazikurudishwa au kurejeshwa na Hazina kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.12.**

**Jedwali Na. 12: Kutorejeshwa kwa fedha zilizochukuliwa na Hazina**

| A:Fedha za miradi ya maendeleo ambazo hazikupelekwa Hazina | | | |
|---|---|---|---|
| Na. | Halmashauri | Upungufu uliobainika | Kiasi (Sh.) |
| 1 | H/W Momba | Mwishoni mwa mwaka wa fedha, kulikuwa na salio lililosalia kutokana na miradi ya maendeleo kiasi cha Sh. milioni 23.08 ambacho haikurudishwa kwenda Hazina. | 23,082,342 |

| A:Fedha za miradi ya maendeleo ambazo hazikupelekwa Hazina | | | |
|---|---|---|---|
| **Na.** | **Halmashauri** | **Upungufu uliobainika** | **Kiasi (Sh.)** |
| 2 | H/W Bumbuli | Mwishoni mwa mwaka wa fedha, kulikuwa na salio lisilotumika la maendeleo jumla ya kiasi cha Sh. milioni 528.11ambalo halikurudishwa kwenda Hazina. | 528,114,373 |
| Jumla | | | 551,196,715 |
| **B: Fedha za miradi ya maendeleo ambazo hazikurudishwa kutoka Hazina** | | | |
| **Na.** | **Halmashauri** | **Maelezo** | **Kiasi (Sh.)** |
| 1 | H/W Shinyanga | Mwishoni mwa mwaka wa fedha wa 2021/22, Halmashauri ilipokea kiasi cha Sh. bilioni 2.7 kwa ujenzi wa ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ofisi za utawala wa Halmashauri. Mpaka tarehe 30 Juni 2022, Halmashauri ilikuwa imetumia kiasi cha Sh. bilioni 2.02, ikisalia kiasi cha Sh. milioni 676.85 ambazo zilitumwa kurudishwa Hazina kupitia barua yenye kumbukumbu Na. SH/W.F.1.32/126 ya tarehe 1/11/2022. Hata hivyo, fedha zilizohamishwa zenye thamani ya Sh. 676.85 hazikupokelewa katika mwaka wa fedha wa 2022/23 kuruhusu utekelezaji wa shughuli zilizosalia. | 676,847,672 |
| 2 | H/W Bahi | Hazikurudishwa kutoka hazina | 53,152,923 |
| 4 | H/W Sikonge | Hazikurudishwa kutoka hazina | 9,678,637 |
| 5 | H/W Nsimbo | Hazikurudishwa kutoka hazina | 11,319,932 |
| 6 | H/W Mpimbwe | Hazikurudishwa kutoka hazina | 28,629,021 |
| 8 | H/W Kilolo | Hazikurudishwa kutoka hazina | 44,739,010 |
| 9 | H/W Makete | Hazikurudishwa kutoka hazina | 8,224,965 |
| **Jumla** | | | **832,592,160** |
| **Jumla kuu (A+B)** | | | **1,381,926,014** |

Ufuatiliaji usioridhisha wa menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kumesababisha kuchelewa katika kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Ninashauri maofisa masuuli wa mamlaka za serikali za mitaa kuzijumuisha katika bajeti fedha zilizosalia na kuzitumia kutekeleza shughuli zilizoidhinishwa bila kuchelewa. Aidha, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kushirikiana na Wizara ya Fedha kutatua masuala yote yanayohusiana na vifungu vya bajeti kwa fedha za bakaa ambayo yanaweza kusababisha kuchelewa kutumika kwa fedha hizo.**

**Pia, ninapendekeza menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, wafanye mawasiliano na Hazina ili kuhakikisha kwamba fedha za bakaa kiasi cha Sh. milioni 832.60 zinarejeshwa mapema na kuhakikisha kuwa kiasi kilichobaki mwisho**

**wa mwaka ambacho ni Sh. milioni 551.20 kinahamishiwa Hazina. Hii itawezesha utekelezaji wa shughuli zilizosalia za miradi. Aidha, kusimamia utekelezaji wa shughuli za miradi kwa kuhakikisha kuwa inakamilika kwa wakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.**

### 4.2.8 Fedha za miradi zilizochepushwa na kutumika katika shughuli ambazo hazikukusudiwa Sh. bilioni 7.73

Wakati wa ukaguzi, nilibaini mamlaka za serikali za mitaa 25 zilichepusha jumla ya Sh. bilioni 7.73 kutekeleza miradi na shughuli za kawaida ambazo hazikupangwa. Uchepushaji huu wa fedha unadhihirisha kwamba shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa kama ilivyokusudiwa, hivyo kuathiri uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa katika kutoa huduma bora kwa jamii kama ilinavyoelezwa katika **Kiambatisho Na.11.**

Hii inakiuka Agizo Na. 18(4) la memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 ambalo limeweka zuio la kuhamisha fedha baina ya bajeti ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Agizo hilo linaeleza kuwa hakutakuwa na uhamisho wa fedha baina ya bajeti ya maendeleo na matumizi ya kawaida, pasipo kupata idhini ya Baraza la Madiwani ambapo michango kwa ajili ya matumizi ya kawaida kutoka vyanzo vya mapato ya ndani kwenye bajeti ya maendeleo inaweza kutofautiana.

Aidha, Kifungu Na. 27(4) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, kinahitaji rasilimali zilizoidhinishwa kutumika kwa lengo lililokusudiwa na kwa kuzingatia vifungu mbalimbali vilivyobainishwa kwenye makadirio ya taasisi za serikali. Aidha, Kifungu Na.41 cha Sheria ya Bajeti, [Sura ya 439], kinazuia kubadili matumizi ya fedha za maendeleo kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Uchepushaji wa fedha umeathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa, hivyo kuathiri utoaji wa huduma bora na zilizokusudiwa kwa jamii.

**Ili kutatua hali hii, ninasisitiza menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuzingatia taratibu na miongozo ya bajeti. Hii inajumuisha kubainisha shughuli zote muhimu mwanzoni ili kupunguza kufanya mabadiliko ya vifungu vya matumizi wakati wa utekelezaji wa bajeti na hivyo kubaki katika lengo la bajeti.**

### 4.2.9 Fedha zilizobadilishwa matumizi bila kuidhinishwa na mamlaka husika na utumiaji wa nyaraka za kubadili matumizi za udanganyifu kiasi cha Sh. bilioni 4.88

Nilibaini kwamba mamlaka nne za serikali za mitaa zilibadilisha matumizi ya kiasi cha Sh. bilioni 4.88 bila kupata idhini kutoka kwa mamlaka husika, zikiwamo Baraza la Madiwani na Waziri wa Fedha. Kati ya hizo, nilibaini H/W Mpimbwe ilipanga kutumia bajeti ya kiasi cha Sh. bilioni 7.06 kwa ajili ya kulipa mishahara; hata hivyo, bajeti hiyo ilibadilishwa kwa kuongeza kiasi cha Sh. bilioni 2.07. Kati ya kiasi kiasi hicho kilichotengwa, Sh. bilioni 1.61 tu ndizo zilizotumika.

Pia, nilibaini nyaraka za mihutasari ya kikao cha kamati ya fedha, mipango na uongozi kilichofanyika tarehe 5 Juni 2023 zilighushiwa na kuwasilishwa Hazina kwa ajili ya kuomba kibali cha kubadili vifungu vya bajeti ya mishahara, ingawa kikao hicho hakikufanyika kama inavyoelezwa kwenye **Jedwali Na.13.**

Hii ni kinyume na Kifungu Na. 41(2) cha Sheria ya Bajeti, [Sura ya 439], ambacho kinaeleza kwamba ofisa masuuli hatabadilisha matumizi ya fedha endapo fedha hizo zinapaswa kuhamishwa kwenda kwa mtu au kwa taasisi zingine za serikali.

Maombi ya kubadilisha matumizi ya fedha yanapaswa kuambatishwa na taarifa inayoelezea kikamilifu sababu za ukosefu wa fedha zilizoidhinishwa awali. Baada ya kujadiliwa na kamati ya fedha mipango na uongozi, maombi hayo huwasilishwa kwa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kuidhinishwa.

Pia, Kifungu cha 41(1&2) cha Sheria ya Bajeti, [Sura ya 439], kinaruhusu ofisa masuuli, kwa idhini ya waziri, kubadili matumizi kutoka kwenye matumizi yaliyoidhinishwa. Hata hivyo, Ofisa masuuli hatabadili matumizi ya fedha katika mazingira yafuatayo: ambapo fedha zimetengwa kwa ajili ajili ya kazi maalum; fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuhamishwa kwenda kwa mtu au taasisi zingine za serikali; fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya shughuli zinazohusiana namaendeleo; fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara kwenda kwenye matumizi mengine yasiyo ya mishahara; na uhamishaji wa fedha mwingineo unaweza kusababisha ukiukwaji wa kanuni za kifedha.

**Jedwali Na. 13: Kubadili matumizi ya fedha bila kibali**

| Na | Halmashauri | Upungufu uliobainika | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Mwanza | Kubadilisha matumizi ya fedha bila idhini kamili ya Baraza la Madiwani kiasi cha Sh. 2,190,988,679 na kiasi cha Sh. 180,000,000 ambazo hazikuidhinishwa na Waziri wa Fedha. | 2,370,988,679 |
| 2 | H/Jiji Dodoma | Kubadili matumizi bila kibali cha waziri wa fedha | 264,000,000 |
| 3 | H/M Sumbawanga | Kubadili matumizi bila kibali cha Waziri wa Fedha | 184,693,826 |
| 4 | H/W Mpimbwe | Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe ilipanga bajeti ya kiasi cha Sh. 7,053,390,000 kwa mishahara ya wafanyakazi, hata hivyo; bajeti hiyo ilibadilishwa kwa kuongeza kiasi cha Sh. 2,065,204,500 ambayo inazidi kiwango kilichoidhinishwa kwa kiasi cha Sh. 2,065,204,500. Kati ya kiwango kilichoidhinishwa, Kiasi cha Sh. 1,607,135,124 zilitumika kwenye Halmashauri. Pia, ilibainika kuwa, Kikao cha kamati ya fedha, mipango na uongozi kilichofanyika tarehe 05 Juni 2023 zilighushiwa na kuwasilishwa Hazina kwa ajili ya kibali cha kubadilisha matumizi ya bajeti ya mishahara ya wafanyakazi wakati kikao hakikuwa kimefanyika na hivyo hakikuidhinishwa na Baraza la Wafanyakazi. | 2,065,204,500 |
| **Jumla** | | | **4,884,887,005** |

Upungufu katika uzingatiaji wa miongozo ya bajeti unaweza kusababisha kubadili matumizi ya fedha bila kupata idhini kutoka kwenye mamlaka husika.

**Ninasisitiza menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zizingatie miongozo ya bajeti kwa kuhakikisha kwamba idhini ya kubadili matumizi ya fedha inapatikana kutoka kwa mamlaka husika.**

**Pia, hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya wote waliohusika katika malipo ya udanganyifu. Hatua hii itasaidia kupunguza kubadili fedha matumizi isivyoruhusiwa wakati wa utekelezaji wa bajeti, hivyo kuhakikisha mchakato wa kupata idhini unazingatiwa ili kulinda uadilifu wa uzingatiaji bajeti.**

# SURA YA TANO




## USIMAMIZI WA UNUNUZI NA MIKATABA

### 5.0 Utangulizi

Kifungu cha 48(1) (b) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410, kinawataka maofisa masuuli kuhakikisha ununuzi unazingatia taratibu zilizowekwa; na pia, Kifungu Na. 48(3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410, kinanitaka kufanya tathmini ya kubaini endapo taasisi nunuzi zilizingatia vifungu vya sheria ya ununuzi wa umma pamoja na kanuni zake.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini maeneo kadhaa ambayo taasisi zilizokaguliwa hazikuzingatia sheria za ununuzi pamoja na taratibu zilizowekwa. Dosari hizo zinaanzia kwenye upungufu wa nyaraka hadi usimamizi duni, hivyo kusababisha kukosekana kwa ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma.

### 5.1 Usimamizi wa ununuzi

#### 5.1.1 Ukosefu wa ufanisi katika bodi za zabuni

Kanuni ya 47(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inamtaka afisa masuuli kutomteua mtu kwenye bodi ya zabuni iwapo mtu huyo atakuwa anakaimu majukumu ya afisa masuuli mara kwa mara. Pia, aya ya 5 ya jedwali la pili la sheria ya ununuzi wa umma, Sura ya 410, inazitaka bodi za zabuni kukutana kila robo mwaka.

Nimefanya tathmini ya utendaji wa bodi za zabuni na vitengo vya ununuzi na kubaini kuwa, maofisa ambao walikaimishwa mara kwa mara majukumu ya maofisa masuuli walikuwa pia wajumbe wa bodi za zabuni katika mamlaka nne za serikali za mitaa.

Vilevile, nilibaini kuwa bodi ya zabuni ya halmashauri ya manispaa ya Kigamboni haikuitisha vikao katika robo tatu za mwaka wa fedha 2022/23 kama ilivyobainishwa kwenye **Jedwali Na.14**.

**Jedwali Na. 14: Upungufu ya utendaji bodi za zabuni**

| Na | Halmashauri | Upungufu |
|---|---|---|
| 1. | H/W Karatu | Wajumbe wa bodi ya zabuni kukaimishwa majukumu ya ofisa masuuli |
| 2. | H/W Kibaha | |
| 3. | H/W Maswa | |
| 4. | H/W Masasi | |
| 5. | H/M Kigamboni | Vikao vitatu katika robo tatu za mwaka havikufanyika |

Aidha, Kanuni ya 58 (1) ya kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 inaelekeza kuwa uamuzi wa bodi ya zabuni unaweza kufanywa kupitia azimio kwa njia ya waraka, kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa na mamlaka ya kudhibiti ununuzi wa umma (PPRA).

Aya ya 11.2 ya mwongozo wa PPRA wa uamuzi wa bodi ya zabuni kupitia azimio la waraka uliotolewa Mei 2020, inaelekeza muhtasari wa uamuzi wa ununuzi kwa njia ya maazimio ya waraka kuwasilishwa katika kikao cha bodi ya zabuni kinachofuata.

Nilipitia uamuzi wa ununuzi uliofanywa kupitia maazimio kwa njia ya waraka na kubaini kuwa, katika mamlaka sita za serikali ya mitaa, ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 3.28 ulipitishwa kupitia maazimio kwa njia ya waraka. Hata hivyo, maazimio hayo hayakutolewa taarifa kwenye vikao vya kawaida vya bodi za zabuni kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa na PPRA. Maelezo zaidi yanaoneshwa kwenye **Jedwali Na.15.**

**Jedwali Na. 15: Ununuzi kwa njia ya waraka ambayo haujaripotiwa**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 1. | H/M Ubungo | 1,940,894,854 |
| 2. | H/W Mkuranga | 1,017,203,677 |
| 3. | H/Jiji Tanga | 155,952,100 |
| 4. | H/Mji Kibaha | 92,818,218 |
| 5. | H/W Mpanda | 37,731,904 |
| 6. | H/Mji Bariadi | 31,618,942 |
| | **Jumla** | **3,276,219,695** |

Aidha, Kanuni ya 58(4) ya Kanuni za Ununuzi inaelekeza kuwa, nusu ya wajumbe wa bodi ya zabuni wanaunda akidi ya uamuzi wa bodi ya zabuni kupitia azimio kwa njia ya waraka.

Ukaguzi wangu ulibaini mamlaka za serikali za mitaa tano zilifanya uamuzi kupitia maazimio kwa njia ya waraka kwa ununuzi wenye thamani

ya Sh. milioni 258.76 wakiwa pungufu ya akidi. Hii ni kinyume na kanuni iliyotajwa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.16.**

**Jedwali Na. 16: Uamuzi ya wajumbe wa bodi ya zabuni pungufu ya akidi**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Kalambo | 119,257,763 |
| 2. | H/W Busega | 66,554,746 |
| 3. | H/W Igunga | 30,469,320 |
| 4. | H/W Ikungi | 28,908,530 |
| 5. | H/W Mbinga | 13,566,645 |
| | **Jumla** | **258,757,004** |

Upungufu uliobainika ulitokana na kutokuzingatiwa kikamilifu kwa matakwa ya sheria, kanuni na miongozo ya ununuzi wa umma. Aidha, muundo na utendaji usioridhisha wa bodi ya zabuni unaweza kusababisha michakato ya ununuzi isiyofaa na yenye upendeleo; hivyo kusababisha kukosekana kwa thamani ya fedha na kutoa nafasi ya ubadhirifu wa fedha za umma.

**Ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa husika kuzingatia kanuni za ununuzi ili kuleta ufanisi wa bodi za zabuni katika kutekeleza jukumu lake la usimamizi. Hii ni muhimu ili kuwezesha ununuzi wa gharama nafuu na kulinda fedha za umma.**

### 5.1.2 Ununuzi uliofanyika nje ya mpango wa ununuzi Sh. bilioni 28.87

Kanuni ya 69(3) ya kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 inaitaka taasisi nunuzi kufanya makisio ya mahitaji yake ya bidhaa, huduma, na ujenzi kwa usahihi kadiri iwezekanavyo kwa kuzingatia huduma au shughuli ambazo zipo katika mpango kazi na kujumuishwa katika makadirio ya kila mwaka.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kwamba, mamlaka 22 za serikali za mitaa zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 28.87 nje ya mipango yao ya ununuzi wa mwaka, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.17.**

**Jedwali Na. 17: Ununuzi nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Ulanga | 5,551,451,725 | | H/W Msalala | 440,000,000 |
| 2. | H/M Kinondoni | 4,638,346,190 | 13. | H/W Butiama | 369,001,602 |
| 3. | H/W Bukombe | 4,032,503,239 | 14. | H/M Shinyanga | 270,250,000 |
| 4. | H/M Temeke | 2,669,567,475 | 15. | H/W Bahi | 231,782,474 |
| 5. | H/W Lindi | 2,493,516,043 | 16. | H/W Busega | 138,390,200 |
| 6. | H/W Iramba | 1,897,400,000 | 17. | H/W Maswa | 134,938,900 |

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 7. | H/Jiji Dar es Salaam | 1,724,034,561 | 18. | H/W Kilindi | 115,810,000 |
| 8. | H/W Karatu | 1,584,274,793 | 19. | H/W Serengeti | 29,443,890 |
| 9. | H/W Nzega | 881,400,000 | 20. | H/W Meru | 17,200,000 |
| 10. | H/Mji Kibaha | 878,067,420 | 21. | H/M Musoma | 14,182,974 |
| 11. | H/W Mvomero | 750,000,000 | 22. | H/Mji Bariadi | 9,382,500 |
| | | | | **Jumla** | **28,870,943,986** |

Kushindwa kutumia kikamilifu udhibiti wa ndani uliopo na kutokuhuisha mipango ya ununuzi wa mwaka kwa kiasi cha fedha zilizopokelewa nje ya bajeti iliyoidhinishwa, kulisababisha ununuzi kufanywa nje ya mipango ya ununuzi.

Ununuzi uliofanywa nje ya mipango ya ununuzi na bajeti unaweza kusababisha matumizi yasiyopangwa na kushindwa kutekeleza shughuli zilizopangwa katika mipango ya ununuzi na bajeti.

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa zihakikishe zinafanya ununuzi kulingana na mipango yao ya ununuzi iliyoidhinishwa; na zinapaswa kuboresha mchakato wa kupanga bajeti zao ili kuhakikisha bajeti zinakuwa na uhalisia.**

### 5.1.3 Ununuzi ambayo haukuidhinishwa na bodi za zabuni - Sh. bilioni 4.79

Kanuni ya 55 (2), 163 (4) na 185 (1) za Kanuni za Ununuzi za Mwaka za mwaka 2013 zinazuia mamlaka za serikali za mitaa kutoa zabuni, isipokuwa kama zabuni hiyo imeidhinishwa na bodi ya zabuni.

Kinyume na matakwa ya Kanuni, nilibaini kuwa mamlaka 19 za serikali za mitaa zilifanya ununuzi ya bidhaa mbalimbali zenye thamani ya Sh. bilioni 4.79 bila ya kuidhinishwa na bodi za zabuni za mamlaka husika kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 18.**

**Jedwali Na. 18: Ununuzi usioidhinishwa na bodi za zabuni**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Kigamboni | 1,458,720,100 | 11. | H/W Songea | 113,574,160 |
| 2. | H/M Temeke | 773,473,558 | 12. | H/Mji Mbinga | 112,211,500 |
| 3. | H/M Kigoma/Ujiji | 491,421,916 | 13. | H/W Mpimbwe | 103,624,053 |
| 4. | H/W Mlele | 346,822,918 | 14. | H/W Busega | 89,658,801 |
| 5. | H/W Bumbuli | 238,554,910 | 15. | H/W Meatu | 86,979,849 |
| 6. | H/W Pangani | 209,404,886 | 16. | H/M Singida | 82,164,500 |
| 7. | H/W Kigoma | 191,715,830 | 17. | H/W Lushoto | 47,538,036 |
| 8. | H/W Kasulu | 130,806,808 | 18. | H/W Nachingwea | 39,045,560 |
| 9. | H/W Momba | 128,220,992 | 19. | H/W Mpwapwa | 24,898,170 |
| 10. | H/W Rufiji | 119,180,000 | | **Jumla** | **4,788,016,547** |

Aidha, Kanuni ya 166 (7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2013 inataka ununuzi wowote mdogo kutolewa taarifa katika bodi za zabuni kila mwezi.

Katika ukaguzi wangu nilibaini manunuzi katika mamlaka 10 za serikali za mitaa yenye thamani ya Sh. milioni 965.89 yalifanyika bila kutolewa taarifa kwenye bodi za zabuni kila mwezi, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 19.**

**Jedwali Na. 19: Ununuzi mdogo bila taarifa kwa bodi ya zabuni**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kibiti | 145,987,319 | 6. | H/W Singida | 73,103,815 |
| 2. | H/W Iramba | 254,546,774 | 7. | H/W Kisarawe | 53,475,373 |
| 3. | H/M Lindi | 196,213,091 | 8. | H/W Simanjiro | 39,065,204 |
| 4. | H/Mji Mbinga | 73,836,550 | 9. | H/W Muheza | 38,195,780 |
| 5. | H/W Kilindi | 73,466,831 | 10. | H/W Mpanda | 17,999,400 |
| | | | | **Jumla** | **965,890,137** |

Kukosekana kwa mapitio na kutozingatiwa kwa kanuni za ununuzi zilizowekwa, kulisababisha ununuzi kufanywa bila kibali cha bodi ya zabuni, na kushindwa kutolea taarifa ununuzi mdogo kwenye bodi za zabuni.

Ununuzi unaofanywa bila idhini ya bodi za zabuni huzuia bodi kutekeleza majukumu yake ya usimamizi; hivyo basi masuala ya uwajibikaji, ubora na thamani ya fedha yanaweza kukiukwa.

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa zichukue hatua stahiki, ikiwamo kuongeza udhibiti na mapitio ya taratibu za ununuzi na miamala. Pia, zinapaswa kutokuacha kupitisha ununuzi kwenye bodi ya zabuni.**

### 5.1.4 Ununuzi waliyofanyika nje ya mfumo wa kielekitroni Sh. bilioni 28.13

Kanuni ya 342 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inaeleza kuwa, “Mfumo wa ununuzi wa kielekitroni utatekelezwa na taasisi zote zinazofanya ununuzi kwa ukamilifu au sehemu, sambamba na taratibu za kawaida zilizo kwenye mwongozo”.

Pia, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ilitoa tangazo kujulisha umma na wadau kuhusu ununuzi wa umma kuanza kufanyika kwa njia ya mfumo wa ununuzi wa kielekitroni kuanzia tarehe 20 Agosti 2019.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mamlaka 31 za serikali za mitaa, zilifanya ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 27.43 nje ya mfumo wa ununuzi wa kielekitroni, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.20**.

**Jedwali Na. 20: Ununuzi uliofanyika nje ya mfumo wa kieletroniki**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Geita | 9,410,879,482 | 18. | H/W Sumbawanga | 279,840,407 |
| 2. | H/W Bagamoyo | 2,794,560,000 | 19. | H/W Shinyanga | 275,732,590 |
| 3. | H/W Bukombe | 1,637,358,855 | 20. | H/W Rombo | 252,502,041 |
| 4. | H/W Siha | 1,607,858,694 | 21. | H/W Malinyi | 194,260,749 |
| 5. | H/W Liwale | 1,490,651,300 | 22. | H/W Itigi | 186,683,658 |
| 6. | H/Jiji Dar es Salaam | 1,223,462,150 | 23. | H/W Mbozi | 177,213,620 |
| 7. | H/W Meatu | 1,164,893,034 | 24. | H/M Iringa | 163,404,380 |
| 8. | H/W Itilima | 1,141,083,756 | 25. | H/W Korogwe | 162,660,281 |
| 9. | H/W Mbinga | 1,072,187,388 | 26. | H/Mji Mafinga | 90,873,120 |
| 10. | H/W Chato | 673,377,174 | 27. | H/W Singida | 90,532,745 |
| 11. | H/W Msalala | 531,349,050 | 28. | H/W Maswa | 89,250,000 |
| 12. | H/Mji Mbinga | 509,985,856 | 29. | H/W Songea | 76,639,272 |
| 13. | H/W Ushetu | 450,980,880 | 30. | H/W Kisarawe | 59,830,900 |
| 14. | H/W Mvomero | 429,696,291 | 31. | H/W Iramba | 55,725,720 |
| 15. | H/Mji Nzega | 373,226,882 | 32. | H/W Mbarali | 52,455,281 |
| 16. | H/W Mwanga | 331,831,524 | 33. | H/Mji Kibaha | 296,925,529 |
| 17. | H/W Ulanga | 308,783,979 | | **Jumla** | **27,427,027,687** |

Aidha, mapitio yangu ya mikataba tisa iliyotolewa kwa njia ya kielekitroni yenye thamani ya Sh. bilioni 1.43 katika mamlaka mbili za serikali za mitaa, yalibaini udhaifu kama vile afisa masuuli kushindwa kutoa tuzo za mikataba kwa njia ya kielekitroni, kinyume na Kifungu cha 35 (6) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma,[Sura ya 410]; kamati za tathmini kuwa na wajumbe wachache, kinyume na Kanuni ya 202 (1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 69 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Marekebisho) ya mwaka mwaka 2016 (Tangazo la Serikali Na. 333 ya 30.12.2016); na Kamati za tathmini kushindwa kukamilisha na kuweka taarifa za tathmini ndani ya mfumo wa ununuzi wa kielekitroni, kinyume na Kifungu cha 74 (4) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410. Rejea **Jedwali Na.21.**

**Jedwali Na. 21: Mapungufu katika ununuzi kupitia mfumo wa kielektroni**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) | Idadi ya mikataba |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Lushoto | 1,229,412,200 | 6 |
| 2. | H/M Kigamboni | 203,962,000 | 3 |
| | **Jumla** | **1,433,374,200** | **9** |

Kutokupatikana kwa wazabuni wa kutosha waliojisajili kwenye mfumo wa kielekitroni; kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa maofisa ununuzi wa kutumia mfumo ipasavyo; na kukosekana kwa usaidizi katika matumizi ya mfumo wa kielekitroni vilisababisha mamlaka za serikali za mitaa kushindwa kutumia mfumo kikamilifu.

Maoni yangu ni kwamba kushindwa kutumia mfumo wa kielekitroni kikamilifu kutasababisha kutofikiwa kwa malengo ya serikali ya kuongeza ufanisi, kupunguza muda wa ununuzi, kupunguza vihatarishi, na kuboresha uwazi na haki katika ununuzi wa umma kupitia ununuzi wa kielekitroni.

**Ninashauri maafisa masuuli wa mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kuwa, maafisa ununuzi na TEHAMA wanawezeshwa kupata ujuzi wa kitaalamu kuhusu mfumo wa ununuzi wa kielekitroni na kushirikiana na mamlaka ya kudhibiti ununuzi wa umma kuhamasisha wadau wote kuhusu jinsi ya kufanya kazi kwa ufanisi kutumia mfumo huo wa kielekitroni.**

### 5.1.5 Ununuzi wa bidhaa uliofanyika kwa wazabuni ambao hawakuidhinishwa na GPSA - Sh. bilioni 5.99

Kanuni ya 131 (4) (b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 42 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (marekebisho) ya mwaka 2016 (Tangazo la Serikali Na. 333 la 30/12/2016) inahitaji taasisi nunuzi kununua bidhaa na huduma za matumizi ya kawaida kutoka kwa wazabuni waliopewa mikataba ya Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA) kupitia mkataba mdogo wa ununuzi uliotayarishwa na kitengo cha usimamizi wa ununuzi.

Ukaguzi wa usimamizi wa ununuzi na mikataba ulibaini kuwa, mamlaka 26 za serikali ya mitaa zilifanya ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 5.99 kutoka kwa wazabuni ambao hawajaidhinishwa na Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA), kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na.22.**

**Jedwali Na. 22: Ununuzi kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|---|---|---:|
| 1 | H/M Temeke | 1,335,109,058 | 15 | H/M Shinyanga | 138,244,440 |
| 2 | H/W Magu | 578,305,327 | 16 | H/W Kaliua | 124,173,000 |
| 3 | H/M Musoma | 456,543,439 | 17 | H/W Rorya | 115,888,789 |
| 4 | H/W Tarime | 450,261,376 | 18 | H/Mji Nzega | 91,653,053 |

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | H/Jiji Mwanza | 325,018,387 | 19 | H/Mji Bunda | 84,688,160 |
| 6 | H/Mji Tarime | 281,973,930 | 20 | H/W Mbarali | 73,909,856 |
| 7 | H/W Musoma | 263,257,703 | 21 | H/W Misungwi | 70,422,248 |
| 8 | H/W Sengerema | 213,910,311 | 22 | H/W Serengeti | 67,488,000 |
| 9 | H/W Ukerewe | 201,830,965 | 23 | H/W Nsimbo | 61,282,600 |
| 10 | H/W Msalala | 197,037,446 | 24 | H/W Ileje | 57,391,053 |
| 11 | H/W Urambo | 193,094,202 | 25 | H/W Mbozi | 46,033,500 |
| 12 | H/Mji Tunduma | 192,590,025 | 26 | H/W Mpimbwe | 9,995,425 |
| 13 | H/Mji Korogwe | 182,428,230 | | **Jumla** | **5,994,439,162** |
| 14 | H/M Singida | 181,908,639 | | | |

Kwa sababu ya dhamira duni ya uzingatiaji wa kanuni za ununuzi kwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, walishindwa kuhakikisha kuwa bidhaa zinanunuliwa kutoka kwa wazabuni walioidhinishwa na GPSA pekee.

Kwa maoni yangu, ununuzi kutoka kwa wasambazaji ambao hawako kwenye orodha iliyoidhinishwa na GPSA unaweza kusababisha kununua bidhaa kwa bei ya juu na kupokea bidhaa za ubora wa chini.

**Ninapendekeza maafisa masuuli wa mamlaka za serikali za mitaa wahakikishe ununuzi wa bidhaa na huduma unafanywa kutoka kwa wasambazaji walioidhinishwa na GPSA ili kupata bidhaa bora na kwa bei nafuu.**

### 5.1.6 Ununuzi uliofanyika pasipo ushindanishi wa bei - Sh. bilioni 4.65

Kanuni ya 164(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaagiza taasisi inayofanya ununuzi kupata nukuu za bei kutoka kwa wazabuni/wauzaji wasiopungua watatu.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini ununuzi wenye jumla ya Sh. bilioni 4.65 ulifanyika katika mamlaka 36 za serikali za mitaa bila kuitisha nukuu za ushindanishi wa bei, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.23**.

**Jedwali Na. 23: Ununuzi uliofanyika bila ushindanishi wa bei**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Mbinga | 559,759,587 | 20 | H/W Namtumbo | 84,692,512 |
| 2 | H/W Bunda | 501,288,939 | 21 | H/W Igunga | 75,702,000 |
| 3 | H/M Kinondoni | 450,000,000 | 22 | H/Jiji Dar es Salaam | 58,643,915 |
| 4 | H/W Mbozi | 352,916,305 | 23 | H/Mji Geita | 54,535,238 |
| 5 | H/M Kigoma | 238,496,146 | 24 | H/W Kisarawe | 50,636,000 |
| 6 | H/W Msalala | 197,037,446 | 25 | H/W Kongwa | 48,442,914 |
| 7 | H/W Mlele | 188,575,495 | 26 | H/W Kasulu | 45,220,606 |
| 8 | H/M Shinyanga | 161,045,536 | 27 | H/W Iramba | 45,081,313 |
| 9 | H/W Bariadi | 158,530,696 | 28 | H/W Songea | 38,350,571 |

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 10 | H/W Mpanda | 157,444,898 | 29 | H/W Itigi | 37,456,090 |
| 11 | H/W Ileje | 154,295,792 | 30 | H/W Serengeti | 34,597,030 |
| 12 | H/W Kilindi | 134,359,300 | 31 | H/W Manyoni | 29,402,558 |
| 13 | H/W Ushetu | 125,727,345 | 32 | H/W Ikungi | 27,339,730 |
| 14 | H/W Kishapu | 114,400,000 | 33 | H/W Itilima | 27,138,000 |
| 15 | H/W Ukerewe | 112,908,780 | 34 | H/W Kakonko | 24,201,960 |
| 16 | H/W Tunduru | 102,814,060 | 35 | H/W Misungwi | 14,779,280 |
| 17 | H/W Mpimbwe | 88,557,579 | 36 | H/W Newala | 9,162,688 |
| 18 | H/W Meatu | 86,979,849 | | **Jumla** | **4,649,975,978** |
| 19 | H/W Kigoma | 86,593,820 | | | |

Mamlaka za serikali za mitaa hazikuzingatia ipasavyo sheria na taratibu za ununuzi, hivyo kusababisha kufanyika kwa ununuzi bila ushindanishi wa bei.

Ununuzi ambao ulihusisha Sh. bilioni 4.65 bila kutumia nukuu za bei kutoka kwa wazabuni, ulipunguza uwezekano wa mamlaka za serikali za mitaa kufikia bei nafuu zaidi na kupata thamani ya fedha katika ununuzi huo.

**Ninaishauri OR-TAMISEMI kuelekeza mamlaka za serikali za mitaa kuzingatia sheria na kanuni za ununuzi wa umma ili kupata thamani ya fedha, pamoja na kutoa fursa na haki sawa kwa wazabuni wote.**

### 5.1.7 Ununuzi wa bidhaa bila kubainisha viwango/vipimo - Sh. bilioni 2.64

Kanuni ya 164 (2) (b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inasema "Barua ya mwaliko wa nukuu ya bei na viambatisho vyovyote vitakuwa na maelezo kamili ya bidhaa, kazi au huduma zitakazonunuliwa, ikijumuisha sifa za kiufundi au ubora unaohitajika, vipimo, miundo, mipango, na michoro inayostahili".

Nilibaini kuwa ununuzi wa madirisha ya aluminiamu, meza na viti vya ofisi, mashine za kufulia nguo, na vigae vyenye thamani ya Sh. 2.64 bilioni katika mamlaka 24 za serikali za mitaa ulifanyika bila kubainisha viwango/vipimo vya kina kuhusu bidhaa hizo kwa wazabuni, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.24.**

**Jedwali Na. 24: Ununuzi wa bidhaa bila kuanisha viwango/vipimo**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Tunduma | 414,428,400 | 14 | H/W Busega | 66,929,000 |
| 2 | H/Jiji Tanga | 281,400,000 | 15 | H/W Musoma | 64,389,107 |
| 3 | H/W Butiama | 214,736,000 | 16 | H/W Handeni | 58,238,400 |
| 4 | H/W Kalambo | 205,494,758 | 17 | H/W Namtumbo | 55,865,285 |

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | H/W Maswa | 166,042,500 | 18 | H/W Nyasa | 52,311,650 |
| 6 | H/W Mbozi | 151,705,725 | 19 | H/Jiji Arusha | 45,391,250 |
| 7 | H/W Mpwapwa | 140,000,000 | 20 | H/W Mkalama | 43,999,000 |
| 8 | H/W Manyoni | 119,742,105 | 21 | H/W Kondoa | 36,496,464 |
| 9 | H/M Singida | 112,662,200 | 22 | H/W Lushoto | 28,126,154 |
| 10 | H/M Sumbawanga | 100,352,725 | 23 | H/W Serengeti | 19,999,855 |
| 11 | H/W Nsimbo | 92,615,800 | 24 | H/Mji Korogwe | 19,194,393 |
| 12 | H/Mji Kasulu | 80,404,100 | | **Jumla** | **2,640,318,375** |
| 13 | H/W Mpimbwe | 69,793,504 | | | |

Aidha, Kanuni ya 239 (8) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inakataza kukaribisha zabuni kwa wakandarasi wadogo na wazabuni kwa mikataba ya kazi, hadi michoro na vipimo viwe vimekamilika na makadirio ya gharama yameandaliwa.

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Butiama ilitekeleza ufungaji wa mifumo mbalimbali katika jengo la utawala kama vile mfumo wa umeme, vitambua-moto, mifumo ya kengele, kamera za CCTV, mfumo wa sauti, mfumo wa kutolea matangazo, na viyoyozi kupitia wakandarasi wadogo kwa thamani ya Sh. milioni 522 bila nyaraka zozote kuelezea mifumo hiyo, ikiwamo michoro, usanifu, miundo na vipimo vya kiufundi. Hali hii inaweza kusababisha kufungwa kwa mifumo isiyokidhi ubora unaotakiwa.

Pia, kwa kushindwa kutoa michoro na maelezo ya kina kwa wakandarasi wadogo wa mifumo iliyofungwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikuzingatia sheria, na huenda bei iliyolipwa haikuwa sahihi.

**Napendekeza OR-TAMISEMI iimarishe ufuatiliaji na usimamizi wa mamlaka za serikali za mitaa. Pia, maafisa masuuli wa mamlaka za serikali za mitaa wanatakiwa kuhakikisha kuwa maelezo ya kitaalamu ya ununuzi yanaandikwa vizuri ili kuepuka kupokea bidhaa zisizohitajika, hatimaye kushindwa kupata thamani ya fedha.**

### 5.1.8 Matumizi ya mzabuni mmoja au wachache badala ya njia ya ushindanishi kwa ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 4.87

Kanuni ya 76 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 iliyorekebishwa na Kanuni ya 27 ya Kanuni za ununuzi wa Umma (Marekebisho) ya mwaka mwaka 2016 (Tangazo la Serikali Na. 333 ya tarehe 30.12.2016) inaitaka taasisi nunuzi inayojihusisha na ununuzi, huduma, bidhaa na kazi ya uondoaji wa mali za umma kwa zabuni, kufanya hivyo kwa njia ya ushindani wa zabuni.

Tathmini yangu ya usimamizi wa ununuzi ilibaini kuwa, ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 4.87, uliofanywa na mamlaka 16 za serikali za mitaa, kwa kutumia mzabuni mmoja, au wachache badala ya njia ya ushindanishi, kinyume na matakwa ya sheria. Taasisi hizo zimeorodheshwa kwenye **Jedwali Na.25.**

**Jedwali Na. 25: Taasisi zilizotumia njia ya ununuzi wa mzabuni mmoja au wachache**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Njia ya ununuzi |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dar es Salaam | 1,800,000,000 | Mzabuni Mmoja |
| 2 | H/Mji Mbulu | 750,473,162 | Mzabuni Mmoja |
| 3 | H/W Tarime | 469,273,400 | Wazabuni wachache |
| 4 | H/W Uvinza | 410,801,600 | Mzabuni Mmoja |
| 5 | H/W Rorya | 349,887,021 | Wazabuni wachache |
| 6 | H/W Rombo | 192,500,000 | Mzabuni Mmoja |
| 7 | H/W Kongwa | 155,000,000 | Wazabuni wachache |
| 8 | H/M Musoma | 130,729,423 | Wazabuni wachache |
| 9 | H/W Muleba | 110,000,000 | Mzabuni Mmoja |
| 10 | H/M Iringa | 95,894,553 | Mzabuni Mmoja |
| 11 | H/Jiji Arusha | 95,121,034 | Mzabuni Mmoja |
| 12 | H/W Butiama | 85,323,559 | Mzabuni Mmoja |
| 13 | H/Mji Kasulu | 73,865,952 | Mzabuni Mmoja |
| 14 | H/Mji Bunda | 67,979,238 | Wazabuni wachache |
| 15 | H/W Kisarawe | 41,293,495 | Mzabuni Mmoja |
| 16 | H/M Ilemela | 39,972,700 | Mzabuni Mmoja |
| | **Jumla** | **4,868,115,137** | |

Pia, Kanuni ya 73 (1) kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 inakataza taasisi nunuzi kugawanya ununuzi wake katika mikataba tofauti ili kuepuka matumizi ya njia za kiushindani wa kimataifa au kitaifa.

Wakati wa ukaguzi wa halmashauri ya wilaya ya Butiama, nilibaini kugawanywa kwa makusudi kwa ununuzi wenye thamani ya Sh. milioni 214.74 kwa ajili ya ununuzi wa samani kuwa Sh. milioni 119.4 na Sh. milioni 95.33. Kugawanywa huku kulifanywa ili kuepuka matumizi ya njia za ushindani wa zabuni ya kitaifa na kubaki ndani ya ukomo wa ununuzi kwa njia ya nukuu ya Sh. milioni 120 kwa ajili ya bidhaa, kwa mujibu wa matakwa ya jedwali la saba la Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013.

Kutokuwapo kwa nyaraka za uhalali wa kutumia mzabuni mmoja au wachache badala ya ushindani kunaonesha udhaifu katika usimamizi wa ununuzi na uelewa wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma.

Ununuzi kwa kutumia mzabuni mmoja au wachache bila sababu za msingi na kugawanya ununuzi kunapunguza uwazi na haki sawa kwa wazabuni kushindana. Hii inahatarisha matumizi bora ya fedha za umma.

**Ninapendekeza kuwa OR-TAMISEMI iwajengee uwezo maofisa husika katika mamlaka za serikali za mitaa. Pia, mamlaka za serikali za mitaa husika zinahimizwa kuweka vipaumbele kwa njia za ununuzi shindanishi ili kuhakikisha kuwa mchakato wa ununuzi unakuwa wa haki, uwazi na ushindani, isipokuwa kama kuna haja ya kutumia mzabuni mmoja au wachache.**

### 5.1.9 Ujenzi wa miradi bila kufanya tathmini ya athari za mazingira - Sh. bilioni 22.18

Kanuni ya 241(3) ya kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 inazitaka taasisi zinazofanya ununuzi kufanya tathmini ya athari za kimazingira katika hatua ya maandalizi ya mradi kabla ya kuanza mchakato wa ununuzi. Aidha, Kifungu cha 81(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, [Sura ya 191], kinataka utafiti wa tathmini ya athari za mazingira ufanyike kabla ya kuanza au kufadhili mradi.

Nimepitia majalada ya miradi na kubaini kuwa, mamlaka nane za serikali za mitaa zilianza utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 21.05 bila kufanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza miradi hiyo, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.26.**

**Jedwali Na. 26: Ujenzi wa miradi bila tathmini ya athari za mazingira**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 1 | H/M Moshi | 6,592,504,416 |
| 2 | H/W Bunda | 3,650,000,000 |
| 3 | H/W Mwanga | 3,150,000,000 |
| 4 | H/Mji Kahama | 2,581,699,462 |
| 5 | H/W Sikonge | 2,069,097,548 |
| 6 | H/W Urambo | 1,223,600,000 |
| 7 | H/W Moshi | 1,000,000,000 |
| 8 | H/W Mkinga | 780,500,000 |
| | **Jumla** | **21,047,401,426** |

Aidha, halmashauri ya wilaya ya Kibaha imetumia Sh. bilioni 1.13 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika eneo lililowekwa kizuizi na baraza la taifa la usimamizi wa mazingira (NEMC) kutokana na kubainishwa kuwa ardhi oevu. Hii ni kinyume na Kifungu cha 81(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira,[Sura. 191], ambayo inahitaji utafiti

wa tathmini ya athari za mazingira ufanyike kabla ya kuanza au kufadhili mradi.

Kushindwa kufanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya utekelezaji wa miradi kulitokana na changamoto za kifedha na pia masuala ya kimazingira kutopewa kipaumbele na mamlaka za serikali za mitaa.

Kuanzisha miradi bila kufanya tathmini ya athari za mazingira kutasababisha taasisi nunuzi kuwajibika kwa adhabu na faini zinazotozwa na baraza la taifa la usimamizi wa mazingira. Vilevile, kunaweza kusababisha athari mbaya za kimazingira, ikiwamo upotevu wa viumbe hai, hewa, maji, uchafuzi wa udongo, athari za mabadiliko ya hali ya hewa, uharibifu wa mandhari ya asili, na kuvurugwa kwa mifumo ya ikolojia.

**Naishauri OR-TAMISEMI kuhakikisha kwamba mamlaka za serikali za mitaa zinafanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza mradi wowote wa ujenzi. Hatua hii ni muhimu ili kuhakikisha miradi inafanikiwa na kuzuia athari mbaya za kimazingira.**

### 5.1.10 Mikataba ambayo haikuhakikiwa na mwanasheria yenye thamani ya Sh. bilioni 14.75

Kanuni za 59(1) na (5), na 60 za Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na kanuni 2 na 3 za Kanuni za Ununuzi wa Umma (Marekebisho) za mwaka mwaka 2016 (Tangazo la serikali Na. 121 la tarehe 22.4.2016) zinamtaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakiki mikataba rasmi inayotokana na kukubalika kwa zabuni yenye thamani kuanzia Sh. bilioni moja na kuendelea, na kwa mikataba inayohusisha ushindanishi wa kimataifa.

Pia, maafisa sheria wa taasisi nunuzi wanatakiwa kuhakiki mikataba ambayo thamani yake iko chini ya sh. bilioni moja kabla haijasainiwa na wahusika. Aidha, maafisa masuuli, wanapaswa kuzingatia ushauri wa kisheria uliotolewa na mwanasheria mkuu na kuujumuisha katika rasimu za mikataba.

Vilevile, Kanuni za 59(1) ya kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na kanuni ya 2 ya kanuni za ununuzi wa umma (Marekebisho) za mwaka mwaka 2016 inaeleza kwamba mikataba ambayo haijahakikiwa na mwanasheria mkuu inachukuliwa kuwa batili.

Ukaguzi wangu wa usimamizi wa mikataba ulibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 14 zilisaini mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 9.95 kabla ya kuhakikiwa na maofisa wa sheria husika, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.27.**

**Jedwali Na. 27: Mikataba ambayo haikuhakikiwa na mwanasheria**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Ludewa | 4,975,180,028 | 9 | H/W Kongwa | 155,000,000 |
| 2 | H/Jiji Dar es Salaam | 2,041,283,561 | 10 | H/W Missenyi | 131,625,866 |
| 3 | H/W Biharamulo | 683,978,527 | 11 | H/W Ulanga | 128,664,941 |
| 4 | H/Mji Tunduma | 505,000,000 | 12 | H/W Mvomero | 100,065,000 |
| 5 | H/W Mlele | 458,423,820 | 13 | H/W Iramba | 62,478,000 |
| 6 | H/W Rufiji | 233,180,000 | 14 | H/W Mkinga | 56,750,000 |
| 7 | H/W Simanjiro | 211,313,200 | | **Jumla** | **9,950,217,443** |
| 8 | H/M Singida | 207,274,500 | | | |

Aidha, nilibaini mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 4.80 katika mamlaka tatu za serikali za mitaa ambapo maoni na ushauri uliotolewa na mwanasheria mkuu wa serikali na maofisa wa sheria haukuzingatiwa kabla ya kusaini mikataba hiyo, kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na.28.**

**Jedwali Na. 28: Mikataba isiyozingatia maoni ya wanasheria**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/Mji Kahama | 2,581,699,462 |
| 2 | H/W Kilindi | 2,024,000,000 |
| 3 | H/W Missenyi | 196,192,000 |
| | **Jumla** | **4,801,891,462** |

Kushindwa kuhakiki mikataba kunaashiria kutozingatiwa kwa taratibu za ununuzi zilizowekwa kisheria.

Ninaichukulia mikataba inayosainiwa kabla ya kuhakikiwa kama ilivyobainishwa katika Kanuni za 59 na 60 za Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa katika Kanuni ya 2 na 3 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Marekebisho) za mwaka 2016 (Tangazo la Serikali Na. 121 iliyochapishwa tarehe 22.4.2016), kuwa ni batili, na inaziweka halmashauri katika hatari za migogoro ya kimkataba au madai ambayo yanaweza kusababisha hasara.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI ichukue hatua stahiki ili kuhakikisha kuwa mamlaka za serikali za mitaa zinazingatia masharti ya kisheria ya ununuzi na kubuni taratibu za ufuatiliaji zitakazohakikisha kuwa**

**sheria za ununuzi zinafuatwa, ikiwamo kuzingatia maoni ya mwanasheria mkuu wa serikali katika mikataba kabla ya kusainiwa.**

### 5.1.11 Malipo yaliyofanyika kwa ununuzi wa bidhaa kabla ya kupokelewa na bidhaa ambazo hazijapokelewa Sh. bilioni 2.14

Kanuni ya 242 (1) na 248 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 zinataka malipo ya bidhaa na huduma kufanyika baada ya bidhaa kupokelewa, kukaguliwa na kukubaliwa. Aidha, hati ya kukubalika kwa bidhaa iliyosainiwa itolewe kwa mzabuni na nakala ya hati hiyo zitatumiwa na taasisi nunuzi kusaidia uchakataji wa malipo.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kwamba mamlaka 13 za serikali za mitaa zilifanya malipo yenye thamani ya Sh. bilioni 1.45 kwa ununuzi wa bidhaa ambazo hazikupokelewa. Sambamba na hilo, malipo ya Sh. milioni 472.56 yalifanywa na mamlaka zingine tano za serikali za mitaa kwa ununuzi wa bidhaa kabla ya kupokelewa na Halmashauri hizo.

Vilevile nimebaini katika mamlaka nne za serikali za mitaa ambapo bidhaa zilizolipiwa kiasi cha Sh. milioni 216.78 kuandikwa kwamba zimepokelewa lakini bidhaa hizo bado hazikuwa zimepokelewa. **Jedwali Na. 29** linaonesha kwa muhtasari juu ya malipo hayo.

**Jedwali Na. 29: Malipo yaliyofanyika kabla ya bidhaa kupokelewa**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Malipo ya bidhaa ambazo hazikupokelewa** | | | | | |
| 1 | H/ Mji Mbinga | 763,041,130 | 8 | H/W Babati | 42,900,000 |
| 2 | H/W Bunda | 132,111,340 | 9 | H/M Mtwara | 28,830,000 |
| 3 | H/W Handeni | 104,030,500 | 10 | H/W Shinyanga | 22,255,461 |
| 4 | H/W Butiama | 95,334,000 | 11 | H/W Sengerema | 11,926,000 |
| 5 | H/W Rorya | 87,241,000 | 12 | H/W Korogwe | 7,103,388 |
| 6 | H/W Magu | 83,230,879 | 13 | H/W Kiteto | 6,680,000 |
| 7 | H/Jiji Tanga | 65,563,500 | | **Total** | **1,450,247,198** |
| **Malipo ya bidhaa ambazo zililipwa kabla ya kupokelewa** | | | | | |
| 1 | H/W Kaliua | 302,633,398 | 4 | H/W Kishapu | 14,400,000 |
| 2 | H/Mji Tarime | 138,156,873 | | **Total** | **472,561,201** |
| 3 | H/W Mvomero | 17,370,930 | | | |
| Malipo ya bidhaa ambazo zimeandikwa kama zimepokelewa lakini bado kupokelewa | | | | | |
| 1 | H/W Kigoma | 104,679,820 | 4 | H/W Mlele | 8,600,000 |
| 2 | H/Mji Mbinga | 92,252,398 | | **Jumla** | **216,782,218** |
| 3 | H/W Mpanda | 11,250,000 | | **Jumla Kuu** | **2,139,590,617** |

Hali hii ilisababishwa na kutokuwapo usimamizi na utekelezwaji wa sheria za ununuzi kutokana na kushindwa kuzingatia taratibu za ununuzi za kuagiza, kupokea na malipo ya vifaa vilivyonunuliwa.

Ninaona kuwa, malipo kwa wazabuni kabla ya kupokea bidhaa yanaiweka taasisi nunuzi husika kwenye hatari ya upotevu wa fedha endapo wauzaji watashindwa kuleta bidhaa husika. Pia, ikiwa bidhaa zilizowasilishwa hazitimizi vigezo vya vipimo au kuwa na kasoro inakuwa na ugumu kwa mzabuni kurejesha fedha au kubadilisha bidhaa hizo.

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa zizingatie mahitaji ya ununuzi kama yalivyobainishwa katika sheria na kanuni. Aidha, zinapaswa kuzingatia taratibu za kifedha ambapo malipo yanapaswa kufanywa tu baada ya kupokea bidhaa kwa idadi na ubora unaostahili.**

### 5.1.12 Mapokezi ya vifaa vilivyonunuliwa vyenye thamani ya shiling bilioni 3.1 bila kukaguliwa

Kanuni ya 244(1) na 245 ya kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 inataka taasisi inayofanya ununuzi kukagua bidhaa zinazoletwa na wazabuni na kuzikubali iwapo tu zinakidhi masharti ya mkataba.

Kinyume na Kanuni hiyo, nilibaini mamlaka 21 za serikali za mitaa zilipokea vifaa vyenye thamani ya Sh. bilioni 3.1 kwa wazabuni bila kukaguliwa na kamati zilizoteuliwa, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.30.**

**Jedwali Na. 30: Mapokezi ya vifaa/bidhaa bila ukaguzi**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Bunda | 692,663,776 | 13 | H/W Mpanda | 49,880,250 |
| 2 | H/W Butiama | 616,760,984 | 14 | H/W Namtumbo | 48,100,772 |
| 3 | H/W Mbozi | 331,421,831 | 15 | H/W Madaba | 47,248,540 |
| 4 | H/W Bumbuli | 235,427,457 | 16 | H/W Tarime | 43,449,900 |
| 5 | H/Jiji Tanga | 221,080,100 | 17 | H/M Temeke | 42,914,023 |
| 6 | H/Mji Tarime | 149,940,000 | 18 | H/W Mpimbwe | 34,395,229 |
| 7 | H/W Nyang'hwale | 109,443,950 | 19 | H/W Kishapu | 31,743,178 |
| 8 | H/W Singida | 100,695,345 | 20 | H/W Lushoto | 25,088,835 |
| 9 | H/W Songea | 84,550,836 | 21 | H/W Malinyi | 24,600,000 |
| 10 | H/W Mafia | 76,636,191 | | | |
| 11 | H/W Misungwi | 66,025,733 | | **Jumla** | **3,096,275,370** |
| 12 | H/W Kakonko | 64,208,440 | | | |

Hali hii ilisababishwa na upungufu katika usimamizi na uwajibikaji wakati wa kupokea bidhaa zilizonunuliwa, kwani kamati zilizoteuliwa zilishindwa kukagua bidhaa kulingana na barua zao za uteuzi.

Kufanya malipo na mapokezi ya bidhaa na huduma bila kukaguliwa na kamati husika kunaweza kuhatarisha ubora na ulinganifu wa vipimo, na inaweza kusababisha upatikanaji wa bidhaa duni au zisizo na ubora.

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa zizingatie kanuni za Ununuzi kwa kukagua ubora na wingi wa bidhaa na huduma zilizonunuliwa kabla ya kupokea na kufanya malipo kwa wazabuni.**

### 5.1.13 Matumizi ya vifaa vya ujenzi bila kufanyiwa vipimo vya ubora - Sh. bilioni 1.52

Kanuni ya 244(1) ya Kanuni za Ununuzi wa umma (2013) inasema, bidhaa zitakazowasilishwa zinahitajika kukaguliwa, zichukuliwe sampuli na kupimwa na taasisi inayofanya ununuzi; na hazitokubalika kama zitakuwa chini ya viwango vilivyobainishwa kwenye mkataba.

Pia, Kanuni ya 246 inasema kuwa, ikiwa bidhaa itahitaji jaribio la kiufundi au la kisayansi, mtaalamu au mjuzi wa taaluma husika ataalikwa kwa mashauriano, au bidhaa zaweza kutumwa kwa mjuzi huyo kwa ajili ya kufanyiwa vipimo.

Nilibaini mamlaka 16 za serikali za mitaa zilinunua na kutumia vifaa vya ujenzi, zikiwamo nondo na matofali, vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.52 katika miradi ya ujenzi bila kufanyiwa vipimo vya ubora kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.31.**

**Jedwali Na. 31: Vifaa vya ujenzi ambavyo havikupimwa ubora wake**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Ushetu | 301,143,803 | 10 | H/Mji Bunda | 79,855,000 |
| 2 | H/M Shinyanga | 231,763,422 | 11 | H/Mji Tarime | 60,728,700 |
| 3 | H/W Nyasa | 217,341,986 | 12 | H/W Shinyanga | 53,518,000 |
| 4 | H/M Temeke | 155,839,175 | 13 | H/W Namtumbo | 51,679,021 |
| 5 | H/Jiji Mwanza | 151,365,713 | 14 | H/W Ukerewe | 48,434,580 |
| 6 | H/Mji Mbinga | 145,863,192 | 15 | H/W Rombo | 41,690,180 |
| 7 | H/W Rorya | 89,094,632 | 16 | H/W Bumbuli | 25,284,000 |
| 8 | H/W Songea | 84,079,656 | | **Jumla** | **1,515,897,230** |
| 9 | H/W Mbozi | 84,066,170 | | | |

Kutofanyika kwa majaribio kwenye vifaa vya ujenzi kunaweza kuziweka mamlaka za serikali za mitaa katika hatari ya kutumia vifaa duni ambavyo vinaweza kuathiri ubora wa miradi inayotekelezwa.

**Ninaishauri OR-TAMISEMI kuzingatia sheria na kanuni za ununuzi. Pia, maafisa masuuli wa mamlaka za serikali za mitaa, wanatakiwa**

**kuzingatia matakwa ya sheria katika miradi ya ujenzi ikiwamo kufanya majaribio ya vifaa vya ujenzi ili kupata uhakikisho wa ubora.**

### 5.1.14 Kutotumika kwa nyaraka za zabuni zilizoidhinishwa - Sh. bilioni 1.69

Kifungu cha 70(1) cha Sheria ya ununuzi wa Umma,[Sura ya 410], kinaelekeza taasisi nunuzi kutumia nyaraka za zabuni zilizobainishwa katika kanuni za ununuzi husika.

Vilevile, kanuni ya 184(3) ya kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 inataka taasisi nunuzi kutumia nyaraka za zabuni zinazotolewa na mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma, kushughulikia masuala mahususi ya mradi kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma.

Nilipitia mchakato wa ununuzi na kubaini kuwa, mamlaka saba za serikali za mitaa hazikutumia nyaraka za zabuni zilizotolewa na mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma ili kupata wazabuni wenye sifa kwa ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 1.69 kinyume na kanuni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.32.**

**Jedwali Na. 32: Halmashauri zenye nyaraka za zabuni zisizoidhinishwa**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 1 | H/W Nkasi | 736,625,295 |
| 2 | H/W Ileje | 196,626,645 |
| 3 | H/W Kalambo | 182,101,346 |
| 4 | H/W Bariadi | 183,792,200 |
| 5 | H/W Kilolo | 173,893,348 |
| 6 | H/W Bumbuli | 118,110,100 |
| 7 | H/W Mbozi | 103,939,360 |
| | **Jumla** | **1,695,088,294** |

Hali hii imesababishwa na kutokuwa na dhamira ya dhati ya kuzingatia taratibu za ununuzi wa umma kuhusu matumizi ya nyaraka za zabuni na mikataba zilizotolewa na mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma.

Kutumia nyaraka za zabuni na mikataba isiyoidhinishwa huruhusu kuachwa kwa masharti muhimu kwa usimamizi wa kazi za miradi.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI ihakikishe Halmashauri zote zinatumia nyaraka za kawaida za zabuni zinazotolewa na mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma kwa ajili ya ununuzi wa kazi, huduma za ushauri na huduma zisizo za ushauri.**

## 5.2 Usimamizi wa mikataba

Lengo la ukaguzi wa usimamizi wa mikataba lilikuwa kutathmini ufanisi wa mifumo inayotumika kusimamia kandarasi katika miradi mingi inayofanywa na mamlaka za serikali za mitaa. Tathmini hii ililenga kubainisha uzingatiaji wa kanuni na majukumu ya kimkataba, matumizi ya kanuni za jumla za usimamizi wa mradi, na kutathmini ufanisi wa jumla wa michakato ya usimamizi wa mkataba.

### 5.2.1 Malipo kwa kazi ambazo hazijapimwa au hazijatekelezwa - Sh. bilioni 2.95

Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inataka taasisi inayofanya ununuzi kuidhinisha malipo kulingana na vipimo na uthibitisho, katika vipindi au hatua zilizooneshwa katika mikataba; na kwamba, asilimia kadhaa ya thamani ya kazi zilizotekelezwa kutoka kila cheti cha malipo inaweza kukatwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya matazamio endapo mkataba utaweka takwa hilo.

Ukaguzi wangu wa vyeti vya malipo ulibaini mamlaka 10 za serikali za mitaa, zililipa kiasi cha Sh. bilioni 2.95 kwa kazi za ujenzi zilizotekelezwa na wakandarasi na mafundi bila kuwapo na nyaraka za vipimo vya kazi zilizofanyika, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.33**.

**Jedwali Na. 33: Malipo kwa kazi ambazo hazijapimwa/hazijatekelezwa**

| S/N | Name of LGA | Amount (TZS) | S/N | Name of LGA | Amount (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Sumbawanga | 1,485,723,050 | 7 | H/W Bariadi | 21,310,500 |
| 2 | H/Jiji Dar es Salaam | 521,896,552 | 8 | H/W Kilindi | 18,549,300 |
| 3 | H/W Njombe | 521,003,248 | 9 | H/W Kilosa | 12,787,000 |
| 4 | H/M Kinondoni | 290,723,068 | 10 | H/W Manyoni | 9,138,040 |
| 5 | H/W Mkalama | 38,732,500 | | **Total** | **2,946,593,258** |
| 6 | H/W Ludewa | 26,730,000 | | | |

Aidha, mapitio yangu ya hati za malipo yalibaini malipo kwa wakandarasi kwa kazi ambazo hazikutekelezwa katika mamlaka nne za serikali za mitaa zenye thamani ya Sh. milioni 346.69. Hii ni kinyume na kifungu cha 14.3 cha GCC kinachomtaka mkandarasi kuwasilisha taarifa kwa meneja wa mradi kila mwisho wa mwezi ikionesha kwa kina kiasi ambacho anastahili kulipwa.

Taarifa hiyo itajumuisha makadirio ya thamani ya mkataba wa kazi zilizotekelezwa na kiasi ambacho mkandarasi anastahili kulipwa. Halmashuri zilizolipa kazi ambazo hazijafanyika zimeoneshwa katika **Jedwali Na.34.**

**Jedwali Na. 34: Malipo kwa kazi ambazo hazijatekelezwa**

| S/N | Name of LGA | Amount (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Kiteto | 300,982,670 |
| 2 | H/W Mbulu | 19,507,000 |
| 3 | H/W Sumbawanga | 19,100,000 |
| 4 | H/W Tarime | 7,100,000 |
| | **Total** | **346,689,670** |

Malipo yanayofanywa kwa kazi ambazo hazijapimwa na kuthibitishwa na wasimamizi wa mradi na kazi ambazo hazijatekelezwa yanachangiwa na usimamizi usioridhisha wa mikataba.

Kutokuwapo kwa ushahidi wa upimaji wa kazi kunakwamisha uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa malipo, hivyo kuwa vigumu kufuatilia na kuhakiki malipo kwa usahihi. Pia, huibua wasiwasi kuhusu ufanisi wa usimamizi na udhibiti wa miradi.

**Ninaishauri OR-TAMISEMI iimarishe udhibiti wa usimamizi ili kuhakikisha kuwa taratibu zilizowekwa zinatumika ipasavyo katika mchakato wa ununuzi, hasara zisizo za lazima zinaepukika, na fedha zinazotumika kufikia thamani ya fedha. Kadhalika, mamlaka za serikali za mitaa zinashauriwa kuzingatia ipasavyo taratibu za ununuzi kwenye miradi ili kuepusha kuongezeka kwa gharama za miradi na ucheleweshaji.**

### 5.2.2 Mikataba iliyotekelezwa bila dhamana ya kazi - Sh. bilioni 9.91

Kanuni ya 29 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inahitaji taasisi nunuzi kutaka dhamana ya utendaji kutoka kwa mzabuni aliyeshinda zabuni ili kuhakikisha utendaji wa mkataba wenye uaminifu na malipo ya wafanyakazi wote, wasambazaji, mafundi na wakandarasi wasaidizi wa mradi, kama wapo.

Pia, aya ya 4.2.3 ya masharti ya jumla ya mkataba inamtaka mkandarasi kuhakikisha kuwa dhamana ya utendaji ni halali na hai hadi mkandarasi atakapokuwa ametekeleza kazi na kukamilisha marekebisho ya kasoro zozote zitakazojitokeza katika mradi.

Nilibaini halmashauri ya wilaya ya Mafia ilitekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la utawala lenye thamani ya Sh. bilioni 5.54 bila kudai dhamana ya utendaji kazi kutoka kwa mkandarasi kama inavyotakiwa na kanuni za ununuzi wa umma.

Vilevile, nilipitia majalada ya miradi na kubaini kuwa mamlaka mbili za serikali za mitaa zilitekeleza mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 4.37 bila kuhuisha dhamana za utendaji zilizoisha muda wake kwa siku 58 hadi siku 2022, kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na.35.**

**Jedwali Na. 35: Upungufu katika uandaaji wa sanifu za miradi**

| Na | Jina la Halmashauri | Thamani ya Mkataba (Sh) | Idadi ya siku ambazo kazi ilifanyika bila dhamana |
|---|---|---|---|
| **Mikataba iliyofanyika bila kuwa na dhamana ya utendaji-kazi** | | | |
| 1 | H/W Mafia | 5,539,233,443 | |
| **Dhamana za utendaji zilizoisha muda wake** | | | |
| 1 | H/W Mpanda | 3,606,981,750 | 2022 |
| 2 | H/W Sumbawanga | 767,280,407 | 58 |
| **Jumla** | | **4,374,262,157** | |
| **Jumla Kuu** | | **9,913,495,600** | |

Aidha, nilipitia mkataba wenye thamani ya Sh. billion 4.52 kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa jengo la utawala la halmashauri ya wilaya ya Ushetu na kubaini kuwa mkandarasi alileta dhamana ndogo ya utendani kuliko ilivyotakiwa kwa pungufu ya Sh. milioni 210.95.

Utofauti huo ni kinyume na Aya ya 50.1 ya masharti maalumu ya mkataba, ambayo inamtaka mkandarasi kutoa dhamana ya utendaji-kazi yenye thamani ya Sh. milioni 452.5, sawa na 10% ya thamani ya mkataba. Hata hivyo, mkandarasi aliwasilisha dhamana ya utendaji kazi yenye thamani ya Sh. milioni 241.55 badala ya kiasi kilichohitajika; hivyo Kusababisha dhamana kuwa pungufu ya Sh. milioni 210.95.

Kutokuwapo kwa dhamana ya utendaji kazi kunaziweka mamlaka za serikali za mitaa husika kwenye hatari ya kupoteza rasilimali zao endapo wakandarasi watashindwa kutekeleza mikataba kikamilifu kulingana na masharti ya mikataba husika.

**Nazishauri mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kuwa hatari za kushindwa kufanya kazi vizuri zinashughulikiwa vyema kwa kuwa na dhamana halali na zilizohuishwa ili kuboresha utekelezaji wa miradi.**

### 5.2.3 Upungufu kwenye sanifu za miradi uliosababisha mabadiliko yasiyo ya lazima - Sh. bilioni 2.26

Kanuni ya 321(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inamtaka mtaalamu mshauri kutekeleza kazi kwa umakini na kwa kuzingatia viwango vilivyopo.

Pia, Kanuni Na. 239(8) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inaelekeza taasisi nunuzi kutokutangaza zabuni za kazi, isipokuwa kama michoro na maelezo kamili yamekamilika na makadirio ya gharama yameandaliwa.

Nilipitia mafaili ya miradi na kubaini mapungufu katika sanifu za miradi na utayarishaji wa nyaraka za awali za miradi kama vile michoro na makisio ambavyo vilisababisha mabadiliko ya kazi zenye thamani ya Sh. bilioni 2.26 katika mamlaka sita za serikali za mitaa kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na.36.**

**Jedwali Na. 36: Upungufu katika usanifu za miradi**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Msanifu |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Mwanza | 1,707,593,498 | Idara ya ujenzi ya Halmashauri |
| 2 | H/W Ushetu | 309,447,260 | Wakala wa ujenzi Tanzania(TBA) |
| 3 | H/M Iringa | 193,560,944 | Idara ya ujenzi ya Halmashauri |
| 4 | H/Jiji Tanga | 22,444,910 | Idara ya ujenzi ya Halmashauri |
| 5 | H/W Bumbuli | 17,423,795 | Idara ya ujenzi ya Halmashauri |
| 6 | H/W Njombe | 12,042,000 | Idara ya ujenzi ya Halmashauri |
| | **Jumla** | **2,262,512,407** | |

Maoni yangu ni kwamba, mchakato wa mapitio ya michoro na makisio ya miradi haukufanywa na mkandarasi na mamalaka za serikali za mitaa kabla ya utekelezaji wa kazi na kwamba kuongezeka kwa gharama za miradi kuliathiri utekelezaji wa shughuli zingine za maendeleo zilizopangwa.

**Ninapendekeza kwamba OR-TAMISEMI ifanye mapitio ya mara kwa mara ya tathmini ya miradi na vihatarishi wakati wa utekelezaji wa miradi ili kubaini na kuziwezesha mamlaka za serikali za mitaa kuwa na uwezo wa kutosha katika kusanifu na kutekeleza miradi kulingana na matakwa ya sheria ya manunuzi na kanuni zake.**

### 5.2.4 Ucheleweshwaji wa Malipo kwa Kazi zilizofanyika yenye thamani ya Sh. bilioni 2.22

Kanuni ya 44(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inasema kuwa, kwa madhumuni ya kusaidia ukuaji wa makampuni ya ndani na kuwezesha makampuni hayo kutimiza majukumu yao ya kimkataba, taasisi nunuzi zitahakikisha kwamba malipo yanafanyika kwa wazabuni kwa wakati.

Pia, masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) yanawataka waajiri kuwalipa wakandarasi kiasi kilichoidhinishwa na wasimamizi wa miradi ndani ya siku 28 kuanzia tarehe ya kuwasilishwa cheti cha madai ya malipo ya mkandarasi.

Nilipitia uzingatiwaji wa sheria na masharti yaliyobainishwa kwenye mikataba na kubaini kuwa, mamlaka saba za serikali za mitaa zina madai ya wakandarasi kiasi cha shiling bilioni 2.22 ambayo hayajalipwa kwa muda wa kati ya siku 55 hadi 270 tangu tarehe ya kuthibitishwa kwa madai hayo. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali Na.37.**

**Jedwali Na. 37: Kucheleweshwa kwa malipo ya Wakandarasi**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Idadi ya Siku za Ucheleweshaji |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Tarime | 683,917,649 | 71 |
| 2 | H/W Mtama | 499,116,430 | 110 |
| 3 | H/W Mlele | 355,630,974 | 180 |
| 4 | H/W Kalambo | 284,319,433 | 261 |
| 5 | H/Jiji Dar es Salaam | 201,396,936 | 55 |
| 6 | H/W Mpanda | 160,475,725 | 180 |
| 7 | H/W Rufiji | 38,364,875 | 270 |
| | **Jumla** | **2,223,222,022** | |

Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi unatokana na ucheleweshaji wa fedha kutoka hazina kwenda mamlaka za serikali za mitaa.

Ucheleweshaji uliobainika sio tu kwamba unaziweka mamlaka za serikali za mitaa katika hatari ya gharama za ziada kwenye miradi husika kupitia riba ya ucheleweshaji, bali pia huathiri kwa kiasi kikubwa mzunguko wa fedha wa wakandarasi ambao unaathiri kukamilika kwa miradi kwa wakati.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha wahakikishe fedha za miradi ya ujenzi zinatolewa kwa wakati. Hii**

**itarahisisha utekelezaji mzuri wa miradi hiyo na kuepusha riba na adhabu zisizo za lazima.**

### 5.2.5 Mabadiliko ya kazi yaliyofanyika bila kuidhinishwa yenye thamani ya Sh. bilioni 2.03

Kanuni ya 110(7) ya Kanuni za ununuzi wa Umma za mwaka 2013, iliyorekebishwa na kanuni ya 36 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (zilizorekebishwa) za mwaka mwaka 2016 (Tangazo la Serikali Na. 333 la tarehe 30.12.2016.) inaelekeza kuwa mabadiliko yaliyopendekezwa kupelekwa kwenye bodi ya zabuni kwa ajili ya kuidhinishwa.

Nilipitia majalada ya miradi na kubaini kuwa, mamlaka tisa za serikali za mitaa zilifanya mabadiliko ya kazi na kubadili bei zao za awali za mikataba bila kupata kibali kutoka kwa bodi za zabuni husika kiasi cha Sh. bilion 2.03 kama inavyofafanuliwa kwenye **Jedwali Na. 38.**

**Jedwali Na. 38: Mabadiliko ya kazi yaliyofanyika bila kibali**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/M Shinyanga | 807,350,000 | 6 | H/Jiji Dar es Salaam | 83,823,300 |
| 2 | H/W Biharamulo | 683,978,527 | 7 | H/W Sengerema | 79,966,000 |
| 3 | H/W Simanjiro | 114,168,500 | 8 | H/W Msalala | 49,315,506 |
| 4 | H/M Iringa | 111,283,500 | 9 | H/W Bunda | 6,240,000 |
| 5 | H/W Magu | 95,427,072 | | **Jumla** | **2,031,552,405** |

Mabadiliko yaliyofanywa baada ya kusaini mikataba bila idhini ya bodi za zabuni yanaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Napendekeza OR-TAMISEMI ihakikishe mamlaka za serikali za mitaa zinawasilisha mabadiliko ya kazi kwenye vikao kwa ajili ya kuidhinishwa na bodi ya zabuni kwa kuzingatia Kanuni ya 110(7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013, kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 36 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2016 (Tangazo la Serikali Na. 333 la tarehe 30.12.2016).**

### 5.2.6 Madai ya riba yaliyolimbikizwa kwa kuchelewesha malipo - Sh. bilioni 2.23

Kifungu cha 45.1 cha masharti ya jumla ya mkataba (GCC) kinamtaka mwajiri kumlipa mkandarasi kiasi kilichoidhinishwa na msimamizi wa mradi ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kila cheti. Ikiwa mwajiri atafanya malipo kwa kuchelewa, mkandarasi atalipwa riba ambayo itahesabiwa kuanzia tarehe ambayo malipo yalipaswa kufanywa hadi tarehe ya malipo kwa kutumia kiwango cha riba inayoendana na mkopo wa kibiashara kwa kila malipo.

Kuvunjwa kwa halmashauri ya jiji la Dar es Salaam, tarehe 24 Februari 2021, kulisababisha mkataba wa ujenzi wa kituo cha mabasi kilichopo Mbezi Luis ambao ulijumuisha mkataba wa ujenzi wenye thamani ya Sh. bilioni 50.95 pamoja na makubaliano ya mshauri wa mradi yenye thamani ya Sh. bilioni 1.58 kuhamishiwa halmashauri ya manispaa ya Ubungo.

Nilipitia mchakato wa usimamizi wa mikataba katika halmashauri ya manispaa ya Ubungo na kubaini kuwa jumla ya madai ya Sh. bilioni 8.92 yaliyowasilishwa na mkandarasi wa mradi pamoja na mkandarasi mshauri hayakulipwa na kusababisha riba iliyotokana na madai hayo kufikia Sh. bilioni 2.23 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.39.**

**Jedwali Na. 39: Malimbikizo ya riba kwa kuchelewesha malipo**

| Na | Namba ya Mkataba | Madai (Sh.) | Riba (Sh.) | Jumla ya deni na riba (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | LGA/018/2017/ 2018/W/10 | 6,721,159,349 | 1,907,889,705 | 8,629,049,054 |
| 2 | LGA/180/2021/ 2022/CS/06 | 2,194,232,099 | 322,087,750 | 2,516,319,849 |
| | **Jumla** | **8,915,391,448** | **2,229,977,455** | **11,145,368,903** |

Ucheleweshaji wa utoaji wa fedha za mradi kutoka hazina ulisababisha kuchelewa kwa malipo ya vyeti vya mkandarasi na mkandarasi mshauri.

Halmashauri inakabiliwa na hatari ya kutumia zaidi ya Sh. bilioni 2.23 kulipa riba zisizo za lazima kwa wakandarasi, hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma.

**Ninaishauri halmashauri ya manispaa ya Ubungo iwasiliane na OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha ili kulipia hati za wakandarasi ambao hawajalipwa ili kuzuia ulimbikizaji zaidi wa tozo za riba, hivyo kulinda fedha za umma; na kufanya majadiliano na wakandarasi ili kuondoa malipo ya riba, kwa lengo la kuokoa fedha za umma.**

### 5.2.7 Malipo ya awali ambayo hayajarejeshwa - Sh. milioni 531.24

Aya ya 23.1 ya masharti ya jumla ya mkataba kinabainisha kuwa "Mwajiri atatoa malipo ya awali kwa mkandarasi hadi 20% ya thamani ya mkataba baada ya kuwasilishwa na mkandarasi wa dhamana ya utendaji ya kiasi sawa”.

Ukaguzi wangu wa usimamizi wa mikataba ulibaini kwamba halmashauri ya wilaya ya Karagwe iliingia mkataba kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari ya Mto Kagera kwa mkataba wa Sh. bilioni 2.8 na kutoa malipo ya awali yenye thamani ya Sh. milioni 600 kwa Mkandarasi. Hata hivyo,

mkataba huo ulisitishwa 10 Januari 2023 ikiwa kiasi cha Sh. milioni 68.76 tu za malipo ya awali zilirejeshwa na kiasi cha Sh. milioni 531.24 kikiwa bado hakijarejeshwa.

Usimamizi usioridhisha wa mikataba na ufuatiliaji usio mzuri kutoka kwa wadhamini ulisababisha kutorejeshwa kwa malipo ya awali.

Kutorejeshwa kwa malipo ya awali ya Sh. milioni 531.24 kunaathiri utekelezaji wa shughuli za miradi iliyokusudiwa na kuchukuliwa kuwa ni upotevu wa fedha wa umma.

**Ninapendekeza halmashauri ya wilaya ya Karagwe kufanya jitihada za kurejesha malipo ya awali kutoka kwa wadhamini ili kuepuka upotevu wa fedha. Pia, katika siku zijazo, kuwe na hali ya uzingativu wa masharti ya mikataba, ikiwamo dhamana za uhakika za malipo ya awali kutoka benki zinazotambulika badala ya dhamana ya utendaji tu.**

## 5.3 Tathmini ya ununuzi uliofanywa kupitia matumizi ya rasilimali za ndani

Kwa mujibu wa kifungu cha 64 (6) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, [Sura ya 410], matumizi ya rasilimali za ndani (*Force account*) humaanisha mchakato wa kazi ambao unafanywa na idara au wakala wa umma kwa kutumia wafanyakazi wake na vifaa au kwa ushirikiano na umma wowote au chombo binafsi.

Masharti yanayoweza kuhalalisha matumizi ya rasilimali za ndani na taasisi nunuzi yameorodheshwa chini ya kifungu cha 64(5) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, [Sura ya 410] na Kanuni ya 167 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 64 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (marekebisho) ya mwaka 2016 (Tangazo la Serikali Na. 333 la 31/12/2021).

Masharti hayo ni pamoja na: kazi ziwe ndogo; zilizotawanyika; ziko katika maeneo ya mbali ambako haiwezekani kwa kampuni za ujenzi zenye sifa kutoa zabuni kwa bei nzuri; kazi inatakiwa ifanyike bila kukwamisha shughuli zinazoendelea; kuna dharura inayohitaji uangalizi wa haraka; kuwapo kwa hatari za kukatishwa kazi zinazoweza kuepukika, hivyo ni bora kubebwa na taasisi nunuzi au mamlaka ya umma kuliko mkandarasi; taasisi nunuzi ina wafanyakazi wenye sifa zinazotambuliwa na vyombo husika vya kitaaluma kutekeleza na kusimamia kazi zinazohitajika; au matengenezo au ujenzi ni sehemu ya shughuli za kawaida za taasisi nunuzi.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini maeneo kadhaa ambayo taasisi zilizokaguliwa hazikuzingatia taratibu za matumizi ya rasilimali za ndani (*Force account*) zilizowekwa.

### 5.3.1 Kutekeleza miradi kwa njia ya matumizi ya rasilimali za ndani bila kukasimu majukumu ya afisa masuuli - Sh. bilioni 2.03

Aya ya 30 (2) ya mwongozo wa kufanya kazi kwa njia ya matumizi ya rasilimali za ndani na taasisi nunuzi nchini Tanzania kinasema "Afisa masuuli atakasimu kazi za ununuzi za afisa masuuli kwa mtumishi wa ngazi za chini za serikali kwa miradi yote ya ujenzi inayofanywa kwa njia ya kwa njia ya matumizi ya rasilimali za ndani ambapo ununuzi unofanyika unatokana na fedha za umma zilizopokelewa moja kwa moja kutoka serikalini".

Mapitio yangu ya majalada ya miradi yalibaini kuwa mamlaka tatu za serikali za mitaa zilitekeleza miradi kwa kutumia njia ya ununuzi wa matumizi ya rasilimali za ndani (*Force account*) yenye thamani ya Sh. bilioni 2.03 bila maafisa masuuli kukasimu majukumu ya ununuzi kwa mtumishi wa ngazi za chini za serikali, katika kutekeleza miradi hiyo kwa niaba yake. Taasisi husika zimeoneshwa kwenye **Jedwali Na.40**.

**Jedwali Na. 40: Miradi iliyotekelezwa pasipo kukasimu majukumu ya afisa masuuli**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/M Kahama | 977,000,000 |
| 2 | H/W Liwale | 955,000,000 |
| 3 | H/W Tarime | 100,000,000 |
| | **Jumla** | **2,032,000,000** |

Uelewa mdogo wa maofisa wa ununuzi na kushindwa kwa maafisa ununuzi kumshauri afisa masuuli kuhusu mahitaji ya miongozo ya matumizi ya rasilimali za ndani kulisababisha kutofuatwa kwa mwongozo huo.

Maoni yangu ni kwamba kutofuata mwongozo wa ununuzi kwa njia ya matumizi ya rasilimali za ndani kunaweza kusababisha mgongano wa maslahi, ambapo malengo ya mradi yanaweza yasifikiwe.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI ihakikishe kuwa mamlaka za serikali za mitaa zinazotekeleza miradi ya ujenzi kwa kutumia njia ya matumizi ya rasilimali za ndani (*force account*), zinazingatia kikamilifu miongozo inayotolewa na mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma.**

### 5.3.2 Vifaa vya ujenzi ambavyo havijatumika - Sh. milioni 868.43

Aya ya 13 (5) ya Mwongozo wa Kufanya Kazi kwa Kutumia ya rasilimali za ndani (*Force Account*) kwa Taasisi zinazofanya ununuzi nchini Tanzania inataka utaratibu wa ununuzi wa vifaa vitakavyotumika katika utekelezaji wa kazi vinunuliwe ndani ya uwezo unaoweza kudhibitiwa na taasisi husika.

Katika mapitio yangu ya taarifa za utekelezaji wa miradi na kutembelea maeneo ya utekelezaji wa miradi, nilibaini mamlaka za serikali za mitaa 11 zilinunua vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 868.43, zaidi ya mahitaji ya miradi husika kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.41.**

**Jedwali Na. 41: Vifaa vya ujenzi ambavyo havijatumika**

| S/N | Name of LGA | Amount (TZS) | S/N | Name of LGA | Amount (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Tanga | 424,362,740 | 6 | H/W Liwale | 30,044,520 |
| 2 | H/W Shinyanga | 244,477,211 | 7 | H/W Bunda | 23,444,050 |
| 3 | H/Mji Ifakara | 42,592,000 | 8 | H/W Morogoro | 21,906,885 |
| 4 | H/W Kilwa | 37,261,490 | 9 | H/W Serengeti | 10,164,500 |
| 5 | H/Mji Bunda | 34,178,100 | | **Total** | **868,431,496** |

Hali hii inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma zilizowekwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Maoni yangu ni kwamba ununuzi wa vifaa kwa kuzidi kiasi kinachohitajika ina maana kwamba kiasi cha fedha kilichotumika kingeweza kutumika kugharamia hatua zinazofuata za miradi au kugharamia miradi mingine katika mamlaka za serikali za mitaa.

**Ninapendekeza kwamba mamlaka za serikali za mitaa ziwe na makadirio ya kuridhisha na yanayokubalika ambayo yamehusisha wasanifu majengo, wahandisi na wakadiriaji majengo katika mchakato wa makadirio. Pia, wanapaswa kuhakikisha kuwa vifaa ambavyo havijatumika vinatumika katika kutekeleza miradi mingine au kuuzwa ili kupata thamani ya fedha.**

### 5.3.3 Ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambao haukufanywa kutoka viwandani au kwa mawakala wa viwanda walioidhinishwa Sh. milioni 854.77

Aya ya 13 (1) ya mwongozo wa kufanya kazi kwa njia ya matumizi ya rasilimali za ndani ya taasisi zinazofanya ununuzi nchini Tanzania inasema "Kwa madhumuni ya kupata thamani ya fedha, wakati wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi, upendeleo utatolewa katika ununuzi wa vifaa moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji au wakala walioidhinishwa."

Nilifanya mapitio ya mchakato wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi vinavyotumika katika miradi iliyotekelezwa kwa njia ya matumizi ya rasilimali za ndani na kubaini kuwa mamlaka sita za serikali za mitaa zilinunua vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 854.77 bila kutoa upendeleo kwa wazalishaji au wakala walioidhinishwa, kinyume na matakwa ya mwongozo, kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na.42.**

**Jedwali Na. 42: Vifaa vya ujenzi ambavyo havikununuliwa viwandani**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Chunya | 213,131,870 |
| 2 | H/Mji Bunda | 205,373,240 |
| 3 | H/Mji Nanyamba | 184,511,924 |
| 4 | H/W Liwale | 114,950,980 |
| 5 | H/W Rorya | 106,620,200 |
| 6 | H/M Mtwara/Mikindani | 30,185,000 |
| | **Jumla** | **854,773,214** |

Aidha, barua yenye Na. AB.39/156/01/"B"/44 ya tarehe 20 Januari 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu TAMISEMI inazitaka mamlaka za serikali za mitaa kabla ya kununua bati kujiridhisha kuwa bati ni za geji "28", zinazofikia kiwango cha shirika la viwango cha Sh.1477:2020/EAS 468:2019(E) na kupata hati ya waranti isiyopungua miaka mitano.

Kinyume chake, nilibaini mamlaka tatu za serikali za mitaa zilinunua bati za thamani ya Sh. milioni 166.88 kwa wazabuni bila ushahidi kwamba bati hizo zilikidhi viwango vya Sh.1477:2020/EAS 468:2019(E) na bila kuwa na hati za waranti ya miaka mitano. Mchanganuo wa hoja hii umeoneshwa kwenye **Jedwali Na.43.**

**Jedwali Na. 43: Mabati yaliyonunuliwa bila ushahidi viwango vya ubora**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Lushoto | 94,778,941 |
| 2 | H/W Bumbuli | 38,070,000 |
| 3 | H/Jiji Tanga | 34,027,669 |
| | **Jumla** | **166,876,610** |

Kwa maoni yangu, mamlaka za serikali za mitaa zinaweza kuwa zilitumia gharama kubwa za ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa kununua kwa bei za rejareja, jambo ambalo linaweza kusababisha gharama za ziada zisizo za lazima kwenye miradi. Pia, mabati yaliyonunuliwa bila ushahidi wa kukidhi viwango vya shirika la viwango yanatia shaka iwapo yatadumu kwa muda ndefu.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI ihakikishe kuwa mamlaka za serikali za mitaa zinafuata miongozo ya ununuzi wa umma ili kufikia thamani ya fedha katika matumizi ya fedha za umma; pia ubora na viwango vya vifaa vya ujenzi vizingatiwe.**

## 5.4 Tathmini ya ununuzi katika ngazi za chini za serikali

Kwa mujibu wa Aya ya 29.1 ya mwongozo wa Kufanya Kazi njia ya matumizi ya rasilimali za ndani kwa taasisi zinazonunua Tanzania, ngazi za chini za serikali zinamaanisha shule, vituo vya afya na taasisi zinazofanana na hizo zinazopokea fedha moja kwa moja kutoka serikalini kwa ajili ya kufanya kazi na shughuli zinazohusiana.

Kwa kuzingatia kuongezeka kwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika ngazi za chini za serikali, niliamua kufanya tathmini ya michakato na taratibu zinazotumika katika ununuzi.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini matukio kadhaa ambapo taasisi zilizokaguliwa zilishindwa kuzingatia taratibu za ununuzi kwa kutumia njia ya matumizi ya rasilimali za ndani zilizowekwa katika ngazi za chini kama ifuatavyo:

### 5.4.1 Kutojumuishwa kwa ununuzi wa ngazi ya chini katika ripoti ya ununuzi wa robo mwaka - Sh. bilioni 15.39

Kifungu cha 38 (o) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma,[Sura ya 410], kinataka kitengo cha usimamizi wa ununuzi (PMU) kuandaa na kuwasilisha kwenye vikao vya menejimenti, ripoti za robo mwaka za utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa mwaka. Aidha, Kanuni ya 114 (a) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inahitaji taasisi nunuzi kuwajibika kwa usimamizi madhubuti wa ununuzi wowote ya bidhaa, huduma au kazi inayofanyika na itafuatilia gharama na utoaji wa bidhaa na huduma kwa wakati kwa kiwango sahihi na kwa ubora uliobainishwa katika kila mkataba.

Nilibaini kuwa katika mamlaka tatu za serikali za mitaa ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 15.39 wa bidhaa, huduma na kazi katika ngazi za chini za serikali haukujumuishwa katika ripoti zao za robo mwaka kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.44.**

**Jedwali Na. 44: Kutojumuishwa kwa ununuzi wa ngazi ya chini katika ripoti ya manunuzi**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Monduli | 8,348,467,361 |
| 2 | H/Mji Mbulu | 3,826,154,830 |
| 3 | H/W Mbogwe | 3,213,283,115 |
| | **Jumla** | **15,387,905,306** |

Maoni yangu ni kwamba, kutoripoti thamani kubwa ya bidhaa zinazonunuliwa na kazi zilizofanyika katika ngazi za chini za serikali kunaleta wasiwasi juu ya uwazi na uwajibikaji; hivyo kuondoa uhalisia wa kiasi cha ununuzi kilichooneshwa katika utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa mwaka.

Jambo hili linaweza kuleta hatari kubwa ya matumizi mabaya ya rasilimali za umma kutokana na kukosekana kwa usimamizi wa karibu katika ngazi za chini za serikali.

**Ninapendekeza halmashauri zitoe taarifa sahihi ili kuimarisha uwajibikaji, na ufuatiliaji endelevu wa thamani ya fedha. Pia, ziimarishe udhibiti kwa kufanya usuluhishi wa taarifa kwa vipindi vya wiki na mwezi ili kuwa na taarifa sahihi za robo mwaka.**

### 5.4.2 Ununuzi bila kushirikisha kamati ya ununuzi na meneja mradi - Sh. milioni. 525.81

Aya za 30.5 na 30.6 za mwongozo wa kufanya kazi kwa njia ya matumizi ya rasilimali za ndani kwa taasisi nunuzi zinaeleza kuwa iwapo ofisi ya afisa masuuli iliyokasimiwa ina mtaalamu aliyehitimu, iunde bodi ya zabuni iliyokasimiwa na Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi (PMU) kwa ajili ya ununuzi kwa kuzingatia sheria ya ununuzi wa umma, [Sura ya 410]. Ikiwa hakuna mtaalamu anayepatikana, afisa masuuli aliyekasimiwa anapaswa kuteua wafanyakazi wawili hadi watatu kwa ajili ya ununuzi wa mradi chini ya uongozi wa kitengo cha ununuzi.

Pia, Aya ya 24.2 ya mwongozo wa kufanya kazi kwa njia ya matumizi ya rasilimali za ndani kwa taasisi nunuzi inataka vifaa vya ujenzi vinunuliwe kwa kuendana na mahitaji na vipimo vilivyoidhinishwa na meneja wa mradi.

Nilipitia miradi iliyotekelezwa katika ngazi ya chini ya serikali na kubaini kuwa, katika mamlaka tatu za serikali za mitaa, vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. Milioni 525.81 vilinunuliwa bila kushirikisha kamati ya

ununuzi wala meneja wa mradi kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 45.**

**Jedwali Na. 45: Ununuzi pasipo kushirikisha kitengo cha ununuzi**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Upungufu |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Bumbuli | 246,438,400 | Meneja wa mradi hajahusishwa |
| 2 | H/W Kondoa | 142,306,706 | Kamati za ununuzi hajizahusishwa |
| 3 | H/W Nyasa | 137,060,934 | |
| **Jumla** | | **525,806,040** | |

Utendaji wa kamati zilizokabidhiwa majukumu ya ununuzi haukuwa na ufanisi; hivyo, kusababisha kutofuatwa kwa miongozo na kanuni zinazotumika za ununuzi.

Ununuzi uliofanywa bila kushirikisha kamati iliyokabidhiwa ununuzi au idara ya ununuzi unakwamisha vyombo husika kutekeleza majukumu yao ya kiutendaji. Hivyo, kanuni za uwazi kwenye ununuzi wa umma zilikiukwa.

**Ninapendekeza kuwa maafisa masuuli wa mamlaka za serikali za mitaa husika wahakikishe miongozo iliyowekwa inafuatwa kikamilifu katika utekelezaji wa miradi katika ngazi ya chini ya serikali ili kufikia thamani ya fedha.**



# SURA YA SITA

## USIMAMIZI WA MAPATO

### 6.0 Utangulizi

Ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ni suala muhimu sana katika kuimarisha maendeleo na ustahimilivu wa mamlaka za serikali za mitaa.

Unachangia katika kukuza na kuwezesha dhana ya uwekezaji katika rasilimaliwatu, miundombinu, na utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Nimeangalia mwenendo wa miaka mitatu wa ukusanyaji wa mapato toka vyanzo vya ndani katika mamlaka ya serikali za mitaa na kubaini kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ambapo Sh. bilioni 912.12 zilikusanywa katika mwaka wa fedha 2022/23, ikilinganishwa na miaka iliyopita kama inavyooneshwa katika **Kilelezo Na.1** na kufafanuliwa katika **Kiambatisho Na.12.**

**Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa makusanyo ya Mapato**




***Chanzo:*** *Taarifa za hesabu*

Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato ya serikali za mitaa (LGRCIS), TAUSI, Mfumo wa taarifa za kifedha unaotumiwa katika ngazi za chini za halmashauri (FFARS), na Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania (GoT-HoMIS) ndiyo mifumo mahususi inayohusika katika ukusanyaji wa mapato kwenye mamlaka za serikali za mitaa. Mifumo hii inabeba jukumu la kutoa taarifa za ukusanyaji wa mapato, kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi fedha.

Kwa kutumia mifumo hii, mamlaka za serikali za mitaa zinaweza kufuatilia na kurahisisha mchakato wa ukusanyaji wa mapato ambayo yatawezesha mamlaka husika kutoa huduma muhimu kwa jamii husika.

Aidha, katika kutathmini mtiririko wa ukusanyaji wa mapato katika mamlaka ya serikali za mitaa pamoja na kuhakikisha wanazingatia sheria, kanuni, mipango ya bajeti pamoja na maelekezo mbalimbali yanayohusu usimamizi wa mapato, upungufu ufuatao ulibainika:

## 6.1 Kutokusuluhishwa kwa madai katika Mfumo wa LGRCIS yanayoweza kusababisha hasara ya Sh. bilioni 45.02

Aya ya 6.7 ya Mwongozo wa usimamizi wa mapato ya mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2019 inataka utengenezaji wa hati za madai na usimamizi wa madai ya mapato ufanyike kupitia Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato na walipakodi wenye madeni wafuatiliwe kupitia mfumo huo. Aidha, maelekezo ya barua yenye Kumb. Na. EB.151/297/02/10 ya tarehe 31 Januari 2023 kutoka OR-TAMISEMI yanazitaka mamlaka za serikali za mitaa, kukamilisha usimikaji na kuanza kuutumia mfumo wa TAUSI kabla au ifikapo tarehe 31 Machi 2023.

Aidha, maelekezo hayo yanasisitiza kwamba mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kusajili mashine zote za POS, kufanya usuluhishi wa wadaiwa kwenye mfumo wa mapato LGRCIS, kutumia leseni, vibali na moduli zote za mfumo wa TAUSI kwa ukamilifu, na kusitisha shughuli zote za ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa LGRCIS.

Kwa mujibu wa maelekezo kutoka OR-TAMISEMI, mamlaka za serikali za mitaa ziliagizwa kufanya usuluhisho na kusimamisha shughuli zote za ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa LGRCIS ndani ya muda ulioainishwa. Hata hivyo, nilibaini kuwapo kwa kiasi cha Sh. bilioni 45.02 ambacho hakikukusanywa katika mamlaka 125 za serikali za mitaa kutoka vyanzo mbalimbali ndani ya mfumo wa mapato wa LGRCIS.

Kwa tathmini niliyofanya katika mfumo wa mapato wa LGRCIS, nimebaini kukosekana kwa umakini na juhudi thabiti za kufuatilia madeni. Hali hii inaweza kusababisha hasara ya upotevu wa mapato kwa mamlaka za serikali za mitaa zenye madeni, hasa kwa kuzingatia kwamba serikali imeanza kutumia mfumo wa TAUSI ambao hausomani na mfumo wa LGRCIS. Maelezo ya kiasi kinachodaiwa yameoneshwa katika **Kiambatisho Na.13**.

Licha ya jitihada zinazofanywa na serikali za mitaa za kupunguza kiasi cha wadaiwa hawa, kiasi cha deni la sh. bilioni 45.02 katika mfumo wa mapato wa LGRCIS kinaleta wasiwasi wa uwezekano wa kupotea kwa mapato haya, hasa ikizingatiwa kuwa mfumo huu umetakiwa kutotumika kuanzia 31 Machi 2023.

**Ninapendekeza kuwa menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa husika zifanye juhudi za makusudi katika kufanya ufuatiliaji wa madeni yaliyopo katika mfumo wa mapato wa LGRCIS na kuhakikisha kuwa madai yote yanalipwa.**

## 6.2 Mapato ambayo hayakukusanywa katika vyanzo muhimu - Sh. bilioni 61.15

Nilikagua mchakato wa kukusanya mapato kupitia mfumo wa kukusanya mapato wa LGRCIS na kubaini kwamba, kiasi cha Sh. bilioni 61.15 hakikukusanywa kutoka mamlaka 130 za serikali za mitaa. Kiasi hiki kinatokana na vyanzo mbalimbali vya mapato vikijumuisha: kodi za kukodisha maduka yaliyo katika stendi za mabasi na masoko ya halmashauri, vibanda vya soko, kodi za nyumba, uuzaji wa viwanja, ada za uzoaji taka, leseni za biashara, leseni za vileo, kodi za upangishaji wa maeneo ya wazi yaliyokodishwa, ada za maegesho na vyanzo vingine vya mapato.

Hali hii ni kinyume na agizo Na. 7 (d) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linalomtaka mkurugenzi wa halmashauri kuwajibika kwa usimamizi wa ujumla wa mapato, matumizi, mali pamoja na madeni ya halmashauri anayoiongoza.

Muhtasari wa taarifa za vyanzo vya mapato pamoja na kiasi ambacho hakikukusanywa unaelezewa katika **Jedwali Na.46** na maelezo ya kina yameoneshwa katika **Kiambatisho Na.14.**

**Jedwali Na. 46: Vyanzo vya mapato visivyokusanywa**

| Na. | Chanzo cha Mapato | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Mauzo ya Viwanja | 23 | 42,536,221,960 |
| 2 | Kodi za pango | 43 | 7,482,506,132 |
| 3 | Mapato mengine | 22 | 6,317,825,455 |
| 4 | Maeneo wazi | 4 | 1,529,690,473 |
| 5 | Ada ya maegesho | 9 | 1,036,929,558 |
| 6 | Leseni za biashara | 14 | 855,806,998 |
| 8 | Ada za ukusanyaji taka | 5 | 803,106,330 |
| 9 | Leseni za vileo | 3 | 346,768,998 |
| 10 | Ada za uchimbaji madini | 7 | 242,976,855 |
| **Jumla** | | **130** | **61,151,832,760** |

***Chanzo:*** *LGRCIS, TAUSI na rejesta za mapato*

Kutokana na hali ya ufuatiliaji wa madeni usioridhisha, mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika zipo katika hatari ya kupoteza mapato.

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika, kuimarisha na kusimamia mifumo ya udhibiti wa ndani.**

**Hiyo ihusishe uhuishaji wa kanzidata ya walipaji, ukumbushaji wa wadaiwa/walipakodi kwa kuwatumia ankara husika kupitia ujumbe wa simu. Pia, pawe na ufuatiliaji wa karibu kupitia kikosi kazi cha ukusanyaji wa mapato na utoaji wa taarifa za wadaiwa na mbinu za ufuatiliaji kila mwezi ili kuongeza ukusanyaji katika vyanzo vyote vya mapato na kuhakikisha urejeshwaji wa madeni ambayo hayajakusanywa.**

## 6.3 Kutowasilishwa benki mapato yaliyokusanywa kupitia POS - Sh. bilioni 6.19

Kifungu cha 42 (2) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kinaelekeza kuwa, stakabadhi zote zinazohusiana na mamlaka ya serikali za mitaa zitalipwa katika akaunti ya benki au akaunti iliyothibitishwa na mamlaka hiyo.

Ukaguzi unaonesha kuwa mfumo wa ukusanyaji mapato wa LGRCIS ulianza kutumika katika mamlaka za serikali za mitaa kuanzia mwaka wa fedha 2012/13 hadi mwezi Machi 2023 ambapo serikali ilianzisha mfumo mpya wa TAUSI. Kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa na OR-TAMISEMI kwa barua yenye Na. EB.151/297/02/10 ya tarehe 31 Januri 2023, mamlaka za serikali za mitaa zilielekezwa kutumia kikamilifu mfumo wa TAUSI ifikapo tarehe 31 Machi 2023. Mifumo yote miwili hutumia mashine za POS kwa ajili ya kutoa stakabadhi kwa walipaji wa mapato mbalimbali.

Nimepitia taarifa za mapato zilizoandaliwa kutoka katika mifumo ya LGRCIS na TAUSI na kubaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 6.19 kilichokusanywa kupitia mashine za POS katika mamlaka 96 za serikali za mitaa hakikuwasilishwa katika akaunti husika za benki.

Taarifa kuhusu mapato ambayo hayakupelekwa benki zinapatikana kwenye **Kiambatisho Na.15** na mwenendo wa makusanyo ambayo hayajawasilishwa benki kwa miaka mitatu mfululizo umeoneshwa katika **Kielelezo Na.2.**

**Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa makusanyo yasiyowalishwa benki**




Kuwapo kwa Sh. 6.19 bilioni zisizowasilishwa benki katika mamlaka za serikali za mitaa kunapunguza uwezo wa halmashauri husika kutekeleza shughuli ilizojipangia na kusababisha kuongeza utegemezi kwa Serikali Kuu.

**Napendekeza kwamba, OR-TAMISEMI itathmini taratibu za kupeleka benki mapato yanayokusanywa kupitia POS na kuandaa sera za makubaliano kati ya mamlaka za serikali za mitaa na waendeshaji wa POS ili kukubaliana muda maalumu wa kuwasilisha makusanyo benki. Aidha, vifungu vya malipo vinapaswa kujumuisha fidia kwa ajili ya kucheleweshwa kwa muda mrefu kupeleka makusanyo benki ili kuhakikisha uhamisho wa haraka wa fedha zilizokusanywa na kurejesha mapato yasiyowasilishwa benki.**

**Vilevile, kuna haja ya kuchunguza kwa kina njia za malipo ya kielekitroni na uhamisho wa fedha za simu kupitia benki ili kurahisisha**

**kuweka benki kwa wakati wa makusanyo ya mapato yanayotokana na PoS.**

## 6.4 Kutokuwa na ufanisi katika makadirio na ukusanyaji wa ushuru wa huduma - Sh. bilioni 4.18

Vifungu vya 6(1) (u) na 7(1) (y) vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kama iliyorekebishwa na Kifungu cha 44 na 45 cha Sheria ya Fedha, Sura ya 348, vinaitaka taasisi au mtu binafsi anayeendesha biashara na mwenye leseni halali ya biashara kulipa ushuru wa huduma.

Ushuru wa huduma hutakiwa kulipwa na mtu au taasisi ambayo mauzo yake ghafi kwa mwaka yanazidi Sh. milioni nne. Aidha, utozaji ni kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya mauzo ghafi baada ya kupunguza kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa. Zaidi, sheria inataka matawi ya taasisi husika kulipa ushuru wa huduma katika maeneo ya halmashauri husika.

Kifungu hiki huhakikisha kuwa mapato yanayotokana na ushuru wa huduma yanaelekezwa kwenye utambulisho wa ushuru wa huduma kwa mamlaka za serikali za mitaa husika.

Baada ya kutathmini ufanisi wa ukusanyaji wa ushuru wa huduma, nimebaini kwamba mamlaka 37 za serikali za mitaa hazikukusanya ushuru wa huduma wa kiasi cha Sh. bilioni 4.18 kutoka kwa wafanyabiashara waliomo katika mamlaka husika.

Kushindwa kukusanywa kwa ushuru huu kunasababishwa na juhudi hafifu za kupeleka hati za madai kwa taasisi husika pamoja na kukosekana kwa kanzidata ya wafanyabishara iliyohuishwa. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa ambazo hazikukusanya ushuru wa huduma zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 47.**

**Jedwali Na. 47: Ushuru wa huduma usiokusanywa**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Mbeya | 972,584,366 | 21 | H/W Njombe | 19,590,555 |
| 2 | H/Jiji DSM | 950,316,403 | 22 | H/Mji Njombe | 17,724,163 |
| 3 | H/Jiji Tanga | 474,078,841 | 23 | H/W Nyasa | 15,650,518 |
| 4 | H/W Mbeya | 309,409,606 | 24 | H/W Mbozi | 15,461,455 |
| 5 | H/W Mkuranga | 275,925,735 | 25 | H/W Rungwe | 14,573,933 |
| 6 | H/W Handeni | 125,311,516 | 26 | H/Mji Makambako | 13,907,521 |
| 7 | H/Mji Kibaha | 124,612,791 | 27 | H/W Bunda | 11,556,114 |
| 8 | H/W Gairo | 114,586,412 | 28 | H/M Morogoro | 10,684,600 |
| 9 | H/W Serengeti | 107,902,503 | 29 | H/W Ileje | 7,809,551 |
| 10 | H/W Missenyi | 93,511,934 | 30 | H/W Tandahimba | 7,249,515 |
| 11 | H/Mji Tarime | 76,519,486 | 31 | H/W Nanyumbu | 6,568,048 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 12 | H/W Rombo | 67,867,562 | 32 | H/W Korogwe | 6,405,994 |
| 13 | H/W Kishapu | 54,673,437 | 33 | H/W Mpimbwe | 6,149,034 |
| 14 | H/M Shinyanga | 52,829,614 | 34 | H/W Ngara | 5,991,211 |
| 15 | H/M Temeke | 46,240,869 | 35 | H/Mji Newala | 5,544,700 |
| 16 | H/W Musoma | 40,264,135 | 36 | H/Mji Ifakara | 5,300,000 |
| 17 | H/W Mbarali | 30,718,536 | 37 | H/Mji Masasi | 5,223,669 |
| 18 | H/W Makete | 30,640,011 | | | |
| 19 | H/W Tarime | 27,307,550 | | | |
| 20 | H/W Pangani | 25,941,160 | **Jumla** | | **4,176,633,048** |

Nimefanya tathmini na kubaini kuwa kuweka viwango vinavyotofautiana kutoka sifuri hadi asilimia 0.3 kunajenga udhaifu, ambapo makampuni yanaweza kuwa na mwelekeo wa kuepuka kulipa ushuru huo.

Aidha, kushindwa kukusanya ushuru wa huduma kwa mamlaka husika za serikali za mitaa kunaathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

**Ninapendekeza menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa, kwa kushirikiana na watendaji wa kata zao, kuhakikisha kuwa kanzidata za biashara zinahuishwa mara kwa mara. Pia, kuwe na ufuatiliaji wa kutosha kupitia ngazi zote, zikiwamo ngazi za kata na Vijiji, ili kukusanya ushuru wa huduma kwa ukamilifu. Juhudi hizi za pamoja zitawezesha makusanyo ya ushuru wa huduma kuongezeka.**

### 6.5 Makusanyo ya Sh. bilioni 8.15 za ushuru wa huduma bila ripoti za mauzo

Katika ukaguzi wa mifumo ya kukusanya mapato ya LGRCIS, TAUSI na taarifa za benki nilibaini kuwa mamlaka 37 za serikali za mtaa zilikusanya ushuru wa huduma wenye jumla ya kiasi cha Sh. bilioni 8.15 bila kupata ushahidi wa taarifa za mauzo ghafi kutoka mamlaka au taasisi husika ili kuthibitisha kiasi kilichokusanywa.

Suala hilo ni kinyume na aya ya 6.6.1(iii & iv) ya Mwongozo wa usimamizi wa mapato ya mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2019 ambayo inafafanua mkakati na taratibu za ukusanyaji wa ushuru wa huduma ukijumuisha utoaji wa fomu ya kukiri jumla ya mauzo ghafi ambayo hujazwa na mlipakodi.

Fomu hiyo inaweza kutumika katika utozaji wa ushuru wa huduma kwa usahihi na ufanisi. Maelezo zaidi ya ushuru wa huduma uliokusanywa bila vithibitisho vya mauzo ghafi yametolewa katika **Jedwali Na.48**.

**Jedwali Na. 48: Makusanyo ya ushuru wa huduma bila uthibitisho**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/M Temeke | 2,982,894,578 | 20 | H/W Siha | 107,399,439 |
| 2 | H/W Missenyi | 807,814,159 | 21 | H/W Bukombe | 105,904,775 |
| 3 | H/Mji Nzega | 328,157,758 | 22 | H/W Msalala | 97,141,121 |
| 4 | H/Mji Tunduma | 327,583,153 | 23 | H/W Chato | 92,920,814 |
| 5 | H/W Maswa | 284,469,213 | 24 | H/W Tarime | 91,771,963 |
| 6 | H/Mji Bunda | 246,257,412 | 25 | H/W Kibiti | 67,026,798 |
| 7 | H/W Kilolo | 231,768,686 | 26 | H/W Singida | 39,636,360 |
| 8 | H/M Shinyanga | 226,267,620 | 27 | H/W Mafia | 39,279,893 |
| 9 | H/W Serengeti | 224,663,174 | 28 | H/W Mlele | 37,939,500 |
| 10 | H/M Mpanda | 216,397,030 | 29 | H/W Mkinga | 35,915,016 |
| 11 | H/W Nsimbo | 214,294,718 | 30 | H/W Bagamoyo | 31,417,486 |
| 12 | H/W Pangani | 190,374,481 | 31 | H/M Kahama | 29,447,716 |
| 13 | H/Jiji Mwanza | 157,993,799 | 32 | H/W Kishapu | 28,758,356 |
| 14 | H/W Kilindi | 149,538,920 | 33 | H/W Mufindi | 27,371,316 |
| 15 | H/Mji Tarime | 146,582,437 | 34 | H/W Karatu | 24,116,668 |
| 16 | H/W Muleba | 141,733,871 | 35 | H/W Bumbuli | 19,282,869 |
| 17 | H/W Meatu | 139,651,466 | 36 | H/W Ushetu | 14,274,865 |
| 18 | H/W Mpanda | 120,522,314 | 37 | H/W Kakonko | 12,574,225 |
| 19 | H/Mji Kibaha | 112,214,830 | **Jumla** | | **8,151,358,799** |

***Chanzo:*** *LGRCIS na Taarifa za benki*

Hivyo, kuna uwezekano wa makusanyo ya ushuru wa huduma kuwa pungufu kutokana na kukosekana kwa taarifa za mauzo ghafi ambazo zingeweza kutumika katika kukokotoa kiasi stahiki cha ushuru wa huduma ambacho kinatakiwa kulipwa na walipakodi husika.

**Ninapendekeza kwamba, OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania, zihuishe mfumo wa kielekitroni utakaowezesha kupeana taarifa za mauzo ghafi na mamlaka za serikali za mitaa. Mfumo huo utasaidia katika kukokotoa kiasi halisi cha ushuru wa huduma kinachopaswa kulipwa na taasisi husika.**

**Pamoja na hilo, ninahimiza menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini kwa kutumia fomu za kukiri mauzo ghafi inayojazwa na mlipakodi kabla ya kumtoza. Njia hii itaongeza usahihi na ufanisi katika ukusanyaji wa kodi ya ushuru wa huduma.**

## 6.6 Ukusanyaji usioridhisha katika vyanzo vikubwa vya mapato - Sh. bilioni 6.09

Katika kufanya tathmini ya makusanyo ya mapato kwa mwaka wa fedha 2022/23 katika vyanzo vikubwa vilivyoko katika mamlaka za serikali za mitaa nne kwa kupitia ripoti za usimamizi, ripoti za vitabu vya fedha, na ripoti za mifumo ya ukusanyaji mapato, nilibaini kwamba, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa kilikuwa ni Sh. bilioni 8.03.

Hata hivyo, makusanyo halisi yalifikia Sh. bilioni 1.94 tu ikiwa ni 24% ya makadirio ya mapato kutoka katika vyanzo husika. Hivyo, hii ilisababisha upungufu mkubwa wa makusanyo ya Sh. bilioni 6.09 sawa na 76% ya makadirio yaliyowekwa.

Kwa kuzingatia kiasi kidogo kilichokusanywa katika vyanzo husika, nilibaini kwamba menejimenti za mamlaka husika za serikali za mitaa hazikufanya vizuri katika wajibu wao wa ukusanyaji wa mapato. Hii ni kinyume na aya ya 4.2 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 inayoeleza kuwa wajibu wa usimamizi wa mapato ya mamlaka za serikali za mitaa umewekwa chini ya OR-TAMISEMI kupitia sekeretarieti za mikoa na mamlaka ya serikali za mitaa.

Pia, Agizo la 7 (d) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linalomtaka mkurugenzi wa halmashauri kuwajibika kwa usimamizi wa ujumla wa mapato, matumizi, mali, pamoja na madeni ya halmashauri anayoiongoza. Maelezo ya vyanzo vikubwa vya mapato ambavyo havikufanya vizuri yametolewa kwenye **Jedwali Na.49.**

**Jedwali Na. 49: Ukusanyaji usioridhisha katika vyanzo vikubwa vya mapato**

| Na | Jina la Halmashauri | Chanzo cha mapato | Bajeti ya makusanyo (Sh.) | Makusanyo halisi (Sh.) | % | Pungufu (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dodoma | Stendi ya malori Nala | 771,250,000 | 53,421,708 | 7 | 717,828,292 |
| | | Soko la Ndugai | 1,254,408,565 | 314,443,950 | 25 | 939,964,615 |
| | | Stendi kuu ya Nanenane | 2,583,757,600 | 661,306,637 | 26 | 1,922,450,963 |
| | | Soko la Machinga | 238,966,000 | 106,394,658 | 45 | 132,571,342 |
| 2 | H/W Chalinze | Stendi ya Chalinze | 1,000,000,000 | 252,057,500 | 25 | 747,942,500 |
| 3 | H/M Sumbawanga | Stendi ya Katumba Azimio | 704,280,000 | 149,763,800 | 21 | 554,516,200 |
| 4 | H/M Ilemela | Stendi ya Nyamhongolo | 1,475,096,452 | 402,824,100 | 27 | 1,072,272,352 |
| **Jumla** | | | **8,027,758,617** | **1,940,212,353** | **4** | **6,087,546,264** |

Chanzo: LGRCIS: TAUSI na Taarifa za vyanzo husika za mapato

Sababu zinazochangia utendaji duni katika vyanzo hivi ni: mahali ilipojengwa miundombinu ya vyanzo husika, ambapo baadhi ya vyanzo viko maeneo yasiyo na shughuli nyingi za kibinadamu; uhaba wa huduma za kijamii; kutokuwa na mzunguko imara wa biashara; na mtandao mdogo wa usafiri kwenda na kutoka katika vyanzo hivyo.

Hali hii inapunguza idadi ya wateja iliyotarajiwa na kusababisha shughuli za biashara kutokuwa na mwitikio; hivyo, kusababisha wafanyabiashara kushindwa kutekeleza wajibu wao wa kulipa kodi.

Pia, viwango vya juu vya kodi kwa maduka yanayopatikana ndani ya miundombino ya vyanzo hivyo vinachangia wafanyabiashara kushindwa kukodi vyumba vya biashara. Hali hii, kwa upande mwingine, imewalazimisha baadhi ya wafanyabiashara kufanya shughuli zao katika maeneo hayo bila kuwa na mikataba rasmi na mamlaka za serikali za husika.

Hivyo, bila kuchukuliwa kwa hatua madhubuti za kupunguza sababu hizo zilizotajwa, kuna uwezekano wa kuendelea kwa utendaji duni; hivyo thamani ya fedha kutoka kwenye miradi husika kutopatikana kwa wakati.

**Ninapendekeza kwamba, menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika zifanye mikakati, ikiwamo kuongeza mtandao wa usafiri kuelekea maeneo ya miundombinu yenye vyanzo husika vya mapato, ambayo itawezesha kuongezeka kwa mzunguko wa biashara ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kutimia. Pia, ni muhimu kusawazisha viwango vya kodi na kuhakikisha kwamba wafanyabiashara katika maeneo haya wanapewa nyaraka za mkataba ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato.**

## 6.7 Kutowasilishwa kwa Sh. bilioni 5.65 na Mawakala wa Ukusanyaji Mapato

Katika kupitia usimamizi wa mapato kupitia mikataba ya makusanyo katika vyanzo mbalimbali, nilibaini kuwa menejimenti za mamlaka 12 za serikali za mitaa ziliingia mikataba 53 na mawakala kwa ajili ya kukusanya mapato katika vyanzo mbalimbali katika maeneo yao. Mikataba hii ilikuwa na thamani ya Sh. bilioni 14.43.

Nilifanya ukaguzi zaidi katika mifumo ya kukusanya mapato ya LGRCIS pamoja na TAUSI na kubaini kwamba kiasi cha Sh. bilioni 8.89 pekee ndicho kichopokelewa na mamlaka husika za serikali za Mitaa. Hata hivyo, nilibaini kiasi cha Sh. bilioni 5.65 sawa na 39% ambacho hakijawasilishwa kwa mujibu wa mikataba husika.

Hii ni kinyume na kifungu cha 26 (a) na (b) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, ambacho kinamtaka mtu anayestahili kuteuliwa na mamlaka za serikali za mitaa kukusanya na kupokea kiasi stahiki kutoka kwa kila mlipakodi katika eneo ambalo amepangiwa, na kuhakikisha kiasi

chote kilichokusanywa kinalipwa kwa mamlaka ya serikali ya mtaa inayohusika. Makusanyo ambayo hayakuwasilishwa yameoneshwa kwenye **Jedwali Na.50.**

**Jedwali Na. 50: Taarifa ya makusanyo ya mawakala**

| Na | Jina na Halmashauri | Idadi ya mikataba | Kiasi (Sh.) | | | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kimkataba | Kilichowasilishwa | kinachodaiwa | |
| 1 | H/M Kinondoni | 4 | 5,256,952,907 | 2,900,540,955 | 2,356,411,951 | 45 |
| 2 | H/W Kilindi | 2 | 2,507,000,000 | 1,718,089,230 | 788,910,770 | 31 |
| 3 | H/Jiji Mwanza | 15 | 2,425,870,400 | 1,744,574,900 | 681,295,500 | 28 |
| 4 | H/Jiji DSM | 1 | 1,702,894,536 | 1,138,432,770 | 545,806,066 | 32 |
| 5 | H/W Muheza | 1 | 1,210,000,000 | 773,177,906 | 436,822,094 | 36 |
| 6 | H/W Bumbuli | 7 | 373,350,000 | 287,867,850 | 215,082,150 | 58 |
| 7 | H/Mji Korogwe | 3 | 240,005,100 | 84,461,200 | 155,543,900 | 65 |
| 8 | H/W Misungwi | 4 | 252,000,000 | 99,830,800 | 152,169,200 | 60 |
| 9 | H/W Chalinze | 1 | 150,000,000 | 30,542,000 | 119,458,000 | 80 |
| 10 | H/W Mkuranga | 1 | 158,193,438 | 57,938,450 | 100,254,988 | 63 |
| 11 | H/W Mafia | 1 | 107,632,000 | 30,000,000 | 77,632,000 | 72 |
| 12 | H/M Morogoro | 7 | 41,920,200 | 19,030,000 | 23,850,200 | 57 |
| Jumla | | 53 | 14,425,818,581 | 8,884,486,061 | 5,653,236,819 | 39 |

**Chanzo:** Mikataba ya mapato

Mamlaka ya serikali za mitaa moja pekee ilichukua hatua kwa wakala husika aliyekiuka masharti, huku mamlaka nyingine za serikali za mitaa hazikuchukua hatua stahiki kwa mawakala walioshindwa kufikia malengo ya kiasi cha mapato walichokubaliana kuwasilisha kwa mujibu wa mikataba.

Kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kupitia mawakala kunazuia utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika mamlaka za serikali za mitaa husika.

**Ninapendekeza katika siku zijazo, menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zifanye upembuzi yakinifu unaoakisi uhalisi wa malengo ya makusanyo katika vyanzo husika vya mapato. Vilevile, zihakikishe mikataba inaeleza wazi hatua zitakazochukuliwa dhidi ya mawakala watakaoshindwa kuwasilisha kiasi kilichokubaliwa.**

**Kwa mikataba ambayo tayari ina vifungu vinavyoeleza hatua dhidi ya mawakala walioshindwa kuwasilisha makusanyo kulingana na makubaliano, ninashauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa**

**zichukue hatua stahiki dhidi ya mawakala hao ili wawasilishe mapato ambayo hayajarejeshwa.**

## 6.8 Ushuru wa mazao usiokusanywa kiasi - Sh. bilioni 5.22

Ukaguzi wangu wa taarifa za minada ya mazao, mifumo ya taarifa za mapato ya LGRCIS na TAUSI, pamoja na taarifa za vyama vya ushirika vya masoko ya kilimo (AMCOS) na taarifa za bodi za mazao husika ulibaini kuwa mamlaka 20 za serikali za mitaa hazijakusanya jumla ya Sh. bilioni 5.22 katika chanzo kinachohusu ushuru wa mazao.

Kushindwa kukusanya mapato husika ni kinyume na kifungu cha 7(1) (g) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290, ambacho kinaeleza kuwa fedha zote zitokanazo na malipo yoyote yanayolipwa katika chanzo cha mazao ya kilimo au mazao mengine yanayozalishwa katika eneo la halmashauri ya wilaya, zilizowekwa chini ya sheria hii au sheria nyingine yoyote, isipokuwa kwa mazao muhimu yanayosafirishwa kwa ajili ya mauzo ya nje ya nchi ambayo ushuru husika utaanzia kati ya sifuri na asilimia tano ya bei ya lango la shamba. Ushuru huo utalipiwa kwenye chanzo cha mauzo.

Pia, sehemu ya 1 ya Jedwali la Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, inataka malipo ya ushuru wa mazao kwa mnunuzi kutozwa asilimia tatu ya bei ya lango la shamba katika mazao ya biashara. Mchanganuo wa ushuru wa mazao usiokusanywa umeoneshwa kwenye **Jedwali Na.51.**

**Jedwali Na. 51: Ushuru wa mazao usiokusanywa**

| Na | Halmashauri | Zao husika | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---:|
| 1 | H/W Rungwe | Chai | 852,005,350 |
| | | Mazao ya chakula | 421,428,789 |
| 2 | H/M Songea | Mahindi | 646,466,400 |
| 3 | H/Mji Mbinga | Mahindi | 399,410,480 |
| | | Kahawa | 102,796,453 |
| 4 | H/W Hanang’ | Mazao na misitu | 458,686,842 |
| 5 | H/W Masasi | Ufuta | 405,642,242 |
| 6 | H/W Kibiti | Ufuta | 292,566,265 |
| | | Mkaa | 89,020,700 |
| 7 | H/W Mbozi | Kahawa | 338,380,927 |
| 8 | H/W Tunduru | Ufuta | 186,520,986 |
| 9 | H/W Kyela | Kokoa | 165,986,266 |
| 10 | H/W Moshi | Kahawa | 157,185,348 |
| 11 | H/W Nyasa | Kahawa | 131,568,394 |
| 12 | H/W Namtumbo | Ufuta | 116,237,044 |
| | | Mahindi | 163,339,800 |
| 13 | H/W Urambo | Tumbaku | 72,769,281 |
| 14 | H/W Busokelo | Chai | 63,493,465 |
| 15 | H/W Bumbuli | Chai | 27,171,019 |
| | | Mkonge | 7,830,772 |

| Na | Halmashauri | Zao husika | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 16 | H/W Nsimbo | Tumbaku | 29,598,034 |
| 17 | H/W Mbinga | Kahawa | 29,007,301 |
| 18 | H/W Kakonko | Tumbaku | 26,954,312 |
| 19 | H/W Njombe | Chai | 19,244,970 |
| 20 | H/W Nanyamba | Ufuta | 15,723,264 |
| **Jumla** | | | **5,219,034,704** |

*Chanzo: LGRCIS, TAUSI na Taarifa za mazao*

Kutokukusanywa kwa ushuru husika wa mazao kunazinyima mamlaka husika za serikali za mitaa uwezo wa kuboresha huduma zitolewazo kwa jamii iliyokusudiwa.

**Ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa kuboresha ushirikiano kati ya kitengo cha fedha na idara ya kilimo ili kufanya ufuatiliaji wa karibu wa ushuru wa mazao ambao haujalipwa kutoka taasisi na kampuni husika.**

**Lengo la ushirikiano huu ni kuwezesha kukusanywa kwa ushuru wa mazao ambao unadaiwa.**

## 6.9 Kutokukusanywa kwa Sh. bilioni 1.48 za dhamana ya utendaji kwenye mikataba ya mawakala

Nimepitia mikataba iliyotekelezwa ya makusanyo ya mapato katika mamlaka tatu za serikali za mitaa, ambapo, mawakala walisaini mikataba saba yenye jumla ya Sh. bilioni 10.21. Hata hivyo, mawakala hao hawakuwasilisha fedha za dhamana ya utendaji-kazi ya Sh. bilioni 1.48 ambayo walikubaliana kwa mujibu wa mikataba iliyoingiwa.

Hii ni kinyume na agizo la 38 (3) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaloelekeza kwamba, kama mamlaka za serikali za mitaa zitachagua kukusanya mapato kwa njia ya wakala itampasa wakala aliyechaguliwa kuwekeza fedha ambayo ni sawa na makusanyo ya miezi mitatu ya mkataba aliokubaliana, garantii ya benki au aina nyingine ya dhamana itakayokubalika na mamlaka husika.

Suala hili pia limesisitizwa kwenye aya ya 5.2.1 (iv) ya mwongozo wa usimamizi wa mapato ya mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2019 unaofafanua kuwa, mikataba inayoingiwa itahakikisha uzingatiaji wa masharti ya mkataba wa makusanyo ya mapato kupitia malipo ya awali/amana kama ilivyoainishwa kwenye kusaini mkataba na kabla ya utekelezaji wa mkataba. Maelezo ya dhamana ambazo hazikulipwa yameoneshwa katika **Jedwali Na.52.**

**Jedwali Na. 52: Mawasilisho ya dhamana ya kazi pungufu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Jina la wakala | Chanzo cha mapato | Thamani ya mkataba (Sh) | Kiasi cha dhamana kwa mujibu wa mkataba (Sh) | Kiasi cha dhamana kilichotolewa na wakala (Sh) | Tofauti(Sh) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Kilindi | TOGABE COMPANY LTD | ushuru wa biashara | 2,024,000,000 | 506,000,000 | 0 | 506,000,000 |
| | | BEZZU COMPANY LTD | Ushuru wa mifugo | 483,000,000 | 120,750,000 | 27,000,000 | 93,750,000 |
| | | | | | | | |
| 2 | H/M Kinondoni | M/s Web Corporation Limited | ushuru wa maegesho | 4,466,172,480 | 669,925,872 | 55,827,156 | 614,098,716 |
| 3 | H/Jiji DSM | M/S Kajenjere | ushuru wa uzoaji taka | 624,000,000 | 52,000,000 | 0 | 52,000,000 |
| | | M/S Kajenjere | | 1,200,000,000 | 100,000,000 | 0 | 100,000,000 |
| | | M/S Sateki | | 930,000,000 | 77,500,000 | 0 | 77,500,000 |
| | | M/S Sateki | | 480,000,000 | 40,000,000 | 0 | 40,000,000 |
| | **Jumla** | | | **10,207,172,480** | **1,566,175,872** | **82,827,156** | **1,483,348,716** |

Chanzo: Mikataba ya mawakala na Hati za malipo

Kutokulipwa kwa fedha za dhamana ya utendaji kwa mujibu wa mikataba kunaweza kusababisha upotevu wa fedha za serikali, hasa pale ambapo kutatokea uvunjaji wa mkataba.

**Napendekeza menejimenti za mamlaka husika za serikali za mitaa zifuate kwa umakini maelekezo ya mikataba yaliyotolewa katika agizo la 38(3) Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Hii itahakikisha usimamizi bora wa mikataba na kupunguza hatari ya hasara kwa fedha za serikali endapo kutatokea uvunjaji wa mikataba.**

### 6.10 Marekebisho ya ankara yaliyofanyika bila viambatisho toshelevu - Sh. milioni 719.96

Agizo la 37 (6) la Memoranda ya Fedha za mamlaka za serikali za mitaa ya Mwaka 2009 linaeleza kwamba, kama stakabadhi imekosewa, itenguliwe mara moja na itolewe mpya. Stakabadhi halisi iliyotenguliwa ihifadhiwe kwa ukaguzi.

Pia, Aya ya 3.4 (vii) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato katika mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2019 inazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha marekebisho na ufutaji wa ankara zisizo sahihi katika mfumo wa IFMIS au LGRCIS kuidhinishwa na mkurugenzi wa halmashauri.

Katika kupitia marekebisho ya ankara yaliyofanyika katika mfumo wa taarifa za ukusanyaji wa mapato wa LGRCIS, nilibaini kwamba mamlaka

tatu za serikali za mitaa zilirekebisha ankara za kiasi cha Sh. milioni 719.96 bila kuwa na maelezo ya kutosha na/au viambatisho toshelevu. Matokeo yake, miamala hii ilishindwa kuhalalisha marekebisho ya ankara husika yaliyofanyika katika mfumo.

Nilishindwa kufanya uhakiki wa marekebisho yaliyofanywa kutokana na kukosekana kwa viambatisho toshelevu. Ni dhahiri kwamba mamlaka za serikali za mitaa husika hazikutekeleza kikamilifu hatua za udhibiti kama inavyotakiwa na Agizo la 37(6) la Memoranda ya Fedha za mamlaka za serikali za mitaa ya mwaka 2009 na Aya ya 3.4 (vii) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya Serikali za Mitaa wa mwaka 2019.

Maelezo ya ankara zilizofanyiwa marekebisho katika mamlaka za serikali za mitaa bila viambatisho toshelevu yametolewa katika **Jedwali Na.53.**

**Jedwali Na. 53: Ankara zilizorekebishwa bila viambatisho toshelevu**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Kilindi | 670,923,060 |
| 2 | H/W Uvinza | 37,812,200 |
| 3 | H/W Mpwapwa | 11,225,750 |
| **Jumla** | | **719,961,010** |

***Chanzo:*** *Mfumo wa mapato wa LGRCIS*

Kwa maoni yangu, marekebisho yanayofanywa bila kuwa na vielelezo vya kutosha pamoja na kibali yanaziweka mamlaka husika za serikali za mitaa kwenye hatari ya ubadhirifu wa mapato bila kugundulika na uongozi wa halmashauri.

**Napendekeza kuwa menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zilizoainishwa ziweke mifumo imara ya kusaidia utunzaji wa viambatisho vya ankara za mapato zinazorekebishwa au kufutwa kwa kuhuisha au kupakia nyaraka husika katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato kabla ya kuidhinishwa na mkurugenzi wa halmashauri.**

# SURA YA SABA



## USIMAMIZI WA MATUMIZI

### 7.0 Utangulizi

Usimamizi wa matumizi ya fedha za umma unahusisha udhibiti wa masuala ya kifedha kwenye mamlaka za serikali za mitaa ili kuhakikisha ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma, kuimarisha uwajibikaji, na kuanzisha usimamizi wa kisheria kwa maslahi endelevu ya umma.

Usimamizi wa matumizi ya fedha za umma unalenga kufanikisha malengo matatu ambayo ni: nidhamu ya fedha, ufanisi kwenye kupanga matumizi pamoja na ufanisi kwenye utendaji. Nidhamu ya fedha ni serikali kufanya matumizi ambayo yako ndani ya uwezo; ufanisi wa kupanga matumizi inahusu kufanya matumizi sahihi ya fedha za serikali kwenye maeneo yenye ufanisi; na ufanisi kwenye utendaji ni utoaji wa huduma kwa umma zenye ubora na gharama zinazostahiki.

Ili kupata matokeo hayo, serikali ilianzisha sheria mbalimbali, kanuni, sera na mifumo ya udhibiti wa ndani inayopaswa kuzingatiwa na Mamlaka zote za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, kupitia ukaguzi nilioufanya nimebaini kutozingatiwa kwa sheria za usimamizi wa fedha, kanuni na miongozo mbalimbali hali inayopelekea matumizi yasiyokuwa na tija kwa mamlaka za serikali za mitaa.

Sura hii inaeleza kwa muhtasari masuala muhimu ambayo, ikiwa hayatatuliwa, yanaweza kuathiri usimamizi wa fedha zinazosimamiwa na mamlaka za serikali za mitaa.

### 7.1 Upungufu uliobainika katika usimamizi wa akaunti za Amana - Sh. bilioni 10.71

Kazi ya msingi ya akaunti ya amana ni kutunza fedha za walioweka amana ili zitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Hivyo, matumizi ya fedha zilizopo katika akaunti hiyo yanapaswa kuendana na lengo kuu la amana hizo.

Kanuni ya 132 ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inamtaka ofisa anayeidhinisha marejesho ya madai ya amana kujiridhisha kwamba amana imetumika kwa lengo lililokusudiwa. Pia, lazima ofisa huyo ajiridhishe kwa kurejea stakabadhi ya awali iliyotolewa ili kuthibitisha mtu anayedai amana ndiye mwekaji halali wa amana au ana haki ya kurejeshewa.

Kinyume na kanuni tajwa, tathmini niliyoifanya kuhusiana na usimamizi wa akaunti za amana katika mamlaka za serikali za mitaa nilibaini dosari zinazofikia jumla ya Sh. bilioni 10.71 kama inavyofafanuliwa hapa chini:

### 7.1.1 Malipo yaliyofanyika kwa shughuli zisizokusudiwa Sh. Bilioni 5.16

Nilibaini kuwa mamlaka 46 za serikali za mitaa zilifanya malipo ya Sh. bilioni 5.16 kutoka katika akaunti za amana kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizokuwa, kinyume na malengo yaliyokusudiwa na fedha hazikurejeshwa kwenye akaunti husika.

Kitendo hiki ni kinyume na Kanuni ya 132 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001, kwani kutumia fedha za akaunti ya amana kutekeleza shughuli zisizokusudiwa kunaathiri upatikanaji wa fedha hizo kwa waweka amana; na huweza kuharibu sifa ya taasisi. Taarifa ya malipo yaliyofanyika imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.16.**

### 7.1.2 Salio pungufu la benki kufidia madai ya waweka Amana Sh. milioni 745.23

Nilibaini kuwa mamlaka tatu za serikali za mitaa zilikuwa na salio pungufu la benki kwa kiasi cha Sh. milioni 745.23, hivyo kutoweza kufidia madai ya waweka amana katika akaunti ya amana.

Kutokuwapo kwa salio la fedha taslimu linalolingana na kiasi cha madai ya waweka amana kunaashiria kuwa, kuna uwezekano kuwa fedha za amana zilitumika kutekeleza shughuli zisizokusudiwa na mamlaka husika za serikali za mitaa, hivyo kuathiri shughuli zilizokusudiwa. Rejea **Jedwali Na.54** hapa chini.

**Jedwali Na. 54: Salio pungufu la benki kufidia madai ya waweka Amana**

| Na. | Jina la Halmashauri | Madai ya Waweka Amana kulingana na Rejesta ya Amana (Sh.) | Kiasi cha Fedha Zilizopo-Akaunti ya Amana (Sh.) | Tofauti (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Mji Korogwe | 498,635,219 | 43,089,257 | 455,545,962 |
| 2. | H/W Arusha | 222,697,361 | 40,050,924 | 182,646,437 |
| 3. | H/W Monduli | 284,379,656 | 177,343,617 | 107,036,039 |
| **Jumla** | | 1,005,712,236 | 260,483,798 | 745,228,438 |

### 7.1.3 Malipo zaidi ya kiasi kilichowekwa kwenye akaunti ya Amana - Sh. Bilioni 1.95

Tathmini yangu ya usimamizi wa akaunti za amana ilibaini kuwa mamlaka 17 za serikali za mitaa zilifanya malipo kwa ajili ya shughuli mbalimbali na kuvuka viwango vilivyowekwa na waweka amana husika kwenye Akaunti hizo kwa kiasi cha Sh. bilioni 1.95 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.55.**

Malipo yaliyofanyika zaidi ya kiasi kilichowekwa kwenye akaunti za amana yanaathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

**Jedwali Na. 55: Malipo zaidi ya kiasi kilichowekwa akaunti ya Amana**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/Manispaa Temeke | 630,356,985 |
| 2 | H/W Uyui | 194,073,013 |
| 3 | H/W Kasulu | 186,785,432 |
| 4 | H/Mji Njombe | 171,358,185 |
| 5 | H/W Monduli | 124,172,329 |
| 6 | H/Mji Babati | 121,290,978 |
| 7 | H/Manispaa Ilemela | 94,187,977 |
| 8 | H/W Arusha | 90,144,440 |
| 9 | H/W Mbinga | 83,890,454 |
| 10 | H/W Iringa | 52,288,714 |
| 11 | H/W Hanang’ | 45,212,418 |
| 12 | H/W Muheza | 40,979,988 |
| 13 | H/W Longido | 33,546,896 |
| 14 | H/W Iramba | 28,495,943 |
| 15 | H/W Kibaha | 26,280,381 |
| 16 | H/W Njombe | 19,076,861 |
| 17 | H/W Mufindi | 8,847,212 |
| **Jumla** | | 1,950,988,206 |

### 7.1.4 Uhamisho wa fedha kutoka akaunti ya Mapato ya ndani kwenda akaunti ya Amana Sh. bilioni 1.91

Aya ya 3 ya Sehemu ya 2 ya Mwongozo uliotolewa na OR-TAMISEMI Septemba 2017 inaelekeza kwamba fedha za mapato ya ndani zitahamishwa kwenda akaunti ya mfuko wa pamoja na akaunti ya miradi ya maendeleo.

Kinyume na maelekezo hayo, nilibaini mamlaka 10 za serikali za mitaa zilihamisha kiasi cha Sh. bilioni 1.91 kutoka kwenye akaunti za mapato ya ndani kwenda akaunti za amana kwa ajili ya matumizi yasiyoidhinishwa.

Mapato ya ndani yaliyohamishiwa kwenye akaunti ya amana yanaweza kutumika isivyokusudiwa, hivyo kusababisha kutotekeleza shughuli zilizokuwa kwenye bajeti na kutekeleza matumizi yasiyokuwa na tija. Rejea **Jedwali Na.56**.

**Jedwali Na. 56: Uhamisho wa mapato ya ndani kwenda akaunti ya Amana**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/Mji Tunduma | 556,458,172 |
| 2. | H/Manispaa | 407,753,593 |
| 3. | H/W Tarime | 347,000,000 |
| 4. | H/W Wang'ing'ombe | 179,950,000 |
| 5. | H/W Msalala | 150,000,000 |
| 6. | H/W Ushetu | 87,889,109 |
| 7. | H/W Moshi | 56,829,599 |
| 8. | H/W Karatu | 47,000,000 |
| 9. | H/W Nyasa | 46,011,172 |
| 10. | H/W Longido | 29,000,000 |
| **Jumla** | | **1,907,891,645** |

### 7.1.5 Malipo yaliyofanywa bila uthibitisho wa fedha kupokelewa akaunti ya Amana - Sh. Milioni 935

Nilibaini mamlaka 15 za serikali za mitaa zilifanya malipo ya kiasi cha Sh. milioni 935 kutoka kwenye akaunti za Amana kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali bila uthibitisho wa stakabadhi zinazoonesha fedha husika kupokelewa katika akaunti ya amana. Hii ni kinyume na matakwa ya Kanuni ya 132 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001.

Matumizi ya aina hiyo huathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kufanyika kupitia akaunti za Amana. Rejea **Jedwali Na.57.**

**Jedwali Na. 57: Malipo bila ya fedha kupokelewa akaunti ya Amana**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Namtumbo | 228,484,000 |
| 2 | H/M Kigoma/Ujiji | 172,775,123 |
| 3 | H/W Buhigwe | 130,002,212 |
| 4 | H/W Serengeti | 75,937,600 |
| 5 | H/W Siha | 51,992,874 |
| 6 | H/W Mpanda | 47,842,496 |
| 7 | H/W Singida | 38,463,821 |
| 8 | H/Mji Kibaha | 32,048,848 |
| 9 | H/W Kibiti | 30,484,900 |
| 10 | H/M Mpanda | 29,691,462 |
| 11 | H/W Bumbuli | 26,988,592 |
| 12 | H/M Musoma | 23,362,250 |
| 13 | H/W Kakonko | 19,512,116 |
| 14 | H/W Handeni | 18,437,446 |
| 15 | H/M Iringa | 8,979,969 |
| **Jumla** | | **935,003,709** |

Upungufu wa mfumo wa udhibiti wa ndani katika usimamizi wa akaunti za amana kwenye mamlaka za serikali za mitaa huchangiwa na usimamizi usioridhisha na malipo yasiyodhibitiwa kutoka katika akaunti hizo.

Kuendelea kutumia fedha za akaunti za amana kwa utekelezaji wa shughuli zisizokusudiwa kunaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma, kuongezeka kwa mzigo wa madai ya waweka amana kwa mamlaka za serikali za mitaa, pamoja na kuchafua taswira ya taasisi hizo.

**Ninapendekeza kuwa OR-TAMISEMI izielekeze menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuimarisha mfumo wa udhibiti katika usimamizi wa akaunti ya amana ili kuendana na matakwa ya sheria na miongozo inayosimamia matumizi ya fedha za akaunti za amana.**

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuweka mikakati ya kurejesha fedha za amana zilizotumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa; pia kuhakikisha kuwa akaunti za amana zina fedha za kutosha kukidhi madai ya waweka amana.**

**Pia, mamlaka za serikali za mitaa zinahimizwa kuhakikisha kuwa uhamisho wa fedha kutoka kwenye akaunti ya mapato ya ndani kwenda kwenye akaunti za matumizi unazingatia miongozo na maelekezo yaliyopo, isipokuwa kwa sababu maalumu inayoweza kuthibitishwa. Fedha kutoka katika akaunti ya mapato ya ndani zinapaswa kuhamishiwa kwenye akaunti ya mfuko wa pamoja na**

**akaunti ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya matumizi kufanyika katika akaunti hizo.**

## 7.2 Malipo yasiyo na stakabadhi za kielektroni Sh. bilioni 7.42

Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Utozaji wa Kodi, Sura ya 438 [iliyorekebishwa mwaka 2019] kinamtaka mtu ambaye anasambaza bidhaa, anatoa huduma au anayepokea malipo kuhusiana na usambazaji wa bidhaa au huduma aliyotoa, kutoa stakabadhi au ankara kwa kutumia mashine za kielekitroni.

Kinyume na kifungu cha sheria tajwa, nilibaini malipo ya Sh. bilioni 7.42 yaliyolipwa na mamlaka 65 za serikali za mitaa kwa wazabuni, wakandarasi, na watoahuduma wengine bila kudai stakabadhi za kielekitroni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 58**.

Kushindwa kuomba stakabadhi za kielekitroni kunahamasisha ukwepaji wa kodi, hatimaye kuzuia Serikali kukusanya mapato.

**Jedwali Na. 58: Malipo yasiyo na stakabadhi za kielektroni**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Butiama | 539,943,471 | 33. | H/Mji Tarime | 67,394,530 |
| 2. | H/W Namtumbo | 442,983,002 | 34. | H/W Rombo | 65,009,369 |
| 3. | H/W Kigoma | 390,568,314 | 35. | H/W Nsimbo | 63,036,374 |
| 4. | H/W Nyasa | 348,474,782 | 36. | H/W Kilindi | 54,710,000 |
| 5. | H/Mji Tunduma | 343,006,350 | 37. | H/W Simanjiro | 53,001,519 |
| 6. | H/M Kigoma/Ujiji | 296,533,706 | 38. | H/W Ukerewe | 45,153,120 |
| 7. | H/W Musoma | 289,331,523 | 39. | H/W Bahi | 44,978,149 |
| 8. | H/M Musoma | 258,930,104 | 40. | H/W Pangani | 44,668,403 |
| 9. | H/Jiji Mwanza | 255,697,760 | 41. | H/W Handeni | 44,193,142 |
| 10. | H/W Mbozi | 240,579,632 | 42. | H/W Kyela | 40,149,914 |
| 11. | H/W Nanyamba | 238,874,442 | 43. | H/Mji Kibaha | 40,057,442 |
| 12. | H/W Kongwa | 195,144,974 | 44. | H/W Momba | 39,805,874 |
| 13. | H/Mji Mbinga | 194,478,080 | 45. | H/W Bariadi | 37,108,584 |
| 14. | H/W Tarime | 193,993,121 | 46. | H/W Msalala | 36,855,502 |
| 15. | H/W Bunda | 190,275,260 | 47. | H/W Rufiji | 33,206,765 |
| 16. | H/W Songea | 182,045,988 | 48. | H/W Tandahimba | 29,778,959 |
| 17. | H/W Madaba | 169,181,346 | 49. | H/W Ngorongoro | 29,041,900 |
| 18. | H/M Mtwara | 147,426,681 | 50. | H/W Ileje | 28,640,250 |
| 19. | H/W Meatu | 146,934,581 | 51. | H/W Urambo | 25,774,980 |
| 20. | H/W Nanyumbu | 146,677,514 | 52. | H/W Ushetu | 18,715,856 |
| 21. | H/W Sengerema | 142,664,907 | 53. | H/W Misungwi | 18,443,755 |
| 22. | H/W Bukombe | 135,532,200 | 54. | H/W Igunga | 17,100,000 |
| 23. | H/M Singida | 130,387,030 | 55. | H/W Mbulu | 15,713,000 |
| 24. | H/W Chamwino | 99,039,414 | 56. | H/W Kilolo | 13,600,760 |
| 25. | H/W Busega | 97,546,225 | 57. | H/Mji Bariadi | 12,474,942 |
| 26. | H/W Malinyi | 81,692,129 | 58. | H/M Mpanda | 12,165,980 |
| 27. | H/Jiji Mbeya | 79,893,536 | 59. | H/W Maswa | 10,959,629 |

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 28. | H/W Iramba | 79,847,204 | 60. | H/W Mkalama | 10,939,500 |
| 29. | H/W Nyang'hwale | 79,822,325 | 61. | H/W Itilima | 10,495,534 |
| 30. | H/W Chato | 75,083,000 | 62. | H/W Mpwapwa | 8,674,750 |
| 31. | H/Mji Kasulu | 75,068,110 | 63. | H/W Newala | 8,089,239 |
| 32. | H/W Mpimbwe | 70,601,470 | 64. | H/W Kondoa | 7,948,897 |
| | H/W Rungwe | 70,452,000 | **Jumla** | | **7,416,596,798** |

Pia, nilibaini kuwapo kwa malipo yenye thamani ya Sh. milioni 147.29 yaliyothibitishwa na stakabadhi bandia za kielekitroni katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

**Ninapendekeza, OR-TAMISEMI ishirikiane na Wizara ya Fedha na mamlaka ya Mapato (TRA) kuhuisha mfumo wa ulipaji serikalini (MUSE) na mfumo wa kodi, ambapo taasisi za umma zitaweza kujiridhisha na taarifa za kikodi za wazabuni na watoa huduma mbalimbali waliosajiliwa na TRA pamoja na kuthibitisha usahihi wa makato ya kodi kabla ya kuidhinisha malipo yao.**

**Pia, ninaishauri TRA kuongeza ufuatiliaji wa kubaini wafanyabiashara wasio waaminifu ambao hawatoi stakabadhi za kielekitroni na kuwachukulia hatua stahiki kwa mujibu wa sheria ya kodi.**

### 7.3 Matumizi yasiyo na tija Sh. milioni 787.49

Matumizi ambayo taasisi ya umma haijapata thamani ya fedha iliyolipa ni malipo yasiyo na manufaa. Malipo haya yanajumuisha kulipa gharama za tozo, adhabu au riba kwa kushindwa kuzingatia vipengele vya mikataba, malipo zaidi ya thamani ya huduma iliyopatikana na ulipaji wa posho kwa watumishi kwa shughuli ambazo hazikufanyika. Hii inasisitizwa zaidi chini ya kanuni ya 21(2) ya Kanuni za Fedha za Umma, (Tangazo la Serikali Na. 132 ya Mwaka 2001).

Nilibaini kuwa, mamlaka 23 za serikali za mitaa zilifanya malipo ya Sh. milioni 787.49 kwa shughuli zisizokuwa na tija. Orodha ya taasisi na kiasi kilicholipwa imeoneshwa kwenye **Jedwali Na.59**.

**Jedwali Na. 59: Matumizi yasiyo na tija**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kigoma | 132,666,933 | | H/W Serengeti | 24,348,000 |
| 2. | H/M Ilemela | 109,097,034 | 14. | H/W Kilindi | 20,845,800 |
| 3. | H/M Temeke | 69,263,976 | 15. | H/M Kigoma/Ujiji | 19,182,241 |
| 4. | H/Jiji Dodoma | 45,457,915 | 16. | H/W Kongwa | 17,630,000 |
| 5. | H/M Kigamboni | 43,932,203 | 17. | H/W Ukerewe | 14,589,763 |
| 6. | H/Jiji Mwanza | 39,268,593 | 18. | H/W Ikungi | 13,134,423 |
| 7. | H/Jiji Mbeya | 36,811,200 | 19. | H/W Mkalama | 11,000,000 |
| 8. | H/W Manyoni | 35,139,663 | 20. | H/W Chemba | 9,933,000 |

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 9. | H/M Musoma | 35,000,000 | 21. | H/W Muheza | 7,786,280 |
| 10. | H/W Kaliua | 33,125,301 | 22. | H/W Mbinga | 7,465,646 |
| 11. | H/W Simanjiro | 28,690,704 | 23. | H/W Meatu | 7,271,600 |
| 12. | H/M Singida | 25,845,390 | | **Jumla** | **787,485,665** |

Kufanyika kwa matumizi yasiyo na tija kunatokana na upungufu katika mfumo wa kudhibiti matumizi hivyo kusababisha kufanya malipo zaidi ya huduma iliyotolewa, adhabu kwa kuchelewesha malipo mbalimbali, kutowasilishwa kwa makato ya watumishi kwa wakati, na malipo kwa shughuli ambazo hazijatekelezwa.

Matumizi yasiyo na tija huathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na taasisi. **Jedwali Na.60** linaonesha mwenendo wa matumizi yasiyo na tija kwa miaka mitatu mfululizo.

**Jedwali Na. 60: Mwenendo wa matumizi yasiyo na tija**

| Na. | Mwaka wa Fedha | Idadi ya Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 2022/23 | 23 | 787,485,665 |
| 2 | 2021/22 | 9 | 898,848,336 |
| 3 | 2020/21 | 24 | 664,001,836 |

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI ihakikishe kuwa mamlaka za serikali za mitaa zinazuia kujirudia kwa matumizi yasiyo na tija kwa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani katika usimamizi wa matumizi; uwasilishwaji makato ya watumishi kwa wakati; na kuzingatia sheria na kanuni katika kufanya uamuzi hivyo malipo kufanyike kwa shughuli halali tu.**

**Pia, hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya maofisa wote wanaohusika na matumizi yasiyo na tija, ikiwamo kuripoti masuala hayo kwa vyombo vya uchunguzi pale inapofaa.**

## 7.4 Malipo yaliyofanyika kwa fedha taslimu Sh. bilioni 1.44

Aya ya 6.7.3 ya mwongozo wa uhasibu wa mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2019 inazitaka mamlaka za serikali za mitaa kufanya malipo yote kwa njia ya kielekitroni katika akaunti ya benki ya mlipwaji, kwa hali yoyote ile mamlaka isilipe kwa hundi au fedha taslimu.

Nilibaini kuwa mamlaka 16 za serikali za mitaa zilifanya malipo yenye thamani ya Sh. bilioni 1.44 kwa fedha taslimu kwa walipwaji mbalimbali, wakiwamo wazabuni na watumishi, kinyume na takwa la mwongozo uliobainishwa.

Ukiukwaji wa taratibu ulitokana na mfumo wa udhibiti wa ndani kutokuwa imara katika uidhinishwaji wa malipo kwenye mamlaka za serikali za mitaa pamoja na baadhi ya mafundi wa ujenzi kutokuwa na akaunti za benki. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zenye malipo taslimu imeoneshwakwenye **Jedwali Na.61**.

**Jedwali Na. 61: Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslimu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dar es Salaam | 253,800,000 |
| 2 | H/W Kondoa | 252,642,112 |
| 3 | H/W Sikonge | 167,304,200 |
| 4 | H/W Kigoma | 153,245,024 |
| 5 | H/W Nkasi | 117,429,000 |
| 6 | H/W Ikungi | 109,482,000 |
| 7 | H/W Sumbawanga | 108,101,700 |
| 8 | H/W Chemba | 60,823,800 |
| 9 | H/W Kwimba | 55,664,512 |
| 10 | H/W Kilindi | 39,100,000 |
| 11 | H/W Arusha | 30,033,696 |
| 12 | H/Mji Kasulu | 26,060,000 |
| 13 | H/W Mpimbwe | 25,642,330 |
| 14 | H/W Urambo | 20,330,000 |
| 15 | H/W Mpanda | 16,511,000 |
| 16 | H/Manispaa Mpanda | 6,063,610 |
| **Jumla** | | **1,442,232,984** |

Ni maoni yangu kwamba, kufanya malipo ya fedha taslimu kunashawishi matumizi mabaya ya fedha za umma. Pia, kunashawishi wazabuni kutolipa kodi stahiki kwa ununuzi nayofanyika.

**Ninapendekeza kwamba OR-TAMISEMI iziagize menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa husika kuzingatia sheria zilizopo wakati wa kufanya malipo kwa wazabuni, mafundi ujenzi, na watumishi ili kuzuia kujirudia kwa ukiukwaji wa taratibu ulioonekana.**

**Pia, ninashauri kuimarishwa kwa majukumu ya kitengo cha ukaguzi wa awali katika mchakato wa malipo pamoja na kufanyika kwa ukaguzi wa mara kwa mara na kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kubaini udhaifu, kutathmini uzingatiaji wa sera na taratibu.**

### 7.5 Kodi ya zuio kutowasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Sh. bilioni 1.74

Kifungu cha 83 (A) na Aya ya 4(c) (v) cha Jedwali la 1 la Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332, kinataka kila taasisi kukatwa 2% kwa bidhaa na 5% kwa huduma zinazotolewa kwa taasisi za Serikali na kiasi kilichozuiliwa kutumwa kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato.

Nilibaini mamlaka 43 za serikali za mitaa zikiwa na deni la makato ya kodi ya zuio kiasi cha Sh. bilioni 1.74. Kiasi hiki kilikuwa kimeorodhesha kwenye orodha ya madeni katika taarifa za hesabu zinazoishia 30 Juni 2023. Deni hilo lilitokana na makato ya kodi ya zuio kutoka kwa wazabuni ambayo hayakuwasilishwa TRA kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.62**.

**Jedwali Na. 62: Kodi ya zuio isiyowasilishwa TRA**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/M Shinyanga | 378,471,592 | 23 | H/W Mpanda | 14,260,129 |
| 2 | H/W Kongwa | 185,034,008 | 24 | H/Mji Nzega | 13,908,049 |
| 3 | H/Jiji Mwanza | 156,905,902 | 25 | H/W Manyoni | 13,762,246 |
| 4 | H/W Chalinze | 126,713,188 | 26 | H/W Mafia | 13,432,015 |
| 5 | H/Jiji Arusha | 77,107,899 | 27 | H/W Ulanga | 12,872,940 |
| 6 | H/W Nyasa | 70,038,844 | 28 | H/M Mtwara | 12,070,874 |
| 7 | H/W Uvinza | 64,592,000 | 29 | H/M Moshi | 11,199,005 |
| 8 | H/W Msalala | 64,009,805 | 30 | H/W Kalambo | 10,100,688 |
| 9 | H/W Kwimba | 53,090,481 | 31 | H/W Butiama | 9,917,680 |
| 10 | H/Mjin Geita | 48,337,517 | 32 | H/W Madaba | 9,518,366 |
| 11 | H/W Kibaha | 46,801,175 | 33 | H/W Mpwapwa | 9,441,664 |
| 12 | H/W Tarime | 34,419,451 | 34 | H/W Korogwe | 9,056,502 |
| 13 | H/W Shinyanga | 33,325,701 | 35 | H/M Ilemela | 7,965,758 |
| 14 | H/M Mpanda | 31,738,663 | 36 | H/M Morogoro | 7,662,302 |
| 15 | H/W Arusha | 27,082,650 | 37 | H/W Ileje | 7,649,190 |
| 16 | H/W Mbogwe | 25,060,972 | 38 | H/W Kiteto | 7,301,717 |
| 17 | H/W Mbogwe | 25,060,972 | 39 | H/Mji Korogwe | 7,000,000 |
| 18 | H/W Bariadi | 20,954,485 | 40 | H/M Kahama | 6,353,256 |
| 19 | H/W Hai | 19,157,200 | 41 | H/W Kasulu | 6,313,917 |
| 20 | H/W Kilwa | 18,621,369 | 42 | H/W Misungwi | 6,028,817 |
| 21 | H/Mji Kibaha | 17,843,838 | 43 | H/W Kishapu | 5,710,217 |
| 22 | H/W Bahi | 17,544,280 | | **Jumla** | **1,743,437,324** |

Kukosekana kwa jitihada za makusudi kwa menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa juu ya kuwasilisha kodi za zuio kwa wakati TRA ndiyo sababu ya kutowasilishwa kwa kodi hiyo. Pia, kuna uwezekano kuwa kodi iliyozuiwa imetumika kwa shughuli zisizokusudiwa.

Kutowasilisha kodi ya zuio kunaikosesha Serikali mapato muhimu ambayo inategemea kugharamia huduma za umma na miradi ya miundombinu.

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kufanya mapitio ya kina ya mifumo ya udhibiti wa ndani inayohusiana na makato ya kodi ya zuio pamoja na uwasilishwaji wake katika Mamlaka ya Mapato Tanzania. Pia, kufuatilia kodi ya zuio isiyowasilishwa na kuhakikisha inawasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuepuka adhabu inayotokana na kuchelewa au kutopeleka kodi ya zuio.**

### 7.6 Kutodhibitiwa kwa matumizi ya mkopo kulikopelekea ongezeko la madeni ya wazabuni na watumishi kwa kiasi cha Sh. bilioni 22.45

Waraka wa Hazina Na.1 wa mwaka 2018/19 wenye Na. CBC.187/575/01/37 unawataka maofisa masuuli wote kutenga fedha kwenye bajeti kwa ajili ya malipo ya madeni yaliyohakikiwa na kuthibitishwa; na kudhibiti kuongeza madeni kutoka kwa wazabuni, wakandarasi na watumishi.

Ukaguzi wangu wa mamlaka 37 za serikali za mitaa ulibaini ongezeko la madeni ya wazabuni na watumishi kutoka Sh. bilioni 64.87 zilizoripotiwa katika mwaka wa fedha 2021/22 hadi Sh. bilioni 87.33 katika mwaka wa fedha 2022/23 na kusababisha ongezeko la Sh. bilioni 22.45 sawa na 35%.

Aidha, nilibaini kuwa katika ongezeko la Sh. bilioni 22.45, Sh. bilioni 9.46 zilitokana na kazi za ujenzi na wazabuni, likiwa ongezeko la 33% kutoka katika kundi la madeni, na Sh. bilioni 12.99 sawa na 36% ikiwa kundi la madeni yatokanayo na stahiki za watumishi kama inavyochambuliwa **Kiambatisho Na.17.**

Ongezeko la madeni limechangiwa zaidi na matumizi yasiyoendana na hali ya kifedha ya taasisi na kucheleweshwa kwa malipo. Hili pia linachangiwa na gharama zinazoingiwa wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na gharama za uendeshaji wa ofisi.

Kwa kiasi kikubwa, madeni ya watumishi hutokana na kutolipwa kwa stahiki za watumishi kama vile posho ya likizo, marejesho ya matibabu, posho ya huduma mbalimbali kwa maofisa wanaostahiki, posho ya mizigo, posho ya kujikimu, posho zingine zinazohusika wakati wa kustaafu au uhamisho, na malimbikizo ya mishahara.

Maoni yangu ni kuwa, kutodhibiti ongezeko la madeni ya wazabuni, wakandarasi, na madeni yatokanayo na stahiki za watumishi, huongeza mzigo kwa Serikali. Pia, huathiri bajeti kwa ajili ya ulipaji wa madeni na kupunguza uaminifu wa wazabuni na wakandarasi kwa taasisi. Aidha,

kutokulipwa kwa madeni yatokanayo na stahiki za watumishi husababisha kupungua kwa ari ya watumishi katika kufanya kazi.

**Napendekeza kuwa Serikali iendelee kutoa kipaumbele kwa kulipa madeni ya wazabuni, wakandarasi na watumishi. Aidha, hatua madhubuti zichukuliwe kuzuia ukuaji wa madeni ya serikali yanayotokana na kazi za ujenzi, usambazaji wa bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni na wakandarasi pamoja na madai ya watumishi.**

# SURA YA NANE




# USIMAMIZI WA RASILIMALIWATU NA MISHAHARA

## 8.0 Utangulizi

Sura hii inasisitiza masuala yanayohusiana na usimamizi wa rasilimaliwatu, ikiwamo usimamizi wa mishahara, posho, faida, na malimbikizo kwa watumishi katika mamlaka za serikali za mitaa.

Licha ya kuwa sababu muhimu inayohamasisha utoaji wa huduma kwa ufanisi katika mamlaka za serikali za mitaa, usimamizi wa rasilimaliwatu unakabiliana na changamoto zifuatazo:

## 8.1 Madai ya watumishi ambayo hayajalipwa - Sh. bilioni 36.47

Kanuni Na. E.23 ya Mwongozo wa Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inataka pale mfanyakazi yeyote wa serikali anapopandishwa daraja au kuteuliwa kwenye nafasi ya kiwango cha juu kwa tarehe ya nyuma, atalipwa malipo ya nyongeza ya mshahara yanayomstahiki, ambayo atatoa posho ya muda ambayo tayari ameshalipwa ambayo sasa hayampasi kutokana na tarehe halisi ya uteuzi au kupandishwa daraja kwake.

Nilipitia mafaili ya watumishi, nyaraka zinazohusiana na madai ya watumishi, na kufanya mahojiano na maofisa rasilimaliwatu katika mamlaka 54 za serikali za mitaa. Nilibaini kuwa kulikuwa na madai ya watumishi yaliyosalia yenye thamani ya Sh. bilioni 36.47 ambayo hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12.

Haya yanajumuisha malimbikizo ya mishahara ya watumishi, wastaafu, na madai mengine kama posho za kisheria kwa viongozi wa idara na vitengo. Maelezo yanapatikana kwa muhtasari katika **Jedwali Na.63** na **Kiambatisho Na.18**.

**Jedwali Na. 63: Madai ya watumishi yasiyolipwa**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|
| Malimbikizo ya Mishahara | 11,420,214,782 |
| Madai Mengine (likizo, kukaimu, kujikimu, safari, uhamisho na posho za kisheria) | 24,341,616,670 |
| Wastaafu | 708,111,184 |
| **Jumla** | **36,469,942,636** |

Kutokuwapo kwa mgao wa kutosha wa fedha kwa mamlaka za serikali za mitaa na serikali kwa ajili ya matarajio ya kupandishwa vyeo, kuajiri watumishi wapya, posho za kisheria (kama vile posho za kukaimu, posho za kujikimu), na madai mengine ya watumishi, kulichangia upungufu uliobainishwa.

Madai hayo yanaongeza madeni kwa mamlaka za serikali za mitaa. Pia, yanaweza kudhoofisha ari ya watumishi katika kutoa huduma kwa ufanisi.

**Ninapendekeza kwamba mamlaka za serikali za mitaa husika kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Hazina zitoe fedha kwa ajili ya kulipa madai ya watumishi ili kuepuka malimbikizo ya madeni.**

### 8.2 Makato ya mishahara kutowasilishwa katika taasisi husika - Sh. bilioni 36.09

Kifungu cha 18 (1) (b) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma ya mwaka 2018 kinahitaji waajiri kuchangia kiasi kinacholingana na 15% ya mshahara wa kila mwezi wa mwanachama uliochangiwa kwenye akaunti ya mwanachama na mwajiri.

Watumishi wa mamlaka za serikali za mitaa hulipwa mishahara ambayo hujumuisha makato ya kisheria na yale ambayo si ya kisheria. Makato haya ni pamoja na michango kwa taasisi kama vile Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma (PSSSF), Kodi ya Mapato, Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF), marejesho ya mikopo kwa taasisi za kifedha, Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS), na michango kwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.

Makato hayo hukatwa kwenye chanzo na taarifa kupelekwa katika mamlaka za serikali za mitaa husika. Kwa upande wa watumishi ambao wanalipwa mishahara kutoka katika mapato ya ndani, mishahara yao hukatwa katika ngazi ya halmashauri husika.

Nimebaini kwamba mamlaka 46 za serikali za mitaa hazikuwasilisha makato jumla ya Sh. bilioni 36.09 kwa taasisi husika. Kati ya fedha zisizowasilishwa, Sh. bilioni 3.59 ilikuwa kwa ajili ya PSSSF.

Nimebaini kuwa, kucheleweshwa kuwasilisha makato kwa taasisi husika kumesababisha serikali kupata hasara kwa kulipa faini yenye thamani ya Sh. bilioni 32.08 kupitia katika mamlaka 56 za serikali za mitaa. Kiasi ambacho hakijachangiwa kwa mwaka ulioishia 2022/23 kimeoneshwa katika **Jedwali Na.64** na **Kiambatisho Na.19.**

**Jedwali Na. 64: Makato kutowasilishwa katika taasisi husika**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---:|
| Mfuko ya Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma | 3,594,289,922 |
| Adhabu/Tozo | 32,075,513,149 |
| Kodi ya Mapato | 51,006,301 |
| Bima ya Afya ya Taifa | 40,550,453 |
| Mfuko ya Hifadhi ya Jamii | 54,585,990 |
| Mfuko wa fidia kwa wafanyakazi | 204,834,010 |
| Taasisi zingine | 68,566,144 |
| **Jumla** | **36,089,345,969** |

Hii inasababisha matumizi yasiyokuwa ya tija kwa serikali ambayo yangeweza kutumika kutekeleza miradi au huduma zingine kwa umma.

Kushindwa kwa mamlaka za serikali za mitaa kuwasilisha kwa kawaida makato haya, hususani kwa mfuko wa PSSSF, kumekuwa na athari mbaya kwa maofisa wanaostaafu, kwani mafao yao ya kustaafu hayawezi kulipwa kwa wakati.

**Ninatoa msisitizo kwa mamlaka za serikali za mitaa husika kuhakikisha kuwa makato ambayo hayakuwasilishwa yanalipwa mara moja kwa taasisi husika bila kuchelewa zaidi ili kuepuka matumizi yasiyokuwa ya lazima kwa kutozwa faini.**

## 8.3 Kutofautiana tarehe ya kuzaliwa kwa Takwimu za mishahara na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa NIDA kwa wafanyakazi 76,536

Taarifa ya mishahara ni muhimu kwa kuhakikisha ustawi wa kifedha wa wafanyakazi, kuzingatia mahitaji ya kisheria, na kukuza uaminifu wa kazi kwa watumishi. Taarifa hizo zina umuhimu katika kusaidia maisha ya watumishi.

Kuwa na rekodi sahihi na zilizohifadhiwa vizuri za mishahara kunaweza kuonesha kuwa waajiri wanathamini kipato cha watumishi wao.

Taarifa za NIDA ni muhimu kwa uthibitisho wa utambulisho, utoaji wa huduma, usalama, kifedha, utawala, na mchakato wa uchaguzi. Kwa kuhifadhi taarifa sahihi na kamili ya raia, mamlaka ya NIDA inachangia katika maendeleo, ufanisi, na uwazi katika sekta mbalimbali. Pia, inaimarisha ustawi wa kijamii na kiuchumi wa nchi.

Agizo C.19 (1) la Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 linasema kwamba taarifa kamili na sahihi na kumbukumbu za utumishi za watumishi wote wa umma lazima zitunzwe katika OR-Utumishi, katika asasi ya mtumishi wa umma, na makao makuu. Tahadhari lazima ichukuliwe ili kuhakikisha kwamba wakati wowote mawasiliano yanapopelekwa Hazina au ofisi yenye dhamana ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma au Tume ya Utumishi wa Umma kuhusu mtumishi binafsi wa umma na pale ambapo mawasiliano haya yana uhusiano na masharti ya utumishi wa mtumishi wa umma, lazima zitolewe taarifa sahihi.

Ukaguzi wa taarifa za mishahara za Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS) na taarifa ya Mamlaka ya kitambulisho cha Kitaifa “NIDA” ulibaini tofauti kubwa ya taarifa hizo mbili. Taarifa za malipo kuhusu tarehe za kuzaliwa zilizohifadhiwa kwenye HCMIS kwa watumishi 76,536 hazilingani na taarifa husika zilizohifadhiwa katika mfumo wa NIDA; hivyo kusababisha kuwa na utata kuhusu tarehe za kuzaliwa za watumishi wa umma.

Aidha, nilibaini kuwa kati ya watumishi 81 wa mamlaka za serikali za mitaa hawakuwa na taarifa za NIDA katika mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu. Kutokuwapo kwa taarifa za NIDA za watumishi kunaweza kusababisha kutokuwa na taarifa sahihi za mtumishi; hivyo kusababisha uongozi wa mamlaka za serikali za mitaa kushindwa kufuatilia na kusimamia kwa usahihi taarifa za watumishi hao katika Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu. Maelezo yamefupishwa katika **Kiambatisho Na.20**.

Kutofautiana huku kunaleta wasiwasi kuhusu usahihi na ukweli wa tarehe za kuzaliwa za watumishi zilizopo kwenye taarifa za malipo ya mfumo wa HCMIS na zile za NIDA. Maelezo yasiyo sahihi ya tarehe ya kuzaliwa ya wafanyakazi husababisha kutokutambuliwa kwa watumishi, makosa

katika malipo ya mishahara, na changamoto katika kuandaa mafao kwa watumishi wanaostaafu.

**Ninatoa ushauri kwa mamlaka za serikali za mitaa husika, kwa kushirikiana na OR-Utumishi, kufanya ukaguzi wa taarifa ili kulinganisha tarehe za kuzaliwa zilizopo kwenye mfumo wa HCMIS na zile za NIDA kwa watumishi wote waliorodheshwa ili kuepusha utata wa tarehe zao za kuzaliwa. Pia, ni muhimu kuchukua hatua za haraka za kukusanya na kuingiza taarifa za NIDA kwa watumishi ambao kwa sasa hawana taarifa hizo kwenye mfumo wa HCMIS.**




# SURA YA TISA

# TATHMINI YA UTAWALA BORA, MIFUMO YA NDANI NA USIMAMIZI WA VIHATARISHI

## 9.0 Utangulizi

Mamlaka za serikali za mitaa zimeelekezwa kuweka mifumo ya ndani yenye udhibiti imara ili kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinasimamiwa kikamilifu kama ilivyoagizwa chini ya Agizo la 11 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa la mwaka 2009.

Katika kutathmini mfumo wa utawala, udhibiti wa ndani na usimamizi wa vihatarishi katika mamlaka za serikali za mitaa, nimebaini maeneo kadhaa yanayohitaji kuangaliwa zaidi ili kufikia malengo ya utawala bora kama yanavyo elezwa hapa chini:

## 9.1 Utawala

Katika mamlaka za serikali za mitaa, utawala ni mfumo wa sheria, taratibu na kanuni zinazoeleza namna mamlaka hizi zinavyosimamiwa na kudhibitiwa.

Utawala wa mamlaka za serikali za mitaa unaongozwa na mfumo wa kisheria unaobainisha mamlaka, kazi, na wajibu wa taasisi hizi. Mfumo huu unajumuisha sheria, kanuni na sera zilizowekwa na serikali kuu, pamoja na zile zinazohusu mamlaka za serikali za mitaa.

Yafuatayo ni mambo muhimu yaliyobainishwa katika utawala wa mamlaka za serikali za mitaa:

### 9.1.1 Kutokuwapo kwa kamati huru ya ukaguzi kama kitengo cha ushauri kwa wasimamizi wa mamlaka za serikali za mitaa

Kwa mujibu wa Agizo la 5 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, Baraza la Madiwani linawajibika kwa uamuzi wote ndani ya mamlaka za serikali za mitaa, ikiwamo masuala ya fedha. Aidha, Agizo la

12. (1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaeleza kwamba "katika kila mamlaka ya serikali za mitaa kutakuwa na kamati itakayojulikana kama Kamati ya Ukaguzi".

Tofauti na muundo wa utawala wa mashirika ya umma ambapo bodi ya wakurugenzi ina kamati huru za ukaguzi zenye wajumbe wenye taaluma ambao jukumu lao kubwa ni kuzishauri bodi, mamlaka za serikali za mitaa hazina utaratibu huo wa usimamizi. Badala yake, kamati za ukaguzi zilizopo ndani ya mamlaka za serikali za mitaa zinaripoti moja kwa moja kwa wakurugenzi watendaji.

Kutokana na hali hiyo, kuna upungufu mkubwa wa chombo huru cha ushauri wa kitaalamu kinachoangazia masuala ya fedha na ukaguzi wa ndani na nje ambacho huripoti moja kwa moja kwa wale wanaohusika na utawala, ambao katika hili ni baraza la madiwani.

Hii inatia shaka kwa kuwa wajumbe wa baraza hawana ulazima wa kuwa na taaluma yoyote, ama ujuzi wa masuala ya fedha, kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 39(2) a-h cha Sheria ya Uchaguzi ya Mamlaka ya Mitaa.

Hali hii inaleta wasiwasi kuhusu ufanisi wa usimamizi wa fedha ndani ya mamlaka za serikali za mitaa.

**Ninashauri OR-TAMISEMI ifanye mapitio ya kina ili kutathmini kama wajibu na majukumu yaliyokabidhiwa kwa wenye dhamana ya utawala katika halmashauri yanaendana na matakwa ya kisheria ya viwango vya taaluma. Ni muhimu kuweka kipaumbele katika uanzishwaji wa kamati za ukaguzi ili kuzisaidia halmashauri kuimarisha utawala na usimamizi wa fedha. Kamati hizi zinapaswa kutoa ushauri bila upendeleo katika masuala ya ukaguzi, kukuza uwazi, uwajibikaji, na kufanya uamuzi wenye tija ndani ya mfumo wa serikali za mitaa.**

### 9.1.2 Upungufu katika utendaji wa Kamati za Ukaguzi

Agizo la 12 (1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaelekeza kuwa katika kila halmashauri kutakuwa na kamati ya ukaguzi ambayo majukumu yake muhimu ni pamoja na kuziwezesha serikali za mitaa kufikia wajibu wake wa kiutawala na usimamizi kuhusiana na taarifa za fedha, udhibiti wa mifumo ya ndani, mfumo wa usimamizi wa vihatarishi, kazi za ukaguzi wa ndani na nje, pamoja na uwajibikaji wa kimaadili.

Nilifanya mapitio ya kamati za ukaguzi katika halmashauri na kubaini dosari zifuatazo:

(i) Kamati za ukaguzi katika mamlaka 13 za serikali za mitaa hazikutayarisha na kuwasilisha taarifa za mwaka kwa waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa, mkuu wa mkoa, na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyobainishwa katika Agizo la 12(5)(g) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Kitendo hiki kimesababisha mamlaka husika kutokupata taarifa za moja kwa moja juu ya majukumu yaliyotekelezwa na kamati.

(ii) Kamati za ukaguzi zilijikita katika masuala ya ukaguzi badala ya kutathmini mifumo ya udhibiti wa ndani ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali na uzingatizi wa sheria na kanuni, hivyo kuhakikisha usahihi wa taarifa za fedha. Nilibaini mamlaka saba za serikali za mitaa ambazo hazikupitia taarifa za fedha.

(iii) Mamlaka tano za serikali za Mitaa hazikufanya mafunzo elekezi kwa wajumbe wapya wa kamati ya ukaguzi ili kuwafanya waelewe majukumu yao na kazi za kamati kwa ujumla. Pia, mamlaka za serikali za mitaa tisa hazikutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wake. Kutokuwapatia wajumbe hao mafunzo elekezi kumesababisha wajumbe wapya kushindwa kutoa michango ya mawazo yao kwa kamati, kuwajengea uwezo, na kuwaongeza ujuzi.

(iv) Mamlaka 14 za serikali za mitaa hazikufanya vikao vya kamati za ukaguzi. Kwa wale waliofanya vikao, msisitizo mkubwa ulikuwa kupitia na kujadili ripoti za ukaguzi wa ndani. Mambo mengine yaliyobainishwa katika miongozo ya kamati ya ukaguzi kama vile mapitio ya ufanisi wa mfumo wa usimamizi wa vihatarishi na ufuatiliaji wa mazingira ya udhibiti wa mifumo ya ndani hayakuzingatiwa.

Upungufu uliobainika unaweza kuzuia kamati za ukaguzi husika kufikia malengo yao ya kutoa uhakika wa udhibiti wa mifumo ya ndani ili kuwezesha mamlaka za utawala kufikia malengo ya utendaji na usimamizi wa rasilimali. **Jedwali Na.65** chini linaelezea kasoro zilizobainishwa:

**Jedwali Na. 65: Upungufu katika utendaji wa kamati za ukaguzi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kutokuandaliwa kwa taarifa za mwaka | Kamati za ukaguzi kutokupitia taarifa za fedha | Kutokufannyika kwa Mafunzo /semina kwa wajumbe wapya | Kutokufanyika kwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe waliokuwapo | Kutokufanyika kwa mikutano ya kamati |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Hai | | x | | X | X |
| 2. | H/W Kigoma | | | X | X | x |
| 3. | H/W Kishapu | X | | | | |
| 4. | H/W Kongwa | X | | | | X |
| 5. | H/M Mpanda | | X | | | X |
| 6. | H/W Mpwapwa | X | | | | X |
| 7. | H/W Ngorngoro | X | | | | X |
| 8. | H/W Nzega | X | | | | X |
| 9. | H/W Pangani | | | | X | X |
| 10. | H/W Rombo | | X | X | X | |
| 11. | H/W Bagamoyo | | x | x | X | |
| 12. | H/W Chamwino | X | X | | | |
| 13. | H/W Kaliua | X | X | | | X |
| 14. | H/W Longido | | | | | X |
| 15. | H/W Mkuranga | X | | | X | X |
| 16. | H/W Morogoro | X | | | | |
| 17. | H/W Mpanda | X | | | | X |
| 18. | H/W Mpimbwe | | | X | X | |
| 19. | H/M Tabora | X | | | X | |
| 20. | H/W Kakonko | X | | | X | |
| 21. | H/W Songea | X | | | | X |
| 22. | H/W Kisarawe | | X | X | | X |

**Ninashauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa husika kuziwezesha kamati za ukaguzi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuzipatia rasilimali za kutosha na kufanya mafunzo ya mara kwa mara.**

### 9.1.3 Upungufu katika utendaji na vitendea kazi katika kitengo cha ukaguzi wa ndani

Kifungu cha 48 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kinaitaka halmashauri kuwa na wakaguzi wa ndani ambao watafanya kazi kwa karibu na wakuu wa idara na watatoa taarifa moja kwa moja kwa ofisa masuuli.

Agizo la 13 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa la mwaka 2009 linafafanua ukaguzi wa ndani kuwa kitengo huru cha kufanya tathmini ya udhibiti wa mifumo ya ndani ya mamlaka za serikali za mitaa kwa kuchunguza na kutathmini ufanisi na utoshelevu wa mifumo hiyo.

Nimefanya tathmini ya utendaji wa vitengo vya ukaguzi wa ndani kwa kulinganisha na kuwapo kwa vitendea kazi na kubaini kuwa bado vitengo vya ukaguzi wa ndani vina changamoto za uhaba wa rasilimali muhimu jambo linaloathiri ufanisi katika kutekeleza majukumu yao. Nilibaini uhaba wa rasilimaliwatu kwa kiwango cha watumishi 73 katika mamlaka 36 za serikali za mitaa, uhaba wa bajeti kwa asilimia tatu hadi 100% katika mamlaka 29 za serikali za mitaa, na kutokupata mafunzo ili kuongeza ujuzi katika mamlaka 23 za serikali za mitaa.

Kukosekana kwa rasilimali muhimu kunaweza kusababisha kushindwa kubaini viashiria vya hatari kama vile ubadhirifu, ukiukwaji wa sheria na ufanisi usioridhisha katika utendaji hivyo kuziweka mamlaka za serikali za mitaa katika hatari ya kupata hasara.

Halmashauri zenye upungufu uliobainishwa zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na.21.**

**Ninashauri menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, kufanya jitihada za upatikanaji wa rasilimali zitazowezesha vitengo vya ukaguzi wa ndani kutimiza malengo. Hii itawezesha vitengo vya ukaguzi wa ndani kufanya tathmini huru ya udhibiti wa mifumo ya ndani; hivyo kuboresha uwajibikaji kwa wale waliopewa dhamana ya kusimamia rasilimali za umma.**

## 9.2 Tathmini ya Udhibiti wa Mifumo ya Ndani na Viashiria Hatarishi

### 9.2.1 Mifumo ya udhibiti wa ndani kushindwa kugundua vihatarishi vya ubadhirifu vilivyoonekana katika malipo ya Sh. bilioni 1.23

Katika mapitio ya miamala ya malipo yaliyofanyika Kupitia Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) katika halmashauri ya wilaya Mpimbwe nilibaini malipo ya Sh.bilioni 1.23 yaliyofanyika kutoka akaunti ya mishahara (TSA-PE) kugharamia shughuli mbalimbali ambazo hazikufanyika.

Malipo haya yaliwezeshwa kupitia stakabadhi zisizokuwa halisi (dummy receipts) zilizotumwa katika Akaunti ya TSA - PE kufuatia malipo ya

mishahara kwa wafanyikazi, ambayo hufadhiliwa moja kwa moja na Hazina. Hatahivyo, halmashauri haikupitisha miamala ya ulinganifu wa hesabu ili kuingiza gharama ya mishahara katika akaunti ya mshahara. Badala yake, imefanya miamala ya malipo ambapo fedha taslimu zimelipwa kwa watu mbalimbali.

Upungufu huu katika mfumo wa MUSE uliruhusu malipo ya udanganyifu kufanyika, ikionesha kushindwa kwa mifumo ya udhibiti wa michakato ya uidhinishaji wa malipo, kulikowezesha baadhi ya maofisa kushirikiana katika kufanya udanganyifu. Maelezo ya malipo yamefafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 22**.

**Ninaishauri OR-TAMISEMI, na Wizara ya Fedha kushirikiana katika kuimarisha udhibiti wa mfumo kwa kuhakikisha hautoi mianya ya ubadhirifu uliotokea. Aidha, ni muhimu kwa OR-TAMISEMI kufanya uchunguzi wa kina katika mamlaka zote za serikali za mitaa nchi nzima na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wanaojihusisha na vitendo hivyo vya udanganyifu.**

### 9.2.2 Mapungufu ya muundo wa OR-TAMISEMI katika kusimamia Mfumo wa Malipo Serikalini (MUSE) na akaunti ya amana

Kwa mujibu wa Sura ya 2.5.4 ya Mwongozo wa Taratibu za fedha (2021) wa Mhasibu Mkuu wa Serikali, inapendekezwa kwamba, serikali iwekeze katika hatua za udhibiti wa ndani ili kugawa kazi kati ya maeneo tofauti, hivyo kupunguza uwezekano wa makosa, matumizi mabaya, na ubadhilifu, pamoja na kuimarisha uwajibikaji.

OR-TAMISEMI inawajibika kusimamia fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, ikiwa ni pamoja na kusimamia kumbukumbu za mifumo ya TEHAMA (MUSE-TAUSI), pamoja na kusimamia akaunti ya amana ya Mamlaka za serikali za mitaa (9921169787). Majukumu haya yapo chini ya uangalizi wa Idara ya Serikali za Mitaa - Fedha na yamekasimiwa kwa kitengo cha watu watano. Kitengo hiki kimepewa jukumu la kutoa msaada wa mfumo wa MUSE kwa Halmashauri zote 184, kufanya usuluhishi wa vitabu vya fedha na benki kwa akaunti tisa za halmashauri zote, na kurahisisha marekebisho na uhamisho wa fedha ndani ya account za halmashauri.

Tathmini ya ufanisi wa kitengo ilionesha kukosekana kwa uteuzi rasmi na mgawanyo wa kazi, na hivyo kusababisha utata wa kimajukumu. Zaidi ya hayo, kutokuwepo kwa uanzishwaji rasmi ndani ya Kurugenzi ya Serikali za Mitaa - Fedha kumepelekea kukosekana kwa uwajibikaji.

Zaidi ya hayo, kwa kuwa kuna wafanyakazi watano pekee wanaosimamia shughuli za halmashauri 184, kitengo hicho kimeonekana kuwa na uhaba mkubwa wa wafanyakazi. Upungufu huu wa wafanyakazi umesababisha kutokuwa na usawa katika mzigo wa kazi, kuongeza hatari ya makosa na hatari za ubadhilifu, hususan katika uhamisho wa fedha na usuluhishi wa kibenki. Kwa hivyo, hii imesababisha ugawaji usio sahihi wa fedha, kutokamilika upatanishi wa kibenki, na kuchelewa kuhamisha fedha zinazovuka mwaka kwenda halmashauri husika.

Pia, wafanyakazi wanaohusika na upatanishi wa kibenki pia wanashughulikia uhamisho wa fedha katika akaunti za halmashauri, hivyo kusababisha kukosekana kwa mgawanyo wa majukumu. Upungufu huu huongeza hatari ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika akaunti ya Amana, na kwa hivyo, kusababisha upotezaji wa mapato kwa serikali.

**Ili kukabiliana na masuala haya, ni muhimu kwamba, Mhasibu Mkuu wa Serikali na OR-TAMISEMI washirikiane kuanzisha kitengo cha usuluhishi wa kibenki kitakachofanya kazi kwa ufanisi na ubora unaohitajika, na kiwe na rasilimali watu ya kutosha, na mgawanyo wa madaraka.**

### 9.2.3 Upungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani na usimamizi wa vihatarishi

Serikali ya Tanzania ilitoa waraka Na. HB.114/222/01/62 wenye lengo la kurekebisha mwongozo uliotolewa mwaka 2012 kwa ajili ya kuendeleza na kutekeleza mfumo wa kusimamia vihatarishi.

Mwongozo ulisisitiza kwamba maofisa wa uhasibu wa sekta za umma wanawajibika katika utekelezaji na usimamizi bora wa viashiria vya hatari katika taasisi zao, ikiwamo kutambua, kufuatilia na kusimamia viashiria vya hatari zinazoweza kutokea na madhara yanayoweza kutokea.

Nimefanya tathmini ya udhibiti wa mifumo ya ndani na usimamizi wa vihatarishi katika mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/23 na kubaini upungufu ufuatao:

(i) Mamlaka tisa za serikali za mitaa hazikutunza au kuhuisha rejista za vihatarishi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu na kufuatilia hatari zinazoweza kutokea ili kuchukua hatua za kudhibiti na kupunguza athari zinazoweza kutokea. Kutotunza rejista ya hatari kunaweza kuathiri uzingatizi wa miongozo na kanuni;

(ii) Mamlaka 12 za serikali za mitaa hazikuwa na udhibiti wa mifumo ya ndani kwa kiasi kinachoridhisha kutokana na kutofanyika kwa tathmini ya vihatarishi katika maeneo yenye viashiria vya danganyifu, kwenye taarifa za fedha na katika usimamizi wa mali. Hali hii inaweza kusababisha kuwa na taarifa zisiso sahihi;

(iii) Mamlaka nne za serikali za mitaa hazikuwa na waratibu wa masuala ya vihatarishi ambao wangeweka msisitizo katika usimamizi wa vihatarishi kwa kutoa elimu kuhusu taratibu za udhibiti wa vihatarishi;

(iv) Mamlaka 12 za serikali za mitaa hazikutayarisha sera ya usimamizi wa vihatarishi ili kutimiza malengo ya sera ya vihatarishi na kuweka msingi imara wa kuandaa mfumo jumuishi wa usimamizi wa kudhibiti vihatarishi. Pia, Mamlaka hizi hazikubainisha kanuni elekezi za usimamizi wa vihatarishi hali inayoweza kuathiri mfumo mzima wa udhibiti wa mifumo ya ndani; na

(v) Mamlaka 10 za serikali za mitaa hazikufanya mafunzo kwa watumishi wake juu ya udhibiti wa vihatarishi pamoja na masuala ya ubadhirifu, ikiwamo kuwajengea uwezo juu ya udhibiti wa mambo hayo.

Maelezo ya mamlaka za serikali za mitaa zenye upungufu uliobainishwa yameoneshwa katika **Jedwali Na.66**.

**Jedwali Na. 66: Upungufu katika udhibiti wa mifumo na viashiria vya hatari**

| Na | Halmashauri | Kutokuwapo kwa rejista ya vihatarishi | Kutokufanyika kwa tathmini ya udhibiti wa mifumo ya ndani | Kutokuteuliwa kwa waratibu wa masuala ya vihatarishi | Kutokuwapo kwa sera ya usimamizi wa vihatarishi | Kutokuwajengea watumishi uwezo na ujuzi juu ya masuala ya vihatarishi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | | X | | | |
| 2. | H/W Igunga | X | X | | | X |
| 3. | H/W Karatu | | | | X | |
| 4. | H/Mji Kibaha | | X | x | | |
| 5. | H/W Malinyi | | X | | X | |
| 6. | H/Mji Mbinga | | X | | X | X |
| 7. | H/w Meru | x | X | | | |
| 8. | H/M Mpanda | X | X | X | | |
| 9. | H/W Ngorongoro | X | X | | | |
| 10. | H/M Singida | | X | | | |

| Na | Halmashauri | Kutokuwapo kwa rejista ya vihatarishi | Kutokufanyika kwa tathmini ya udhibiti wa mifumo ya ndani | Kutokuteuliwa kwa waratibu wa masuala ya vihatarishi | Kutokuwapo kwa sera ya usimamizi wa vihatarishi | Kutokuwajengea watumishi uwezo na ujuzi juu ya masuala ya vihatarishi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 11. | H/W Ushetu | X | | X | | X |
| 12. | H/W Bagamoyo | | | | | X |
| 13. | H/W Chamwino | | X | | | X |
| 14. | H/W Kaliua | X | X | | | X |
| 15. | H/M Morogoro | X | | | X | X |
| 16. | H/W Mpanda | X | | | X | X |
| 17. | H/W Mvomero | | | | X | |
| 18. | H/W Nanyamb | X | | X | X | X |
| 19. | H/W Itilima | | | | X | |
| 20. | H/W Tarime | | X | | X | |
| 21. | H/W Kibiti | | | | X | |
| 22. | H/W Nyanwgw'ale | | | | X | X |
| 23. | H/Mji Njombe | | | | X | |

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa husika kusimamia na kuhimiza utekelezaji wa sera na taratibu zilizowekwa juu ya mfumo wa usimamizi wa vihatarishi. Pia, mfumo wa usimamizi wa vihatarishi upitiwe mara kwa mara na kuboreshwa na watendaji wenye dhamana ili kuhakikisha kuwapo kwa ufanisi katika kufikia malengo katika utendaji.**

### 9.2.4 Upungufu uliobainishwa katika mifumo ya kihasibu na TEHAMA

Agizo la 7(i) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa 2009 linamtaka mkurugenzi wa halmashauri kuhakikisha mifumo ya kompyuta inafanya kazi. Pia, agizo la 11(2) linasisitiza mkurugenzi na mtunza hazina kuhakikisha ufanisi katika mfumo wa udhibiti wa ndani.

Kwa mwaka wa fedha 2022/23 nimetathmini teknolojia ya habari (TEHAMA) na mifumo ya uhasibu katika halmashauri na kubaini upungufu ufuatao:

**(i)** Mamlaka 12 za serikali za mitaa zilikuwa na uhaba wa watumishi katika kitengo cha TEHAMA, upungufu wa bajeti kwa kiwango cha 57% hadi 100%, pamoja na uhaba wa vitendea kazi kama kompyuta na magari. Hali hii inaweza kusababisha kutokuwapo kwa mgawanyo wa kazi, hivyo kutofikia malengo ya halmashauri husika;

(ii) Mamlaka sita za serikali za mitaa hazikuwa na sera ya mifumo ili kufafanua kanuni na taratibu zinazopaswa kusisitizwa katika masuala ya TEHAMA, hivyo kusababisha ugumu katika kupima utendaji-kazi wa masuala yanayohusiana na TEHAMA;

(iii) Hakukuwa na kamati ya kimkakati iliyoidhinishwa wala mpango mkakati katika masuala ya TEHAMA katika Mamlaka tisa za serikali za mitaa, jambo ambalo linaweza kusababisha kutotolewa kwa mwongozo juu ya masuala ya TEHAMA na kukosekana kwa ufuatiliaji wa ufanisi wa TEHAMA katika halmashauri;

(iv) Mamlaka 18 za serikali za Mitaa hazikuratibu mipango ya kurejesha taarifa na huduma panapotokea majanga ili kujikinga na upotevu wa taarifa endapo yangetokea majanga kama vile moto, mafuriko au hitilafu za umeme. Mamlaka hizi za serikali za mitaa hazikuwa na muundo sahihi wa kuhakikisha kuwa mifumo ya TEHAMA inalindwa dhidi ya majanga ya uharibifu kwa kuhakikisha kuwapo kwa vifaa vya kutosha kama vile vifaa vya kuzima moto, mifumo ya kutambua kuwapo kwa moto na viyoyozi; na

(v) Mamlaka 11 za serikali za mitaa hazikuwa zimetoa mafunzo kwa watumishi wake kuhusu TEHAMA na mifumo ya uhasibu ili kuhakikisha wana ujuzi wa kutosha katika kutatua changamoto mbalimbali za kimfumo zinazojitokeza.

Upungufu katika udhibiti wa TEHAMA, ikiwamo mifumo ya uhasibu, umeoneshwa katika **Jedwali Na.67.**

**Jedwali Na. 67: Upungufu katika mifumo ya TEHAMA na uhasibu**

| Jina la Halmashauri | Uhaba wa vifaa vya TEHAMA | Ufinyu wa bajeti | Uhaba wa watumishi wa TEHAMA | Kukosekana kwa sera/ mpangomkakati wa TEHAMA | Kukosekana kwa kamati za mipangomikakati | Kukosekana kwa mikakati ya kurudisha taarifa yakitokea majanga | Kutokfanyika kwa mafunzo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| H/Jiji Arusha | x | | | | x | X | x |
| H/Mji Bariadi | X | | | | X | X | X |
| H/Mji Igunga | X | | | | | | |
| H/Mji Kibaha | | | | | | X | |
| H/Mji Korogwe | x | | | | | X | X |
| H/W Misungwi | | | | | | X | |
| H/M Moshi | X | | | x | | X | |
| H/M Mpanda | | | 2 | x | | X | x |

| Jina la Halmashauri | Uhaba wa vifaa vya TEHAMA | Ufinyu wa bajeti | Uhaba wa watumishi wa TEHAMA | Kukoseka na kwa sera/ mpangom kakati wa TEHAMA | Kukosekan a kwa kamati za mipangom ikakati | Kukosekana kwa mikakati ya kurudisha taarifa yakitokea majanga | Kutokfa nyika kwa mafunz o |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| H/W Muheza | | 100 | 3 | | | | |
| H/W Mwanga | | | | | | X | |
| H/W Nzega | X | | | | X | | |
| H/W Same | | | | X | | X | |
| H/W Siha | | | | | | X | |
| H/W Sikonge | | | | | | X | |
| H/W Bagamoyo | | 57 | | | X | X | |
| H/W Biharamulo | | | | | | X | X |
| H/W Kaliua | X | | | | | | |
| H/W Mbogwe | | | | | | X | |
| H/W Mpanda | | | | | X | | |
| H/W Nanyamba | x | | | X | | X | X |
| H/W Newala | | | | | X | X | X |
| H/W Nzega | X | | | | | | |
| H/W Rufiji | | | | | X | | |
| H/Jiji Tanga | X | | 4 | | | | X |
| H/W Urambo | | | | | X | | |
| H/W Kasulu | | | | | | | |
| H/W Handeni | X | | | | | X | X |
| H/M Mafinga | | | | | X | | |
| H/W Kibiti | | | | | | X | |
| H/W Kisarawe | X | | | | | | X |
| H/M Morogoro | | | | X | | | |
| H/W Busega | | 100 | 1 | X | | | X |

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa husika kufanya juhudi za kuboresha vitengo hivyo kwa kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa kitengo na kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA ili kufikia malengo ya kuwa na udhibiti bora wa mifumo na utoaji huduma bora kwa jamii.**

### 9.2.5 Changamoto zilizobainika katika mabadiliko ya matumizi ya mfumo wa LGRCIS Kwenda TAUSI

Tarehe 07 Februari 2023, makatibu tawala wa mikoa walitoa barua Na. FA.119/272/01/47 kuagiza menejimenti za halmashauri kuhama kutoka mfumo wa zamani wa taarifa za ukusanyaji wa mapato (LGRCIS) na kwenda kwenye mfumo mpya wa ukusanyaji mapato (TAUSI).

Barua hiyo ilisisitiza kila halmashauri kutumia mfumo mpya katika ukusanyaji wa mapato ya vyanzo vyote, kusajili vifaa vyote vinavyotumika katika ukusanyaji (POS), pamoja na utoaji wa leseni na

vibali. Agizo hilo pia lilielekeza kwamba moduli zote katika mfumo mpya zitumike na matumizi ya mfumo wa LGRCIS yasitishwe kabla au tarehe 31 Machi 2023.

Nilifanya tathmini ya utekelezaji wa agizo hilo, utendaji kazi wa mfumo mpya, na ufanisi katika matumizi ya mfumo mpya, hasa katika kipindi cha mpito, na kubaini yafuatayo:

(i) Kutokutumika kwa baadhi ya moduli za mfumo ambazo ni pamoja na mirabaha ya misitu, kodi za pango, ushuru wa zao la pamba, ada za usafi wa mazingira, tozo ya huduma, ada za maegesho na ada za zabuni, Hali hii inasababisha kuwapo kwa taarifa zisizo sahihi katika halmashauri husika, kwani makusanyo yatokanayo ya vyanzo hivyo hayatakuwa yamehesabika katika mfumo.

(ii) Ucheleweshaji katika utoaji wa leseni za biashara hutokea kutokana na maombi kutakiwa kuidhinishwa na idara zaidi ya tatu (Idara ya Ardhi, Idara ya Afya, Idara ya Biashara). Hivyo inapotokea ucheleweshaji usio wa lazima katika idara moja unasababisha leseni kutokutoka kwa wakati, hali inayoathiri ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

(iii) Takwimu za wadeni ambazo hazijafanyiwa ulinganifu wakati wa kuhama kutoka mfumo wa zamani kwenda TAUSI, ambapo Sh.884,798,347 kwa H/W Misenyi; Sh. 673,727,504 kwa H/W Biharamulo; na Sh.1,528,219,585 kwa H/M Bukoba. Katika ukaguzi nilibaini kuwa wakati wa kuhama kutoka mfumo wa zamani kwenda mfumo mpya wa mapato hakukufanyika usuluhishi wa taarifa.

Kusitishwa kwa matumizi ya mfumo wa LGRCIS kulisababisha kulimbikizwa kwa ankara zisizolipiwa katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai 2022 hadi tarehe 30 Juni 2023. Wadaiwa wengi na leseni zilizoisha muda wake hazijashughulikiwa, mathalani katika H/W Misenyi, H/W Biharamulo na H/M Bukoba.

(iv) Mfumo hautoi nafasi kwa wadeni kulipa madeni yao, kwani unatoza ada kwa mwaka husika tu. Hii ni kwa sababu hakuna mwingiliano wa taarifa kati ya mfumo uliositishwa wa LGRCIS na mfumo mpya wa TAUSI.

Kubainika kwa kasoro kwenye mfumo mpya wa mapato kunaashiria kuwapo kwa taarifa za makusanyo ya mapato zisizo sahihi. Hii inaweza kusababisha upotevu wa mapato katika mamlaka za serikali za mitaa husika.

**Ninazishauri menejimenti za halmashauri husika zikishirikiana na OR-TAMISEMI kuchukua hatua stahiki katika kasoro zilizobainika. Hii inajumuisha uidhinishwaji na utolewaji wa leseni za biashara kwa wakati, matumizi ya mfumo kikamilifu na matumizi sahihi ya vifungu/moduli za mfumo katika kuongeza ufanisi kwenye ukusanyaji wa mapato.**

**Aidha, hatua zinapaswa kuchukuliwa kufuatilia taarifa za ambao hawakuwasilisha makusanyo na kuzihuisha katika mfumo mpya. Pia, jitihada zifanyike ili kukusanya madeni kutoka kwa wadaiwa waliobainika katika mfumo wa awali.**

### 9.2.6 Upungufu katika udhibiti wa usimamizi wa magari na kutotengeneza au kuuza magari chakavu

Aya ya 14 ya Mwongozo wa Rasilimali za Umma [iliyorekebishwa mwaka 2019] inamtaka kila ofisa masuuli kuhakikisha anaandaa mpango wa matengenezo na marekebisho ya mali, na kuhakikisha mali zinabaki katika hali nzuri, zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa, zinatoa huduma, na taasisi inanufaika kiuchumi.

Nilifanya tathmini ya udhibiti wa mifumo ya ndani, hasa kuhusiana na magari, ambapo nilipitia rejista ya utunzaji, matengenezo pamoja na rejista ya mauzo ya magari. Nilibaini kuwa mamlaka 13 za serikali za mitaa zilikuwa na jumla ya magari mabovu 127 ambayo yameachwa bila kufanyiwa huduma za matengezo au kuuzwa kulingana na taratibu za uuzaji wa mali za umma. Hii ni kinyume na agizo la 45(1) la memoranda ya fedha za serikali ya mwaka 2009.

Kutotengeneza magari kunaweza kuongeza uchakavu na kufupisha muda wa matumizi ya gari husika, hivyo manufaa yaliyotarajiwa huenda yasipatikane. Pia, kunaweza kupunguza utekelezaji wa shughuli ambazo zilipaswa kuwezeshwa na magari hayo; matokeo yake kuzorotesha utendaji wa uendeshaji wa halmashauri husika.

Orodha ya halmashauri zenye magari chakavu imeoneshwa kwenye **Jedwali Na.68**.

**Jedwali Na. 68: Magari ambayo hayajafanyiwa matengenezo au kuuzwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Aina ya Mali iliyoachwa bila kufanyiwa matengenezo | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Mpimbwe | Magari | 05 |
| 2 | H/W Mtama | Magari/Pikipiki | 34 |
| 3 | H/W Mvomero | Magari | 09 |
| 4 | H/W Rufiji | Magari | 08 |
| 5 | H/W Ulanga | Magari | 19 |
| 6 | H/W Itilima | Magari | 04 |
| 7 | H/W Ludewa | Magari | 12 |
| 8 | H/W Kibiti | Magari | 02 |
| 9 | H/W Geita | Magari | 03 |
| 10 | H/W Wang'ing'ombe | Magari | 3 |
| 11 | H/W Busokelo | Magari | 5 |
| 12 | H/W Mbeya | Magari | 16 |
| 13 | H/W Rungwe | Magari | 7 |
| | **Jumla ya magari, mabasi na pikipiki mabovu yaliyoachwa bila kufanyiwa matengenezo** | | **127** |



# SURA YA KUMI

## MFUKO WA WANAWAKE, VIJANA, NA WATU WENYE ULEMAVU

### 10.0 Utangulizi

Mwaka 1993, Serikali ilianzisha Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa ajili ya kuinua kiuchumi vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu waliokosa fursa ya kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha kwa sababu ya kutokuwa na dhamana. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa, katika kikao kimojawapo, ilijadili na kuazimia mamlaka za serikali za mitaa kuchangia asilimia 10 ya vyanzo vyake visivyolindwa kwenye Mfuko.

Kwa vile maagizo hayo yalikosa msukumo wa kisheria, mamlaka zote za serikali za mitaa hazikuweza kuyatekeleza kikamilifu. Hivyo, mwaka 2019 Serikali ilifanyia marekebisho Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290, na kuongeza kifungu cha 37A ambacho kinaziagiza mamlaka za serikali za mitaa kutenga asilimia 10 ya makusanyo ya vyanzo vyao kutoka katika mapato kwa ajili ya kutoa mikopo hii kwa uwiano wa 40% kwa wanawake, 40% kwa vijana, na 20% kwa watu wenye ulemavu. Miongozo hiyo ilirekebishwa tena mwaka 2021.

Hata hivyo, pamoja na kutambua juhudi hizo, mfuko ulikumbana na changamoto nyingi, ikiwamo upotevu wa fedha uliofanywa na watumishi wa serikali au kutoa mikopo kwa vikundi hewa badala ya walengwa, hivyo kusababisha kutorejesha kwa mikopo.

Baada ya kupokea taarifa ya mwaka kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mnamo tarehe  29 Machi 2023, Mh. Rais Dkt. Samia

Suluhu Hassan aliagiza yafanyike mapitio ya taratibu za utoaji mikopo, ikiwamo uwezekano wa kutoa mikopo kupitia benki.

Kufuatia agizo hilo, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, aliagiza mamlaka zote za serikali za mitaa nchini kusitisha utoaji wa mikopo kuanzia Aprili 2023. Usitishaji huo ulilenga kutoa muda kwa Serikali kuweka utaratibu mpya wa utoaji wa mikopo na kushughulikia changamoto zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Hadi tarehe 30 Juni 2023, thamani ya mfuko kwa halmashauri 177 ilifikia Sh. bilioni 245.31, kama inavyoelezwa katika **Kiambatisho Na.23.**

Kabla ya kusitishwa kwa utoaji wa mikopo mwezi Aprili 2023, mamlaka 176 za serikali za mitaa zilitenga Sh. bilioni 62.69 kwa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu na kutoa mikopo ya Sh. bilioni 73.41 kwa mwaka wa fedha 2022/23 kama ilivyobainishwa katika **Viambatisho Na. 26 na 27.**

Kwa kuzingatia uanzishwaji unaoendelea wa mfumo mpya wa usimamizi wa mfuko, sura hii inaangazia hitilafu zilizoonekana katika mwaka wa fedha wa 2022/23, kwa ajili ya Serikali kuzingatia.

## 10.1 Michango ambayo haikuwasilishwa kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu - Sh. bilioni 7.27

Kifungu cha 37(A) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura ya 290 kilichorekebishwa mwaka 2019) kinaziagiza mamlaka za serikali za mitaa kutenga na kupeleka 10% ya makusanyo ya mapato yao kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Nilipokagua, nilibaini kuwa mamlaka 62 za serikali za mitaa zilishindwa kuchangia kikamilifu 10% ya mapato yao ya ndani kwenye mfuko huu. Jumla ya michango ambayo haijachangwa ilifikia Sh. bilioni 7.27, kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na.69.**

**Jedwali Na. 69: Michango isiyowasilishwa kwenye Mfuko wa Vikundi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/M Ilemela | 562,668,829 | 33 | H/Mji Mbozi | 82,417,720 |
| 2 | H/M Kinondoni | 534,362,855 | 34 | H/Mji Nzega | 81,865,313 |
| 3 | H/W Chalinze | 488,005,043 | 35 | H/W Mpimbwe | 73,138,218 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | H/M Morogoro | 344,420,326 | 36 | H/W Wanging'ombe | 68,545,596 |
| 5 | H/W Morogoro | 331,687,619 | 37 | H/W Lushoto | 68,036,233 |
| 6 | H/M Shinyanga | 326,333,761 | 38 | H/W Nkasi | 63,939,663 |
| 7 | H/M Singida | 295,984,497 | 39 | H/W Chamwino | 63,420,084 |
| 8 | H/M Kigamboni | 260,064,641 | 40 | H/W Bariadi | 62,823,592 |
| 9 | W/W Rufiji | 250,119,000 | 41 | H/W Shinyanga | 62,483,446 |
| 10 | H/M Ubungo | 203,901,682 | 42 | H/Mji Kibaha | 57,656,252 |
| 11 | H/M Kigoma Ujiji | 154,401,328 | 43 | H/W Masasi | 52,824,504 |
| 12 | H/W Muleba | 137,204,552 | 44 | H/W Mbarali | 51,932,262 |
| 13 | H/W Manyoni | 148,171,879 | 45 | H/Mji Masasi | 50,865,981 |
| 14 | H/W Mbinga | 129,612,767 | 46 | H/W Handeni | 50,110,869 |
| 15 | H/W Korogwe | 129,047,179 | 47 | H/W Missenyi | 48,770,501 |
| 16 | H/W Igunga | 128,913,223 | 48 | H/W Rorya | 47,925,523 |
| 17 | H/Jiji Dar | 123,383,880 | 49 | H/W Songwe | 44,643,307 |
| 18 | H/W Mbogwe | 120,929,744 | 50 | H/W Kaliua | 43,898,419 |
| 19 | H/W Mufindi | 119,155,989 | 51 | H/W Momba | 39,884,290 |
| 20 | H/W Maswa | 118,040,304 | 52 | H/W Mvomero | 32,386,878 |
| 21 | H/Jiji Mwanza | 107,178,580 | 53 | H/M Iringa | 30,000,000 |
| 22 | H/W Ngara | 106,366,362 | 54 | H/Mji Bunda | 27,750,775 |
| 23 | H/W Meatu | 105,109,924 | 55 | H/Mji Njombe | 26,955,615 |
| 24 | H/Mji Makambako | 102,024,983 | 56 | H/W Mkinga | 26,541,217 |
| 25 | H/W Hanang' | 98,816,477 | 57 | H/W Itigi | 24,431,030 |
| 26 | H/W Kalambo | 97,851,271 | 58 | H/W Kiteto | 23,592,245 |
| 27 | H/M Sumbawanga | 92,684,792 | 59 | H/W Kilindi | 14,016,532 |
| 28 | H/W Rungwe | 90,060,710 | 60 | H/Mji Ifakara | 12,124,614 |
| 29 | H/W Bariadi | 87,961,945 | 61 | H/W Ikungi | 11,066,300 |
| 30 | H/W Mkuranga | 87,924,817 | 62 | H/W Kigoma | 6,835,338 |
| 31 | H/M Mpanda | 85,993,969 | **Jumla** | | **7,267,488,679** |
| 32 | H/W Chemba | 85,427,986 | | | |

**Jedwali Na.70** linaonesha mwenendo wa michango ya 10% ambayo haikuwasilishwa kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa miaka mitatu mfululizo.

**Jedwali Na. 70: Mwenendo wa michango ambayo haikuwasilishwa**

| Na. | Mwaka wa fedha | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 2022/23 | 62 | 7,267,488,679 |
| 2 | 2021/22 | 53 | 5,062,050,675 |
| 3 | 2020/21 | 83 | 6,857,306,654 |

Kushindwa kuwasilisha michango kunasababisha halmashauri kuwa katika hatari ya kuwa na madeni, kupunguza upatikanaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, na kupunguza ufanisi wa mfuko.

**Ninapendekeza kwa OR-TAMISEMI na menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa husika kuhakikisha zinatenga na kuchangia10% ya mapato yake kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kama sheria inavyotaka.**

### 10.2 Mikopo Iliyotolewa bila kuzingatia uwiano wa utoaji mikopo - Sh.bilioni 38.81

Kifungu cha 37A (1-2) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2019 (Sura ya 290, kilichorekebishwa mwaka 2019), pamoja na Kanuni ya 4 (1-2) ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2019, inaeleza kuwa mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kutenga 10% ya makusanyo ya mapato ya ndani ili kufadhili vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa uwiano wa 40% kwa wanawake, 40% kwa vijana, na 20% kwa watu wenye ulemavu.

Baada ya tathmini, nilibaini kuwa mamlaka 94 za serikali za mitaa zilitoa mikopo ya Sh. bilioni 38.81 kwa vikundi bila kuzingatia uwiano wa utoaji wa mikopo. **Kiambatisho Na.26** kinatoa orodha ya mamlaka za serikali za mitaa husika. Utoaji wa mikopo bila kuzingatia matakwa ya kanuni iliyoainishwa kunaweza kuvinyima vikundi vingine fursa ya kuwezeshwa.

**Ninapendekeza menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa husika kuzingatia sheria na kanuni zilizotajwa hapo juu ili kuhakikisha ufanisi katika utoaji na usimamizi wa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.**

### 10.3 Mikopo ambayo haijarejeshwa kutoka kwenye vikundi - Sh. bilioni 79.76

Kanuni ya 10(1) ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana, na Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2019 inaviagiza vikundi vyote vilivyokopeshwa kuanza kurejesha mikopo baada ya miezi mitatu toka siku waliyopata mkopo.

Pia, kanuni ya 10(2) inataka marejesho yafanyike kila mwezi na kwa mujibu wa makubaliano kati ya halmashauri na kikundi cha wanufaika wa mkopo. Zaidi, kanuni ya 11(1) hadi (4) inaeleza taratibu za halmashauri kufuata endapo wanufaika wa mikopo wanashindwa kurejesha kiasi cha fedha kilichokopeshwa.

Tathmini yangu ya utendaji wa mfuko ilibaini kuwa, hadi tarehe 30 Juni 2023 wanufaika wa mikopo katika Mamlaka 151 za serikali za mitaa

walishindwa kurejesha jumla ya Sh. bilioni 79.76 toka kwenye mikopo iliyotolewa. Kati ya mikopo ambayo haijarejeshwa, kiasi cha Sh. bilioni 27.67 ilikuwa mikopo iliyotolewa mwaka 2022/23, kama inavyofafanuliwa katika **Kiambatisho Na.27.**

Kutorejeshwa kwa mikopo kulitokana na upande wa menejimenti kutofanya bidii ya kutosha katika kutekeleza kanuni zilizotajwa hapo juu.

**Ninapendekeza kuwa OR-TAMISEMI na menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa waimarishe udhibiti katika Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa kuhakikisha zinazingatia matakwa ya Kanuni ya 11 (1-4) za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019. Pia, zihakikishe wadaiwa wote wanarejesha mikopo yao.**

## 10.4 Mikopo inayodaiwa kwenye vikundi vilivyositisha shughuli za biashara - Sh. bilioni 5.70

Kanuni ya 13 (1) (d)-(f) ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019 inamtaka ofisa maendeleo ya jamii wa mamlaka ya serikali za mitaa kufuatilia jinsi vikundi vinavyoendesha miradi, uwepo wa vikundi, urejeshaji wa mikopo iliyotolewa, kuhakikisha kuwa mikopo inatumika kama ilivyokusudiwa, na kuratibu mafunzo kwa wana vikundi.

Baada ya kufanya tathmini ya mikopo iliyotolewa kwenye vikundi, nilibaini kuwa halmashauri 46 zilikuwa na mikopo isiyolipwa ya jumla ya Sh. bilioni 5.70 kutoka kwa vikundi 1334 vilivyositisha shughuli zake kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 71.**

**Jedwali Na. 71: Mikopo isiyorejeshwa na vikundi vilivyositisha biashara**

| Na | Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Kiasi (Sh.) | Na | Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kaliua | 289 | 917,053,848 | 24 | H/W Musoma | 7 | 56,712,000 |
| 2. | H/M Temeke | 23 | 724,625,912 | 25 | H/W Msalala | 10 | 51,374,000 |
| 3. | H/Jiji Dar | 14 | 581,755,000 | 26 | H/Mji Masasi | 26 | 36,708,600 |
| 4. | H/Jiji Dodoma | 20 | 420,993,000 | 27 | H/W Sikonge | 52 | 34,619,500 |
| 5. | H/W Kilosa | 27 | 371,967,811 | 28 | H/W Uvinza | 18 | 32,365,700 |
| 6. | H/W Urambo | 113 | 294,988,778 | 29 | H/W Rombo | 10 | 31,505,271 |
| 7. | H/W Njombe | 84 | 274,955,000 | 30 | H/W Bunda | 10 | 22,266,500 |
| 8. | H/M Shinyanga | 23 | 249,760,319 | 31 | H/M Iringa | 3 | 20,575,000 |
| 9. | H/W Mkuranga | 63 | 177,859,890 | 32 | H/M Tarime | 4 | 20,488,000 |
| 10. | H/W Liwale | 25 | 141,003,529 | 33 | H/M Nzega | 8 | 20,437,000 |
| 11. | H/W Nanyamba | 73 | 133,145,100 | 34 | H/W Bunda | 15 | 20,205,200 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12. | H/W Sumbawanga | 27 | 116,703,000 | 35 | H/M Tabora | 22 | 18,334,550 |
| 13. | H/W Moshi | 107 | 116,113,000 | 36 | H/M Handeni | 9 | 18,050,000 |
| 14. | H/M Mtwara | 32 | 101,342,050 | 37 | H/W Butiama | 5 | 17,600,000 |
| 15. | H/M Kigoma Ujiji | 22 | 94,539,000 | 38 | H/W Itilima | 4 | 17,347,200 |
| 16. | H/W Muleba | 28 | 81,030,000 | 39 | H/W Rorya | 2 | 16,471,000 |
| 17. | H/W Ludewa | 5 | 78,200,000 | 40 | H/W Siha | 10 | 15,791,700 |
| 18. | H/W Nyasa | 21 | 77,507,368 | 41 | H/Mji Mbulu | 21 | 15,441,700 |
| 19. | H/W Mwanga | 21 | 73,282,300 | 42 | H/Mji Mbinga | 1 | 12,314,000 |
| 20. | H/W Nkasi | 29 | 68,657,711 | 43 | H/W Manyoni | 11 | 9,064,045 |
| 21. | H/W Kilwa | 6 | 66,985,774 | 44 | H/W Meatu | 8 | 8,877,000 |
| 22. | H/M Musoma | 5 | 62,669,000 | 45 | H/M Sumbawanga | 7 | 8,683,900 |
| 23. | H/W Bukoba | 12 | 62,094,200 | 46 | H/M Bumbuli | 2 | 7,021,519 |
| | | | Jumla | | | | **5,701,107,775** |

**Ninaishauri OR-TAMISEMI na menejimenti za halmashauri kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa uendeshaji wa miradi na kutoa mafunzo kwa wana vikundi. Pia, wahakikishe fomu za maombi ya mikopo na maandiko ya miradi iliyopendekezwa na kuibuliwa na wanakundi inachunguzwa kwa kina kabla ya mikopo kutolewa. Pia, waripoti suala hilo kwa mamlaka za kiuchunguzi kwa ajili ya urejeshwaji wa mikopo hiyo.**

### 10.5 Mabadiliko ya miradi ambayo haikuidhinishwa na Kamati ya Kudumu ya Fedha, Mipango na Uongozi - Sh. bilioni 2.43

Kanuni ya 9(1)(2) ya Kanuni za Kutoa na Kusimamia Mikopo kwa Makundi ya Wanawake, Vijana, na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019 inaagiza mikopo itumike mahususi kwa miradi iliyoidhinishwa na Kamati ya Kudumu ya Fedha, Mipango na Uongozi. Vilevile, mabadiliko yoyote katika pendekezo la mradi yanahitaji kupata idhini kutoka kwa kamati hiyo.

Nilibaini kuwa vikundi 216 kutoka katika halmashauri 24 vilibadilisha shughuli za miradi iliyoidhinishwa bila kupata kibali kutoka kwenye Kamati. Katika mikopo hiyo, Sh. bilioni 1.14 zinahusiana na mabadiliko ya miradi ndani ya vikundi na Sh. bilioni 1.29 wanavikundi waliamua kugawana fedha. Michanganuo imeoneshwa katika **Jedwali Na.72**.

**Jedwali Na. 72: Mabadiliko ya miradi ya vikundi bila idhini ya Kamati**

| | Jina la Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Kiasi cha mkopo | | Jina la Halmashauri | Idadi ya vikundi | Kiasi cha mkopo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (Sh.) | | | | (Sh.) |
| **Halmashauri ambazo vikundi viligawana mkopo** | | | | **Halmashauri ambazo vikundi vilibadili mradi** | | | |
| 1. | H/W Njombe | 30 | 641,840,000 | 1. | H/Jiji Dar es Salaam | 14 | 662,755,000 |

| | Jina la Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Kiasi cha mkopo | | Jina la Halmashauri | Idadi ya vikundi | Kiasi cha mkopo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | H/W Musoma | 30 | 183,352,950 | 2. | H/Jiji Arusha | 11 | 157,900,000 |
| 3. | H/M Kinondoni | 12 | 75,020,000 | 3. | H/W Rungwe | 10 | 138,500,000 |
| 4. | H/Mji Tarime | 10 | 69,000,000 | 4. | H/W Mbarali | 14 | 109,000,000 |
| 5. | H/W Kalambo | 22 | 63,200,000 | 5. | H/W Serengeti | 3 | 25,000,000 |
| 6. | H/W Liwale | 12 | 59,417,600 | 6. | H/W Mwanza | 2 | 20,000,000 |
| 7. | H/W Mkuranga | 5 | 40,000,000 | 7. | H/W Shinyanga | 5 | 19,012,000 |
| 8. | H/Mji Mafinga | 4 | 35,335,038 | 8. | H/M Morogoro | 1 | 17, 800,000 |
| 9. | H/W Ludewa | 19 | 33,600,000 | 9. | H/M Ubungo | 1 | 5,000,000 |
| 10. | H/Jiji Dar es Salaam | 1 | 30,000,000 | 10. | H/M Mtwara | 1 | 5,000,000 |
| 11. | H/W Nzega | 4 | 22,000,000 | | **Jumla** | **62** | **1,142,167,000** |
| 12. | H/W Mlele | 2 | 19,000,000 | | | | |
| 13. | H/M Kigamboni | 2 | 11,000,000 | | | | |
| 14. | H/W Nachingwea | 1 | 10,000,000 | | | | |
| | **Jumla** | **154** | **1,292,765,588** | | **Jumla Kuu** | | **2,434,932,588** |

Kuanzisha biashara ambayo haijaidhinishwa kunaweza kuifanya isiwe endelevu, hivyo kusababisha mikopo isiyolipika.

**Ninapendekeza menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kwamba wanufaika wa mikopo wanatekeleza miradi iliyoidhinishwa. Endapo itaonekana kuna umuhimu wa kufanya mabadiliko, vikundi vitalazimika kuomba na kupata idhini kutoka kwenye Kamati.**

## 10.6 Fedha za WYD kwenye akaunti ya Amana ambazo hazijapelekwa kwenye akaunti ya Mfuko Sh. milioni 322.47

Kanuni ya 22(1-2) ya utoaji na usimamizi wa mikopo ya Wanawake, Vijana, na Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2019 inaitaka kila mamlaka ya serikali ya mtaa kufungua na kuendesha akaunti maalumu ya mkopo katika mojawapo ya benki zinazotoa huduma katika eneo la mamlaka ya serikali ya mtaa, na mkurugenzi wa halmashauri kuwajibika kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikopo iliyotolewa chini ya kanuni hizi na marejesho ya mikopo zinawekwa kwenye akaunti maalumu ya mkopo.

Tathmini yangu ilibaini salio la Sh. milioni 322.47 katika akaunti za amana kwa mamlaka sita za serikali za mitaa, ikijumuisha marejesho ya mikopo na salio la miaka ya nyuma. Hata hivyo, fedha hizi hazikuhamishwa

kwenda kwenye akaunti maalumu za mfuko kama inavyotakiwa na Kanuni iliyotajwa hapo juu. Fedha hizo zimechanganuliwa katika **Jedwali Na.73**.

**Jedwali Na. 73: Fedha za Mfuko wa Vikundi katika akaunti ya Amana**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | H/M Singida | 152,539,103 | Bakaa ya miaka ya nyuma katika akaunti ya Amana |
| 2. | H/W Manyoni | 11,776,000 | Rejesho la mikopo Nov-Okt 2022 kutokana na tatizo la kimfumo kwenye TPLMIS |
| 3. | H/M Mtwara | 27,000,000 | Bakaa ya miaka ya nyuma katika akaunti ya amana |
| 4. | H/Jiji Arusha | 53,704,575 | Bakaa ya miaka ya nyuma katika akaunti ya amana |
| 5. | H/W Kibaha | 60,375,269 | Bakaa ya miaka ya nyuma katika akaunti ya amana |
| 6. | H/Mji Njombe | 17,070,900 | Rejesho la mikopo |
| **Jumla** | | **322,465,847** | |

Fedha ambayo haijawekwa kwenye akaunti ya Mkopo inaweza kutumiwa vibaya.

**Ninapendekeza maofisa masuuli kuhamisha fedha za Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kutoka akaunti za amana kwenda kwenye akaunti maalumu za mfuko bila kuchelewa ili ziweze kufanya shughuli kusudiwa.**

## 10.7 Ukiukwaji uliobainika katika usimamizi wa mikataba

### a) Mikopo iliyotolewa kabla ya kuingia mkataba - Sh. bilioni 2.41

Kanuni ya 8(2) ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana, na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019 inaelekeza kuwa baada ya kuidhinishwa kwa mkopo, mamlaka za serikali za mitaa zinatakiwa kuingia mikataba na vikundi husika kabla ya kutoa mkopo.

Ukaguzi kuhusu uzingatiaji wa Kanuni hii ulibaini kuwa mamlaka 12 za serikali za mitaa zilitoa mikopo ya jumla ya Sh. bilioni 2.41 kwa vikundi 248 vya wanufaika kabla ya kuingia mikataba, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.74.**

**Jedwali Na. 74: Mikopo iliyotolewa kabla ya kusainiwa kwa mikataba**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Ifakara | 46 | 481,855,290 |
| 2 | H/W Kilosa | 25 | 335,532,101 |
| 3 | H/W Kaliua | 27 | 306,374,000 |
| 4 | H/W Igunga | 29 | 249,056,516 |
| 5 | H/W Muheza | 28 | 236,500,000 |
| 6 | H/W Dodoma | 10 | 220,769,600 |
| 7 | H/Mji Korogwe | 32 | 193,500,000 |
| 8 | H/W Nsimbo | 23 | 148,350,000 |
| 9 | H/W Mpimbwe | 8 | 96,000,000 |
| 10 | H/W Urambo | 6 | 82,057,000 |
| 11 | H/W Korogwe | 6 | 39,000,000 |
| 12 | H/Mji Handeni | 8 | 23,600,000 |
|  | **Jumla** | **248** | **2,412,594,507** |

Kukosekana kwa mikataba kunamaanisha kuwa hakuna upande wowote unaofungwa kisheria, jambo linaloweza kusababisha kutokuelewana na kuleta migogoro siku za baadaye.

**b) Mikataba iliyosainiwa bila kuhakikiwa na mwanasheria wa halmashauri - Sh. bilioni 4.14**

Baada ya mapitio ya mikataba yenye jumla ya Sh. bilioni 4.14 kwa vikundi 327, nilibaini halmashauri tatu ziliingia mikataba na vikundi vilivyopata mkopo toka Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu bila kuhakikiwa na mwanasheria wa halmashauri kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 75.**

**Jedwali Na. 75: Mikataba isiyo hakikiwa na Mwanasheria**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/M Temeke | 275 | 3,913,074,327 |
| 2. | H/W Singida | 41 | 104,997,611 |
| 3. | H/W Iramba | 11 | 117,777,080 |
|  | **Jumla** | **327** | **4,135,849,018** |

Kutekeleza mikataba isiyohakikiwa kunaongeza hatari ya kuweka vifungu vyenye utata, ukiukwaji wa matakwa ya kisheria, na kutolindwa ipasavyo maslahi ya pande zote mbili.

**c) Mikopo iliyotolewa kwa vikundi zaidi ya kiasi kilichoombwa - Sh. milioni 84.27**

Ulinganisho uliofanywa kati ya maandiko ya mikopo ya kikundi yaliyowasilishwa na kiasi cha mikopo iliyotolewa na halmashauri ulionesha kuwa Halmashauri 2 ziliidhinisha na kutoa mikopo kwa vikundi 13 zaidi ya kiasi kilichoombwa kwa Sh. milioni 84.27, bila ushahidi

wowote wa kuhalalisha sababu za kutoa mikopo hiyo zaidi ya kiasi kilichoombwa kama ilivyofafanuliwa katika **Jedwali Na. 76**.

**Jedwali Na. 76: Mikopo iliyotolewa zaidi ya kiasi kilichoombwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Mkopo (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/M Temeke | 12 | 64,271,713 |
| 2 | H/Mji Njombe | 1 | 20,000,000 |
| **Jumla** | | **13** | **84,271,713** |

Kutoa mikopo zaidi ya kiasi kilichoombwa kunatia shaka juu ya uadilifu wa viongozi wa halmashauri husika.

**Ninapendekeza halmashauri husika zihakikishe masuala yote ya kisheria yanashughulikiwa kikamilifu kabla ya fedha kutolewa. Hii itasaidia kupunguza migogoro inayoweza kutokea, kulinda maslahi ya pande zote mbili, na kuweka mfumo thabiti wa kisheria. Pia, kutoa mikopo kulingana na maandiko ya Miradi ya kikundi yaliyowasilishwa, na ikihitajika kutoa zaidi ya kiasi cha mkopo ulioombwa, vikundi vitapaswa kutoa sababu zilizothibitishwa.**

## 10.8 Mapitio ya utendaji wa Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mikopo kwa Asilimia Kumi (TPLMIS)

### a) Upungufu wa TPLMIS

Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mikopo kwa Asilimia Kumi ulianzishwa ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utoaji wa mikopo, usimamizi na urejeshaji wa mikopo iliyotolewa kwa Wanawake, Vijana na vikundi vya watu wenye ulemavu.

Mfumo huo ulianzishwa mahususi ili kupunguza msongamano wa wananchi katika ofisi ya halmashauri, kwani unaruhusu mtu yeyote kujiandikisha kutoka mahali popote.

Pia, unazuia kurudiwa kwa majina ya vikundi kwa sababu mfumo huo ulikusudiwa kusajili jina la kikundi mara moja tu. Mfumo unasaidia kuweka kumbukumbu za vikundi kwa kuwa kitabu cha usajili tayari kipo kwenye mfumo na kuwazuia watu binafsi kuchukua mikopo mingi bila kurejesha mikopo iliyotolewa awali kwa vile mfumo unatumia namba za NIDA ambazo hukubali kuingizwa kwenye mfumo mara moja tu.

Ukaguzi wa utendaji wa mfumo ulibainisha upungufu ufuatao kama ulivyofafanuliwa katika **Jedwali Na.77.**

**Jedwali Na. 77: Upungufu katika matumizi ya mfumo wa TPLMIS**

| Na. | Jina la Halmashauri | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dar es Salaam, H/M Moshi, H/W Mwanga, H/W Kibaha, H/W Mbeya, H/W Mbarali, H/W Chunya, H/W Busokelo<br><br>H/Mji Njombe | **Kutokuwapo kwa taarifa zinamzofaa mtumiaji wa TPLMIS**<br><br>Nilifanya ukaguzi wa taarifa zilizotolewa na TPLMIS, nilibaini kuwa mfumo hatoi taarifa ya malipo na marejesho ya mikopo na taarifa ya fedha zitakazowawezesha watumiaji kufanya kazi zao na kufikia malengo.<br><br>Kwa mfano, ili kupata taarifa ya vikundi vilivyosajiliwa, mikopo iliyotolewa na taarifa za urejeshaji, wahusika wanatakiwa wafanye kazi nje ya mfumo kwa kunakili na kubandika data kwenye mfumo wa *Excel* kwa kuwa mfumo hauna vipengele vya kusafirisha. |
| 2 | H/Jiji Dar es Salaam, H/Mji Kondoa, H/W Momba, H/W Chemba, H/W Misenyi, H/M Bukoba | **Kutopewa haki ya kutumia TPLMIS kwa Wafanyakazi Muhimu**<br><br>Wadau muhimu kama wakaguzi wa ndani hawajapewa haki kutumia mfumo wa TPLMIS |
| 3 | H/Jiji Dar es Salaam | **Kutowiana kwa Taarifa katika TPLMIS**<br><br>Barua Na. AB.66/163/02/62 ya tarehe 02 Agosti 2022 kutoka OR-TAMISEMI inaitaka halmashauri kutunza na kuboresha taarifa zote za wanufaika wa mkopo kupitia TPLMIS. Hata hivyo, nilibaini tofauti kati ya taarifa zilizohifadhiwa katika mfumo wa TPLMIS na daftari linalotunzwa na halmashauri |
| 4 | H/M Kigamboni & H/W Ubungo & H/W Mwanga, H/W Bagamoyo, H/W Kisarawe, H/W Momba H/W Mbarali, H/W Busokelo, H/W Mafia | **Kutokuwa na haki ya kufanya marekebisho ya miamala yenye makosa katika mfumo wa mkopo wa TPLMIS**<br><br>Nilibaini kuwa watumiaji wa mfumo hawapewi haki ya kufanya marekebisho kosa linapotokea. |
| 5 | H/W Kasulu, H/W Uvinza, H/W Kibiti, H/W Kibaha, na H/W Momba | **Tathmini ya maombi ya mkopo kutokufanyika kwenye mfumo**<br><br>Tathmini ya ombi la pendekezo kutoka kwa vikundi hufanywa nje ya mfumo na kamati maalumu ya mkopo badala ya kufanywa kwenye TPLMIS.<br><br>Moduli ya usuluhishi kutotumika<br>Nilibaini halmashauri tatu ambazo hazikutumia moduli ya usuluhishi inayoruhusu usuluhishi kufanywa kupitia mfumo wa kiasi kilichokusanywa na kilichowekwa kwenye akaunti ya benki dhidi ya kitabu cha fedha (*Cashbook*). |
| 6 | H/W Mbozi, H/Jiji Mbeya | Kiasi cha mikopo iliyotolewa na marejesho ya mikopo kilichooneshwa kwenye dashibodi na kilichooneshwa kwenye ripoti ya hali ya mikopo na urejeshaji kwenye mfumo wa TPLMIS hutofautiana. |

Mfumo wa TPLMIS kutotoa taarifa pamoja na utegemezi wa kutengeneza taarifa nje ya mfumo inaweza kuleta hatari za utengenezaji na utoaji wa taarifa zisizo sahihi na kusababisha utendaji usio na tija.

Kuhifadhi kanzidata ya TPLMIS yenye data zisizo sahihi kunaleta wasiwasi juu ya usahihi wa taarifa za fedha. Pia, kunaweza kusababisha mikopo iliyotolewa kurejeshwa pungufu au kutorejeshwa kabisa.

Bila kupewa haki ya kutumia mfumo wa TPLMIS, wakaguzi wa ndani hawawezi kufanya thamini na kutoa maoni kuhusu ufanisi wa mfumo.

**b) Usajili usiokamilika wa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu**

OR-TAMISEMI, kupitia barua yenye Na. AB 65/100/01/24 ya tarehe 12 Julai 2022 iliziagiza halmashauri kusajili vikundi vyote vilivyo na mikopo isiyolipwa katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mikopo (TPLMIS) kabla ya tarehe 30 Julai 2022.

Hata hivyo, tathmini yangu ya utekelezaji wa agizo hilo imebaini kuwa vikundi 802 katika Halmashauri 11 zilizokuwa na mikopo isiyorejeshwa yenye jumla ya Sh. bilioni 2.06 hazijasajili mikopo hiyo katika mfumo wa TPLMIS, kinyume na maelekezo yaliyobainishwa kwenye barua. Maelezo ya kina ya vikundi visivyosajiliwa yameoneshwa kwenye **Jedwali Na.78**.

**Jedwali Na. 78: Kutosajiliwa kwa mikopo ya vikundi kwenye TPLMIS**

| Na. | Halmashauri | Vikundi visivyosajiliwa | Mkopo uliobaki (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Kibaha | 112 | 546,500,000 |
| 2 | H/W Nachingwea | 226 | 464,900,256 |
| 3 | H/W Mbinga | 49 | 315,379,799 |
| 4 | H/M Lindi | 81 | 243,615,968 |
| 5 | H/W Moshi | 42 | 146,830,889 |
| 6 | H/W Igunga | 120 | 120,084,000 |
| 7 | H/W Nzega | 98 | 109,208,900 |
| 8 | H/W Uyui | 45 | 68,922,500 |
| 9 | H/W Rufiji | 5 | 5,121,000 |
| 10 | H/W Songea | 16 | 14,840,000 |
| 11 | H/W Mkuranga | 8 | 22,261,630 |
| | **Jumla** | **802** | **2,057,664,942** |

Usahihi wa ripoti zinazotokana na mfumo unatia shaka kutokana na kukosekana kwa taarifa sahihi kuhusu salio la mikopo na vikundi vilivyopewa mikopo.

**Ninapendekeza uongozi wa halmashauri, kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa, kuhakikisha kuwa taarifa za mikopo kwa vikundi vinavyodaiwa zinawekwa kwenye mfumo wa TPLMIS.**

## 10.9 Kutokuwapo kwa vikundi vilivyopewa mikopo ya Sh. bilioni 2.60

Kanuni ya 13(1)(d-f) ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2019 inamtaka ofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri kufuatilia uendeshaji wa vikundi na kuwapo kwake, urejeshaji wa mikopo, kuhakikisha mikopo inatumika kama ilivyokusudiwa, na kuratibu mafunzo kwa vikundi.

Sikuweza kuthibitisha kuwapo kwa vikundi 850 katika mamlaka 18 za serikali za mitaa zilizoripoti kutoa mikopo ya jumla ya Sh. bilioni 2.6 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.79.**

**Jedwali Na. 79: Kutothibitishwa uwepo wa vikundi vilivyopewa mikopo**

| Na | Jina la Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dar es Salaam | 46 | 832,500,000 | 11 | H/W Msalala | 13 | 77,229,000 |
| 2 | H/W Igunga | 156 | 402,056,896 | 12 | H/W Kilolo | 14 | 56,041,500 |
| 3 | H/W Karatu | 119 | 209,931,500 | 13 | H/W Bariadi | 15 | 47,500,000 |
| 4 | H/W Kaliua | 46 | 197,136,900 | 14 | H/W Itigi | 28 | 36,106,200 |
| 5 | H/W Masasi | 118 | 164,732,050 | 15 | H/W Ikungi | 1 | 25,000,000 |
| 6 | H/M Shinyanga | 38 | 127,650,250 | 16 | H/W Bunda | 8 | 17,740,000 |
| 7 | H/W Serengeti | 75 | 116,148,900 | 17 | H/W Newala | 13 | 17,343,731 |
| 8 | H/W Nzega | 88 | 90,807,300 | 18 | H/M Singida | 10 | 9,841,500 |
| 9 | H/W Musoma | 52 | 84,592,411 | | | | |
| 10 | H/W Mbozi | 10 | 82,896,000 | **Jumla ndogo B** | | **102** | **286,801,931** |
| **Jumla Ndogo A** | | **748** | **2,308,452,207** | **Jumla Kuu (A+B)** | | **850** | **2,595,254,138** |

Hii inazua wasiwasi mkubwa kuhusu uwezekano wa matumizi mabaya ya fedha zilizokopwa; na pia inaashiria kutokuwapo kwa umakini katika kufanya tathmini ya kina kuthibitisha uwepo na uhalali wa vikundi vya mikopo kabla ya kutoa fedha.

**Kutokana na matokeo hayo, ninaishauri OR-TAMISEMI kutoa taarifa kwa mamlaka za uchunguzi na kuweka udhibiti ili kuhakikisha vikundi vyote vinavyopata mikopo vinatambulika na kufikiwa.**

# SURA YA KUMI NA MOJA



# TAMTHMINI YA MIRADI YA MAENDELEO

## 11.0 Utangulizi

Katika mwaka wa fedha 2022/23, miradi mbalimbali ya maendeleo ilitekelezwa na mamlaka za serikali za mitaa, ambapo utekelezaji wake ni chachu kubwa ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania. Kwa ujumla, miradi hii inafadhiliwa na serikali kuu, michango kutoka kwa wadau wa maendeleo, mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani, na michango ya jamii.

Baadhi ya miradi na shughuli za maendeleo zilifadhiliwa na Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF), Programu ya Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari Tanzania (SEQUIP), Programu ya Mafunzo ya Wanafunzi wa Msingi (BOOST), Kapu la Mama, TOZO, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Mpango wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (GPE-LANES), Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (P4R), Mradi wa Maji, Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (SWASH), Mradi wa Maji, Afya na Usafi wa Mazingira (WASH), Uwajibikaji wa Taasisi kwa Jamii (CSR), Mapato yatokanayo na Vyanzo vya Ndani vya mamlaka za serikali za mitaa na Ruzuku ya Serikali Kuu.

Wakati wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi, nilibaini kasoro mbalimbali kuhusiana na matokeo ya utekekelezaji wa miradi na taarifa za fedha kama inavyobainishwa hapa chini:

## 11.1 Kasoro zilizobainika katika utekelezaji wa miradi ya kurudisha kwa jamii (CSR) - Sh. bilioni 4.53

Kifungu cha 105 (1), (2) na (4) cha Sheria ya Madini, Sura ya 123 inawataka wamiliki wa leseni za madini kuandaa mpango wa miradi ya uwajibikaji kwa jamii (CSR) na kuuwasilisha kwa mamlaka za serikali za mitaa katika eneo linalohusika. Zaidi ya hayo, Kifungu cha 105(4) cha Sheria ya Madini,

Sura ya 123, kinaitaka halmashauri kusimamia utekelezaji wa mpango uliowasilishwa.

Katika ukaguzi, nilibaini kuwa kampuni za uchimbaji madini hazikutoa jumla ya Sh. bilioni 1.72 kati ya Sh. bilioni 2.82 zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya uwajibikaji kwa jamii (CSR) katika mamlaka za serikali za mitaa mbili.

Pia, miradi yenye thamani ya Sh. milioni 360 haikutekelezwa na kampuni moja ya uchimbaji madini katika Halmashauri ya Wilaya Kishapu kutokana na kupunguzwa kwa bajeti ya CSR kwa mwaka wa fedha 2022/23. Kupungua huku kulisababishwa na kusitishwa kwa uzalishaji uliotokana na uharibifu wa kuta za bwawa la mgodi, na kusababisha kupunguzwa kwa bajeti kutoka Sh. bilioni 1.2 hadi Sh. milioni 840. Hata hivyo, kiasi kilichopunguzwa hakikujumuishwa katika bajeti ya CSR ya mwaka wa fedha 2023/24 kama inavyoelekezwa na Aya ya 11 ya hati ya makubaliano iliyosainiwa tarehe 6 Septemba 2022.

Aidha, nilibaini Mamlaka nne za serikali za mitaa hazikutoa mwongozo kwa makampuni yanayoshughulika na uchimbaji wa madini katika maeneo yao. Hivyo, hali iliyosababisha makampuni hayo kutokuwa na mpango wa uwajibikaji kwa jamii wala kutotekelezwa kwa miradi inayotokana na uwajibikaji. Maelezo yameonesha kwenye **Jedwali Na.80.**

**Jedwali Na. 80: Upungufu katika utekelezaji wa miradi ya CSR**

| Mamlaka za serikali za mitaa ambazo hazijatoa miongozo | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Na. | Jina la Halmashauri | Jina la Kampuni | Mahali kampuni inapofanyia shuhuli za uchimbaji | Aina ya madini | Maoni |
| 1 | W H/Butiama | CATA Mining Company | Kiabakari Gold Mine | Dhahabu | Kampuni haijawasilisha mpango wake wa uwajibikaji kwa jamii Halmashauri haikuandaa muongozo pia, haikufanya ufuatiliaji |
| 2 | H/W Kibaha | Uchimbaji wa malighafi za ujenzi | Kibaha | Malighafi a ujenzi | Kutokuwasilisha mpango wa uwajibikaji kwa jamii. Hakuna mwongozo wa halmashauri |
| 3 | H/W Ludewa | Ludewa Maxcoal, Shamcoal companies, and Blue Sky | Usafirishaji wa makaa ya mawe kutoka vijiji vya Nkomang'omb | Makaa ya mawe | Kutokuwasilisha mpango wa uwajibikajikwa jamii. Hakuna mwongozo wa halmashauri |

| Mamlaka za serikali za mitaa ambazo hazijatoa miongozo | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Na. | Jina la Halmashauri | Jina la Kampuni | Mahali kampuni inapofanyia shuhuli za uchimbaji | Aina ya madini | Maoni |
| | | International Exploration Ltd | e, Luilo, Masimavalafu | | |
| 4 | H/W Uvinza | Nyanza Mines (T) | H/W Uvinza | Uchimbaji wa chumvi | Kutokuwasilisha mpango wa uwajibikaji kwa jamii, pia halmashauri haijatoa mwongozo |

Vilevile, nilibaini kuwa Kituo cha Mafunzo kwa Wafanyabiashara Wadogo na wa Kati kilichojengwa na kukamilika kwa thamani ya Sh. bilioni 2.42 hakijaanza kutumika kwa kipindi cha miaka mitano katika Halmashauri ya Mji Geita. Maelezo ya kasoro zilizobainika yameoneshwa kwenye **Jedwali Na.81**.

**Jedwali Na. 81: Upungufu katika utekelezaji wa miradi ya CSR**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Geita | 2,417,436,714 | Kituo cha mafunzo kilichojengwa kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo na wa kati ambacho hakitumiki kwa kipindi cha miaka mitano. |
| 2 | H/W Msalala | 1,176,676,395 | Kampuni ya madini haikutoa fedha zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya CSR. |
| | H/W Kishapu | 540,000,000 | Kampuni ya madini haikutoa fedha zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya CSR. |
| 3 | | 360,000,000 | Kupunguzwa kwa bajeti ya CSR kutokana na kusimama kwa uzalishaji kulikotokana na kuvunjika kwa kingo za bwawa la amdini. |
| 4 | H/W Butiama | 40,000,000 | Kutokuandaliwa na kuwasilsihwa kwa Mpango wa utekelezaji miradi ya CSR. |
| **Jumla** | | **4,534,113,109** | |

Kutotekelezwa kwa miradi ya CSR na kutotumika kwa miradi iliyokamilika kunaweza kukwamisha azma ya serikali ya kuhakikisha jamii katika maeneo ya migodi inanufaika na uchimbaji wa madini katika mazingira yao.

**Ninapendekeza kuwa OR-TAMISEMI ihakikishe mamlaka za serikali za mitaa husika zinasimamia miradi yote ya CSR inayopangwa kutekelezwa na makampuni ya uchimbaji katika maeneo yao. Pia, naishauri menejimenti ya Halmashauri ya Mji Geita kuchukua hatua za kuhakikisha mradi uliokamilika unaanza kutumika ili jamii ipate manufaa yaliyokusudiwa.**

**Menejimenti za H/W Msalala na Kishapu zinapaswa kufuatilia ili kuhakikisha michango ambayo haikutolewa inatolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyopangwa; hivyo kuhakikisha jamii inayoizunguka migodi inanufaika kutokana na kuwapo kwa shughuli za kampuni za uchimbaji madini.**

## 11.2 Miradi ya maendeleo ya Mfuko wa Jimbo iliyotekelezwa pasipo kuibuliwa na jamii - Sh. milioni 452.44

Kifungu cha 11 cha Sheria ya Mfuko wa Jimbo, Sura ya 96, kinaitaka Kamati ya Mfuko wa Jimbo kuidhinisha mapendekezo yote ya miradi kutoka kata zote za jimbo na miradi mingine yoyote ambayo kamati inaona kuwa na manufaa kwa jimbo.

Nilibaini mamlaka nane za serikali za mitaa zilitumia Sh. milioni 452.44 za mfuko wa jimbo kwa shughuli ambazo hazikuibuliwa na jamii. Maelezo ya mamlaka za serikali za mitaa zenye miradi ambayo haikuibuliwa na jamii yameoneshwa katika **Jedwali Na.82.**

**Jedwali Na. 82: Miradi ya Mfuko wa Jimbo isiyoibuliwa na jamii**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 1. | H/W Lushoto | 140,202,000 |
| 2. | H/W Butiama | 69,500,000 |
| 3. | H/W Nanyumbu | 56,490,000 |
| 4. | H/M Musoma | 55,124,700 |
| 5. | H/W Kongwa | 50,000,000 |
| 6. | H/W Handeni | 44,946,199 |
| 7 | H/W Ludewa | 20,500,000 |
| 8 | H/W Hanag’ | 15,678,500 |
| **Jumla** | | **452,441,399** |

Kutokuzingatia matakwa ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo na mkazo mdogo kwenye miradi inayoibuliwa na jamii wakati wa uchaguzi wa miradi ni miongoni mwa sababu za upungufu huu.

Kutekeleza miradi ambayo haikuibuliwa na jamii kunaifanya jamii husika kutoshiriki kikamilifu katika utekelezaji wake.

**Ninazishauri mamlaka husika za serikali za mitaa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo, Sura 96, kwa kutekeleza shughuli zilizoibuliwa na wanajamii na kuidhinishwa na Kamati za Mfuko wa Jimbo.**

## 11.3 Miradi Iliyotelekezwa kwa muda mrefu yenye thamani ya Sh. bilioni 20.24

Kanuni ya 114 (c) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaitaka taasisi nunuzi kuwajibika kwa usimamizi madhubuti wa ununuzi wa bidhaa, huduma au kazi inazofanya na kufuatilia utekelezaji na ukamilishaji wa kazi kwa wakati kulingana na masharti ya kila mkataba.

Tathmini ya hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ilibaini miradi ikiwa katika hatua mbalimbali za ukamilishaji katika mamlaka 18 za serikali za mitaa yenye thamani ya Sh. bilioni 20.24 ikiwa imetelekezwa kwa kipindi cha muda kati ya miaka miwili hadi 21. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zenye miradi iliyotelekezwa imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.28.**

Mipango duni, usimamizi duni wa miradi, mabadiliko ya vipaumbele vya serikali, na uhaba wa fedha ulichangia kutelekezwa kwa mradi hiyo. Hii inaashiria mgawanyo mbaya wa rasilimali, kukosekana kwa tija kwa jamii, na kutatiza uamuzi wa ufadhili kwa siku zijazo.

**Ninaishauri OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kuweka mikakati ambayo itahakikisha miradi iliyotelekezwa inakamilika bila kuchelewa zaidi. Mamlaka husika za serikali za mitaa zifanye tathmini ya kazi zilizosalia kwa miradi iliyotelekezwa, kuweka kipaumbele cha kukamilisha miradi hiyo kabla ya kuanza mipya. Pia zinapaswa kufuatilia, kusimamia na kuhamasisha jamii juu ya kuchangia michango kwa ajili ya kukamilisha miradi iliyotelekezwa.**

**Pia, ninaishauri Serikali kupitia OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha, kutoa fedha za kutosha kukamilisha miradi iliyotelekezwa na kuhakikisha katika siku zijazo, mipango na usanifu wa miradi hiyo inazingatia upatikanaji wa fedha ili ikamilike kwa wakati na kufikiwa malengo yaliyokusudiwa.**

## 11.4 Miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 11.21 imekamilika lakini haitumiki

Tathmini yangu ya utekelezaji wa miradi kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023 ilibaini mamlaka 29 za serikali za mitaa zenye miradi ya thamani ya Sh. bilioni 11.21 ambayo imekamilika lakini haijaanza kutumika kama ilivyokusudiwa.

Kutotumika kwa miradi husika kunatokana na uhaba wa rasilimali kama vile samani, vifaa-tiba, ukosefu wa umeme na maji, watumishi na vifaa vingine muhimu vya kufanyia kazi. Orodha ya mamlaka za serikali za

mitaa zenye miradi iliyokamilika lakini haitumiki imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.29.**

Ni maoni yangu kuwa kutokuwa na mipango mahsusi kabla ya utekelezaji wa miradi na ufinyu wa bajeti ni miongoni mwa sababu zinazokwamisha utoaji wa huduma kwa jamii inayolengwa mara miradi inapokamilika.

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa husika kuchukua hatua stahiki katika kuhakikisha kwamba miradi iliyokamilika inatumika ili kufikia lengo lililokusudiwa na kupata thamani ya fedha kutokana na matumizi yaliyofanyika.**

## 11.5 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotumika kufadhili shughuli zisizokusudiwa Sh. bilioni 5.10

Kifungu cha 27 (4) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 kinaelekeza bajeti ya serikali na taasisi ya umma iliyopitishwa kutumika tu kwa mujibu wa lengo lililokusudiwa na ndani ya kikomo kilichowekwa ndani ya makadirio ya serikali na taasisi ya umma. Pia, Agizo Na. 23(1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linaelekeza kutumia fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kinyume chake, nilibaini kuwa mamlaka 14 za serikali za mitaa zilielekeza jumla ya Sh. bilioni 5.10 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kufadhili shughuli ambazo hazikukasimiwa. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zilizotumia fedha za miradi kinyume na malengo yaliyokusudiwa imeoneshwa kwenye **Jedwali Na.83**.

**Jedwali Na. 83: Fedha za Miradi zilizobadilishwa matumizi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Mwanza | 3,046,565,098 |
| 2 | H/M Shinyanga | 1,000,000,000 |
| 3 | H/M Singida | 326,999,403 |
| 4 | H/M Musoma | 132,594,823 |
| 5 | H/Jiji Tanga | 120,117,620 |
| 6 | H/W Sengerema | 105,174,906 |
| 7 | H/W Mkinga | 101,189,729 |
| 8 | H/W Monduli | 83,264,400 |
| 9 | H/W Pangani | 58,213,496 |
| 10 | H/Mji Mbinga | 44,920,000 |
| 11 | H/W Buchosa | 25,611,500 |
| 12 | H/W Muheza | 24,228,240 |
| 13 | H/W Ngorongoro | 21,785,252 |
| 14 | H/W Bumbuli | 11,626,300 |
| **Jumla** | | **5,102,290,767** |

Kubadilishwa kwa matumizi ya fedha za miradi kumeathiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo zilizopangwa; pia hii inaweza kuathiri malengo ya mamlaka za serikali za mitaa ya kutoa huduma bora kwa jamii.

**Ninapendekeza kwamba OR-TAMISEMI iziagize mamlaka za serikali za mitaa husika kuzingatia taratibu za usimamizi wa fedha ili kuzuia ubadilishwaji wa matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo bila kibali.**

**Pia, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuzingatia kasma za bajeti kwa kuainisha shughuli zote kwa kipaumbele ili kupunguza uhitaji wa kufanya mabadiliko ya matumizi wakati wa utekelezaji wa bajeti.**

### 11.6 Ucheleweshaji wa uanzishwaji wa miradi iliyopokea fedha yenye thamani ya Sh. bilioni 9.32

Kifungu cha 27 (4) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinaelekeza pale ambapo bajeti ya serikali na taasisi ya umma imepitishwa, itatumika tu kwa mujibu wa lengo lililokusudiwa.

Kupitia ukaguzi wangu, nilibaini kuwa mamlaka 10 za serikali za mitaa zilichelewa kwa muda mrefu katika uanzishaji wa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 9.32 kwa kipindi cha kati ya miezi minne hadi 20 baada ya kupokea fedha zilizotengwa.

Ucheleweshaji uliokithiri wa utekelezaji wa mradi huongeza athari ya kuongezeka kwa bajeti kutokana na kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi. Aidha, huenda malengo ya mradi yasifikiwe kama ilivyopangwa; hivyo, kuathiri faida zilizokusudiwa kwa wadau na walengwa. Maelezo ya miradi husika yanaoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.30.**

**Naishauri OR-TAMISEMI kuhakikisha mamlaka za serikali za mitaa zinaweka mifumo na taratibu madhubuti katika kuhakikisha shughuli zote zilizopangwa na kutengewa rasilimali zinatekelezwa na kukamilika kwa wakati.**

**Pia, ninaishauri OR-TAMISEMI kuhakikisha mamlaka za serikali za mitaa zinafanya tathmini juu ya upangaji wa miradi ili kubaini vikwazo vinavyoweza kujitokeza na kukabiliana na hatari zinazohusiana na utekelezaji wa miradi kwa kutenga muda ulio wazi, kufafanua majukumu, na kuweka malengo ya utekelezaji wa miradi.**

## 11.7 Kasoro zilizobainika katika utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 13.81

Kanuni ya 114 (c) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inaitaka taasisi nunuzi kuwa na usimamizi bora wa ununuzi wa bidhaa, huduma au kazi yoyote inayofanya na kuchukua au kuanzisha hatua za kurekebisha au kuadhibu ukiukwaji wa masharti ya mkataba.

Kinyume chake, tathmini yangu ya hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ilibaini kasoro mbalimbali kwenye miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 13.81 bilioni iliyotekelezwa na mamlaka 14 za serikali za mitaa. Maelezo ya miradi iliyobainika kuwa na kasoro katika mamlaka za serikali za mitaa yameoneshwa katika **Kiambatisho Na.31**.

Kasoro zilizoonekana zinachangiwa kwa kiasi kikubwa na usimamizi wa miradi usioridhisha, na wataalamu wa idara zinazohusika na utekelezaji wa mradi kutouunga mkono mradi kwa kiasi cha kutosha. Kuwapo kwa kasoro hizo kunaathiri ubora na ufanisi wa jumla wa miradi iliyotekelezwa pamoja na ustahimilivu wake wa muda mrefu. Pia, mamlaka za serikali za mitaa zinaweza kutumia gharama za ziada kurekebisha kasoro zilizoonekana.

**Ninapendekeza kwamba mamlaka za serikali za mitaa zihakikishe hatua zinachukuliwa kurekebisha kasoro zilizoonekana katika miradi husika. Pia, hatua zinapaswa kuchukuliwa kwa kuimarisha udhibiti wa ubora na ufuatiliaji wakati wa utekelezaji wa miradi. Hii itazuia kasoro hizo kujitokeza katika siku zijazo.**

## 11.8 Miradi isiyokamilika yenye thamani ya Sh. bilioni 272.88

Kanuni ya 114(b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inaitaka taasisi nunuzi kuwajibika kwa usimamizi bora wa ununuzi wa bidhaa au huduma ambayo inafanya na itafuatilia maendeleo na ukamilishaji wa kazi kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba.

Katika ukaguzi, nilibaini miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 206.89 katika mamlaka 94 za serikali za mitaa ambayo haijakamilika hadi tarehe ya ukaguzi huu kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.32**.

Pia, nilibaini kuwa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 20.78 iliyotekelezwa na mamlaka 20 za serikali za mitaa haijakamilika licha ya kuisha kwa muda wa utekelezaji kama inavyofafanuliwa kwa kina katika **Kiambatisho Na.33.**

Aidha, tathmini ya maendeleo ya utekelezaji wa miradi dhidi ya muda wa mkataba uliokubaliwa ilibaini miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 45.21 ambayo ilikuwa inatekelezwa kwa kasi ndogo katika mamlaka mbili za serikali za mitaa kutokana na ufuatiliaji mdogo na uhaba wa fedha kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.84**.

**Jedwali Na. 84: Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi**

| Na. | Halmashauri | Maelezo ya mradi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Mwanza | Ujenzi wa Soko Kuu - Mwanza: tarehe ya kuanza kwa mkataba 19 Oktoba 2020 na tarehe ya awali ya kukamilisha mradi ilikuwa 18 Aprili 2022. | 25,272,127,777 |
| 2. | H/M Moshi | Ujenzi wa Kituo cha Mabasi cha Kimataifa cha Moshi-Ngangamfumuni: Mkataba ulisainiwa 28 Januari 2019 na tarehe ya awali kukamilisha mradi ilikuwa 28 Januari 2021. | 19,932,910,740 |
| Jumla | | | 45,205,038,517 |

Kwa ujumla, kutokamilika kwa miradi hii kunachangiwa na kuchelewa na kutotolewa kwa fedha za kutosha, ucheleweshaji wa taratibu za ununuzi, usimamizi na ufuatiliaji hafifu wa miradi, na ushiriki mdogo wa jamii katika miradi inayotekelezwa kwenye ngazi za chini za mamlaka za serikali za mitaa.

Kutokamilisha miradi hii kwa wakati kunaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama kutokana na kuongezeka kwa bei ya vifaa vya ujenzi kunakochangiwa na mfumuko wa bei. Aidha, kuchelewa kukamilika kwa miradi kunainyima jamii inayoizunguka miradi husika manufaa yaliyokusudiwa.

**Ninapendekeza kwamba, OR-TAMISEMI, kupitia mamlaka za serikali za mitaa, kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mradi kwa kutembelea maeneo ya miradi mara kwa mara, kuandaa taarifa za maendeleo ya utekelezaji, na kufanya tathmini ya utekelezaji ili kubaini vikwazo na kuchukua hatua za kurekebisha. Aidha, menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zinashauriwa kuhamasisha jamii kuchangia katika utekelezaji wa miradi inayotekelezwa katika ngazi za chini.**

**Vilevile, ninaishauri Serikali, kupitia OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha, kufanya tathmini ya kina ya miradi inayotekelezwa na mamlaka za serikali za mitaa na kutoa kiasi cha fedha kinachohitajika ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ili hiyo kuepusha kuchelewa kwa ukamilishaji wake.**

**11.9 Miradi isiyotekelezwa kutokana na ufinyu wa bajeti - Sh. bilioni 20.57**

Kifungu cha 27 (4) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 kinaelekeza bajeti ya serikali na taasisi ya umma iliyopitishwa kutumika tu kwa mujibu wa lengo lililokusudiwa.

Hatahivyo, mapitio ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2022/23 yalibaini kuwa shughuli za miradi ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 20.57 hazikutekelezwa katika mamlaka 53 za serikali za mitaa kutokana na kutokutolewa kwa fedha na hazina, washirika wa maendeleo, na mapato ya vyanzo vya ndani vya mamlaka za serikali za mitaa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa. Maelezo yameoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.34.**

Kutokutolewa kwa fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa kunahusishwa na kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato na uwekaji wa malengo yasiyo na uhalisi wakati wa uandaaji wa bajeti na mamlaka husika. Miradi iliyopangwa haikutekelezwa kikamilifu, hivyo manufaa yaliyokusudiwa kwa walengwa hayakufikiwa.

**Ninaishauri Wizara ya Fedha kuendelea kutathmini utekelezaji wa bajeti dhidi ya mapato na matumizi halisi ili kubaini tofauti zozote kwenye bajeti iliyopangwa na kuchukua hatua stahiki za kurekebisha. Wizara ya Fedha inapaswa kuimarisha juhudi zinazoendelea za serikali za kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali ili kufikia malengo ya taifa ya bajeti.**

**Pia, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuzishughulikia athari zinazotokana na kutokutolewa kwa fedha kulingana na bajeti na kujumuisha katika bajeti zijazo shughuli ambazo hazikutekelezwa kutokana na uhaba wa fedha.**

**11.10 Kasoro zilizobainika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia Rasilimali za Ndani (Force Account) - Sh. bilioni 7.7**

Tarehe 22 Mei 2020, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ilitoa mwongozo wa kutekeleza miradi kwa kutumia rasilimali za ndani kwa taasisi nunuzi nchini Tanzania. Madhumuni ya jumla ya mwongozo huo ni kuziongoza taasisi nunuzi (PEs) juu ya matumizi sahihi ya rasilimali za ndani katika kutekeleza miradi; huku madhumuni mahususi yakiwa ni kuweka taratibu za ununuzi wa nguvu kazi na vifaa vya ujenzi; na kutumia rasilimali mbalimbali zilizopo ndani ya taasisi.

Tathmini ya miradi ya maendeleo iliyotekelezwa chini ya matumizi ya rasilimali za ndani niliyoifanya katika mamlaka za serikali za mitaa tano ilibaini kasoro kadhaa kama inavyoelezwa hapa chini:

**(i) Miradi ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 6 iliyotekelezwa bila kuteuliwa kwa meneja wa mradi na timu ya utekelezaji**

Nilibaini miradi 28 yenye thamani ya Sh. bilioni 6 ambayo ilitekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya Kigoma kwa kutumia rasilimali za ndani bila kuteuliwa kwa meneja na timu ya utekelezaji kwa ajili ya kusimamia miradi hiyo.

Hii ni kinyume na matakwa ya Aya ya 9 na 10 ya Mwongozo wa PPRA wa kutekeleza miradi kwa kutumia rasilimali za ndani kwa taasisi nunuzi Tanzania wa mwaka 2020 ambao unaagiza uteuzi wa meneja wa mradi na timu ya utekelezaji kusimamia utekelezaji wa mradi.

**(ii) Mradi wa ujenzi wa madarasa wenye thamani ya Sh. milioni 775 uliotekelezwa kinyume na usanifu wa mradi ulioidhinishwa**

Katika ukaguzi, nilibaini kuwa mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa wenye thamani ya Sh. milioni 775 katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza ulitekelezwa kinyume na usanifu wa mradi ulioidhinishwa bila kibali cha mabadiliko hayo.

Usanifu wa awali wa ujenzi wa madarasa uliainisha ujenzi wa madarasa ya muundo wa ghorofa badala ya muundo wa mlalo. Hata hivyo, wakati wa hatua ya utekelezaji, mabadiliko yalifanywa kwenye usanifu bila kuwapo kwa sababu za msingi. Mathalani, muundo wa madarasa 12 kati ya 29 yalijengwa katika usanifu wa mlalo badala ya ghorofa kama ilivyopendekezwa hapo awali.

**(iii) Vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 424.36 vilivyotelekezwa kwa miezi 15**

Halmashauri ya Jiji la Tanga ilinunua vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 424.36 kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Machinga.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa vifaa hivi vilikuwa vimeachwa bila kutumika, huku vikiathirika kwa mvua na jua, kwa takribani miezi 15.

**(iv) Ununuzi wa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 290.65 zaidi ya mahitaji**

Vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 290.65 vilinunuliwa zaidi ya mahitaji yaliyobainishwa kwenye jedwali la makisio ya vifaa vya ujenzi wa miradi katika Halmashauri ya Manispaa Shinyanga. Miradi hiyo ilijumuisha ujenzi wa jengo la utawala, soko kuu, idara ya matibabu ya dharura, na Soko la Ngokolo.

Utaratibu huu wa ununuzi unakiuka matakwa ya Aya ya 24.2 ya Mwongozo wa PPRA wa kutekeleza miradi kwa kutumia rasilimali za ndani kwa taasisi nunuzi wa mwaka 2020.

**(v) Ununuzi wa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 246.43 bila kuidhinishwa na meneja wa mradi**

Nilibaini kuwa ununuzi wa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 246.44 katika vituo vitatu vya afya katika Halmashauri ya Wilaya Bumbuli ulifanyika bila ya kupata kibali cha meneja wa mradi, kinyume na matakwa ya Aya ya 24.2 ya Mwongozo wa PPRA wa kutekeleza miradi kwa kutumia rasilimali za ndani kwa taasisi nunuzi Tanzania.

Kasoro zilizobainika zilichangiwa na utendaji usioridhisha wa watumishi katika idara ya ujenzi na idara zingine za halmashauri zenye wajibu wa kusimamia miradi inayotekelezwa kwa kutumia rasilimali za ndani ya taasisi. Sababu za kutokea kwa kasoro zilizobainika katika utekelezaji wa miradi kupitia matumizi ya rasilimali za ndani ni: upungufu katika usimamizi wa miradi, michakato ya ununuzi, na ukosefu wa utaalamu katika usimamizi wa fedha miongoni mwa maofisa wa ngazi za chini.

Usimamizi duni wa miradi inayotekelezwa kupitia matumizi ya rasilimali za ndani husababisha kazi zisizokuwa na ubora, hasara kutokana na ununuzi wa vifaa kupita mahitaji, na ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi.

Ninapendekeza OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa, kufanya yafuatayo:

(a) Kutoa mafunzo ya kina na kuandaa programu za kuwajengea uwezo watumishi wanaohusika katika utekelezaji wa miradi, kwa kuangazia usimamizi wa miradi, michakato ya ununuzi, usimamizi wa fedha, na ujuzi wa kitaalamu kulingana na majukumu yao;

(b) Kuhakikisha usimamizi wa karibu na wa kina wa miradi inayotekelezwa katika ngazi za chini kwa kutengeneza mifumo thabiti ya kufuatilia maendeleo ya mradi, matumizi ya fedha na viwango vya ubora;

(c) Kuboresha taratibu za ununuzi ili kuongeza uwazi, ufanisi na uzingatizi wa taratibu za ununuzi. Pia, kutekeleza hatua za kuzuia ununuzi kupita kiasi na kupunguza dosari zinazohusiana na ununuzi;

(d) OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora zifanye tathmini ya mahitaji na kuajiri watumishi wenye sifa zinazoendana na usimamizi wa miradi ili kusimamia miradi yote inayotekelezwa kwa njia ya kutumia rasilimali za ndani ya taasisi katika halmashauri na ngazi za chini.

# SURA YA KUMI NA MBILI




## UFANISI WA KIUTENDAJI KATIKA SEKTA YA ELIMU

### 12.0 Utangulizi

OR-TAMISEMI ina jukumu la kusimamia ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari, watu wazima na elimu isiyo rasmi Tanzania Bara ili kuhakikisha kuwa elimu bora inatolewa. Ili kufanikisha lengo hili, inatakiwa kuwa na rasilimali za kutosha kama walimu wenye uwezo, na miundombinu kama vile madarasa na vifaa vya kufundishia.

Ili kufikia malengo hayo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikiandaa Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) na Sera ya Elimu na Mafunzo. Mifumo hii ya kimkakati imeandaliwa ili kushughulikia mahitaji anuai katika sekta ya elimu kwa kuzingatia mahitaji ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia.

Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) inatokana na vipaumbele vya vya Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025. Dira hii imejikita katika kufafanua vigezo vya maendeleo ya sekta ya elimu kupitia mipango ya maendeleo ya miaka mitano, ambapo utekelezaji wa mpango wa sasa ni awamu ya III kuanzia mwaka 2021/22 hadi 2025/26.

Serikali, kupitia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, iliandaa Sera ya Taifa ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na kuweka vipengele vitakavyotekelezwa ili kufikia malengo kusudiwa katika mipango ya maendeleo.

Kuibuka kwa changamoto katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kulitokana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, sayansi na teknolojia; pamoja na Serikali ya Tanzania kuridhia mikataba ya kikanda na kimataifa kuhusu elimu na mafunzo. Hivyo, Serikali, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ililazimika kuifanyia marekebisho Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na kuja na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la 2023.

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa na OR-TAMISEMI katika usimamizi wa sekta ya elimu ndani ya mamlaka yake kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Yafuatayo ni maeneo yanayohitaji maboresho:

## 12.1 Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kutotoa fedha kiasi cha Sh. bilioni 1.25 kwa ajili ya elimu bila malipo

Aya ya 1 & 2 ya waraka wa ruzuku kwa shule za serikali kuhusu utoaji wa elimu bila malipo wenye Na. DC.297/507/01/39 (kwa shule za msingi) na Na. DC.297/507/01/40 (kwa shule za sekondari) uliotolewa tarehe 28 Desemba 2015 unaitaka serikali kutoa fidia ya Sh. 10,000 na Sh. 25,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kwa shule za msingi na sekondari mtawalia.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali haikutoa Ruzuku ya fedha za kugharamia elimu bila malipo Sh. bilioni 1.25 kati ya Sh. bilioni 11.83 zilizohitajika katika mamlaka za serikali za mitaa 15. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zilizopokea fedha pungufu imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 35.**

Kutolewa kwa fedha pungufu kunaathiri uwezo wa shule kupata mahitaji na vifaa muhimu vya kufundishia na kujifunzia, na kufanya ukarabati wa miundombinu ya kutolea elimu.

**Ninapendekeza Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI kuhakikisha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia utoaji wa elimu bila malipo zinapelekwa katika mamlaka za serikali za mitaa ili kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa utoaji bora wa elimu nchini.**

## 12.2 Upungufu wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 hadi 2025/26) umebainisha malengo muhimu katika elimu yanayotakiwa kufikiwa ifikapo mwaka 2026. Malengo hayo ni: kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari kwa kujenga vyumba vya madarasa; kununua madawati na vitabu vya kiada; kuboresha uwiano wa vyoo; na kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu katika ngazi zote(ikiwemo kutoa malipo yenye tija na makazi karibu na maeneo ya kazi).

Pamoja na jitihada za Serikali za kukabiliana na tatizo la upungufu wa miundombinu katika shule kwa kujenga shule mpya na kukarabati vyumba vya madarasa kwa shule zenye msongamano wa wanafunzi, pia jitihada kubwa zimefanyika kuboresha nyumba za walimu, mabweni na hosteli za wanafunzi, miongoni mwa mambo mengine.

Tathimini ya utoshelevu wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari ilibaini kuwa mamlaka 18 za serikali za mitaa zilikuwa na upungufu wa miundombinu mbalimbali kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.85, Kiambatisho Na.36** na **Kiambatisho Na.37.**

**Jedwali Na. 85: Upungufu wa miundombinu**

| Idara | Aina ya Miundombinu | Mahitaji | Kilichopo | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| Shule za Msingi | Viti na Meza | 1,245 | 8,955 | 12,290 |
| | Madarasa | 24,666 | 13,628 | 11,038 |
| | Madawati | 309,161 | 224,334 | 84,827 |
| | Vyoo vya wanafunzi | 41,827 | 20,434 | 21,393 |
| | Vyoo vya walimu | 484 | 111 | 373 |
| | Nyumba za walimu | 20,052 | 4,296 | 15,756 |
| | Ofisi za walimu | 1,297 | 680 | 617 |
| | Bwalo la chakula | 186 | 15 | 171 |
| | | | | |
| Shule za Sekondari | Madarasa | 168,581 | 162,230 | 6,351 |
| | Madawati | 4,869 | 4,514 | 355 |
| | Vyoo vya wanafunzi | 7,334 | 4,657 | 2,677 |
| | Vyoo vya walimu | 283 | 222 | 61 |
| | Nyumba za walimu | 17,503 | 10,668 | 6,835 |
| | Ofisi za Walimu | 703 | 254 | 449 |
| | Mabweni | 819 | 355 | 464 |
| | Maabara | 1,146 | 727 | 416 |
| | Bwalo la Chakula | 151 | 39 | 112 |

**Chanzo**: *Tarifa za Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari*

Msongamano katika madarasa na mabweni; uwiano usiosawia wa vyoo kwa idadi ya wanafunzi; pamoja na uhaba wa maabara, viti, meza, na madawati huathiri mazingira ya kujifunzia. Aidha uhaba wa nyumba za walimu, ofisi na samani huathiri mazingira ya kufundishia, hatimaye huathiri ufaulu wa wanafunzi.

**Ninapendekeza kwamba OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, itoe fedha kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa ili kuondoa au kupunguza upungufu wa miundombinu. Pia, wahakikishe wanaweka mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa elimu bora.**

## 12.3 Upungufu wa walimu katika shule za msingi na sekondari

Awamu ya III ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2021 hadi 2025/26 unaeleza kuwa uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika shule za msingi unatakiwa kuwa 1:50 (mwalimu mmoja kwa wanafunzi 50) na kwa shule za sekondari kuwa 1:20 (mwalimu mmoja kwa wanafunzi 20) hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2026.

Tathmini niliyofanya katika uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika mamlaka 13 za serikali za mitaa nilibaini kuwa, kati ya walimu 32,406 wanaohitajika kwa shule za msingi na sekondari, kulikuwa na walimu 20,076. Takwimu hii inamaanisha kuwapo kwa upungufu wa walimu 12,330 sawa na 38% kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.86 na Kiambatisho Na.38.**

**Jedwali Na. 86: Upungufu wa walimu**

| Na | Shule | Mahitaji | Waliopo | Upungufu | Upungufu (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | shule za msingi | 24,609 | 14,622 | 9,987 | 41 |
| 2. | shule za sekondari | 7,797 | 5,454 | 2,343 | 30 |
| **Jumla** | | **32,406** | **20,076** | **12,330** | **38** |

**Chanzo:** *Taarifa za Idara ya Elimu Msingi na Sekondari*

Upungufu wa walimu unatokana na serikali kutoajiri idadi ya kutosha ya walimu, sambamba na ongezeko la idadi ya wanafunzi, kupungua kwa idadi ya walimu kunakotokana na kustaafu katika utumishi wa umma, vifo, na kuacha kazi kwa sababu mbalimbali kama vile mazingira yasiyovutia katika kufanya kazi, ujira usivutia, na kukosekana motisha.

Upungufu wa walimu niliobaini katika mamlaka 13 za serikali za mitaa una athari za moja kwa moja katika ufaulu duni wa wanafunzi wa shule za umma.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Utumishi na Utawala Bora, ipeleke walimu katika shule zilizoathirika zaidi na upungufu. Aidha, serikali inashauriwa kuweka juhudi zaidi katika kuboresha mazingira ya kufundishia kwa kujenga nyumba za watumishi, madarasa, na kusambaza vifaa vya kufundishia, kuboresha stahiki za walimu kama mishahara, kulipa madeni na kutoa motisha ili kuvutia walimu kuendelea na utumishi.**

**Pia, Serikali inapaswa kuwekeza katika miundombinu ya TEHAMA ili kuweza kutoa elimu mtandao (*e-learning*) ambayo itatoa fursa ya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi kwa upana zaidi kutoka katika chanzo kimoja.**

## 12.4 Kutotenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya ruzuku ya uendeshaji na chakula kwa shule za msingi na sekondari - Sh. bilioni 2.47

Aya ya 1 & 2 ya Waraka wenye nambari ya kumbukumbu DC.297/507/01/39 (kwa shule za msingi) na Na. DC.297/507/01/40 (kwa shule za sekondari) ya tarehe 28 Desemba 2015, kwa ajili ya kutoa elimu bila malipo, inaitaka serikali kutoa fidia ya Sh. 10,000 na Sh. 25,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kwa shule za msingi na sekondari mtawalia.

Pia, aya ya 2.0 & 3.2(vii) ya Waraka Na. 3 wa mwaka mwaka 2016 wenye nambari ya kumbukumbu FD/OKE/NE/Vol.I/01/71 kuhusu utekelezaji wa elimu bila malipo ulibatilisha matumizi ya waraka wa elimu Na. 9 wa mwaka 1998, waraka Na. 11 wa mwaka 2004, waraka Na. 8 wa mwaka 2011, waraka Na. 1 wa mwaka 2021, na waraka Na. 1 wa mwaka 2013. Aidha, serikali iliazimia kulipa ada za shule kwa shule za sekondari za bweni na kutwa.

Pia, Serikali iliazimia kutoa 50% na 60% ya Sh. 25,000 na Sh. 10,000 zilizotengwa kwa ajili ya ruzuku kwa shule za sekondari na msingi na kuzipeleka moja kwa moja katika shule husika.

Aidha, aya ya 3.5(i) ya Waraka Na. 3 wa mwaka 2016 inamtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji/Manispaa/Mji na Wilaya kuandaa mipango na bajeti ya utoaji wa elimu bila malipo kwa kuzingatia idadi ya wanafunzi waliopo ili kutumika kama msingi wa mgao wa fedha kwa ajili ya ruzuku ya elimu bila malipo.

Mamlaka tisa za serikali za mitaa zilitenga bajeti ya Sh. bilioni 7.45 kwa ajili ya ruzuku ya chakula na ruzuku ya uendeshaji wa shule. Uandaaji wa bajeti kwa kuzingatia idadi ya wanafunzi kwa kiwango cha Sh. 540,000 kwa ajili ya ruzuku ya chakula kwa kila mwanafunzi na ruzuku ya uendeshaji wa shule kwa kiwango cha Sh. 6,000 na Sh. 12,500 kwa kila mwanafunzi wa shule za msingi na sekondari mtawalia, ulibaini kuwa ilihitajika bajeti ya Sh. bilioni 9.92. Hivyo, kusababisha bajeti iliyoandaliwa na kuidhinishwa kuwa chini kwa kiasi cha Sh. bilioni 2.47. kama ilivyofafanuliwa katika **Kiambatisho Na.39.**

Bajeti iliyotengwa kuwa chini ya kiwango cha Sh. 540,000 ya chakula kwa mwanafunzi wa bweni katika shule ya sekondari na msingi, na Sh. 6000 na Sh. 12,500 ya ruzuku ya uendeshaji kwa shule za msingi na sekondari mtawalia inasababisha fedha iliyotengwa kugawanywa kwa wanafunzi kwa uwiano sawia; hivyo, kuathiri utoaji wa elimu bora.

**Ninapendekeza kuwa Serikali, kupitia OR-TAMISEMI, ifanye uchambuzi wa kina wa bajeti kutoka katika mamlaka za serikali za mitaa wakati wa uandaaji wa mpango na bajeti ili kuhakikisha kuwa mgawanyo wa ruzuku kwa vipengele husika vya ruzuku ya elimu bila malipo, yaani ruzuku ya uendeshaji wa shule, ruzuku ya chakula, na fidia ya ada, unazingatia mahitaji halisi kulingana na idadi ya wanafunzi walioandikishwa.**

## 12.5 Kutosambazwa kwa vitabu vya kiada vyenye thamani ya Sh. bilioni 10.6

Aya ya 3.2(vii) ya Waraka Na.3 wa mwaka 2016 wenye nambari ya kumbukumbu ED/OKE/NE/Vol.I/01/71 wa tarehe 25 Mei 2016 kuhusu utekelezaji wa mpango wa elimu bila malipo unaelekeza OR-TAMISEMI kutenga 40% na 50% ya fedha za ruzuku ya uendeshaji kwa shule za msingi na sekondari mtawalia kwa ajili ya ununuzi wa vitabu.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, OR-TAMISEMI ililipa jumla ya Sh. bilioni 10.6 kwa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya shule za msingi Tanzania Bara. Taasisi hiyo iliingia mikataba na kampuni nne za uchapishaji kwa ajili ya uchapishaji na usambazaji wa vitabu milioni 2.51, lakini menejimenti husika hazikuweza kuwasilisha taarifa za kina kuhusiana na kusambazwa kwa vitabu vya kiada kwenye shule za msingi.

Kutosambazwa kwa vitabu vya kiada katika shule za msingi kumesababishwa na ucheleweshwaji wa uchapishaji wa vitabu, kutokuwapo kwa hati ya makubaliano kati ya OR-TAMISEMI na Taasisi ya Elimu Tanzania ambayo inaweka masharti ya uchapishaji na usambazaji wa vitabu kwa shule za msingi.

Kwa maoni yangu, kutosambazwa kwa vitabu vya kiada vilivyonunuliwa na serikali kunazorotesha utoaji wa elimu bora na huenda lengo la uwiano 1:1 wa kitabu kwa mwanafunzi ifikapo 2025/26 lisifikiwe kwa wakati. Vilevile, mapitio ya uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi, yalibaini upungufu wa vitabu 936,780 sawa na 57% katika mamlaka nne za serikali za mitaa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.87.**

**Jedwali Na. 87: Upungufu wa vitabu vya kiada katika shule za msingi**

| Na. | Halmashauri | Mahitaji | Vilivyopo | Upungufu | % ya Upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Hai | 220,530 | 124,390 | 96,140 | 44 |
| 2 | H/W Magu | 528,738 | 218,543 | 310,195 | 59 |
| 3 | H/W Siha | 73,782 | 68,402 | 5,380 | 7 |
| 4 | H/M Kinondoni | 825,091 | 300,026 | 525,065 | 64 |

| Na. | Halmashauri | Mahitaji | Vilivyopo | Upungufu | % ya Upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumla | | 1,648,141 | 711,361 | 936,780 | 57 |

**Chanzo:** *Taarifa za Idara ya Elimu Msingi na Sekondari*

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI ifanye ufuatiliaji wa karibu kwa Taasisi ya Elimu Tanzania na kuhakikisha vitabu lengwa vinasambazwa kwenye shule za msingi. Aidha, serikali iendelee kutenga bajeti na kutoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitabu ili kufikia lengo la uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi ifikapo 2025/26.**

# SURA YA KUMI NA TATU



## UFANISI WA UENDESHAJI KATIKA SEKTA YA AFYA

**13.0 Utangulizi**

Wizara ya Afya, kupitia tangazo la Serikali Na.144 la tarehe 22 Aprili 2016, imepewa jukumu la kuandaa mikakati, mpangokazi na sera ya afya na kufanya tathmini, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wake katika maeneo yote. OR-TAMISEMI inatakiwa kutafsiri sera hizi, kusimamia, kuratibu na kuwezesha utekelezaji wake sambamba na Mpangomkakati wa Sekta ya Afya.

Mamlaka za serikali za mitaa, chini ya usimamizi wa wakurugenzi watendaji wa halmashauri, zimeanzisha Timu ya Usimamizi wa Afya ngazi ya Halmashauri (CHMT) yenye jukumu la kusimamia na kutoa huduma za afya katika halmashauri zao. Hii ni pamoja na kuandaa na kutekeleza Mpango Kabambe wa Afya katika ngazi ya Halmashauri (CCHP) kwa ajili ya huduma za afya ya msingi na mipango ya afya ya ngazi ya jamii kwa kila kata na kijiji.

Sura hii inatathmini ufanisi wa utendaji katika sekta ya afya, hususani kuhusu mahitaji ya utoaji wa huduma bora za afya, ikiangazia utoshelevu wa miundombinu ya afya, upatikanaji wa bidhaa za afya, masuala yanayohusiana na rasilimaliwatu katika sekta ya afya, na ufadhili wa huduma za afya.

**13.1 Tathmini ya utoshelevu wa miundombinu katika sehemu za kutolea huduma ya afya**

**13.1.1 Kuchelewa kukamilika kwa sehemu za kutolea huduma ya afya zenye thamani ya Sh. bilioni 13.50**

Katika ukaguzi wa mwaka huu wa fedha, nimeendelea kubaini kuwa katika mamlaka 17 za serikali za mitaa nilizokagua, ujenzi wa sehemu za kutolea huduma ya afya zenye thamani ya Sh. bilioni 13.50 umeshindwa kukamilika kwa wakati. Kufuatia hali hiyo, mamlaka sita za serikali za

mitaa ziliwasilisha maombi ya Sh. bilioni 3.85 za ziada kwa OR-TAMISEMI ili kukamilisha miradi hiyo.

Kuna uwezekano wa miradi iliyoombewa fedha za ziada kuendelea kuchelewa kwa kuwa ni dhahiri kuwa maombi hayo yanapaswa kupitia mchakato mrefu wa kibajeti katika ngazi za halmashauri na wizara. Mchanganuo wa miradi ya Afya ambayo ukamilishwaji wake umechelewa upo katika **Kiambatisho Na.40**.

Uongozi wa mamlaka husika ulitoa maelezo kuwa ucheleweshwaji huo umetokana na upungufu wa fedha zilizotolewa, ambao ulisababishwa na makadirio yasiyo halisi yaliyofanywa na OR-TAMISEMI. Imekuwa kawaida kwa mamlaka za serikali za mitaa kuchelewa kukamilisha miradi ya sekta ya afya.

Licha ya mapendekezo ya mara kwa mara katika ripoti zangu zilizopita, bado suala hili halijapata ufumbuzi kutoka kwa viongozi wanaohusika.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI ihakikishe inazishirikisha ipasavyo mamlaka za serikali za mitaa wakati wa kuandaa bajeti za miradi ili gharama za mradi ziendane na makadirio ya fedha zinazopangwa. Aidha, ninaishauri OR-TAMISEMI kuharakisha mchakato wa bajeti wa kupata mgao wa fedha za ziada ili kukamilisha miradi iliyokwama.**

### 13.1.2 Upungufu wa magari ya kubeba wagonjwa katika Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya

Tathmini yangu ya Hospitali za Wilaya katika Halmashauri 20 imebaini kuwa Hospitali 10 kati ya 14 za Wilaya hazina magari ya kubebea wagonjwa huku vituo vya afya 43 kati ya 75 havina magari ya kubebea wagonjwa. Vilevile, hospitali moja ya wilaya na vituo vinne vya afya vilikuwa na magari ya kubebea wagonjwa mabovu kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.41.**

Hali hii ni kinyume na Aya ya 7.1.1 (v) ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 ambayo inataka vituo cha afya kuwa na magari ili kurahisisha usafiri wa wagonjwa wanaohitaji matibabu ya dharura.

Pamoja na kutambua juhudi ambazo tayari zimechukuliwa na serikali katika kuboresha secta ya afya, sambamba na ufinyu wa bajeti ikilinganishwa na mahitaji yaliyopo, bado kuna haja ya OR-TAMISEMI kuwa na mpango mkakati wa haraka wa kukabiliana na uhaba mkubwa wa

magari ya kubeba wagonjwa uliopo katika hospitali na vituo vya afya nchini.

**Naishauri OR-TAMISEMI ijumuishe katika mpangomkakati wake, hatua za muda mfupi na mrefu ili kukabiliana na upungufu uliopo wa magari ya kubeba wagonjwa, hususan katika hospitali za wilaya na vituo vya afya. Aidha, OR-TAMISEMI inashauriwa kuwa na ubunifu kwa kutafuta mbinu mbadala za huduma za usafiri wa dharura ambao ni nafuu zaidi kama suluhisho la muda mfupi.**

### 13.1.3 Upungufu wa Jenereta za dharura katika Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya

Tathmini yangu ya hali ya utayari ya vituo vya afya wakati dharura ya kukatika kwa umeme ilibaini kuwa Hospitali 2 kati ya 14 za Wilaya hazina jenereta za dharura huku vituo vya afya 49 kati ya 75 havikuwa na jenereta za dharura. Vilevile, hospitali mbili za Wilaya na Vituo vya Afya vitatu vilikuwa na jenereta mbovu. Mgawanyo wa majenereta katika vituo vyote vya afya umeoneshwa katika **Kiambatisho Na.42.**

Ni maoni yangu kuwa, kuna umuhimu wa kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vinakuwa na mfumo wa umeme wa dharura, hususani katika nyakati za matibabu ya dharura, ili kupunguza athari kwa wagonjwa na utendajikazi wa vituo vya kutolea huduma pindi kunapojitokeza changamoto za umeme.

**Naishauri OR-TAMISEMI kujumuisha katika mpangomkakati wake, hatua za muda mfupi na mrefu ili kukabiliana na uhaba uliopo wa majenereta ya dharura, hususan katika hospitali za wilaya na vituo vya Afya. Vivyo hivyo, OR-TAMISEMI inashauriwa kuja na mbinu mbadala kama vile kufunga mifumo ya umeme utokanao na nishati ya jua, hususani katika sehemu za kutolea huduma za afya zilizopo vijijini.**

### 13.1.4 Kukosekana kwa Vifaa Muhimu vya Matibabu katika Sehemu za Kutolea huduma za afya

Tathmini niliyoifanya katika mamlaka 20 za serikali za mitaa imebaini kuwa kati ya vifaa-tiba muhimu 1,359 vinavyohitajika katika hospitali za wilaya na vituo vya afya, vifaa 703 vilithibitika kuwapo, wakati vifaa 27 vilibainika kuwa na hitilafu; hivyo kufanya jumla ya upungufu wa vifaa-tiba muhimu kufikia 629 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.88** na **Kiambatisho Na.43**.

**Jedwali Na. 88: Uhaba wa vifaa-tiba katika sehemu za kutolea huduma za afya**

| Vifaatiba | Mahitaji | Vilivyopo | Vibovu | Pungufu |
|---|---|---|---|---|
| Mashine ya Ganzi | 140 | 69 | 4 | 67 |
| Majokofu ya Kutunzia Damu | 177 | 92 | 4 | 81 |
| Vitanda vya Kujifungulia | 535 | 321 | | 214 |
| Darubini | 256 | 139 | 15 | 102 |
| Mashine ya Ultra-sound | 142 | 54 | 2 | 86 |
| Mashine ya Picha ya Mionzi | 109 | 28 | 2 | 79 |
| **Jumla** | **1,359** | **703** | **27** | **629** |

Hivyo, uhaba wa vifaa-tiba uliosababishwa na vilivyopo kutofanya kazi au kutonunuliwa ni kikwazo katika kutoa huduma stahiki za afya.

**Ninapendekeza kwamba OR-TAMISEMI ihakikishe kunakuwa na bajeti na msaada wa kiufundi kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya kununua vifaa vinavyohitajika pamoja na kukarabati vifaa-tiba vyenye kasoro.**

**Mbinu hii itasaidia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za afya na kuhakikisha kuwa vifaa-tiba vilivyopo vinaleta tija kama ilivyokusudiwa.**

### 13.1.5 Vifaa-tiba vilivyonunuliwa na sehemu za huduma za afya zilizokamilika lakini hazitumiki zenye thamani ya Sh. bilioni 4.94

Nilibaini kuwa sehemu za kutolea huduma za afya katika mamlaka 10 za serikali za mitaa zilinunua vifaa-tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 2.42.

Hata hivyo vifaa hivyo havikutumika kama ilivyokusudiwa kutokana na sababu kadhaa. Miongoni mwazo ni kutokukamilika kwa ujenzi wa baadhi ya majengo katika sehemu za kutolea huduma za afya, ambapo vifaa hivyo vilipangwa kutumika; masuala ya kiufundi; pamoja na wataalamu wenye ujuzi wa kutumia vifaa maalumu. Maelezo yanaoneshwa kwenye **Jedwali Na.89.**

**Jedwali Na. 89: Vifaa tiba vilivyonunuliwa lakini havitumiki**

| Na | Halmashauri | Sehemu ya Huduma ya Afya | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | Zahanati ya Mwandet | 100,000,000 |
| | | Kituo cha Afya cha Oldonyosambu | 100,000,000 |
| | | Kituo cha Afya cha Olorien | 100,000,000 |
| 2. | H/W Buchosa | Hospitali ya Wilaya ya Buchosa | 398,286,828 |
| 3. | H/Jiji Dodoma | Kituo cha Afya cha Chang'ombe | 148,930,000 |
| | | Zahanati Mpamaa | 47,251,000 |
| | | Kituo cha Afya cha Nkuhungu | 59,490,600 |

| Na | Halmashauri | Sehemu ya Huduma ya Afya | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| | | Kituo cha Afya cha Zepisa | 64,930,600 |
| 4. | H/Mji Kibaha | Kituo cha Afya cha Pangani | 186,627,489 |
| 5. | H/W Kwimba | Hospitali ya Wilaya ya Kwimba | 411,684,115 |
| 6. | H/W Meru | Kituo cha Afya cha Makiba | 43,497,630 |
| 7. | H/W Mkalama | Zahanati ya Gumanga | 113,862,600 |
| | | Zahanati ya Ilunda | 78,658,720 |
| 8. | H/W Lushoto | Vituo vya Afya vya Kwekanga, Mtae, Lunguza na Zahanati za Boheloi na Kigulunde | 263,833,150 |
| 9. | H/W Mlele | Hospitali ya Wilaya ya Mllele na Kituo cha Afya cha Ilunde | 110,493,549 |
| 10. | H/W Kiteto | Vituo vya Afya na Zahanati | 196,000,000 |
| **Jumla** | | | **2,423,546,281** |

Pia, nilibaini kuwa mamlaka sita za serikali za mitaa zilikamilisha ujenzi wa sehemu za kutolea huduma za afya wenye thamani ya Sh. bilioni 1.75 lakini majengo hayo hayatumiki kikamilifu.

Katika vituo kadhaa vya afya vilivyoanza kufanya kazi, kulikuwa na huduma chache katika baadhi ya idara. Maelezo ya vituo vya afya ambavyo havitumiki ipasavyo yametolewa katika **Jedwali Na.90**.

**Jedwali Na. 90: Miundombinu ya afya ambayo haitumiki ipasavyo**

| Na. | Halmashauri | Maelezo ya Mradi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kilwa | Zahanati nne zilizokamilika, ambazo ni Tilawandu, Hongwe, Mirumba na Liwiti | 200,000,000 |
| 2. | H/W Lushoto | Jengo la Upasuaji na wodi ya Wazazi na Jengo la kufua katika kituo cha afya Lunguza. | 250,000,000 |
| 3. | H/W Tandahimba | Kituo cha Afya Litehu | 250,000,000 |
| 4. | H/W Tandahimba | Kituo cha Afya Maheha | 400,000,000 |
| 5. | H/W Tandahimba | Kituo cha Afya  Kitama | 400,000,000 |
| 6. | H/W Korogwe | Majengo ya OPD na Maabara katika kituo cha Afya Mnyuzi | 250,000,000 |
| **Jumla** | | | **1,750,000,000** |

Mamlaka za serikali za mitaa zilihusisha miundombinu isiyotumika katika sekta ya afya na uhaba wa vifaa-tiba pamoja na dawa na uhaba wa watumishi katika kada ya Afya.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI kuhakikisha fedha zinatengwa ili kuwezesha upatikanaji wa wataalamu na vifaa-tiba vya kutosha ili majengo ya kutolea huduma za afya yaliyokamilika yaanze kufanya kazi. Pia, ninapendekeza vituo vya afya vihakikishe ununuzi wa bidhaa za matibabu uendane na mahitaji yao halisi. Ununuzi ufanyike pale**

**inapothibitika kwamba miundombinu muhimu kwa ajili ya kuwezesha matumizi ya vifaa hivyo imekamilika.**

## 13.2 Tathmini ya Hali ya Rasilimaliwatu katika Kada ya Afya

### 13.2.1 Athari katika utoaji wa huduma kutokana na uhaba mkubwa wa Wahudumu wa Afya

Katika tathmini yangu kuhusu utoaji huduma za afya kwa jamii katika halmashauri, nilibaini kuwa hospitali na vituo vya afya vya wilaya katika mamlaka za serikali za mitaa 12 zilizofanyiwa ukaguzi havikuweza kutoa huduma stahiki za afya kwa wagonjwa kutokana na upungufu wa watumishi, kinyume na miongozo ya kiutendaji inayotolewa mara kwa mara na OR-TAMISEMI na Wizara ya Afya.

Nilifanya ulinganifu wa wahudumu wa afya wanaohitajika na waliopo na nikagundua kuwa vituo vya afya nilivyovikagua vilikuwa na mahitaji ya wahudumu wa afya 3,827. Hata hivyo, wahudumu waliopo ni 1,497 tu sawa na 39% kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.91** na **Kiambatisho Na.44** mtawalia.

**Jedwali Na. 91: Uhaba wa wahudumu wa afya**

| Kada | Mahitaji | Waliopo | Pungufu | Upungufu (%) |
|---|---|---|---|---|
| Ofisa Tabibu | 545 | 229 | 316 | 58 |
| Wataalamu wa Meno | 122 | 18 | 104 | 85 |
| Madaktari | 393 | 160 | 233 | 59 |
| Wauguzi | 2,471 | 1,022 | 1,449 | 59 |
| Wataalamu wa Macho | 107 | 8 | 99 | 93 |
| Wafamasia | 189 | 60 | 129 | 68 |
| **Jumla** | **3,827** | **1,497** | **2,330** | **61** |

Kwa ujumla, tathmini yangu ilibaini kuwa vituo vya afya vinakabiliwa na upungufu mkubwa wa wahudumu wa afya wenye vigezo stahiki katika kada na sekta mbalimbali za afya, hususani katika maeneo ya vijijini.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI na Wizara ya Afya kutenga fedha za kutosha kwa sekta ya afya ili kuhakikisha kuwa sehemu za kutolea huduma katika mamlaka za serikali za mitaa zinakuwa na wahudumu wa afya wa kutosha. Watumishi watakaopatikana watasaidia kupunguza pengo lililopo na kuwezesha utoaji wa huduma za stahiki za afya kwa jamii.**

## 13.3 Tathmini ya huduma inayotolewa na bohari ya dawa (MSD) kwa halmashauri

Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ilianzishwa kwa Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 kama idara inayojitegemea chini ya Wizara ya Afya, yenye jukumu la kuandaa, kutunza na kusimamia mfumo wa uzalishaji, ununuzi, uhifadhi na ufanisi katika usambazaji wa bidhaa za afya zilizoidhinishwa kwa vituo vyote vya afya vya umma na kwa gharama nafuu.

### 13.3.1 Vifaa-tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.78 kuchelewa kupokelewa kutoka MSD

Katika mwaka wa fedha unaoangaziwa, mamlaka 15 za serikali za mitaa zililipa MSD kiasi cha Sh. bilioni 3.05 kwa ajili ya kununua vifaatiba mbalimbali, ambapo bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 1.78 sawa na 58% hazikupokelewa kinyume na Kanuni ya 242 (1) na 248 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013. Maelezo ya bidhaa za afya ambazo hazikupokelewa yameoneshwa kwenye **Jedwali Na.92**.

**Jedwali Na. 92: Vifaa-tiba ambavyo havikupokelewa kutoka MSD**

| Na. | Halmashauri | Malipo kwa MSD (Sh.) | Vifaa vilivyopokelewa (Sh.) | Vifaa havijapokelewa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Buhigwe | 500,000,000 | 41,003,096 | 458,996,904 |
| 2. | H/W Tandahimba | 373,259,592 | 75,182,794 | 298,076,798 |
| 3. | H/W Mbeya | 312,299,309 | 34,942,252 | 277,357,057 |
| 4. | H/W Malinyi | 188,655,947 | 0 | 188,655,947 |
| 5. | H/Mji Tarime | 146,941,299 | 18,601,299 | 128,340,000 |
| 6. | H/W Lushoto | 110,000,000 | 10,545,258 | 99,454,742 |
| 7. | H/W Rorya | 349,022,000 | 261,781,000 | 87,241,000 |
| 8. | H/W Magu | 243,297,233 | 160,066,354 | 83,230,879 |
| 9. | H/W Mtama | 68,374,099 | 0 | 68,374,099 |
| 10. | H/W Kondoa | 150,000,000 | 115,000,000 | 35,000,000 |
| 11. | H/W Shinyanga | 22,255,462 | 0 | 22,255,462 |
| 12. | H/W Sengerema | 85,487,500 | 73,561,500 | 11,926,000 |
| 13. | H/W Kiteto | 6,680,000 | 0 | 6,680,000 |
| 14. | H/W Rufiji | 486,000,000 | 480,348,000 | 5,652,000 |
| 15. | H/W Mkinga | 5,639,372 | 0 | 5,639,372 |
| **Jumla** | | **3,047,911,813** | **1,271,031,553** | **1,776,880,260** |

Kwa maoni yangu, uchelewaji wa mapokezi ya bidhaa za Afya unachelewesha huduma za afya na kusababisha Serikali kushindwa kufikia malengo kwa ujumla katika utoaji huduma za afya.

**Napendekeza mamlaka za serikali za mitaa zifuatilie kwa karibu Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ili kuhakikisha kuwa bidhaa ambazo hazijawasilishwa zinawasilishwa kwa wakati.**

**Pia, nashauri OR-TAMISEMI na MSD zifanye tathmini ya pamoja ya matakwa ya MSD kuzitaka mamlaka za serikali za mitaa kulipa kabla ya kupokea bidhaa za afya kwa kuwa utaratibu huu unakiuka Kanuni ya 242 (1) na 248 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013.**

### 13.3.2 Kiasi kikubwa cha Bakaa ya Fedha zilizowekwa MSD - Sh. bilioni 8.37

Katika mwaka wa fedha unaoangaziwa, mamlaka 15 za serikali za mitaa zilikuwa na amana kiasi cha Sh. bilioni 11.91 katika Akaunti ya MSD zilizopokelewa kutoka Wizara ya Afya.

Hata hivyo, MSD iliweza kusambaza bidhaa za afya kwa mamlaka za serikali za mitaa zenye thamani ya Sh. bilioni 3.61 sawa na 30% na kubakia na kiasi cha Sh. bilioni 8.37 sawa na 70%, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.93.**

**Jedwali Na. 93: Bidhaa za afya ambazo hazikupokelewa kutoka MSD**

| Na | Halmashauri | Kiasi Kilichopo (Sh.) | Matumizi (Sh.) | Bakaa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Kahama | 2,049,428,679 | 616,455,304 | 1,432,973,376 |
| 2. | H/W Masasi | 1,480,497,056 | 182,540,952 | 1,297,956,104 |
| 3. | H/W Maswa | 1,410,085,263 | 583,667,291 | 826,417,971 |
| 4. | H/Mji Mbinga | 763,041,130 | 0 | 763,041,130 |
| 5. | H/W Bariadi | 739,076,258 | 0 | 739,076,258 |
| 6. | H/Mji Masasi | 747,447,413 | 72,271,249 | 675,176,164 |
| 7. | H/W Arusha | 1,014,795,048 | 349,186,783 | 665,608,265 |
| 8. | H/Mji Bariadi | 852,293,741 | 506,755,922 | 417,751,301 |
| 9. | H/W Korogwe | 345,765,396 | 0 | 345,765,396 |
| 10. | H/W Tunduru | 448,843,923 | 103,501,667 | 345,342,257 |
| 11. | H/W Longido | 541,125,720 | 293,909,876 | 248,003,045 |
| 12. | H/W Nyang'hwale | 808,725,163 | 576,545,442 | 232,179,723 |
| 13. | H/W Namtumbo | 175,667,618 | 0 | 175,667,618 |
| 14. | H/W Madaba | 155,424,432 | 0 | 155,424,432 |
| 15. | H/W Ruangwa | 374,817,127 | 322,808,936 | 52,008,221 |
| Jumla | | **11,907,033,967** | **3,607,643,422** | **8,372,391,261** |

Kwa kuzingatia uhaba wa rasilimali na ufinyu wa fedha katika sekta ya afya ambazo zimekua zikitengwa miaka ya hivi karibuni, kuwapo kwa bakaa kubwa ya fedha za afya ambazo hazitumiki ni jambo linalofikirisha namna ya kukabiliana nalo.

**Ni muhimu kwa OR-TAMISEMI na Wizara ya Afya kuchunguza kwa kina na kutafuta ufumbuzi wa vikwazo vinavyokabili vituo vya kutolea huduma za afya wakati vinapojaribu kununua bidhaa za afya kupitia fedha zao zilizopo Bohari Kuu ya Dawa (MSD).**

**Aidha, katika hali ambapo bidhaa za afya hazipatikani MSD, kuwe na utaratibu mbadala ili kuwezesha mamlaka za serikali za mitaa kununua bidhaa za afya kutoka kwa wasambazaji wengine. Hatua hii ni muhimu ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika matumizi ya fedha na kuboresha upatikanaji wa bidhaa za afya kwa umma.**

## 13.4 Tathmini ya Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF)

Waraka Na. 1 ulitolewa mwaka 2018, unaitaka Sekretarieti ya Mkoa kusimamia muundo ulioboreshwa wa usimamizi wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF). Katika tathmini yangu ya utekelezaji wa Waraka huo Na. 1 wa 2018, nilibaini upungufu ufuatao:

### 13.4.1 Fedha za makusanyo ya iCHF ambazo hazijatumika -Sh. bilioni 2.25

Katika mwaka wa fedha 2022/23, sekretarieti 17 za mikoa zilikusanya Sh. bilioni 3.34 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za iCHF. Pia, kulikuwa na salio kutoka mwaka uliopita kiasi cha Sh. bilioni 2.65 na kufanya jumla ya fedha zote kufikia Sh. bilioni 5.99.

Hata hivyo, ni Sh. bilioni 3.74 pekee ndizo zilizotumika kutoka katika mfuko huu, hivyo kubaki na salio la Sh. bilioni 2.25 ambalo halikutumika, sawa na 38% ya fedha zote zilizokuwapo katika mwaka wa fedha unaoangaziwa kama ilivyobainishwa katika **Jedwali Na.94**.

**Jedwali Na. 94: Ufanisi wa kifedha wa mfuko wa iCHF**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---:|
| Salio Anzia 01/07/2022 | 2,645,535,931 |
| Jumlisha: Fedha iliyopokelewa | 3,342,250,799 |
| Jumla ya fedha za iCHF Zilizokuwapo | 5,987,786,730 |
| Toa: Matumizi katika mwaka husika | 3,735,224,049 |
| **Bakaa 30/06/2023** | **2,252,562,681** |

**Chanzo:** Taarifa za Fedha

Kwa ujumla, suala la salio ambalo halijatumika linashawishi matumizi mabaya ya fedha za iCHF. Aidha, fedha nyingi ambazo hazijatumika huvutia umakini wa umma na wasiwasi kutokana na uhaba wa rasilimali za umma na nakisi kubwa ya kifedha ambayo sekta ya afya inakabiliwa nayo katika miaka ya hivi karibuni.

Nilihusisha fedha ambazo hazijatumika na uzembe katika mfumo na utaratibu wa jumla wa usimamizi wa mpango wa iCHF.

**Ninapendekeza sekretarieti za mikoa husika kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha na kuhakikisha kuwa fedha zinazokusanywa zinatumika kwa wakati na kwa malengo yaliyokusudiwa.**

### 13.4.2 Kutofikiwa kwa malengo ya uandikishaji wa wanachama wa iCHF

Sekretarieti za mikoa ziliagizwa na OR-TAMISEMI kufanya uhamasishaji kwa jamii ili watu wajiunge na mfuko wa iCHF na kuhakikisha kila mkoa unafikia lengo la uandikishaji wa kaya mpya, rejea Waraka Na. 1 (Na.CD.151/161/01') 'C"/46) wa tarehe 06 Aprili 2018.

Hata hivyo, nilibaini kuwa katika mamlaka 52 za serikali za mitaa, Kaya zilizoandikishwa hadi tarehe 30 Juni 2023 zilikuwa 103,008 kati ya kaya 604,519 zilizolengwa sawa na 17%, wakati ni kaya 22,414 tu sawa na 22% ya kaya zilizoandikishwa zilikuwa na bima iliyo hai. Hali ya uandikishaji kwa sekretarieti za mikoa na kwa kila halmashauri imeoneshwa katika **Jedwali Na.95** na **Kiambatisho Na.45**.

**Jedwali Na. 95: Uandikishaji katika ngazi ya Sekretarieti ya Mkoa**

| Maelezo | Idadi |
|---|---:|
| Idadi ya sekretarieti za mikoa | 8 |
| Idadi ya Kaya | 2,191,195 |
| Idadi ya Usajili iliyolengwa 2022/23 | 604,519 |
| Kaya zilizosajiliwa 2022/23 | 103,008 |
| Kaya Zisizosajiliwa 2022/23 | 501,511 |
| Kaya zenye Usajili Hai | 22,414 |
| Asilimia ya Kaya Zilizosajiliwa 2022/23 | 17 |

Pamoja na maboresho yaliyofanywa, ufanisi katika uandikishaji wa wanachama wapya wa mfuko wa iCHF bado hauridhishi. Hali hii inatishia ustawi na uendelevu wa mfuko.

Menejimenti ya mamlaka ya serikali za mitaa ilihusisha kushindwa kufikia malengo ya uandikishaji na ufinyu wa bajeti iliyotengwa kwa ajili ya uhamasishaji na changamoto za mfumo wa IMIS hususan, katika mchakato wa usajili, pamoja na maofisa uandikishaji katika ngazi za Kata/Vijiji kuacha kazi.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji, kutatua vikwazo vya kibajeti, hususani katika masuala yanayohusu uhamasishaji, yatatuliwe ipasavyo na kwa wakati ili kuongeza ufanisi wa Mfuko.**

### 13.4.3 Ruzuku ya Makusanyo ambayo haijatolewa- Sh. bilioni 1.9

Katika Ukaguzi wa makusanyo ya fedha za iCHF ngazi ya Mikoa nilibaini kuwa wanufaika wa iCHF katika mamlaka 11 za serikali za mitaa walichangia jumla ya Sh. bilioni 1.9. Hata hivyo, Serikali Kuu ilishindwa kutoa ruzuku sawa kulingana na fedha zilizokusanywa ili kusaidia Mfuko, kinyume na Aya ya 1.1 ya mwongozo wa iCHF wa mwaka 2018 kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na.96.**

**Jedwali Na. 96: Ruzuku ya makusanyo ambayo haijatolewa**

| Na. | Halmashauri | Bakaa ya Ruzuku (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dar Es Salaam | 998,460,000 |
| 2. | H/W Kondoa | 347,018,412 |
| 3. | H/W Chamwino | 148,701,873 |
| 4. | H/W Manyara | 105,360,000 |
| 5. | H/Jiji Dodoma | 93,174,326 |
| 6. | H/W Mpwapwa | 55,953,479 |
| 7. | H/W Njombe | 50,310,000 |
| 8. | H/W Kongwa | 43,851,689 |
| 9. | H/W Chemba | 32,947,145 |
| 10. | H/W Bahi | 16,459,778 |
| 11. | H/Mji Kondoa | 7,673,235 |
| **Jumla** | | **1,899,909,937** |

**Ninapendekeza Serikali Kuu itenge na kupeleka fedha za iCHF kwa sekretarieti za mikoa mara moja. Mgao huu unapaswa kujumuisha malimbikizo yote ya kusaidia utekelezaji na uendelevu wa iCHF katika ngazi ya jamii. Hii itahakikisha kwamba rasilimali muhimu za kifedha zinapatikana kwa ajili ya uendeshaji bora wa mpango wa ICHF na kunufaisha jamii inayohudumia.**

## 13.5 Tathmini ya uwezekano wa hasara na ubadhirifu wa fedha za Sekta ya Afya

### 13.5.1 Hasara inayotokana na madai yaliyokataliwa na NHIF- Sh. milioni 908.71

Kifungu cha 27(2) cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura ya 395 kinasema Mfuko unaweza kukataa au kupunguza malipo ya madai ya uongo au yasiyo sahihi au pale wadai wanaposhindwa kuzingatia kanuni au kanuni za malipo ya madai yaliyotolewa chini ya Sheria hii.

Katika tathmini niliyoifanya katika mamlaka 26 za serikali za mitaa, niligundua kuwa NHIF imekataa kulipa madai ya jumla ya Sh. milioni 908.71. Kukataliwa huku kumetokana na dosari mbalimbali, ikiwamo uidhinishaji batili, taarifa za magonjwa zisizo sahihi, na ukiukwaji wa miongozo ya matibabu. Rejea **Jedwali Na.97** kwa maelezo zaidi.

**Jedwali Na. 97: Madai yaliyokataliwa na NHIF**

| No. | Health facilities | Rejected claims (TZS) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Bagamoyo | 58,748,796 |
| 2. | H/W Bariadi | 8,950,290 |
| 3. | H/Mji Bariadi | 23,642,507 |
| 4. | H/W Biharamulo | 15,500,730 |
| 5. | H/W Chamwino | 155,041,755 |
| 6. | H/Jiji Dodoma | 175,265,670 |
| 7. | H/W Hai | 59,702,634 |
| 8. | H/W Hanang | 8,018,817 |
| 9. | H/W Itigi | 3,682,448 |
| 10. | H/M Kahama | 23,384,520 |
| 11. | H/W Kaliua | 14,495,365 |
| 12. | H/W Kasulu | 13,565,260 |
| 13. | H/M Kigamboni | 44,463,195 |
| 14. | Kigoma Ujiji | 22,946,885 |
| 15. | H/W Kilosa | 53,810,185 |
| 16. | H/W Kishapu | 14,571,395 |
| 17. | H/W Korogwe | 29,240,956 |
| 18. | H/Mji Korogwe | 10,146,310 |
| 19. | H/W Lushoto | 14,134,153 |
| 20. | H/Mji Masasi | 23,824,090 |
| 21. | H/W Maswa | 27,717,615 |
| 22. | H/W Mbogwe | 10,662,670 |
| 23. | H/Mji Mbulu | 9,803,516 |
| 24. | H/W Mkinga | 49,353,536 |
| 25. | H/Mji Nzega | 12,904,378 |
| 26. | H/W Sumbawanga | 25,129,577 |
| | **Total** | **908,707,253** |

Ni muhimu kutambua kuwa hasara inayotokana na madai yaliyokataliwa inaathiri moja kwa moja mtaji wa vituo vya kutolea huduma za afya. Pia, inapunguza uwezo vituo hivyo kutoa huduma muhimu za afya kwa Jamii.

Hivyo ni vyema kushughulikia na kurekebisha dosari zinazosababisha kukataliwa kwa madai hayo ili kuongeza ufanisi wa matumizi bora ya rasilimali na utoaji wa huduma za afya ambao ni endelevu.

**Ninapendekeza vituo vya kutolea huduma za afya vikague kwa uangalifu madai yake kabla ya kuyawasilisha NHIF kwaajili ya kulipwa. Pia, OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na NHIF, waimarishe ukaguzi wa ndani pamoja na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa kada ya afya ili wajaze kwa usahihi fomu za madai kutoka NHIF.**

**Hatua hizi zitasaidia kuzuia kujirudia kwa dosari hizo na kusaidia madai kushughulikiwa kwa urahisi na kurahisisha mchakato ya ulipaji, hivyo kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa ujumla.**

### 13.5.2 Hasara kutokana na ununuzi kutoka kwa wazabuni binafsi bila taarifa ya kukosekana kwa bidhaa kutoka MSD -Sh. milioni 101.51

Kwa mujibu wa Kanuni ya 140 (5) ya Kanuni za Ununuzi ya Umma za mwaka 2013, taasisi nunuzi inatakiwa kupata taarifa ya kutopatikana kwa bidhaa za matibabu kutoka MSD kabla ya kuzinunua kutoka kwa wazabuni binafsi.

Nilibaini kuwa mamlaka tatu za serikali za mitaa zilinunua dawa na vifaa-tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 681.41 kutoka kwa wazabuni binafsi bila kibali cha MSD kinachothibitisha kokosekana kwa vifaa hivyo. Hii ni kinyume na kanuni na Miongozo ya Ununuzi wa Umma inayotolewa mara kwa mara. Orodha ya vituo vya kutolea huduma imeoneshwa kwenye **Jedwali Na.98.**

**Jedwali Na. 98: Ununuzi bila kibali cha kukosekana vifaa kutoka MSD**

| Na | Halmashauri | Kituo cha Huduma | Mzabuni | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | Zahanati ya Oldonyosambu | Bowman Healthcare (T) Ltd | 80,040,500 |
| | | Olorien Dispensary | Bowman Healthcare (T) Ltd | 93,253,500 |
| | | Zahanati ya Lengijave + Lesiraa | Bowman Healthcare (T) Ltd | 33,956,000 |
| | | Zahanati ya Mwandet | Bowman Healthcare (T) Ltd | 79,927,500 |
| 2. | H/W Butiama | CHMT | Vasco Pharmaceutical Company Limited | 78,109,650 |
| | | CHMT | Nkwabi Chemicals and Reagents | 154,265,602 |
| | | Hospitali ya wilaya ya Butiama | Vasco Pharmaceutical Company Limited | 11,222,750 |
| | | Hospitali ya wilaya ya Butiama | Vasco Pharmaceutical Company Limited | 8,375,576 |
| 3. | H/W Musoma | Hospitali ya wilaya ya | | 142,255,533 |
| **Jumla** | | | | **681,406,611** |

Pia, nilibaini tofauti kubwa za bei kati ya bei zilizonukuliwa na MSD na zile zinazotolewa na wazabuni binafsi. Katika mamlaka nne za serikali za mitaa nilibaini hasara ya Sh. milioni 101.51 iliyotokana na ununuzi wa bidhaa za matibabu kutoka kwa wazabuni binafsi bila kibali cha kukosekana kwa bidhaa hizo MSD kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na.99.**

**Jedwali Na. 99: Hasara itokanayo na ununuzi bila kibali cha MSD**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Butiama | 48,748,411 |
| 2. | H/Mji Masasi | 35,704,956 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 3. | H/W Magu | 10,057,612 |
| 4. | H/Mji Mbulu | 7,000,000 |
| **Jumla** | | **101,510,979** |

**Ninapendekeza vituo vya afya vihakikishe ununuzi wowote wa dawa na vifaa vingine vya hospitali haufanywi kutoka kwa wazabuni binafsi pasipo na uthibitisho wa kukosekana kwa vifaa hivyo kutoka MSD kama kanuni zinavyotaka.**

### 13.5.3 Uchepushwaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Vifaa-tiba - Sh. milioni 156.97

Aya ya 3.2(i) ya Maelekezo ya Usimamizi wa Mfuko wa Uchangiaji Gharama yaliyotolewa na Wizara ya Afya mwaka 2017 inataka 50% ya makusanyo ya mapato ya ada ya mtumiaji wa huduma za afya itengwe kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaatiba.

Nilifanya tathimini ya usimamizi wa fedha za uchangiaji wa huduma za afya katika vituo 26 vya kutolea huduma za afya katika mamlaka tatu za serikali za mitaa na kubaini kuwa jumla ya Sh. milioni 519.45 zilikusanywa. Kati ya fedha hizo Sh. milioni 259.73 sawa na 50% ya fedha zilizokusanywa, zilitakiwa kutengwa kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya.

Hata hivyo, nilibaini jumla ya Sh. milioni 156.97 zilichepushwa na kugharamia shughuli zingine, kama vile malipo ya posho na matumizi mengine ya kawaida kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.100.**

**Jedwali Na. 100: Fedha za vifaa-tiba zilizochepushwa**

| Na | Halmashauri | Makusanyo (Sh.) | Kiasi Stahiki (Sh.) | Matumizi Stahiki (Sh.) | Kiasi Kilicho Chepushwa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Longido | 184,844,105 | 92,422,053 | 27,563,510 | 64,858,543 |
| 2. | H/W Lushoto | 242,075,245 | 121,037,623 | 73,754,575 | 47,283,048 |
| 3. | H/M Shinyanga | 92,530,609 | 46,265,305 | 1,433,000 | 44,832,305 |
| **Jumla** | | **519,449,959** | **259,724,980** | **102,751,085** | **156,973,895** |

Matumizi ya fedha kinyume na malengo yaliyokusudiwa, hususani kutenga kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa-tiba unakwamisha juhudi za Serikali za kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa jamii. Tabia hii inadhoofisha ufanisi wa huduma za afya na inapunguza ubora wa huduma inayotolewa kwa umma.

**Ninavisisitiza vituo vya kutolea huduma za afya katika mamlaka za serikali za mitaa kuzingatia Aya 3.2(i) ya Maelekezo ya Usimamizi wa Mfuko wa Uchangiaji Gharama za Afya yaliyotolewa na Wizara ya Afya mwaka 2017 na Aya ya 4.3 ya Mwongozo wa CCHP Toleo la 5 wa mwaka 2020. Ni muhimu kwamba 50% ya fedha za kuchangia gharama zitumike katika ununuzi ya bidhaa za afya.**

**Kwa kufanya hivyo, vituo vya kutolea huduma za afya vitakua na matumizi sahihi ya fedha, hivyo kuimarisha upatikanaji wa vifaa muhimu vya matibabu na kuboresha huduma za afya kwa jamii.**

# SURA YA KUMI NA NNE



# MAPITIO YA UTENDAJI WA UWEKEZAJI KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

## 14.0 Utangulizi

Katika sura hii, ninaanglia kwa kina jukumu muhimu la mamlaka za serikali za mitaa katika kufanya uwekezaji wa kimkakati uliolenga kuongeza mapato ya ndani ili kusaidia maendeleo ya jamii, kuchochea ukuaji wa uchumi na kuboresha utoaji wa huduma. Pia, kuhakikisha kwamba fedha za umma zimetengwa kwa uwekezaji ulioonekana kuwa na tija na kufuata vigezo vilivyowekwa.

Katika mchakato wa ukaguzi, nilibaini mamlaka za serikali za mitaa zimewekeza katika taasisi za kifedha, viwanda vya kutengeneza matofali, vituo vya mabasi, na masoko.

Wakati wa tathmini, lengo langu lilikuwa kuangalia uzingatiaji wa sheria, kanuni, sera, miongozo, na mifumo ya udhibiti inayosimamia uwekezaji.

Pia, nimefanya tathmini ya mda utakaotumika kurudisha gharama za uwekezaji (return on investment), ufanisi wa uendeshaji wa miradi ya kimkakati iliyotekelezwa miaka iliyopita, ikiwamo vituo vya mabasi na masoko. Lengo la ukaguzi lilikuwa kupima ufanisi wa miradi husika katika kufikia malengo yaliyokusudiwa, ikiwamo kuchochea ukuaji wa uchumi, kuzalisha mapato, na kutoa huduma.

Kupitia tathmini ya kina, ninawasilisha mapendekezo yakijumuisha hatua za kuchykua za muda mfupi na mrefu, ili kushughulikia udhaifu uliobainika na kuboresha uwekezaji ndani ya mamlaka za serikali za mitaa.

## 14.1 Uwekezaji katika Hisa

### 14.1.1 Utendaji mbaya wa uwekezaji katika benki ya DCB

Mamlaka za serikali za mitaa katika Mkoa wa Dar es Salaam mwaka 2001 zilikubaliana kuanzisha Benki ya Jamii ya Dar es Salaam ambayo ilianza kazi zake mwaka 2002. Mamlaka hizo ni H/Jiji Dar es Salaam, H/M Ilala, H/M Kinondoni, H/M Temeke, H/M Kigamboni, na H/M Ubungo. Kwa pamoja zimewekeza jumla ya Sh. bilioni 26.89 katika hisa 31,923,990.

Hata hivyo, nimebaini kwamba thamani ya hisa imekuwa ikipungua mwaka baada ya mwaka, kwani mwaka 2002 ilikuwa Sh. 1,000; mwaka 2018/19 ilikuwa Sh. 250; na bei ya hisa ya sasa ni Sh. 140. Mwenendo unaonesha kupungua kwa thamani ya hisa (hasara) kwa Sh. bilioni 22.37 kama inavyoelezwa katika **Jedwali Na.101.**

**Jedwali Na. 101: Uwekezaji wa taasisi**

| Na | Halmashauri | Idadi ya Hisa | Thamani ya Hisa 2002 @Sh 1000/ na 2018/19 @Sh 250 | Thamani ya hisa tarehe 30 Juni, 2023 @Sh 140 | Hasara iliyopatikana mpaka 30 Juni, 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dar es Salaam | 6,832,094 | 6,832,094,000 | 956,493,160 | 5,875,600,840 |
| | | 3,396,254 | 849,063,500 | 475,475,560 | 373,587,940 |
| 2 | H/M Ilala | 6,357,426 | 6,357,426,000 | 890,039,640 | 5,467,386,360 |
| | | 1,509,434 | 377,358,500 | 211,320,760 | 166,037,740 |
| 3 | H/M Kinondoni | 3,750,013 | 3,750,013,000 | 525,001,820 | 3,225,011,180 |
| | | 1,875,006 | 468,751,500 | 262,500,840 | 206,250,660 |
| 4 | H/M Temeke | 3,422,252 | 3,422,252,000 | 479,115,280 | 2,943,136,720 |
| 5 | H/M Kigamboni | 2,281,502 | 2,281,502,000 | 319,410,280 | 1,962,091,720 |
| 6 | H/M Ubungo | 2,500,009 | 2,500,009,000 | 350,001,260 | 2,150,007,740 |
| **Jumla** | | **31,923,990** | **26,838,469,500** | **4,469,358,600** | **22,369,110,900** |

**Chanzo:** Taarifa ya uwekezaji DCB

Uwekezaji huu umeonyesha kutokuwa na tija katika soko la fedha, ukiashiria haja ya haraka ya kufanya uamuzi kuhusiana na uwekezaji huu, kwani nimebaini kwamba Benki ya DCB imekumbana na matatizo ya ukata na kushindwa kutangaza gawio kwa zaidi ya miaka minne.

Ufuatao ni uchambuzi maalumu wa utendaji wa uwekezaji:

**a) Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni**

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Halmashauri ina hisa 15,000 katika kampuni ya Sigara Tanzania (TCC), ambapo thamani yake imebaki

palepale kwa miaka ya fedha 2019/20, 2021/22, na 2022/23, na kupungua kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Kupungua kwa thamani ya hisa za Kampuni ya Sigara Tanzania kumesababisha halmashauri kupata hasara kufikia Sh milioni 89.35 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.102**.

**Jedwali Na. 102: Hasara inayotokana na uwekezaji katika hisa**

| Mwaka wa fedha | Kampuni | Maelezo | Thamani ya hisa | Uthamani faida/hasara |
|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | TCC | Upotevu wa thamani ya hisa 15,000 TCC | Bei ilishuka kwa Sh.5,950 TCC | 89,350,000 |

**Chanzo:** Taarifa ya fedha 2022/23

**b) Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam**

Nimebaini kwamba, Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam (DDC) limewekeza Sh. milioni 120.10 katika hisa za DCB, TCCL, na TBL kwa ajili ya kupata gawio.

Hata hivyo, ukaguzi wa ripoti ya ukusanyaji wa gawio na ripoti za Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE), umebaini kwamba kampuni hizi kwa sasa zinafanya vibaya, hivyo kusababisha malipo ya gawio kucheleweshwa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.103.**

**Jedwali Na. 103: Makampuni yenye mwenendo usioridhisha**

| Jina la kampuni | Idadi ya hisa | Bei ya hisa kwa sasa (Sh.) | Thamani ya hisa (Sh.) | Gawio (Sh.) | Muda toka kupokea gawio la mwisho |
|---|---|---|---|---|---|
| Kampuni ya saruji Tanga (TCCL) | 5000 | 1460 | 7,300,000 | 118,750 | Oktoba 2017 hadi Novemba 2023 ( miaka saba) |
| Benki ya biashara DCB | 19678 1 | 140 | 27,549,340 | 187,029 | Oktoba 2020 hadi Novemba 2023 (miaka miwili) |
| TBL | 7821 | 10,900 | 85,248,900 | 1,894,637 | Januari 2022 hadi Novemba 2023 (mwaka mmoja na miezi tisa) |
| **Jumla** | | | **120,098,240** | | |

**Chanzo:** Taarifa ya fedha 2022/23

Kutokana na matokeo ya ukaguzi niliyoelezea hapo juu, ni dhahiri kwamba uwekezaji uliofanywa na H/M Kinondoni, H/M Temeke, H/Jiji Dar es Salaam, H/M Kigamboni, H/M Ubungo, na Shirika la Maendeleo la

Dar es Salaam unafanya vibaya, kwani bei ya hisa inapungua na hakuna gawio lililotangazwa kwa zaidi ya miaka minne.

**Ninapendekeza kwa menejimenti za Halmashauri na Shirika na Maendeleo Dar es salaam kufanya tathmini upya ya utendaji wa uwekezaji uliofanyika na kuchukua hatua zinazohitajika ili kuzuia hasara zaidi kwenye fedha zilizowekezwa.**

**Aidha, ninashauri uongozi kuandaa na kupitisha sera ya uwekezaji ili kutoa mwongozo wa wazi juu ya mambo yanayohusiana na uwekezaji ambao unaweza kuleta mapato mazuri ikizingatiwa uchache wa rasilimali.**

## 14.2 Uwekezaji katika Masoko

### 14.2.1 Upotevu wa mapato kwenye uwekezaji kutokana na matumizi ya viwango visivyoidhinishwa - Sh. bilioni 1.72

Usimamizi makini wa viwango vya kodi ya pango ni muhimu kwa mamlaka za serikali za mitaa ili kuongeza mapato na kuwa na fedha toshelevu ili kukidhi mahitaji ya jamii zao. Viwango vya kodi ya pango mara nyingi hupangwa kwa kufuata taratibu za kisheria na kupitishwa na mamlaka husika ili kuhakikisha haki na uwiano.

Katika tathmini za hivi karibuni, nimebaini matukio mengi ambapo viwango visivyoidhinishwa vya kodi ya pango vilitumika na kusababisha hasara ya Sh. bilioni 1.72.

**Jedwali Na.104** linaonesha mifano halisi ambapo matumizi ya viwango visivyoidhinishwa vya kodi ya pango na mamlaka za mitaa hali iliyosababisha changamoto za kifedha.

**Jedwali Na. 104: Upotevu wa mapato kwa kutumia viwango visivyoidhinishwa**

| | Maelezo | | | A: mapato kulingana na sheria | | B: mapato kulingana na mkataba | | Upotevu wa mapato (A-B) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Halmashauri | Eneo | Maduka/vibanda/maegesho/ghala | Kipindi | Kodi kwa mwezi Sh. | Kodi ya mwaka Sh. | Kodi kwa mwezi Sh. | Kodi ya mwaka Sh. | Sh. |
| H/W Pangani | Soko jipya la Masanga na Selemara | 137 | 12 | 20,000 | 32,880,000 | 15,000 | 24,660,000 | 8,220,000 |

| | Maelezo | | | A: mapato kulingana na sheria | | B: mapato kulingana na mkataba | | Upotevu wa mapato (A-B) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| H/Mji Korogwe | Soko la Manundu | 112 | 12 | 20,000 | 26,880,000 | 10,000 | 13,440,000 | 13,440,000 |
| H/M Kigoma /ujiji | Soko la Kigoma | 442 | 12 | 50,000 | 265,200,000 | 25,000 | 132,600,000 | 132,600,000 |
| | Mwanga community centre | 102 | 12 | 50,000 | 61,200,000 | 25,000 | 30,600,000 | 30,600,000 |
| | Stesheni | 24 | 12 | 50,000 | 14,400,000 | 25,000 | 7,200,000 | 7,200,000 |
| | Soko la Masanga | 737 | 12 | 25,000 | 221,100,000 | - | - | 221,100,000 |
| | Soko la Selemara | 486 | 12 | 25,000 | 145,800,000 | - | - | 145,800,000 |
| H/W Korogwe | Soko la Manundu | 112 | 12 | 20,000 | 26,880,000 | 10,000 | 13,440,000 | 13,440,000 |
| H/M Kinondoni | Maegesho ya Coco beach | 55,729 | 1 | 2,500 | 139,322,500 | 1,000 | 55,729,000 | 83,593,500 |
| H/W Mtama | Ghala la Ilulu Mtama | 3,713,317 | 1 | 52 | 193,092,484 | 12 | 44,559,804 | 148,532,680 |
| | Ghala la Hazina | 3,673,626 | 1 | 52 | 191,028,552 | 12 | 44,083,512 | 146,945,040 |
| | Ghala la Ilulu Mtama | 479,717 | 1 | 38 | 18,229,246 | 12 | 5,756,604 | 12,472,642 |
| | Ghala Hazina | 552,315 | 1 | 38 | 20,987,970 | 12 | 6,627,780 | 14,360,190 |
| | Ghala la Ilulu Mtama | 488,052 | 1 | 52 | 25,378,704 | 12 | 5,856,624 | 19,522,080 |
| | Ghala la Hazina | 1,494,106 | 1 | 52 | 77,693,512 | 12 | 17,929,272 | 59,764,240 |
| H/W Kakonko | Soko la Kakonko | 121 | 12 | 50,000 | 72,600,000 | 10,000 | 14,520,000 | 58,080,000 |
| H/M Ubungo | Soko la Shekilango | 279 | 12 | 140,000 | 468,720,000 | 15,000 | 50,220,000 | 418,500,000 |
| H/Mji Njombe | Maduka ya Eneo la Mahakami | 42 | 36 | 150,000 | 75,600,000 | 30,000 | 15,120,000 | 181,440,000 |
| **Jumla** | | | | | | | | **1,715,610,372** |

Halmashauri zinapoteza Sh. bilioni 1.72 kila mwaka kutokana na kutozingatia vifungu vya sheria ndogo, ambapo fedha hizo zingeweza kutumika kufadhili shughuli zilizopangwa kwenye bajeti.

**Ninashauri OR-TAMISEMI, sekretarieti za mikoa, na halmashauri kuhakikisha kuna usimamizi bora wa ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha viwango vilivyobainishwa kwenye sheria za halmashauri vinafuatwa, na kuchukua hatua muhimu dhidi ya wale wanaohusika na kutumia viwango visivyoidhinishwa.**

### 14.2.2 Uendeshaji usio na ufanisi katika masoko ya halmashauri yenye thamani ya Sh. bilioni 1.02

Baada ya kupitia uendeshaji wa masoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang', nilibaini kwamba, licha ya uwekezaji mkubwa wa kifedha kwenye masoko ya Measkron, Gendabi, Masakta, na Bassotu yenye thamani ya Sh. milioni 140 (sawa na Sh. milioni 35 kila soko), masoko husika hayafanyi kazi kwa muda mrefu.

Aidha, Soko la Kimataifa la Mazao huko Endagawa, lenye thamani ya Sh. bilioni 1.02, halifanyi kazi kama ilivyotarajiwa kwa muda mrefu. Wakati wa ukaguzi tarehe 4 Oktoba 2023 nilitembelea soko na nilibaini kuwapo kwa mazao ndani ya soko, lakini sikupata kufahamu mapato yaliyopatikana kutokana na kutokuwapo kwa mikataba rasmi kutoka kwa wakulima walioweka mazao yao.

Kutokufanya kazi kwa muda mrefu kwa miundombinu ya soko na kukosekana kwa mikataba rasmi na wakulima kumebabisha upotevu wa mapato, hususani kutokana na ushuru wa mazao.

**Ninapendekeza uongozi wa halmashauri kufanya tathmini kamili ya uwezekaji katika masoko yaliyoanzishwa, ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika miundombinu muhimu kama mizani, na ujenzi wa mifumo ya majitaka ili kuongeza ufanisi wa masoko. Pamoja na hayo, juhudi zinapaswa kuongezwa ili kuelimisha na kuhamasisha wafanyabiashara kutumia masoko haya kwa ufanisi.**

## 14.3 Uwekezaji katika vituo vya mabasi

### 14.3.1 Kodi zisizokusanywa kwenye vituo vya mabasi Sh. milioni 742.75

Kifungu Na. 6(1)(m) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kinasema kuwa mapato ya mamlaka za serikali za mitaa yatajumuisha fedha zinazotokana na ada zilizolipwa kutokana na kodi za maduka, machinjio, vibanda vya masoko, ada za watumiaji, ada za huduma, na kodi za burudani kwa matangazo ya biashara kwenye mabango, michoro, au taarifa.

Ukaguzi uliofanywa kuhusu utendaji wa uendeshaji wa vituo vya mabasi ulibaini kwamba katika mwaka wa fedha 2022/23, kodi ya Sh. milioni 742.75 haikukusanywa kutoka kwa maduka na vibanda vilivyokamilika vilivyopo kwenye vituo vya mabasi kama inavyoelezwa katika **Jedwali Na.105.**

**Jedwali Na. 105: Kodi zisizokusanywa kwenye vituo vya mabasi**

| Na | Halmashauri | Eneo | Kiasi kilichosalia |
|---|---|---|---|
| 1. | H/M Ubungo | Kituo cha basi Magufuli | 165,102,400 |
| 2. | H/M Musoma | Kituo cha basi Bweri | 151,738,138 |
| 3. | H/Mji Geita | Kituo cha basi Geita Mji | 79,760,256 |
| 4. | H/M Ilemela | Nyamhongolo investment property | 69,615,000 |
| 5. | H/Mji Mbulu | kituo cha basi Mizengo Pinda | 50,550,000 |
| 6. | H/W Pangani | Maduka na vibanda kituo kikuu cha basi | 45,534,797 |
| 7. | H/Mji Handeni | kituo kikuu cha basi Chogo | 39,822,140 |
| 8. | H/Mji Makambako | Kituo cha basi Makambako | 37,072,050 |
| 9. | H/Mji Mbinga | Kituo cha basi Mbinga | 35,930,000 |
| 10. | H/J Babati | kituo cha basi Magugu | 18,000,000 |
| 11. | H/W Lushoto | Lushoto kituo cha basi | 14,050,000 |
| 12. | H/M Kigamboni | Kituo cha basi ( standi ya zamani) | 12,044,758 |
| 13. | H/M Mpanda | Kituo cha basi maeneo ya Ujenzi | 10,401,000 |
| 14. | H/W Rufiji | kituo cha basi Ikwiriri | 7,180,000 |
| 15. | H/W Karatu | Karatu kituo cha basi | 5,950,000 |
| **Jumla** | | | **742,750,539** |

Kukosekana kwa udhibiti wa kutosha katika michakato ya ukusanyaji wa mapato, kama vile kutokuhuisha mikataba ya umiliki na ufuatiliaji wa malipo ya kodi, kumesababisha mapato kupungua.

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa ziweke mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani. Hii ni pamoja na kuhuisha mifumo ya taarifa ya wapangaji, kusimamia mikataba yenye viwango vilivyoidhinishwa, na kuwa na usimamizi makini. Kuweka kipaumbele katika ukusanyaji wa kiasi kinachodaiwa kutoka kwa wapangaji ni muhimu kwa kuboresha usimamizi wa mapato na kuwa na uhakika wa fedha.**

### 14.3.2 Upotevu wa Sh. milioni 726.40 uliosababishwa na uendeshaji usiokuwa na ufanisi wa vituo vya mabasi katika mamlaka za serikali za mitaa

Wakati wa ukaguzi, nilibaini vituo vya mabasi vikiwa na ufanisi mdogo wa uendeshaji ambapo, baadhi ya maduka, vioski, na fremu hazikukodishwa kwa wapangaji; hivyo kubaki bila shughuli kwa sehemu au mwaka mzima wa fedha.

Kama maeneo haya ya kuegesha magari, kioski, na fremu za maduka yangekodishwa, kodi isiyokusanywa yenye thamani ya Sh. milioni 726.40 ingepatikana. Kwa kutokukodisha fremu za stendi za mabasi, kioski na maduka, Halmashauri hazitaweza kufikia malengo ya ukusanyaji kwenye uwekezaji uliofanywa; pia, malengo yaliyokusudiwa ya utoaji wa huduma hayatafikiwa. Maelezo yanaoneshwa kwenye **Jedwali Na.106.**

**Jedwali Na. 106: Upotevu wa mapato ya masoko kwa kukosekana ufanisi**

| Na | Halmashauri | Eneo | Maelezo | Idadi | Kodi kwa mwezi Sh. | Kipindi | Kiasi Sh. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Ilemela | Nyamhongo kituo cha basi | Vyumba vya tiketi | 37 | 155,000 | 11 | 63,085,000 |
| | | | Maduka madogo | 15 | 153,000 | 11 | 25,245,000 |
| | | | mgahawa | 1 | 936,000 | 11 | 10,296,000 |
| | | | Supermarket | 2 | 5,925,000 | 11 | 130,350,000 |
| | | | Benki | 2 | 7,242,000 | 11 | 159,324,000 |
| | | | Maduka makubwa | 2 | 992,000 | 11 | 21,824,000 |
| | | | maduka | 2 | 2,543,000 | 11 | 55,946,000 |
| | | | Gereji | 1 | 1,544,000 | 11 | 16,984,000 |
| 2 | H/Jiji Mwanza | Nyegezi kituo cha basi | maduka | 65 | | | 112,848,555 |
| 4 | H/Jiji Dar ses salaam | Kisutu kituo cha kisasa cha basi | maegesho | 18 | 2,000 | 365 | 13,140,000 |
| | | | vibanda | 245 | 30,000 | 12 | 88,200,000 |
| | | | kiosks | 8 | 60,000 | 12 | 5,760,000 |
| 5 | H/W Chato | Kahumo kituo cha basi | maduka | 23 | 50,000 | 12 | 13,800,000 |
| | | | Baa na mgahawa | 8 | 100,000 | 12 | 9,600,000 |
| **Jumla** | | | | | | | **726,402,555** |

**Chanzo:** Ripoti ya Ofisa wa Masoko na ukaguzi wa eneo

Uendeshaji usioridhisha wa stendi hizi za mabasi kunatokana na mazingira duni ya biashara, ukosefu wa maegesho ya kutosha, na kuwapo kwa stendi za zamani. Kushindwa kuzitumia stendi za mabasi zilizojengwa kikamilifu, kunaweza kuchukua muda mrefu kurudisha uwekezaji uliofanywa.

**Ninapendekeza kuwa mamlaka za serikali za mitaa, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, kushughulikia suala hili kwa kufunga stendi za zamani za mabasi ili kuvutia wapangaji kuhamia stendi mpya.**

### 14.3.3 Uendeshaji duni katika kituo cha mabasi cha Magufuli kinachoendeshwa na H/M Ubungo

#### a) Mapato yasiyofichuliwa yaliyokusanywa katika hoteli ya kituo cha mabasi Magufuli

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kwamba kiasi cha Sh. milioni 45.64 ambazo ni mapato kutoka huduma za hoteli katika kituo cha mabasi Magufuli kwa Desemba 2022 (Sh. milioni 27.32) na Januari 2023 (Sh. milioni 18.32) yaliyokusanywa na Rahabu Logistics Co. Ltd kama wakala wa ukusanyaji

hayakuwekwa katika akaunti za benki za halmashauri kama ilivyo kwa mujibu wa Agizo la 50 (5) la Memorandamu ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

Aidha, niliomba ripoti za ukusanyaji mapato kwa huduma za hoteli kuanzia Februari hadi Juni 2023 lakini hazikutolewa kwa ajili ya ukaguzi; na hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha kama mapato yaliyokusanywa wakati huo yalikuwa yameingizwa katika akaunti za halmashauri.

Pia, nilibaini kwamba kuanzia Februari hadi Juni 2023, wakala wa ukusanyaji mapato alifanya kazi bila mkataba uliosainiwa na halmashauri ambao unazua wasiwasi kuhusu masharti na hali za uendeshaji wa hoteli wakati huu.

Kushindwa kuwasilisha taarifa za ukusanyaji mapato zilizoombwa kwa madhumuni ya ukaguzi, kunapunguza wigo wa ukaguzi kwa ukamilifu wa kutathmini uwazi na usimamizi wa kifedha.

**b) Kituo cha Taifa cha Takwimu za Mtandao (NIDC) kufanya kazi bila mkataba**

Nilibaini kwamba, makubaliano ya awali kati ya Halmashauri na Kituo cha Taifa cha Takwimu za Mtandao (NIDC) yalikuwa kwa ajili ya kuweka mageti katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli. Halmashauri ilikuwa na jukumu la kuweka mfumo wa ukusanyaji mapato. Hata hivyo, kutokana na kucheleweshwa kwa utekelezaji wa mfumo mpya wa mapato wa TAUSI, Halmashauri iliruhusu NIDC kukusanya mapato kwa kutumia programu yao kwa muda wakati wakisubiri mfumo mpya. Tangu tarehe 20 Februari 2023, NIDC imekuwa ikifanya kazi na mashine za N-Card kwa ajili ya ukusanyaji mapato katika kituo cha mabasi bila mkataba rasmi na Halmashauri.

Baadaye, NIDC iliomba Halmashauri kulipa 7.2% ya jumla ya mapato yaliyokusanywa kwa kutumia mfumo wa N-Card, kama ilivyobainishwa katika barua yenye kumbukumbu namba 23/NIDC/MNG.06/15 iliyotolewa tarehe 28 Juni 2023, lakini Halmashauri bado halijaitikia ombi hilo.

Mikakati duni ya usimamizi wa Halmashauri katika kufuatilia usimamizi wa mikataba na ukusanyaji wa mapato na wakala katika kituo cha basi Magufuli inaweza kusababisha ubadhirifu wa mapato.

**c) Matumizi yaliyotumika na Halmashauri kwa malipo ya maji na umeme - Sh. milioni 563.02**

Halmashauri ililipa jumla ya Sh. milioni 563.02 kama gharama za umeme (Sh. milioni 333.48) na huduma za maji (Sh. milioni 229.54) katika kituo cha basi Magufuli.

Matumizi haya yangeweza kupunguzwa sana kama kila mpangaji angelipia matumizi yake ya maji na umeme, kama ilivyoelekezwa katika mikataba yao.

**Ninapendekeza hatua zifuatazo zifanywe na uongozi:**

**(a) Kuhakikisha Sh. milioni 45.64 zilizokusanywa kutoka katika operesheni za hoteli katika mwezi Desemba 2022 na Januari 2023 zinatolewa hesabu; kuhakikisha kuwa ripoti za ukusanyaji mapato zilizoombwa kuanzia Februari hadi Juni 2023, pamoja na taarifa za benki, zinawasilishwa kwa wakati kwa ajili ya ukaguzi; na kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya maofisa ambao walizuia kutoa taarifa kuhusu mapato yaliyokusanywa kutoka biashara ya hoteli wakati huu.**

**(b) Kuchunguza na kuchukua hatua stahiki dhidi ya maofisa wa Halmashauri ambao waliruhusu mawakala kufanya kazi kwa niaba ya Halmashauri bila mkataba.**

**(c) Kueleza kwa uwazi katika mikataba ya upangaji kiasi ambacho kila mpangaji anatakiwa kulipa gharama za umeme na maji, au vinginevyo kufanya usakinishaji wa mita za umeme za kujitegemea kwa ajili ya wapangaji ili kupima matumizi kwa usahihi.**

## 14.4 Uwekezaji katika makampuni tanzu

### 14.4.1 Uendeshaji usiofaa katika Kampuni ya Nyama Arusha (Arusha Meat Company LTD)

Kampuni ya Nyama ya Arusha, iliundwa kwa lengo la kutoa bidhaa za nyama zenye ubora wa hali ya juu na huduma zinazohusiana, ikijikita katika uzalishaji na uuzaji wa aina mbalimbali za nyama, sausage, na bidhaa zingine za nyama.

Wakati wa tathmini ya ufanisi wa uendeshaji katika mwaka wa fedha 2022/23, yafuatayo yalibainika:

**i) Kuandaa bajeti isiyo na uhalisia**

Kwa mwaka wa fedha 2022/23, kampuni ilipanga kukusanya Sh. bilioni 3.60 kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwa pamoja na Sh. milioni 56 kama ruzuku ya mapato kutoka Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Hata hivyo, hadi tarehe 30 Juni 2023, Kampuni ilikusanya Sh. bilioni 3.07 na ruzuku kutoka Halmashauri ya Jiji la Arusha ilikuwa Sh. milioni 27.18. Hii ilionesha kutokusanywa kwa Sh. milioni 527.13 sawa na 15%.

Aidha, uchunguzi wa maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya Kampuni kwa mwaka wa fedha tuliokagua ulibaini kuwa licha ya kuwa na marekebisho ya bajeti katikati ya mwaka, kulikuwa na tofauti kubwa katika utekelezaji wa bajeti, ikiwa na tofauti kubwa kati ya -489% hadi 100%.

Ukaguzi ulitilia shaka kuhusu tofauti hii kubwa kati ya fedha zilizopangwa kukusanywa na fedha halisi zilizokusanywa, zikionesha uwezekano wa uwepo wa tatizo katika kupanga na kutekeleza masuala ya kifedha.

**ii) Udhaifu katika mfumo wa uhasibu wa QuickBooks**

Nilibaini udhaifu katika mfumo wa uhasibu wa QuickBooks kwenye sehemu ya ukusanyaji wa mapato katika Kitengo cha Uzalishaji, hususani kuhusu namna ya kushughulikia miamala inayostahili kodi na isiyostahili kodi, pamoja na kuweka miamala ya aina mbalimbali, kama ifuatavyo:

a) Mfumo hauwezi kutofautisha kati ya miamala inayostahili kodi na isiyostahili kodi, ikisababisha makosa katika kutengeneza ankara kwa huduma zisizostahili kodi kama ada za kuchinja. Hii inasababisha kupitisha kiwango cha ada kutoka Sh. 19,900 kwa ng'ombe hadi Sh. 23,482, hatimaye kusababisha hitilafu za kifedha.

b) Mfumo hauwezi kushughulikia kwa ufanisi muktadha wa miamala miwili tofauti. Kwa mfano, wakati unaweza kuweka ada ya kupooza ya Sh. 5,000 kwa siku kwa kila mnyama, unahitaji kuingiza kwa mikono wakati mnyama zaidi ya mmoja watahifadhiwa kwa siku nyingi, hii husababisha ufanisi mdogo na makosa yanayowezekana katika kuandaa hesabu za ankara.

**iii) Kampuni iliingia matumizi yasiyokuwa na tija yanayofikia Sh. milioni 50.78**

Ukaguzi wa nyaraka mbalimbali za kodi zinazohusiana na Kampuni kwa mwaka wa fedha uliopitiwa ulibaini kuwa Kampuni ilipata faini na riba kutoka TRA na PSSSF. Faini hizi, za jumla ya Sh. milioni 50.78, zilikuwa zimejikusanya kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2022/23 kutokana na kuchelewesha kuwasilisha makato na kulipa kodi.

Katika kulitatua hili, uongozi umelipa riba ya Sh. milioni 24.03 kwa PSSSF, lakini bado haijatatua faini iliyosalia ya Sh. milioni 26.75 kwa TRA. Hii inaonesha kiwango kikubwa cha matumizi yasiyo na faida.

**Ninashauri uongozi wa Kampuni ujipange kwa kuandaa bajeti yenye uhalisia na kufanya marekebisho ya vifungu vinavyokabiliwa na upungufu wa fedha wakati wa mapitio ya bajeti katikati ya mwaka. Pia, washirikiane na mwandishi wa mfumo wa kompyuta ili kushughulikia kasoro katika mfumo kwa lengo la kupunguza kuingiza taarifa kwa mkono na kuongeza kuaminika kwa taarifa.**

**Aidha, ifuate sheria na kanuni, hususani kwa kuwasilisha malipo ya kisheria kwa wakati. Hii ni muhimu sana ili kuepuka faini na riba, huku ikihakikisha usimamizi bora wa fedha na kufuata sheria zilizopo.**

## 14.5 Uwekezaji katika viwanda

### 14.5.1 Upotevu wa fedha uliotokana na uwekezaji katika operesheni ya uchimbaji bila uchunguzi wa kijiolojia Sh. milioni 105.65

Tarehe 28 Septemba 2019, H/W Kilindi ilianzisha Kampuni ya Umma ya Uchimbaji Madbini (MIVYASA Mining) ili kufanya operesheni za uchimbaji madini katika Msitu wa Pumula, ulioko ndani ya Wilaya ya Kilindi.

Lengo kuu la kuunda Kampuni hiyo lilikuwa kupata mapato kwa kugawana faida kati ya wachimbaji wadogo, wakati, na wakubwa ambapo wachimbaji hao watapata 70% wakati kampuni itapata 30%. Faida inayopatikana itagawiwa kwa kiwango cha 80% kwenda kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri na 20% itabaki kwa operesheni za kampuni.

Tarehe 18 Mei 2023, Mkurugenzi Mtendaji wa H/W Kilindi, kupitia barua yenye nambari ya kumbukumbu KDC/L.30/3/VOLIII/89, aliiomba Ofisi ya Kamishna wa Uhifadhi, Mamlaka ya Huduma ya Misitu Tanzania kufuta Sh. milioni 44.34 za ada za uhifadhi wa misitu kwa shughuli za uchimbaji

katika Msitu wa Uhifadhi wa Pumula. Ombi hili lilifanywa kwa niaba ya MIVYASA, ambayo inakabiliana na changamoto za kiufundi kutokana na kuwapo kwa maji katika eneo la uchimbaji, hivyo kuzuia wachimbaji wa wadogo kufanya shughuli za uchimbaji.

Aidha, nilibaini kwamba Sh. milioni 105.65 zilikuwa zimekwisha wekezwa katika Kampuni ya MIVYASA. Hata hivyo, uwekezaji huo ulishindwa, ikionesha kwamba matumizi yaliyofanywa hayakuwa na mafanikio, na hakuna faida itakayorudi kutokana na uwekezaji huo.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI na Halmashauri kuhakikisha kwamba uamuzi wa uwekezaji kwa siku za baadaye unatokana na makadirio yenye uhalisia na kufanyika tathmini toshelevu ya vihatarishi.**

### 14.5.2 Kukosekana kwa ufanisi katika uendeshaji wa viwanda vya matofali

Ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya vifaa vya ujenzi nafuu na endelevu, mamlaka za serikali za mitaa zimeanzisha viwanda vya matofali kama suluhisho la kimkakati katika kukabiliana na changamoto za makazi, kukuza maendeleo ya kiuchumi, na kukuza uhifadhi wa mazingira.

Halmashauri ya Wilaya Arusha na Halmashauri ya Wilaya Monduli hivi karibuni zimeanzisha uwekezaji kwa kuanzisha viwanda vya matofali ya kawaida na vitofali vya sakafu (*paving blocks*) katika mamlaka zao. Hata hivyo, licha ya kuwa na malighafi zinazohitajika kama vile mchanga, changarawe, na saruji, viwanda hivyo vilizalisha takribani matofali 24,317 na 10,556 mtawalia wakati wa mwaka wa fedha wa 2022/23.

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa uwezo wa uzalishaji wa viwanda vya matofali haukutosheleza mahitaji ya matofali kwa mamlaka hizo yanayotokana na miradi ya ujenzi wa vituo vya afya, shule, na majengo mengine ya umma ndani ya eneo la mamlaka husika.

Ilibainika kwamba H/W Arusha na H/W Monduli zilitumia jumla ya matofali 116,887 na 146,667 mtawalia, wakati wa mwaka wa fedha wa 2022/23, zikipita uzalishaji wa kila mwaka wa viwanda kwa 80% na 93% mtawalia.

Ukosefu wa ushirikiano wa kutosha kati ya idara zinazozalisha na vitengo vya ununuzi unazuia mchakato wa uzalishaji na kupunguza uwezo wa jumla.

**Ninapendekeza uongozi kutekeleza mfumo wa usimamizi wa mchakato wa ugavi wa kisasa ili kuhakikisha malighafi zinapatikana**

**kwa wakati ili kupunguza gharama za uzalishaji. Pia, zitekeleze mikakati inayolenga kupunguza mchakato, kupunguza uchafu, kuboresha matumizi ya rasilimali, na kuongeza uzalishaji wa jumla.**

### 14.5.3 Kucheleweshwa kwa kuanza kwa operesheni za kiwanda cha chaki chenye thamani ya Sh. bilioni 2.85

Wakati wa ukaguzi wa akaunti na nyaraka zinazohusiana na kiwanda cha chaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, nilifanya uchunguzi wa barua yenye Kumb. Na. 4 /176/ 01S/99 ya tarehe 06 Juni 2023 kutoka kwa Katibu Tawala wa Mkoa kwenda kwa Katibu Mkuu OR-TAMISEMI, kuhusu kulipwa kwa madeni yaliyofikia Sh. bilioni 2.85. Kiasi hiki kinajumuisha Sh. bilioni 2.54 zilizotengwa kwa malipo kwa mkandarasi na Sh. milioni 307.88 zilizokusudiwa kwa majaribio ya mitambo katika kiwanda cha usindikaji wa Chaki na utengenezaji wa jasi.

Uchunguzi wa nyaraka mbalimbali na ripoti ya ziara katika kiwanda iliyofanyika tarehe 13 Agosti 2023 ulibaini kuwa kiwanda kimekamilika na kipo tayari kuanza uzalishaji, lakini bado hakijaanza.

Kucheleweshwa kuanza kwa uzalishaji kumetokana na kutofanyika kwa majaribio ya mitambo ambayo yanatakiwa kufanyika kwa kipindi cha siku 15 kama inavyoelezwa katika mkataba; changamoto za uendeshaji au masuala yanayohusiana na miundombinu ya kiwanda; mlolongo wa usambazaji, au wafanyakazi, ambayo yanazuia kuanza kwa uzalishajii; na taratibu za kiutawala ndani ya OR-TAMISEMI au mamlaka zingine husika ambazo zimesababisha kucheleweshwa kwa idhini au kutolewa kwa fedha zinazohitajika kwa uendeshaji wa kiwanda.

Ninaamini kwamba kuchelewesha kiwanda kuanza uzalishaji kunamaanisha kwamba mapato yanayotarajiwa kutokana na uzalishaji wa chaki na jasi hayajapokelewa, hivyo kusababisha hasara za kiuchumi kwa halmashauri na serikali.

Kutokufuata masharti ya mkataba na mkandarasi kunaweza kupelekea athari za kisheria na kifedha.

**Ninapendekeza kwamba ufuatiliaji zaidi ufanyike kwa OR-TAMISEMI au mamlaka zingine husika ambazo zinaweza kuwa zimesababisha kucheleweshwa kwa idhini au kutolewa kwa fedha zinazohitajika kwa uendeshaji wa kiwanda. Pia, ni muhimu kuhakikisha kufuata kikamilifu mkataba na mkandarasi, ikiwamo kumaliza kipindi cha majaribio ya siku 15, na kuhakikisha kwamba majukumu yote ya mkataba yanatimizwa kwa wakati.**

### 14.5.4 Utunzaji na usimamizi duni wa operesheni za viwanda vya kutengeneza matofali

Agizo la 52 la Memoranda ya Fedha ya mwaka 2009, linatoa miongozo ya kusimamia vizuri uwekezaji, ambapo Halmashauri zilishughulikia suala la mahitaji makubwa ya matofali katika miradi mingi ya ujenzi kwa kuanzisha viwanda vya kutengeneza matofali.

Wakati wa kipindi cha ukaguzi, mamlaka za serikali za mitaa kama H/M Shinyanga, H/W Siha, H/W Mtama, H/Mji Nzega, H/W Mwanga, H/Jiji Tanga, H/M Lindi na H/M Singida ziliendesha viwanda vya kutengeneza matofali ili kukidhi mahitaji yao na mahitaji ya soko. Hata hivyo, tathmini ya ufanisi wa operesheni za mradi ilionesha upungufu na changamoto ambazo zinahitaji kushughulikiwa ili kupata matokeo bora. Upungufu na changamoto hizo ni:

i) **Kutokuwapo kwa mpango wa biashara:**
Halmashauri zilianzisha viwanda vya kutengeneza matofali bila mpango kamilifu wa biashara, kwa ajili ya kufafanua malengo, mikakati, masoko, na makadirio ya kifedha.

ii) **Kutokuwapo kwa sera rasmi za uwekezaji:**
Halmashauri ziliendesha shughuli za viwanda hivyo bila sera rasmi za uwekezaji, hivyo kusababisha ufanisi mdogo katika uendeshaji wa mradi.

iii) **Kutokuwapo kwa akaunti tofauti ya benki:**
Halmashauri zilizo na viwanda vya kutengeneza matofali ya kawaida na matofali ya kuwekea sakafu hazina akaunti za benki zilizotengwa kwa ajili ya kusimamia mapato ya mauzo na uendeshaji wa mradi. Hii ilifanya itumike akaunti moja ya Halmashauri, hivyo kushindwa kusimamia mapato na matumizi yake.

iv) **Kumbukumbu za uhasibu zisi:**
Halmashauri zimeshindwa kuweka kumbukumbu za uhasibu toshelevu, kwa kuchanganya fedha za mradi katika akaunti za jumla, hivyo kuathiri uchambuzi wa utendaji na tathmini ya mali.

v) **Mtaji usiotosha:**
Viwanda vina mtaji mdogo wa kudumisha viwango vya uzalishaji vinavyoendelea, hivyo kusababisha mashine kutotumika ipasavyo na upatikanaji usiridhisha wa bidhaa kwa ajili ya kukidhi mahitaji.

vi) **Kutokuwapo kwa nyaraka toshelevu:**
Ukosefu wa nyaraka za kutosha kuhusu ununuzi wa vifaa na matofali yaliyotolewa unafanya iwe vigumu kufuatilia uzalishaji na kutathmini utendaji. Kutokuwapo kwa kumbukumbu zilizoandaliwa pia kunazua wasiwasi kuhusu uwazi na uwajibikaji.

Ninaamini kwamba udhibiti duni kwenye uendeshaji na usimamizi wa viwanda kunaweza kusababisha ubadhirifu wa fedha, hivyo kusababisha viwanda kushindwa kutoa faida na kukidhi mahitaji yake.

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa husika zitengeneze mipango ya biashara yenye maelezo ya kina kuhusu malengo ya mradi, mikakati, makisio na mtiririko wa fedha za mradi. Pia zianzishe sera za uwekezaji kwa ajili ya kusimamia uanzishwaji, uundaji, na uendeshaji na usimamizi wa mradi kwa uwazi .**

**Miradi hiyo inahitaji kufunguliwa kwa akaunti zake za benki, kutunza vitabu vya fedha, na taarifa za kina za uzalishaji na mauzo ya tofali ili kuongeza uwazi, usimamizi sahihi wa kifedha na tathmini ya utendaji kazi. Mtaji wa kutosha unapaswa kupatikana ili kuboresha shughuli za viwanda na kukidhi mahitaji kwa ufanisi.**

### 14.5.5 Kituo cha mafunzo kilichotelekezwa kwa ajili ya biashara ndogo na za kati kikiwa na thamani ya Sh. bilioni 2.42

Programu ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Geita, kupitia mpango wa pamoja kati ya kampuni ya uchimbaji dhahabu ya Geita (Geita Gold Mine Limited-GGML), Halmashauri ya Mji wa Geita, na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa katika mwaka wa fedha 2014/15 walizindua kituo cha mafunzo kwa ajili ya wafanya biashara wadogo na wakati (SMEs) katika eneo la Magogo. Lengo lilikuwa ni kukuza ukuaji endelevu wa kiuchumi katika Mkoa wa Geita.

GGML ilitenga Sh. bilioni 2.42 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa Magogo na tarehe 11 Mei 2018, makabidhiano rasmi ya mradi wa Magogo kwa H/Mji Geita yalifanyika, ikipewa wajibu wa moja kwa moja kwa ajili ya uendeshaji, udhibiti, ulinzi, na usimamizi wake.

Hata hivyo, kufikia Novemba 2023, miaka mitano baada ya mradi kuanzishwa, mradi huo ulikuwa bado haujafanya kazi na kutokuwa na shughuli, hivyo kukiuka masharti yaliyokubaliwa kati ya GGML na H/Mji Geita. Kutokuanza kwa shughuli za uendeshaji wa mradi kunazua wasiwasi kuhusu kufikiwa kwa malengo yake ya kijamii na kiuchumi iliyokusudiwa na kutilia shaka ufanisi wa juhudi za ushirikiano zilizoelezwa katika programu ya CSR.

Aidha, tarehe 19 Juni 2022, tukio la wizi lilifanyika, likisababisha kupotea kwa mashine na vifaa 12 kutoka kwenye mradi, chini ya ulinzi wa M/s Geita Umoja Security Group Ltd.

Kushindwa kushughulikia masuala haya kunaweza kusababisha hasara za kifedha kwa GGML na H/Mji Geita, kuharibika kwa sifa ya CSR ya GGML, kuathiri uhusiano, na kuzuia maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika eneo hilo.

**Ninahimiza Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) na uongozi wa Halmashauri kutengeneza mpango kamili wa kurejesha tena mradi wa SME wa Magogo.**

**Mpango huu unapaswa kujumuisha mapitio ya kina ya taratibu za makabidhiano kutoka Geita Gold Mine Limited (GGML) kwenda Halmashauri ya Mji wa Geita, lengo likiwa kuhakikisha mapitio rahisi na kuendelea kwa shughuli za mradi. Aidha, jitihada zinapaswa kufanywa ili kurejesha mashine na vifaa vilivyoibiwa kutoka kwa Kampuni ya Ulinzi.**

## 14.6 Uwekezaji katika timu za mpira wa miguu

### 14.6.1 Kushindwa kuthibitisha ufanisi wa utendaji wa klabu za mpira wa miguu za halmashauri kutokana na usimamizi usioridhisha

Wakati wa ukaguzi wa mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini kuwa mamlaka 4 za serikali za mitaa zilianzisha vilabu vya mpira wa miguu kama sehemu ya miradi ya uwekezaji. Vilabu hivi ni: timu ya KMC ambayo ilianzishwa mwaka 2014 na H/M Kinondoni; timu ya Geita Gold iliyoanzishwa mwaka 2009 na H/Mji Geita; timu ya Mbeya City iliyoanzishwa mwaka 2011 na H/M Mbeya; na timu ya Dodoma Jiji iliyoanzishwa mwaka 2020 na H/M Dodoma.

Timu zote hizi zimethibitishwa rasmi na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania na zimekuwa zikishiriki katika Ligi Kuu ya Tanzania kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Halmashauri hushughulikia vilabu hivi; hutoa fedha kutoka vyanzo vya ndani kila mwaka wa fedha. Mbali na ufadhili wa Halmashauri, vilabu hivi pia huongeza mapato kupitia ada za kuingia uwanjani, mauzo ya jezi, na udhamini kutoka kwa mashirika kama Parimatch, Geita Gold Mine, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, na Azam Broadcasting Media. Jumla ya mapato yaliyokusanywa katika mwaka wa fedha 2022/23 yalifikia Sh. bilioni 7.01.

Hata hivyo, mapato na matumizi yaliyofikia Sh. bilioni 7.01 na Sh. bilioni 6.29 mtawalia yalirekodiwa kwa mikono kwenye kitabu cha fedha cha Excel badala ya kuzalishwa moja kwa moja ndani ya mfumo wa IFMIS wa Halmashauri kama inavyotakiwa (Kifungu cha 5.3.1(f) na 5.3.2(c).

Aidha, mapato na matumizi ya vilabu hayakuwasilishwa ili kujadiliwa kwenye mikutano ya kila mwezi ya Kamati ya Fedha. Vilabu pia havikutayarisha taarifa za kifedha, hivyo kufanya iwe vigumu kuthibitisha utendaji wa vilabu hivyo katika uendeshaji. Vilevile halmashauri hazikutambua mapato yaliyopokelewa na matumizi yaliyofanywa na vilabu katika kumbukumbu zao za uhasibu.

Vilevile, kutokuwapo kwa Kanuni na Sheria au katiba inayoelezea usajili na uundaji wa klabu, fedha na utawala, miundombinu, haki za wafanyakazi na wachezaji, mgawanyo wa mapato, maadili, na nidhamu kunasababisha vilabu kutokuwa na mwongozo muhimu wa kisheria.

Natilia shaka kuongezeka kwa utegemezi wa kifedha kutoka kwa Halmashauri ambapo kiasi cha Sh. bilioni 3.66 kati ya mapato yote yanayofikia Sh. bilioni 7.01 kwa mwaka wa fedha 2022/23, kilichangwa na Halmashauri, hivyo kuzidi bajeti iliyopangwa ya Sh. bilioni 2.18 kwa Sh. bilioni 1.48. Hii inaleta athari kwa shughuli zingine za Halmashauri zilizo kwenye bajeti na kutekelezwa kupitia mapato ya ndani, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.107.**

**Jedwali Na. 107: Bajeti ikilinganishwa na michango halisi**

| Halmashauri | Timu | Kusanywa 2022/23 Sh. | Michango ya halmashauri 2022/23 Sh. | Bajeti ya halmashauri 2022/23 Sh. | Mchango wa ziada Sh. |
|---|---|---|---|---|---|
| H/J Mbeya | Mbeya City FC | 1,566,624,876 | 828,641,056 | 230,000,000 | 598,641,056 |
| H/Mji Geita | Geita Gold FC | 1,744,371,344 | 550,000,000 | 500,000,000 | 50,000,000 |
| H/M Kinondoni | KMC FC | 2,083,084,917 | 1,254,182,800 | 750,000,000 | 504,182,800 |
| H/J Dodoma | Dodoma Jiji FC | 1,620,000,000 | 1,031,426,003 | 700,000,000 | 331,426,003 |
| **Jumla** | | **7,014,081,137** | **3,664,249,859** | **2,180,000,000** | **1,484,249,859** |

Kuhusu utatuzi wa migogoro na usimamizi wa wafanyakazi, hakuna maelekezo ya moja kwa moja yanayoonesha masuala hayo yanashughulikiwa kwenye kiwango cha halmashauri au moja kwa moja katika kiwango cha klabu, kwani hakuna kanuni yoyote iliyowekwa.

Udhibiti duni unaotumika juu ya mapato na matumizi ya vilabu vya mpira wa miguu unaweza kutoa nafasi ya ubadhirifu wa fedha za umma. Pia, kuchelewa kwa mchakato wa wa timu kujitegemea na kuwa kampuni ya kusudi maalumu (SPV) unaendelea kuzuia kujitegemea kwa klabu za mpira na Halmashauri.

Kwa hiyo, hali hii inaathiri uwazi, uadilifu, na uwajibikaji wa timu kuhusiana na usimamizi wa mapato na matumizi.

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa husika kutambua na kusimamia mapato yote yanayopokelewa mpaka vilabu hivyo vitakapojitambulisha rasmi kama kampuni huru ndani ya halmashauri. Kwa kuwa vilabu hivyo vya mpira wa miguu vinajiendesha chini ya Halmashauri, inategemewa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika atachukua jukumu kamili la kusimamia uendeshwaji wake.**

**Aidha, nashauri kuharakisha mchakato wa kubadilisha Vilabu vya Mpira wa Miguu kuwa Kampuni ya Kusudi Maalumu (SPV). Mchakato huu utawezesha klabu kuwa na katiba yake, muundo wa usimamizi, na kutumia akaunti zake. Kufuatia hivyo, vilabu hivyo vitaweza kuandaa taarifa za kifedha, kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya fedha zinazotolewa na Halmashauri na wafadhili.**

# SURA YA KUMI NA TANO



## UFANISI KATIKA UDHIBITI WA TAKA

**15.0 Utangulizi**

Usimamizi wa taka wenye ufanisi katika mamlaka za serikali za mitaa una umuhimu mkubwa katika kulinda afya ya jamii, kuhifadhi usafi wa mazingira na kuchochea maendeleo endelevu. Utupaji taka sahihi huzuia kuenea kwa magonjwa na vitu vinavochafua mazingira, hulinda afya ya jamii na huhakikisha mazingira safi na salama ya kuishi.

Usimamizi wa taka katika mamlaka za serikali za mitaa unasimamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 na Kanuni zake za mwaka 2009, ambazo zinaeleza taratibu za kushughulikia aina mbalimbali za taka, ikiwamo zile hatari. Aidha, Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 na Sheria ya Afya ya Umma ya mwaka 2009 zinajumuisha vipengele vya usimamizi wa taka. Aidha, Sheria ya serikali za mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya serikali za mitaa (Mamlaka za Miji), Sura 288 ikizipa mamlaka za serikali za mitaa jukumu la kusimamia udhibiti wa taka katika ngazi za mijini na wilayani. Licha ya mfumo huu wa kisheria, juhudi zaidi zinahitajika ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wa usimamizi wa taka nchini kote.

Mamlaka za serikali za mitaa zinawajibika kwa huduma za usimamizi wa taka, zikijumuisha usimamizi wa ukusanyaji, usafirishaji, na utupwaji wa taka.

Kupitia mipango ya kimkakati na mipango shirikishi, mamlaka za serikali za mitaa zinaweza kuongeza uwezo wao wa kudhibiti taka ipasavyo, na hivyo kukuza malengo ya maendeleo endelevu na kuimarisha ubora wa maisha kwa wananchi wao.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya Sh. bilioni 19.45 zilikusanywa na mamlaka 117 za serikali za mitaa kama ada ya ukusanyaji wa taka kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na.46**.

Hata hivyo, tathmini yangu ya usimamizi na uhifadhi wa taka katika mamlaka za serikali za mitaa imebaini kuwa usimamizi wa taka bado unakabiliwa na changamoto nyingi. Miongoni mwazo ni: upungufu wa wafanyakazi, bajeti ndogo, mazingira yasiyofaa ya kufanyia kazi, miundombinu isiyotosheleza na ongezeko la idadi ya watu linalosababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa taka. Masuala haya kwa pamoja huchangia katika uchafuzi wa mazingira na kueneo kwa magonjwa ya mlipuko.

Sura hii inatoa picha kuhusu changamoto zinazojitokeza katika usimamizi wa taka. Pia, inabainisha maeneo muhimu yanayohitaji kipaumbele. Zaidi, inapendekeza hatua ambazo serikali na wadau wengine wanaweza kuchukua kushughulikia changamoto hizi kwa lengo la kuboresha.

Kwa kuangazia masuala haya na kupendekeza suluhisho zinazowezekana, sura hii inalenga kuchangia katika uboreshaji wa usimamizi wa taka na matokeo yake katika mamlaka za serikali za mitaa.

## 15.1 Upungufu wa miundombinu ya kusimamia taka ngumu katika mamlaka za serikali za mitaa

Kifungu cha 119 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuchagua namna bora ya kukusanya na kuhifadhi taka ngumu katika maeneo yao. Uamuzi huu unapaswa kuzingatia mambo mbalimbali ikiwemo: hali ya hewa, uwezo wa kiuchumi, maslahi kwa jamii; faida za mazingira, usafi na upatikanaji wa maeneo ya kutupa.

Uchambuzi wa mfumo wa usimamizi wa taka ngumu katika mamlaka nane za serikali za mitaa na uchambuzi wa uzalishaji wa taka katika kipindi cha miaka mitatu kama ilivyobainishwa katika **Jedwali Na. 108,** nilibaini kuongezeka kwa uzalishaji wa taka na upungufu katika ufanisi wa mikakati ya usimamizi wa taka ngumu inayotumika. Upungufu huu ulionekana wazi katika maeneo ya uzalishaji wa taka ngumu, ukusanyaji, uhifadhi na utupaji wa taka ngumu.

Mathalani, nilibaini upungufu wa vifaa vya ukusanyaji wa taka na kutokuwapo kwa miundombinu yenye ufanisi, ambayo ina athari kubwa kwa usimamizi wa taka kama inavyoelezwa kwenye **Jedwali Na.109.**

**Jedwali Na. 108: Upungufu wa miondombinu ya taka**

| Vifaa | Vifaa vinavyohitajika | Vilivyo po | Upungufu | % ya Upungufu | Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| Makasha ya kusafirishia taka | 33 | 7 | 24 | 77 | H/M Ubungo H/Jiji Tanga |

| Vifaa | Vifaa vinavyohitajika | Vilivyo po | Upungufu | % ya Upungufu | Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| Vikapu vya kusafirishia taka | 259 | 35 | 124 | 78 | H/M Moshi<br>H/Mji Bariadi<br>H/Mji Nzega<br>H/Jiji Dar es Salaam<br>H/M Mpanda<br>H/W Same |
| Gari la kubeba taka | 44 | 13 | 16 | 55 | |
| Trekta | 12 | 2 | 10 | 83 | |
| Trela | 10 | 2 | 8 | 80 | |
| Magari ya kufagia barabara | 16 | 0 | 16 | 100 | |
| Viyuo vya kukusanyia taka | 83 | 12 | 71 | 85 | |
| Dampo | 14 | 3 | 11 | 79 | |

**Chanzo:** Taarifa ya vitengo vya taka

**Jedwali Na. 109: Uzalishaji wa taka katika Halmashauri kwa miaka mitatu**

| Halmashauri | Mwaka wa fedha | Makundi ya taka | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ngumu | Hatari | Zinazo chakatika | Kikaboni | Zingine | Jumla (tani) |
| H/M Ubungo | 2020/21 | 39,099 | 6,015 | 72,182 | 180,456 | 3,008 | 300,760 |
| | 2021/22 | 38,632 | 6,439 | 77,263 | 193,158 | 6,439 | 321,930 |
| | 2022/23 | 35,733 | 6,497 | 77,964 | 194,910 | 9,746 | 324,850 |
| H/Mji Nzega | 2020/21 | 7,056 | 2,016 | 336 | 672 | - | 10,080 |
| | 2021/22 | 7,392 | 2,016 | 336 | 672 | - | 10,416 |
| | 2022/23 | 8,736 | 2,688 | 672 | 1,680 | - | 13,776 |
| H/Jiji Dar es Salam | 2020/21 | 401,500 | 28,105 | 164,615 | 196,735 | 12,045 | 803,000 |
| | 2021/22 | 401,500 | 28,105 | 164,615 | 196,735 | 12,045 | 803,000 |
| | 2022/23 | 481,800 | 33,580 | 197,465 | 236,155 | 14,600 | 963,600 |
| H/M Mpanda | 2020/21 | 23,725 | 840 | 4,015 | 12,240 | 576 | 41,396 |
| | 2021/22 | 31,390 | 1,095 | 5,475 | 16,200 | 648 | 54,808 |
| | 2022/23 | 37,960 | 1,314 | 6,570 | 19,800 | 1,008 | 66,652 |
| H/M Moshi | 2020/21 | 28,470 | - | 18,250 | 7,300 | - | 54,020 |
| | 2021/22 | 29,200 | - | 16,425 | 5,475 | - | 51,100 |
| | 2022/23 | 36,500 | - | 12,775 | 3,650 | - | 52,925 |
| H/W Siha | 2020/21 | 30,600 | 1,095 | 1,460 | 29,930 | - | 63,085 |
| | 2021/22 | 32,400 | 4,860 | 1,825 | 31,025 | - | 70,110 |
| | 2022/23 | 36,000 | 1,800 | 2,555 | 32,850 | - | 73,205 |
| H/W Same | 2020/21 | 70,163 | 16,425 | - | - | - | 86,588 |
| | 2021/22 | 65,766 | 20,075 | - | - | - | 85,841 |
| | 2022/23 | 67,876 | 23,725 | - | - | - | 91,601 |
| H/Jiji Arusha | 2020/21 | 108,040 | 5,475 | 31,390 | 60,590 | 10,950 | 216,445 |
| | 2021/22 | 112,785 | 5,840 | 32,850 | 63,145 | 11,315 | 225,935 |
| | 2022/23 | 117,895 | 6,205 | 34,404 | 66,065 | 12045 | 236,614 |

**Chanzo:** Taarifa za halmashauri

Upungufu wa miundombinu unaathiri usimamizi wa taka, unachangia uchafuzi wa hewa, na kuathiri moja kwa moja mifumo ya ikolojia. Pia, unaweza kuchangia magonjwa ya mlipuko.

**Ninapendekeza kwamba OR-TAMISEMI, kupitia Halmashauri, ihakikishe miundombinu inayohitajika inapatikana ili kuimarisha usimamizi wa taka na kudumisha mazingira safi. Pia, halmashauri zinaweza kuanzisha ushirikiano na makampuni binafsi kwa lengo la kuboresha miundombinu na huduma za usimamizi wa taka. Ushirikiano wa Umma na Binafsi (PPPs) unaweza kusaidia kutanua wigo wa**

**rasilimali na utaalamu kwa ajili ya ukusanyaji, uchakataji, na utupaji taka kwa ufanisi zaidi.**

### 15.2 Mapato yaliyokusanywa kutoka huduma za usimamizi wa taka yametumika kwa shughuli zisizohusiana - Sh. bilioni 1.25

Kifungu cha 73 (3) cha Sheria ya Afya ya Umma ya mwaka 2009 kinaelekeza mapato yaliyokusanywa kutoka kwenye huduma za usimamizi wa taka kutumika kuboresha huduma za afya ya mazingira.

Kinyume na sheria tajwa, nilibaini kuwa Halmashauri ya Jiji la Arusha ilikusanya Sh. bilioni 1.25 kutoka kwenye shughuli za usimamizi wa taka. Hata hivyo, kiasi hicho kilichokusanywa hakikutumika kikamilifu katika kuboresha huduma za afya na mazingira, hususani usimamizi wa taka ngumu.

Sekta ya mazingira, hususani usimamizi wa taka ngumu, huenda isiboreshwe ikiwa fedha hazitengwi kulingana na mahitaji ya Sheria ya Afya ya Umma ya mwaka 2009.

**Ninashauri uongozi wa Halmashauri kuweka mfumo thabiti wa kufuatilia usimamizi wa taka ili kuhakikisha kuwa, mapato yanayokusanywa kutoka kwenye usimamizi wa taka yanatumika kuboresha huduma za afya ya mazingira.**

### 15.3 Kuwapo kwa eneo la kuhifadhi taka lisilo rasmi katika Mtaa wa Goba Majengo

Nilifanya tathmini ya mfumo wa usimamizi wa taka ngumu katika barabara na masoko mbalimbali ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo na kubaini kuwapo kwa eneo lisilo rasmi la kuhifadhi taka karibu na eneo la makazi mtaa wa Goba Majengo karibu na mto Tegeta.

Aidha, wakati wa ziara ya kutembelea eneo hilo, nilibaini magari mawili, moja likiwa mali ya taasisi binafsi na katika hali ya kushangaza; lingine lilikuwa mali ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, likiwa na taka zisizofunikwa karibu na eneo hilo la kuhifadhi taka lisiloidhinishwa tayari kutupa taka.

Pia, nilibaini kuwa kila gari la kubeba taka limekuwa likitozwa Sh.5,000 kwa safari. Fedha hiyo hulipwa kwa mmiliki wa eneo karibu na mto kama ada ya kuhifadhi taka, licha ya kutokuwa na idhini ya kukusanya ada hizo. Kitendo hiki cha kutupa taka bila kibali kinachafua mazingira na kuhatarisha afya ya kaya katika eneo hilo.

**Ninashauri Halmashauri husika kusitisha kutupa taka kiholela kwa kuanzisha maeneo sahihi ya kutupa taka;. Pia,ifuatilie mapato yaliyokusanywa kutokana na malipo ya ada za kutupa taka kiholela kwa hatua za marekebisho.**

**Pia, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kutekeleza mfumo thabiti wa ukusanyaji wa taka unaofika maeneo yote ya mamlaka hizo. Hii inaweza kuhusisha kuanzisha vituo vya ukusanyaji maalumu au kutumia huduma za ukusanyaji nyumba kwa nyumba.**

## 15.4 Gharama ya kukusanya taka inazidi mapato yaliyokusanywa Sh. milioni 864.06

Sheria za Usimamizi wa Afya na Mazingira, 2022 zinaipa Halmashauri jukumu la kukusanya taka kutoka kwa kaya kwa kiwango kilichowekwa.

Hata hivyo, ukaguzi wangu umebaini kuwa Halmashauri sita kati ya Halmashauri 117 zilikusanya Sh. milioni 645.51 kutoka kwa ada za huduma za ukusanyaji taka, huku zikifanya matumizi ya jumla ya Sh.bilioni 1.51 kwa wakusanyaji na usafirishaji wa taka hadi eneo la kutupa. Hii imesababisha zidio la gharama kwa Sh. milioni 864.06 (57%). Maelezo zaidi yanapatikana kwenye **Jedwali Na.110.**

**Jedwali Na. 110: Mapato na matumizi ya ukusanyaji taka**

| Na | Halmashauri | Mapato yaliyokusanywa (Sh.) | Matumizi (Sh.) | Zidio (Sh.) | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Nkasi | 3,856,100 | 33,995,814 | 30,139,714 | 11 |
| 2 | H/W Bukoba | 0 | 76,467,030 | 76,467,030 | 0 |
| 3 | H/W Mlimba | 249,100 | 20,795,876 | 20,546,776 | 1 |
| 4 | H/W Ukerewe | 0 | 12,360,000 | 12,360,000 | 0 |
| 5 | H/W Njombe | 0 | 140,509,596 | 140,509,596 | 0 |
| 6 | H/M Ilemela | 641,402,835 | 1,225,440,276 | 584,037,441 | 52 |
| **Jumla** | | **645,508,035** | **1,509,568,592** | **864,060,557** | **43** |

**Chanzo**: Taarifa za fedha zilizokaguliwa 2022/23

Kukosekana kwa uwiano wa kifedha katika huduma za ukusanyaji taka kumesababisha matumizi ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani, ambayo awali vilikuwa vimepangwa kwa miradi mingine kutumika.

Uchepushaji wa fedha unaweza kukwamisha uwezo wa halmashauri kutekeleza miradi muhimu ya Maendeleo. Uhamishaji huu wa kifedha umesababisha halmashauri kushindwa kushughulikia mahitaji muhimu ya jamii, hivyo kusimamisha maendeleo na kupunguza ustawi wa jumla wa wananchi.

Aidha, uchepushaji wa mapato ya ndani yaliyokusudiwa kwa miradi mingine hudhoofisha uendelevu wa kifedha wa Halmashauri na kupunguza imani ya umma katika nyanja ya usimamizi wa fedha.

Bila ufadhili wa kutosha kwa ajili ya mipango muhimu; miundombinu ya jamii, afya, na mazingira; kutapelekea kuongezeka kwa changamoto zilizopo na kuzuia ukuaji na ustawi wa muda mrefu.

**Ninatoa ushauri kwa mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini upya na kubuni upya huduma za ukusanyaji taka, kwa njia bora zaidi na yenye ufanisi wa gharama. Pia, kuhakikisha kuwa mapato yanayopatikana kutokana na huduma za ukusanyaji taka yanakidhi gharama zinazohusiana.**

**Hii inaweza kuhusisha mapitio ya sheria za usimamizi wa taka ili kujumuisha viwango rafiki kulingana na maeneo na viwango vya maisha ili kukuza mazingira safi. Vilevile, halmashauri zinashauriwa kuweka kipaumbele katika kuboresha operesheni ya usafi, kuwekeza katika teknolojia za kisasa, na kushirikiana na wadau ili kuboresha matumizi ya rasilimali.**

## 15.5 Usimamizi duni wa mawakala wa kukusanya ada za taka

### i) Mawakala wanakusanya ushuru wa taka bila ya kuwa na dhamana ya utendaji Sh. milioni 301.55

Agizo 38 (3) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaelekeza wakala wa mapato kuweka dhamana kwenye mamlaka ya serikali ya mitaa kiasi cha malipo ya miezi mitatu, dhamana ya benki, au aina zingine za dhamana, kama mamlaka ya serikali ya mitaa itavyoona inafaa. Aidha, kifungu Na. 29 (1) cha Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kinaitaka taasisi nunuzi kumtaka mwombaji aliyeshinda kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi.

Hatua hizi zinakusudia kuhakikisha kuwa majukumu ya kimkataba yanatimizwa kikamilifu, ikijumuisha malipo kwa vibarua wote, wasambazaji bidhaa, mafundi na wakandarasi wasaidizi wanaoshiriki katika utekelezaji wa mradi husika. Hatua hizo ni kinga dhidi athari za kifedha na kuhakikisha kuwa kuna uwajibikaji wakati wote wa mchakato wa ununuzi na ukusanyaji wa mapato pamoja na kuongeza uwazi na ufanisi katika usimamizi wa fedha za umma.

Ukaguzi ulibaini kutofuatwa kwa Agizo 38 (3) la Memoranda ya fedha ya mwaka 2009, na Kifungu 29 (1) cha Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013. Nilibaini kuwa mawakala wa ukusanyaji taka katika halmashauri za jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Iringa hawakuweka malipo ya miezi mitatu inayohitajika au kutoa dhamana inayofaa; badala yake, walitoa "dhamana za bima" zilizotosheleza mwezi mmoja.

Aidha, hakuna dhamana za utendaji zilizowasilishwa baada ya kumalizika kwa dhamana ya awali, na kuruhusu mawakala kufanya kazi bila kutimiza majukumu yao kama inavyoelezwa kwenye **Jedwali Na.111.**

**Jedwali Na. 111: Mawakala wakusanya ushuru wa taka wasio na dhamana**

| Halmashauri | Mkataba | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| H/Jiji Dar es Salam | LGA/015/IMC/2020-2020/HQ/NCS/94-LOT2 | 52,000,000 |
| | LGA/015/IMC/2020-2020/HQ/NCS/24-LOT94 | 100,000,000 |
| | LGA/015/IMC/2020-2020/HQ/NCS/24-LOT43 | 77,500,000 |
| | LGA/015/IMC/2020-2020/HQ/NCS/24-LOT39 | 40,000,000 |
| H/M Iringa | LGA/025/2022/2023/N/01 | 8,013,200 |
| | LGA/025/2022/2023/N/04 | 8,013,200 |
| | LGA/025/2022/2023/N/03 | 8,013,200 |
| | LGA/025/2022/2023/N/02 | 8,013,200 |
| **Jumla** | | **301,552,800** |

**Chanzo**: Mafaili ya mikata ya wakusanya ushuru wa taka

**ii) Mawakala wanaokusanya ada za taka bila mikataba halali Sh. milioni 105.55**

Aya 5.2.1 (b) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato wa Mamlaka za Mitaa (LARAM) wa mwaka 2019 kinaitaka halmashauri kuhakikisha mikataba yote ya ukusanyaji mapato kati ya mawakala na halmashauri inapitiwa na wataalamu wa kisheria na ina makubaliano maalumu ya kuwabana mawakala.

Pia, itahitajika kubainisha kiasi cha mapato kitakachokusanywa na kamisheni itakayolipwa kwa mawakala, hatua na/au adhabu zinazoweza kuchukuliwa kwa ukiukaji wa mikataba na kuruhusu mabadiliko kwa upande wa kuongezeka kwa malipo ya mapato yaliyokusanywa kwa halmashauri.

Hata hivyo, katika ukaguzi wangu wa mikataba iliyoingiwa na mawakala wa taka, nilibaini kuwa mawakala watatu wa ukusanyaji wa ada za taka walifanya kazi bila mikataba halali, na kukiuka Aya 5.2.1 (b) ya LARAM, 2019.

Mikataba hii haikuwa na uhakiki wa kisheria; haikuwa na makubaliano maalumu ya kuwabana; na haikueleza vipengele muhimu kama vile kiasi cha ukusanyaji wa mapato, viwango vya kamisheni, na hatua za kuchukua kwa ukiukwaji wa mkataba, kama inavyoelezwa katika **Jedwali Na.112.**

**Jedwali Na. 112: Ukusanyaji wa ushuru wa taka bila ya mikataba halisi**

| Halmashauri | Mkataba | Tarehe ya kuanza | Tarehe ya kumaliza | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| H/Jiji Dar es Salam | LGA/018/DCC/2021-2022/HQ/NCS/25 LOT 3 | 01 Julai 2022 | 30 Juni 2023 | 30,700,000 |
| | LGA/018/DCC/2021-2022/HQ/NCS/25/LOT 1 | 01 Julai 2022 | 30 Juni 2023 | 44,847,500 |
| | LGA/018/DCC/2021-2022/HQ/NCS/25/LOT 14 | 01 Julai 2022 | 30 Juni 2023 | 30,000,000 |
| **Jumla** | | | | **105,547,500** |

Chanzo: Mafaili ya mikataba ya wakusanya ushuru wa taka

Kutokuwapo kwa dhamana za utendaji na mikataba halali kunaweza kuziweka halmashauri katika hatari ikiwa mawakala wa ukusanyaji ushuru wa taka watashindwa kutekeleza majukumu yao au kutimiza wajibu wao, hivyo kusababisha utata wa kisheria kutokana na migogoro inayoweza kutokea kati ya mawakala na halmashauri.

**Ninapendekeza kwamba uongozi wa Halmashauri husika uangalie ufanisi wa dhamana za bima zinazotumika na kutafuta njia mbadala za dhamana zinazolingana na viwango vya kisheria na kutoa dhamana ya kutosha.**

**Pia, wahuishe mikataba ya mawakala wanaofanya kazi bila makubaliano halali ili kupunguza hatari za kisheria na kifedha zinazohusiana na kufanya kazi bila nyaraka sahihi.**

## 15.6 Upungufu uliobainika katika usimamizi na ukusanyaji wa taka kwenye mamlaka za serikali za mitaa

Halmashauri zimeanzisha mfumo wa ukusanyaji wa taka. Mfumo huu unajumuisha kuingia mikataba na watoahuduma kadhaa wa ukusanyaji wa taka, kuwapa jukumu la kusafisha barabara, kukusanya taka, na kukusanya ada za kutoa huduma kwa niaba ya mamlaka za serikali za mitaa.

Katika mapitio ya mikataba, nilibaini kuwa wakusanyaji wanakusanya taka moja kwa moja pamoja na ada za huduma kutoka kwa wananchi. Hivyo, wanapaswa kuhamisha sehemu iliyobainishwa ya mapato haya kwa mamlaka ya serikali za mitaa kulingana na masharti ya mikataba. Mfumo

huu unalenga kurahisisha shughuli za usimamizi wa taka, huku ukihakikisha uwajibikaji na uwazi katika michakato ya ukusanyaji mapato.

Hata hivyo, licha ya kuwa na mikataba hiyo, nilibaini dosari zifuatazo.

i) **Kulipwa kiwango pungufu ya mkataba na mawakala wa ukusanyaji taka Sh. milioni 485.47**

Mikataba iliyoingiwa kati ya Halmashauri za Wilaya na Mawakala wa ukusanyaji taka, hususani katika vifungu vya 14 na 16 vya masharti maalum, imebainishwa kuwa mawakala wanapaswa kuhamisha asilimia iliyopangwa ya ukusanyaji kwa halmashauri kila mwishoni mwa mwezi.

Katika ukaguzi wangu wa ukusanyaji wa mapato kutoka kwa mawakala, nilibaini kuwa mgao wa halmashauri ulipaswa kuwa Sh. bilioni 1.04. Hata hivyo, kiasi cha Sh. milioni 751 pekee kiliwasilishwa benki, hii ikisababisha upungufu wa Sh. milioni 285.89, kama inavyoelezwa katika **Jedwali Na.113**. Licha ya suala hili kujirudia, mamlaka za serikali za mitaa husika hazijawachukulia hatua stahiki au kukusanya deni hili.

Vilevile, tofauti na masharti yaliyoorodheshwa katika Kifungu Na. 2.5 cha mikataba, ambacho kinahitaji mawakala wa ukusanyaji kuhamisha 50% ya kiasi chochote kilichokusanywa zaidi ya jumla ya mkataba kwa halmashauri kila ifikapo tarehe 15 ya mwezi unaofuata, nilibaini kuwa wakala mwenye mkataba na. LGA/015/IMC/2020-2022/HQ/NCS/24-LOT 41&94 alikusanya ziada ya Sh. milioni 393.88 katika halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ukilinganisha na jumla ya mkataba.

Kwa kuzingatia matakwa ya kimkataba, alipaswa kuwasilisha Sh.milioni 199.58. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuwasilishwa katika akaunti za Halmashauri; na kiasi kilichosalia bado hakijakusanywa.

Ukiukaji huo unaleta athari kubwa za kifedha na kuibua shaka kuhusu ufanisi na usimamizi wa ukusanyaji mapato.

**Jedwali Na. 113: Mawakala waliowasilisha benki kiwango pungufu**

| Halmashauri | Mkataba Na. | Kiasi kilichokusanywa (Sh) | Asilimia ya halmashauri (Sh) | Kiasi kilichopelekwa benki (Sh) | Upungufu (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| H/Jiji Dar es Salam | LGA/018/DCC/2021/2022/HQ/NCS/25 LOT 3 | 343,822,409 | 28,300,800 | 3,000,000 | 25,300,800 |
| H/Jiji Dar es Salam | LGA/015/IMC/2020/2022/ | 4,437,878,923 | 399,162,000 | 370,363,500 | 28,798,500 |

| Halmashauri | Mkataba Na. | Kiasi kilichokusanywa (Sh) | Asilimia ya halmashauri (Sh) | Kiasi kilichopelekwa benki (Sh) | Upungufu (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| | HQ/NCS/24-LOT 41&94 | | | | |
| H/Jiji Dar es Salam | LGA/018/DCC/2021/2022/HQ/NCS/25/LOT 14 | 283,678,132 | 26,457,600 | 16,578,250 | 9,879,350 |
| H/Jiji Dar es Salam | LGA/018/DCC/2021-2022/HQ/NCS/25/LOT 1 | 515,868,426 | 38,030,400 | 24,244,400 | 13,786,000 |
| H/Jiji Dar es Salam | LGA/015/IMC/2020-2020/HQ/NCS/24-LOT43 & 39 | 1,279,597,835 | 110,700,000 | 75,317,084 | 35,382,916 |
| H/Jiji Dar es Salam | LGA/015/IMC/2020-2020/HQ/NCS/24-LOT38 | 717,490,100 | 76,968,480 | 65,242,060 | 11,726,420 |
| H/Jiji Dar es Salam | LGA/015/IMC/2021-2020/HQ/NCS/94-LOT1M/S | 2,852,663,252 | 328,127,616 | 191,407,776 | 136,719,840 |
| H/M Iringa | LGA/025/2022/2023/N/01 | 53,859,420 | 29,921,900 | 5,627,500 | 24,292,400 |
| **Jumla** | | **10,484,858,497** | **1,037,668,796** | **751,780,570** | **285,886,226** |

**Chanzo**: Mikataba ya mawakala, taarifa za makusanyo kutoka kwenye POS 2022/23

**ii) Ada ya taka iliyokusanywa chini ya kiwango cha mikataba Sh. bilioni 1.55**

Nilifanya mapitio ya mikataba iliyotolewa kwa mawakala wa ukusanyaji taka, na dhana kuu ikiwa kuwa mikataba ilitolewa kwa wazabuni waliodhihirisha ukusanyaji wa mapato ya juu.

Hata hivyo, uchambuzi wangu wa mifumo ya ukusanyaji mapato kutoka kwa mawakala umeonesha kutofautiana katika ukusanyaji wa ada ya taka ikilinganishwa na masharti yaliyotajwa katika makubaliano na Halmashauri.

Kutofautiana huku kunaonesha kwamba mawakala hawajakusanya jumla ya Sh. bilioni 1.55, kama inavyoelezwa katika **Jedwali Na.114.** Hata hivyo, hakuna hatua zilizochukuliwa kushughulikia suala hili.

**Jedwali Na. 114: Makusanyo ya ada ya taka chini ya kiwango cha mikataba**

| Halmashauri | Mkataba Na | Kiasi cha mkataba (Sh) | Kiasi kilichokusanywa (Sh) | Upungufu (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| H/Jiji Dar es Salam | LGA/018/DCC/2021-2022/HQ/NCS/25 LOT 3 | 368,400,000 | 343,822,409 | 24,577,591 |
| | LGA/018/DCC/2021-2022/HQ/NCS/25/LOT 14 | 360,000,000 | 283,678,132 | 76,321,868 |
| | LGA/018/DCC/2021-2022/HQ/NCS/25/LOT 1 | 786,510,000 | 515,868,426 | 270,641,574 |
| | LGA/015/IMC/2020-2020/HQ/NCS/24-LOT43 & 39 | 1,410,000,000 | 1,279,597,835 | 130,402,165 |
| | LGA/015/IMC/2020-2020/HQ/NCS/24-LOT38 | 834,000,000 | 717,490,100 | 116,509,900 |
| | LGA/015/IMC/2020-2020/HQ/NCS/94-LOT1M/S | 3,784,799,520 | 2,852,663,252 | 932,136,268 |
| **Jumla** | | **7,543,709,520** | **5,993,120,154** | **1,550,589,366** |

Chanzo: Mikataba ya mawakala/POS

**iii) Upungufu mwingine uliobainika**

Nilifanya tathmini ya usimamizi wa taka katika halmashauri 14 na kubaini upungufu kadhaa. Upungufu huo ni: kutokuwapo kwa eneo maalumu la kutupa taka; baadhi ya maeneo ya kutupa taka kutokuwa na uzio; kucheleweshwa kuondoa taka ngumu kutoka maeneo ya ukusanyaji; aina tofauti za taka ngumu kutotengwa kwa asili na watu binafsi; pamoja na familia, taasisi, masoko na mahali pa kutupa.

Aidha, nilibaini uwapo wa mrundikano wa  taka zisizoondolewa karibu na maeneo ya makazi au biashara na vifaa chakavu vya usimamizi wa taka vilivyoshindwa kutumika au kufanyiwa matengenezo. Upungufu huu unahitaji kushughulikiwa ili kuboresha udhibiti wa taka katika Halmashauri.

Halmashauri husika zinapaswa kuchukua hatua kwa dosari zilizobainishwa ili kuwapo na utunzaji wa mazingira endelevu. Maelezo ya kina juu ya masuala haya yametolewa katika **Kiambatisho Na.47.**

Hasara za kifedha zilizopatikana na Halmashauri, zinazotokana na ukusanyaji duni, upungufu wa kubenki kwa mawakala wa ukusanyaji taka, na upungufu katika mazoea ya usimamizi wa taka, zinaleta changamoto kubwa katika utoaji wa huduma muhimu za ukusanyaji taka.

Vikwazo hivi vya kifedha vinatishia uwezo wa halmashauri katika kushughulikia kwa ufanisi changamoto za usimamizi wa taka na kuhakikisha ustawi wa jamii. Hatua za dharura na kina zinahitajika kupunguza matatizo haya na kuboresha uendelevu na ufanisi wa operesheni za usimamizi wa taka katika halmashauri.

**Ninashauri halmashauri husika kuhakikisha kiasi kinachodaiwa kwa mawakala wa ukusanyaji kinakusanywa na kuwasilishwa benki; iimarishe utaratibu wa usimamizi na ufuatiliaji ili kuhakikisha mawakala wa ukusanyaji wanazingatia masharti ya mkataba, na izingatie hatua za kisheria dhidi ya mawakala wanaokiuka mara kwa mara majukumu yao ya mkataba.**

**Pia, halmashauri zinashauriwa kutathmini viwango vya uzalishaji taka kutoka kwenye viwanda, masoko na kaya na kuweka mkandarasi/wakala kulingana na uwezo wa vifaa, nguvu kazi na uzoefu wake.**

## 15.7 Kituo cha Mabwepande cha kutengeneza mbolea itokanayo na taka kufanya kazi chini ya ufanisi uliokusudiwa - Sh. bilioni 8.20

Kituo cha kutengeneza mbolea isiyo na kemikali itokanayo na taka (mboji) Mabwepande kinachomilikiwa kwa ubia kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na Free Hanseatic City ya Hamburg Ujerumani, kinalenga kusimamia taka kwa ufanisi kwa kuzitengeneza kuwa mbolea isiyo na kemikali.

Mradi huu una gharama ya Sh. bilioni 7.1 na mali zisizo hamishika za jumla ya Sh. bilioni 1.1, kituo kinawakilisha uwekezaji mkubwa katika Nyanja ya uchakataji na udhibiti endelevu wa taka kwa manufaa ya mazingira na jamii kwa ujumla.

Ukaguzi wangu umebaini kuwa kituo kinafanya uzalishaji chini ya matarajio. Kinachakata na kinasindika taka za kikaboni kwa kiwango cha kati ya tani 10 na 25 kwa siku, kikishindwa kufikia uwezo uliopangwa wa tani 50 kwa siku.

Hii inatokana na wakusanyaji taka katika Halmashauri zingine za Dar es Salaam kupendelea kupeleka taka kwenye dampo la Pugu Kinyamwezi kwa kuwa hazilazimiki kutenganisha taka kabla ya kuzitupa kama inavyohitajika na kituo cha kuzalisha mbolea.

Pia, nilibaini palikuwa na mpango wa awali wa Halmashauri kuchukua umiliki kamili wa kiwanda baada ya miaka mitatu ya uendeshaji ambayo ilimalizika Novemba 2023. Hata hivyo, mpango wa urithi haukupatikana wakati ulipohitajika kwa ukaguzi, hivyo kuibua wasiwasi kuhusu kuendelea kwa kituo.

Pia, nilibaini kutokuwapo kwa wafanyakazi waliofundishwa kuchukua jukumu hilo baada ya wamilili muda wao kumalizika. Hii inaweza kuhatarisha malengo ya kituo kutofikiwa.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI na sekretarieti ya mkoa Dar es Salaam kuhamasisha wakazi na biashara kutekeleza utaratibu wa kutenganisha taka katika chanzo kwenye makundi kama vile zinazoweza kuchakatika, taka za kikaboni, na zisizoweza kuchakatika. Pia, itoe makasha tofauti kutenganisha aina za taka; itoe elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutenganisha taka; na ipeleke taka za kikaboni kwenye kituo cha mbolea. Hii itaimarisha uwezo wa kiwanda na kuchangia kudumisha usafi wa Dar es Salaam.**

**Aidha, Halmashauri inapaswa kuunda mpango kamili wa urithi wenye maelezo ya mchakato wa kutambua, kufundisha, na kumhamishia wafanyakazi muhimu. Hii itahakikisha uendeshaji sahihi wa kiwanda cha mbolea mara baada ya kukabidhiwa kwa Halmashauri.**

# SURA YA KUMI NA SITA



# MAPITIO YA USIMAMIZI WA ARDHI

## 16.0 Utangulizi

Sura hii inatathmini migogoro na changamoto zinazohusiana na Ardhi ambazo hazijatatuliwa na iwapo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (MLHHSD), OR-TAMISEMI na Wizara ya Katiba na Sheria zinafanya kazi ipasavyo kushughulikia matatizo hayo.

Nimekagua hesabu za mamlaka za serikali za mitaa na kubaini mambo muhimu yafuatayo ambayo yanapaswa kushughulikiwa na mamlaka husika:

## 16.1 Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK)

### 16.1.1 Ufanisi usioridhisha wa masuala ya Kifedha ya Programu ya KKK

Nimefanya tathmini ya ufanisi wa kifedha katika utekelezaji wa Programu ya KKK na kubaini kuwa OR-TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, zilitoa mikopo ya Sh. bilioni 42.28 kwa mamlaka 58 za serikali za mitaa.

Hata hivyo, mamlaka za serikali za mitaa zilifanikiwa kurejesha mikopo kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kiasi cha Sh. bilioni 20.42 wakati kiasi cha Sh. bilioni 21.85 sawa na 52% hazikurejeshwa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.115** na kuchanganuliwa kwa kina katika **Kiambatisho Na.48**.

**Jedwali Na. 115: Ufanisi wa kifedha wa programu ya KKK**

| | |
|---|---|
| Halmashauri zilizofanyiwa Mapitio | 58 |
| Fedha Zilizopokelewa (Mikopo) | 42,278,468,000 |
| Fedha Zilizorejeshwa (Sh.) | 20,423,922,186 |
| **Kiasi kilichobaki (Sh.)** | **21,854,545,814** |

**Chanzo:** OR-TAMISEMI

Kwa ujumla, ufanisi wa kifedha hauridhishi kutokana na kiasi kikubwa ambacho hakijarejeshwa na Halmashauri.

**Ninatoa rai kwa OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa kushughulikia changamoto zote zilizobainika ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji.**

### 16.1.2 Hasara iliyobainika na matumizi mabaya ya Fedha za Programu ya KKK - Sh. milioni 327.82

Nilifanya ukaguzi maalumu wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya KKK zilizotolewa kwa H/W Shinyanga kiasi cha Sh. milioni 900 na kuwasilisha matokeo ya Ukaguzi kwa Mamlaka ambayo iliomba ukaguzi huo kwa mujibu wa Kifungu cha 29(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Kwa ujumla, nilibaini kuwa H/W Shinyanga ilishindwa kurejesha kiasi cha Sh. milioni 900 kwa Wizara ya Ardhi (MLHHSD) kulikogubikwa na ubadhirifu wa fedha na hasara ya Sh. milioni 327.82. Pia, niliripoti kuhusu udanganyifu katika mchakato wa ununuzi na matumizi ya fedha kwa shughuli ambazo hazihusiani na miongozo ya Programu.

Aidha, H/W Shinyanga ililipa Sh. milioni 307.97 kwa ajili ya kupima viwanja 3,178 katika vijiji viwili ambapo viwanja hivyo haviwezi kuuzwa kwa sababu wahusika hawakulipwa fidia, kinyume na Aya ya 3(3) ya Mwongozo wa Programu.

Funzo mojawapo linalotokana na ukaguzi huo maalumu katika utekelezaji wa Programu ya KKK katika H/W Shinyanga ni kwamba, ubadhirifu uliobainika ni dhahiri upo katika mamlaka za serikali za mitaa zingine, na huenda ubadhirifu wa aina hiyo ukasambaa kwa namna ambayo inaweza kuathiri utekelezaji wa Programu.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI kuhakikisha serikali za mitaa zinaanzisha ukaguzi wa papo kwa hapo katika kila hatua ya utekelezaji wa Programu ili kuondoa changamoto zinazojitokeza kwa wakati. Pia, ninaisihi OR-TAMISEMI kuhakikisha mapendekezo yangu niliyoyatoa kuhusu ukaguzi maalumu wa H/W Shinyanga yanatekelezwa bila kuchelewa na kuchukua hatua stahiki za kurekebisha dosari zilizobainika.**

### 16.1.3 Uwezekano wa kuwapo kwa ubadhilifu kwenye malipo ya fidia ya ardhi katika Kijiji cha Kirongwe - Sh. milioni 468

H/W Rorya ilipokea kiasi cha Sh. milioni 468 na kuzihamishia kwenye akaunti ya masurufu ya H/W Rorya kwa ajili ya malipo ya fidia ya ardhi kwa familia zilizoathirika na utwaaji wa ardhi katika Kijiji cha Kirongwe kupitia hati ya malipo Na. 00773104PV920604 ya tarehe 26 Juni 2022.

Hata hivyo, nilibaini kuwa fidia ya Sh. milioni 17.32 ililipwa kwa watu saba (7) ambao hawakutajwa katika Ripoti ya Tathmini. Kutokana na hali hiyo, walengwa 11 waliobainishwa katika Ripoti ya Tathmini hawakulipwa fidia kiasi cha Sh. milioni 18.20.

Pia, sikuweza kujiridhisha na kiasi cha fedha zilizowekwa kwenye akaunti za benki za walengwa. Fedha hizo ambazo ni Sh. milioni 436.49 zililipwa kupitia malipo ya pamoja (*Bulk payment*) yaliyofanywa na Benki ya NMB kwa sababu ya kutowasilishwa fomu za kuweka fedha na barua za kukiri mapokezi kutoka kwa wanufaika. Upungufu mwingine uliobainika ni pamoja na malipo kufanyika mara mbili na uchepushwaji wa fedha za fidia kiasi cha Sh. milioni 4.40 kutekeleza shughuli ambazo hazikupangwa.

Kwa ujumla, dosari zilizobainishwa zinatia shaka juu ya utendaji haki, uwazi, uaminifu katika ulipaji wa fidia na mchakato mzima wa ulipaji. Hali hii pia inachangia uwezekano wa kuibuka migogoro ya ardhi na uwezekano wa upotevu wa rasilimali fedha za umma.

**Ninapendekeza menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuimarisha vidhibiti na kuhakikisha kuwa fidia zinalipwa kwa mujibu wa nyaraka zilizoidhinishwa. Pia, menejimenti za serikali za mitaa zinapaswa kuhakikisha walipwaji wanakiri mapokezi ya fedha walizolipwa. Mwisho, menejimenti za serikali za mitaa zinapaswa kuchunguza na kuchukua hatua stahiki ili kurekebisha dosari zilizobainika.**

### 16.1.4 Mikopo ya Programu ya KKK ambayo haijarejeshwa - Sh. bilioni 21.85

Ili programu ya KKK iwe endelevu inategemea kwa kiasi kikubwa ufanisi wa Wizara ya Ardhi (MLHHSD) katika kukusanya mikopo kutoka kwa mamlaka za serikali za mitaa. Vilevile, uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa kurejesha mikopo unategemea kasi ya mauzo ya viwanja vilivyopimwa na kulipiwa fidia stahiki.

Kuna kusuasua kwa urejeshaji wa mikopo kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kasi ndogo ya kuuza viwanja vilivyopimwa inayochangiwa na kutokulipwa kikamilifu kwa fidia ya maeneo yaliyotwaliwa na kupimwa. Hali hii inazinyima mamlaka za serikali za mitaa haki ya kuuza viwanja hivyo, hivyo kusababisha mikopo iliyotolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa kutolipika.

Ninazipongeza Halmashauri 12 ambazo zilirejesha mikopo yenye jumla ya Sh. bilioni 9.8 kwa wakati. Hata hivyo, ninatoa angalizo kwa mamlaka 47 za serikali za mitaa ambazo hadi tarehe 08 Februari 2024 zilikuwa hazijarejesha mikopo yenye jumla ya Sh. bilioni 21.85. Mwenendo wa marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa umeoneshwa katika **Kiambatisho Na.48**.

Jambo linalotia shaka na ambalo linatakiwa kupewa umuhimu wa kipekee ni juu ya mamlaka za serikali za mitaa 10 kati ya 60 ambazo zilikuwa zimerejesha Sh. milioni 220.45 tu kati ya Sh. bilioni 9.72 sawa na asilimia mbili ya fedha zilizotolewa kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na.116.**

**Jedwali Na. 116: Halmashauri zisizokamilisha urejeshaji wa Mkopo**

| Na. | Halmashauri | Fedha zilizotolewa (Sh.) | Vilivyopimwa na Kuidhinishwa | Mauzo ya Viwanja (Sh. | Marejesho (Sh.) | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dodoma-Bihawana | 2,208,005,086 | - | - | 0 | - |
| | H/Jiji Dodoma-Ihumwa | 168,000,000 | 1,720 | 21,000,000 | - | - |
| | H/Jiji Dodoma-Mapinduzi | 1,108,545,980 | - | - | 0 | - |
| 2. | H/W Musoma | 200,000,000 | 3,518 | 95,000,000 | 0 | - |
| 3. | H/M Shinyanga | 1,055,000,000 | 2,162 | 865,907,566 | 0 | - |
| 4. | H/M Lindi | 1,600,000,000 | 1,783 | 8,730,000 | 8,730,000 | 1 |
| 5. | H/W Korogwe | 240,000,000 | 3,034 | 12,880,000 | 12,880,000 | 5 |
| 6. | H/Mji Korogwe | 80,000,000 | 1,060 | 5,075,000 | 5,075,000 | 6 |
| 7. | H/W Shinyanga | 900,000,000 | 3,527 | 74,024,332 | 49,647,482 | 6 |
| 8. | H/W Manyoni | 1,520,770,000 | 1,636 | 200,000,000 | 100,000,000 | 7 |
| 9. | H/Mji Mbulu | 455,000,000 | 3,600 | 20,000,000 | 30,000,000 | 7 |
| 10. | H/W Hanang | 187,500,000 | 3,750 | 18,000,000 | 14,120,000 | 8 |
| **Jumla** | | **9,722,821,066** | | | **220,452,482** | **2** |

**Chanzo:** OR-TAMISEMI

Mamlaka za serikali za mitaa kushindwa kutekeleza Makubaliano juu ya usimamizi wa mikopo iliyotolewa kunahatarisha kutofikiwa kwa malengo

ya mradi pamoja na uwezekano wa matumizi mabaya na upotevu wa fedha za Programu.

**Ninapendekeza kuwa OR-TAMISEMI ihakikishe mikopo iliyotolewa inasimamiwa ipasavyo kwa mujibu wa Mkataba uliosainiwa, ikiwamo kuchukua hatua madhubuti dhidi ya mamlaka za selikali za mitaa ambazo hazijarejesha mikopo ili zirejeshe mikopo hiyo kwa Wizara ya Ardhi (MLHHSD) ili mradi uwe endelevu na malengo yake yapatikane.**

### 16.1.5 Wingi wa kesi za ardhi dhidi ya mamlaka za serikali za mitaa unaotia shaka Sh. bilioni 4.18

Nilifanya tathmini na kubaini kuwa, mamlaka kadhaa za serikali za mitaa zilishitakiwa na wananchi katika mahakama na mabaraza ya ardhi. Zinalalamikiwa kutwaa ardhi kwa ajili ya matumizi ya umma pasipo kulipa fidia stahiki, ukosefu wa uwazi katika masuala ya ardhi, ugawaji wa viwanja mara mbili, utwaaji wa ardhi usio rasmi, na kadhalika.

Tathmini yangu ya mashauri yaliyosajiliwa katika mahakama/mabaraza mbalimbali katika mamlaka 19 za serikali za mitaa ilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa zilikuwa zinakabiliwa na mashauri 61 yaliyokuwa yanaendelea. Mashauri hayo yana jumla ya madai ya Sh. bilioni 4.18 na mashauri 33 ya ardhi ambayo hayakuhusisha madai ya fedha. Maelezo ya kesi ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 49.**

Nina shaka na kiasi kikubwa cha kesi za madai dhidi ya mamlaka za serikali za mitaa ambayo bado hayajaamuliwa, iwapo mamlaka za serikali za mitaa zitashindwa kesi hizo zinaweza kuwa na athari kubwa za rasilimali fedha pamoja na kuharibu taswira na sifa za mamlaka za serikali za mitaa.

**Naishauri OR- TAMISEMI, Wizara ya Ardhi (MLHHSD) na Wizara ya Katiba na Sheria kutafuta suluhu kwa pamoja ya migogoro ya ardhi katika mamlaka za serikali za Mitaa.**

**Pia ziangalie uwezekano wa kufanya mapitio ya mfumo wa sheria za ardhi uliopo katika muktadha wa kutatua migogoro ya ardhi kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria na wadau wengine.**

### 16.1.6 Migogoro inayohusishwa na ucheleweshaji au malipo ya fidia ya ardhi isiyostahiki

Katiba ya Jamhuri ya Tanzania, Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, Sheria ya Utwaaji Ardhi, Sura ya 118 na Sheria ya Mipango Miji ya mwaka 2007 zimeweka wazi juu ya ulipaji wa fidia stahiki na kwa wakati kabla ya ardhi kutwaliwa kwa matumizi ya umma. Kinyume chake, nilibaini matukio ya ucheleweshaji au malipo ya fidia yasiyo stahiki katika baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa ambayo kimsingi yanataka kufanana kama ilivyoangaziwa hapa chini.

**(i) Madai ya muda mrefu ya fidia ya ardhi iliyotwaliwa katika eneo la Luchelele kiasi cha Sh. milioni 329.66**

Nilibaini kuwa, Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilifanya uthamini wa ardhi katika eneo la Luchelele kwa ajili ya fidia ya viwanja vya makazi/biashara vilivyopimwa mwezi Mei 2022. Ukaguzi wa hati za malipo, Ripoti ya Tathmini na viambatisho vingine muhimu ulibaini kuwa Halmashauri bado haijalipa fidia kwa walengwa yenye jumla ya Sh. milioni 329.66 kwa zaidi ya miaka 2.

**(ii) Kuchelewa kulipa fidia ya ardhi iliyotwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa shule kwa zaidi ya miaka 13 Sh. milioni 33.51**

Aprili, 2011, Halmashauri ya Manispaa ya Singida ilithamini na kutwaa ardhi yenye thamani ya Sh. milioni 52.86, iliyokuwa chini ya umiliki wa wananchi 10 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi Unyankhae. Hata hivyo, nilibaini kuwa zaidi ya miaka 13 imepita bila malipo ya fidia ya Sh. milioni 33.51 kwa wanufaika watano.

Kucheleweshwa kwa malipo ya fidia ya ardhi iliyotwaliwa kwa lazima kumekuwa chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi huku wamiliki wakikata tamaa na kuamua kuvamia tena ardhi hiyo na kusababisha hatua za kisheria.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI ihakikishe fidia ambazo hazijalipwa kwa muda mrefu zinalipwa bila kuchelewa.**

### 16.1.7 Ujenzi wa majengo ya ofisi za Halmashauri katika eneo lililozuiliwa la Bonde la Mto Ruvu - Sh. bilioni 1.13

Kifungu cha 56 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira , Sura ya 191 kinazitaka, Wizara za kisekta ambazo mamlaka ya eneo lolote la

ardhioevu iko chini yake, kuwajibika kwa usimamizi wa ardhioevu zilizo chini ya mamlaka yao.

Kinyume chake, nilibaini kuwa H/W Kibaha ilijenga majengo ya ofisi ya Halmashauri yenye thamani ya Sh. bilioni 1.13 katika bonde la Mto Ruvu ambalo limebainishwa na NEMC kama eneo lindwa la ardhioevu kama ilivyobainishwa katika taarifa ya Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA) iliyowasilishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kupitia barua yenye Na: BD. 352/362/01 ya tarehe 29 Novemba 2021.

Kufanya shughuli za ujenzi katika eneo lindwa la ardhioevu kunahatarisha usalama wa miundombinu. Pia, ardhioevu lina mchango muhimu katika uhifadhi wa Mazingira. Uvamizi wa maeneo hayo una athari za kudumu za kimazingira na hasara dhahiri ya fedha za umma.

**Ninapendekeza menejimenti ya H/W Kibaha kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, kusitisha haraka shughuli zote za ujenzi katika eneo lindwa la ardhioevu ili kuzuia uharibifu zaidi wa kimazingira na athari zinazohusiana. Pia, OR-TAMISEMI inasisitizwa kuimarisha kazi ya usimamizi kwa kuhakikisha siku zijazo, maeneo ya miradi yanayopendekezwa yanafanyiwa tathmini ya athari za kimazingira kabla ya utekelezaji wa miradi hiyo kuanza.**

### 16.1.8 Kuchelewa kwa miradi ya ujenzi kwa sababu ya kukosekana kwa maeneo ya ujenzi - Sh. milioni 650

Mnamo tarehe 24 Februari 2022, Halmashauri ya Jiji la Arusha ilipokea fedha kutoka Hazina kwa ajili ya kuchochea shughuli za uchumi pamoja na mapambano dhidi ya UVIKO-19-21 mahususi kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa  Soko la Machinga Complex wenye thamani ya Sh. milioni 500. Hata hivyo, kutokana na migogoro ya ardhi na kutoelewana, utekelezaji wa mradi huo ulichelewa kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Vilevile, nilibaini ucheleweshaji wa ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi wa H/W Kibaha kwa zaidi ya mwaka mmoja uliotengewa kiasi cha Sh. milioni 150 ambazo zilipokelewa tarehe 28 Februari 2022 kutokana na kukosekana kwa kiwanja kwa ajili ya ujenzi huo.

Miradi iliyocheleweshwa mara nyingi husababisha kuongezeka kwa gharama za ujenzi. Athari za kifedha za miradi iliyocheleweshwa inaweza kukausha rasilimali za shirika na kuathiri kwa ujumla ustawi wa kifedha.

**Ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kuwa zoezi la upangaji na upimaji wa ardhi linakuwa endelevu ili kuepusha kucheleweshwa ujenzi wa miradi iliyopokea fedha kwa kigezo cha maeneo ya ujenzi ambayo hayajaamuliwa au ukosefu wa viwanja vilivyopimwa.**

### 16.1.9 Miradi mipya iliyojengwa kabla ya kupata hatimiliki - Sh. bilioni 46.71

Nilipitia nyaraka zinazohusu utekelezaji wa miradi mipya yenye thamani ya Sh. bilioni 46.71 katika Mamlaka 25 za Serikali za Mitaa na kubaini kuwa mamlaka za serikali husika hazikuwa na hatimiliki ambapo miradi hiyo ilikojengwa kinyume na kifungu cha 29(1) (b) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113.

Miradi hiyo ni majengo ya utawala yenye thamani ya Sh. bilioni 5.90, ujenzi wa vituo vya afya vyenye thamani ya Sh. bilioni 5.79, na ujenzi wa vyumba vya madarasa vyenye thamani ya Sh. bilioni 35.04. Orodha ya miradi na maelezo yametolewa katika **Jedwali Na.117.**

**Jedwali Na. 117: Miradi mipya iliyojengwa kabla ya kupata hatimiliki**

| Na | Halmashauri | Miundombinu ya Utawala (Sh.) | Vituo vya Afya( Sh.) | Madarasa Sh. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dodoma | | | 1,275,200,000 |
| 2. | H/W Hai | | | 932,780,028 |
| 3. | H/W Igunga | | | 922,600,000 |
| 4. | H/W Kakonko | | | 3,693,091,296 |
| 5. | H/W Kasulu | | 360,000,000 | 3,133,490,552 |
| 6. | H/M Kigoma Ujiji | | 500,000,000 | 1,942,200,000 |
| 7. | H/W Kisarawe | 3,000,000,000 | 105,500,000 | 1,078,000,000 |
| 8. | H/W Korogwe | 2,800,000,000 | 250,000,000 | 568,000,000 |
| 9. | H/W Madaba | | | 331,600,000 |
| 10. | H/W Maswa | | | 1,487,300,000 |
| 11. | H/W Mbarali | | | 347,500,000 |
| 12. | H/W Mbinga | | 1,709,759,588 | 313,616,795 |
| 13. | H/W Mbogwe | | | 1,740,000,000 |
| 14. | H/M Moshi | | | 932,780,028 |
| 15. | H/W Msalala | | 500,000,000 | 1,518,300,000 |
| 16. | H/W Nyang’hwale | 80,000,000 | 100,000,000 | 1,462,138,525 |
| 17. | H/W Nzega | | | 1,084,500,000 |
| 18. | H/Mji Nzega | | 50,000,000 | 265,000,000 |
| 19. | H/W Same | | 2,000,000,000 | 1,379,280,028 |
| 20. | H/W Shinyanga | | | 656,000,000 |
| 21. | H/W Siha | | | 2,324,100,000 |
| 22. | H/W Sikonge | | | 884,797,548 |
| 23. | H/M Tabora | | 142,000,000 | - |
| 24. | H/Mji Tunduma | | | 6,438,392,000 |
| 25. | H/W Tunduru | | 72,864,393 | 334,002,840 |
| **Jumla** | | **5,880,000,000** | **5,790,123,981** | **35,044,669,640** |

Mamlaka za serikali za mitaa zina jukumu kubwa katika kusimamia sheria za ardhi na pia, zinatarajiwa kuwa mfano wa kuigwa katika kuzingatia sheria kwa kuhakikisha wanapata hatimiliki kabla ya ujenzi.

**Ninatoa rai kwa mamlaka za serikali za mitaa kupata hatimiliki kabla ya ujenzi wa miradi mipya ili kuepuka migogoro ya ardhi na hasara inayoweza kujitokeza. Pia, mamlaka za serikali za mitaa zinashauriwa kuharakisha mchakato wa kupata hatimiliki za viwanja vyake bila kuchelewa.**

# SURA YA KUMI NA SABA



## TATHIMINI YA KUKABILIANA NA MAAFA

**17.0 Utangulizi**

Kukabiliana na maafa ni jambo linalosimama kama kipengele muhimu cha usalama kwa umma na ulinzi wa miundombinu.

Sura hii inachunguza na kuchambua matukio ya maafa ambayo yamekuwa yakiathiri mamlaka za serikali za mitaa, kubainisha chanzo na taratibu zinazotumiwa na mamlaka za serikali za mitaa katika kuzuia, kupunguza na kukabiliana na maafa, pamoja na changamoto zinazojitokeza wakati wa kukabiliana na maafa.

Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na matukio yanayohusiana na moto katika maeneo ya vijijini ambapo rasilimali za misitu ni za muhimu kwa maisha, lakini pia katika maeneo ya mijini hasa katika masoko na majengo ya biashara. Mafuriko pia yameathiri maeneo mbalimbali na kuacha athari kubwa kwa jamii:

**17.1 Kutofanyika kwa tathmini ya udhibiti wa moto katika halmashauri na kusababisha hasara ya Sh. bilioni 27.14**

Halmashauri zinakabiliwa na changamoto kubwa ya milipuko ya moto ambayo mara nyingi husababishwa na shughuli za kibinadamu ikiwamo uchomaji wa mkaa, shughuli za kilimo iwe ni kwa kukusudia au kutokukusudia na kusababisha hasara kubwa na uharibifu wa mazingira.

Nimebaini Halmashauri 10 zilipata hasara ya Sh. bilioni 27.14 kutokana na matukio ya moto katika mwaka wa fedha 2022/23. Kwa sasa katika mwaka wa fedha 2023/24, Halmashauri ya Wilaya ya Makete imeripoti hasara ya Sh. bilioni 4.44.

Tathmini yangu ilibaini hasara kubwa kwa Halmashauri husika kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.118.**

**Jedwali Na. 118: Hasara iliyosababishwa na moto**

| Na. | Jina la Halmashauri | Eneo Lililoathiriwa na moto/eka | Umiliki | Mazao yaliyopo | Hasara iliyopatikana Sh. |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Njombe H/Mji | 1412.5 | Binafsi | Miti ya Kupanda | 21,997,725,000 |
| 2 | Makete H/W | 652.5 | Binafsi na Serikali | Miti ya Kupanda | 2,774,565,401 |
| 3 | Njombe H/W | 2513.7 | Binafsi | Tree Plantation | 1,471,845,500 |
| 4 | Ludewa H/W | 4.5 | Private | Miti ya Kupanda | 413,316,000 |
| | | 10318.3 | Serikali | Dense Forest | |
| | | 22.3 | Halmashauri | Miti ya Kupanda | |
| 5 | Wanging'ombe H/W | 43.6 | Binafsi | Miti ya Kupanda | 169,386,000 |
| 6 | Buhigwe H/W | 200 | Halmashauri na Binafsi | Msitu na Miti ya Kupanda | 135,000,000 |
| 7 | Biharamulo H/W | 14,500 | Binafsi | Msitu na Miti ya Kupanda | 35,000,000 |
| | | 13,000 | Serikali | Msitu | 26,000,000 |
| 8 | Rombo H/W | 200 | Serikali | Miti | 57,000,000 |
| 9 | MbozI H/W | 54 | H/w, Binafsi na Serikali | Miti | 30,000,000 |
| 10 | Makambako H/Mji | 18.3 | Binafsi | Miti ya Kupanda | 27,450,000 |
| **Jumla** | | **42,939.70** | | | **27,137,287,901** |

**Chanzo:** Taarifa ya Halmashauri ya Maliasili na Hifadhi ya Mazingira

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa zishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Uratibu wa shughuli za Maafa, na Kikosi cha Zimamoto katika kuishirikisha jamii ili kukuza dhana ya umiliki kupitia mipango ya uwajibikaji kwa jamii.**

**Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuweka kipaumbele katika ushirikishwaji wa jamii katika kazi na majukumu ya kiufundi, kuimarisha mfumo wa tahadhari za mapema, kutenga fedha za dharura na sheria ndogo kwa kila mtu kushiriki katika kuzuia maafa.**

## 17.2 Kutokuwapo kwa usimamizi thabiti wa majanga ya moto katika masoko

Serikali ilitoa mwongozo mwaka 2022 kwa ajili ya kutekeleza mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa vihatarishi katika sekta za umma. unaoamuru udhibiti thabiti wa mifumo ya ndani na usimamizi wa hatari.

Mamlaka za serikali za mitaa zinatakiwa kujumuisha usimamizi wa moto katika miundo ya utawala na mifumo ya utoaji taarifa. Usimamizi wa hatari za moto katika mazingira haya ni muhimu sana ili kuhakikisha usalama wa watu na mali

Kanuni 248 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (Tahadhari za Moto katika Majengo) ya mwaka 2015 inaelekeza mamlaka za serikali za mitaa kushauriana na Jeshi la Zimamoto kabla ya kuidhinisha michoro ya majengo, kuhakikisha uzingatiaji wa kanuni za usalama dhidi ya majanga ya moto wakati wa ujenzi na mabadiliko ya mchoro wa jengo.

Hatua hizi kwa pamoja zinalenga kukuza usimamizi bora wa moto, kulinda maliasili, na kuboresha ustawi wa jamii nchini Tanzania

Mikakati madhubuti ya usimamizi wa moto huhitaji tathmini za kina za hatari, hatua thabiti za kuzuia, mifumo ya kutosha ya kugundua, na taratibu za kukabiliana na dharura.

Nimebaini katika miaka ya hivi karibuni kuungua kwa majengo ya masoko ya Kariakoo, Karume, Mbagala, Vetenari-Tazara, Maduka ya Mwenge na River Side jijini Dar Es Salaam. Pia, yameungua masoko ya Mwanjelwa, SIDO, Makunguru na Uhindini mkoani Mbeya. Mengine yaliyoungua ni: Katoro-Geita, Mbuyuni- Kilimanjaro na Tunduma mkoani Songwe. Matukio hayo yameharibu mamilioni ya mali, na kuathiri wafanyabiashara kiuchumi na kusababisha usumbufu kwa jamii inayowazunguka.

Matukio ya moto yanaongezeka kwa sababu ya uunganishaji duni wa mifumo ya umeme, kutozingatiwa kwa hatua za usalama kwa mamalishe na wachomeaji wa vyuma na kusababisha moto katika masoko, hivyo kuwaathiri kwa kiasi kikubwa wafanyabiashara wasio na bima.

Ninasisitiza umuhimu wa Halmashauri kuweka kipaumbele katika usimamizi wa moto katika maeneo ya masoko na kuwekeza katika hatua madhubuti za kupunguza hatari zinazoweza kutokea na kulinda ustawi wa jamii.

**Kielelezo Na. 3: Masoko yaliyoteketea kwa moto katika Halmashauri kwa miaka iliyopita**

| | | |
|---|---|---|
| Kariakoo DSM  | Karume DSM  | Vetenary-Tazara-  |
| Mwanjelwa Mbeya  | Tunduma Songwe  | SIDO-Mbeya  |

| Mbuyuni Moshi | Katoro Geita | Maduka ya Mwenge |
|---|---|---|
|  |  |  |

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu-Idara ya Uratibu wa shughuli za Maafa na Kikosi cha Zimamoto kuandaa mikakati thabiti ya kukabiliana na moto katika masoko na majengo ya biashara. Hii ni pamoja na kutoa mafunzo na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kukabiliana na moto kama bomba la maji la kuzima moto, vitambua moshi, vitambua joto na na vifaa vya mawasiliano kama vile redio za mawasiliano ("walkie-talkies").**

### 17.3 Usanifu wa majengo yenye thamani ya Sh. bilioni 14 usioidhinishwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Kanuni ya 248 ya Kanuni za Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji (Tahadhari ya Moto katika Majengo) za mwaka 2015 inaelekeza pale inapopendekezwa kujenga jengo au kufanya upanuzi wowote au mabadiliko ya muundo wa jengo na kuhusiana na mapendekezo hayo, na michoro ipo kwa mujibu wa kanuni za ujenzi zilizowekwa na mamlaka ya mtaa, mamlaka ya mtaa iwasiliane na mamlaka ya zima moto kabla ya kuidhinisha michoro hiyo.

Nimebaini Halmashauri tano zimejenga majengo bila kupata kibali kutoka kwa Jeshi la Zimamoto na uokoaji. Aidha, mapendekezo yaliyotolewa na Jeshi la Zimamoto katika jengo jipya la utawala la halmashauri ya wilaya ya Rombo bado hayajatekelezwa.

Vilevile, kutojumuishwa kwa vifaa vya kuzima moto kwenye majengo mapya mawili ya utawala na shule za Kanenwa na Ng'wang'halanga katika Halmashauri ya jiji la Mwanza na Halmashauri ya Manispaa Shinyanga mtawalia.

Hii inaonesha kutozingatia kanuni za usalama na mapendekezo ya wataalamu, hivyo kusababisha hatari zinazoweza kutokea kwa wakaaji na usalama wa miundombinu. Mchanganuo wake unaoneshwa katika **Jedwali Na.119** na **Kiambatisho Na.50**.

**Jedwali Na. 119: Kutoidhinishwa kwa usanifu wa majengo na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Hai | 2,411,700,000 |
| 2 | H/W Moshi | 3,370,582,653 |
| 3 | H/M Moshi | 2,432,780,028 |
| 4 | H/W Same | 3,463,560,056 |
| 5 | H/W Siha | 2,324,100,000 |
| **Jumla** | | **14,002,722,737** |

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa kufuata na kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na wataamu wengine. Pia, OR-TAMISEMI iwawajibishe wahusika kwa kushindwa kufuata na kutekeleza mara moja mapendekezo yaliyotolewa.**

## 17.4 Halmashauri kutokuwa na utayari katika usimamizi wa maafa

Kifungu cha 17 cha Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya mwaka 2015, kinaitaka Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Mkoa na Wilaya kuwa na uwezo wa kuelekeza taasisi zote za mkoa na wilaya kujiandaa, kuzuia, au kupunguza maafa na kuamuru mtu yeyote kuhama kutoka eneo hatarishi.

Kujitayarisha kwa maafa kunajumuisha hatua zinazochukuliwa na Serikali, mashirika, jumuiya au watu binafsi ili kukabiliana vyema na athari za mara moja za maafa, ziwe za kibinadamu au za asili.

Nimebaini maafa yaliyosababishwa na mvua katika baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa kutokana na kutojiandaa; na kutozingatia utekelezaji wa mipango miji wakati wa ujenzi wa makazi ya watu na miundombinu mingine.

Kuhusu ujenzi wa miundombinu ya ofisi unaoendelea katika mkoa wa Dodoma: katika maeneo ya Tambukareli na Mitumba, kuna wasiwasi mkubwa kuhusu udhibiti wa maji ya mvua. Kwa sasa, maji ya mvua katika maeneo ya Tambukareli yanaelekezwa katikati ya Jiji, hivyo kusababisha uwezekano wa changamoto na hatari zinazoweza kutokana na mafuriko.

**Kielelezo Na. 4: Baadhi ya maeneo yaliyoathirika na mafuriko**

| Dar Es Salaam | Manyara | Arusha |
|---|---|---|
|  |  |  |
| Dodoma | Mwanza | Morogoro |



Ninapendekeza Idara ya Mipango Miji kwa kushirikiana na TARURA, TANROADS, Wizara ya Ujenzi na wadau wengine ziweke hatua madhubuti dhidi ya kupunguza hatari za mafuriko na pia kuhakikisha kuwa mbinu za kupunguza maafa zinajumuishwa katika mipango ya taasisi za serikali, sera za maendeleo, mikakati na programu katika ngazi ya kitaifa, kikanda na mitaa.

Kamati za kukabiliana na maafa za Mikoa na Wilaya zitoe maagizo ya kusitisha uendelezwaji usioidhinishwa ili kuzuia makazi yasiyo rasmi na upatikanaji wa huduma muhimu katika maeneo hatarishi. Pia, napendekeza ujenzi wa miundombinu thabiti, uvunaji wa maji ya mvua, mifereji ya maji na mabwawa ya kuhifadhi maji.

# SURA YA KUMI NA NANE




## KAGUZI MAALUM

### 18.0 Utangulizi

Kifungu Na. 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, [Sura ya 418] pamoja na Kanuni ya 78 na 79 (1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009 zinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalumu pale anapoona inafaa au kwa ombi maalumu la maandishi kutoka kwa Ofisa Masuuli, au mtu yeyote, taasisi, mamlaka ya umma, wizara, idara inayojitegemea, wakala, mamlaka ya serikali za mitaa, au chombo kingine chochote.

Katika kipindi ninachotolea taarifa nilifanya kaguzi maalumu tano katika Mamlaka tano za Serikali za Mitaa ambazo zilizoombwa na wadau pamoja na taasisi mbalimbali.

Kaguzi hizi zilifanyika katika halmashauri wilaya mbili, halmashauri za manispaa mbili na halmashauri ya jiji moja na matokeo ya kina ya kaguzi hizi yamewasilishwa kwa mamlaka husika hayajaoneshwa katika ripoti hii. Muhtasari wa kaguzi hizo umeainishwa hapa chini:

### 18.1 Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga

Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kupiti programu ya Kupanga Kupima na Kumilikisha Ardhi ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilipokea mkopo wa Sh. milioni 900

Ukaguzi maalum uliombwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupitia barua Kumb. Na. PCCB/SHY/GCR/110/2022/OP 8, na ulianza rasmi tarehe 16 Septemba 2023 kwa kikao cha ufunguzi na kumalizika tarehe 10 Oktoba 2023.

Ukaguzi huo ulijikita katika kuhakiki taratibu za manunuzi zinazotumika katika kutafuta kampuni kwa ajili ya kutekeleza mpango huu katika halmashauri.

Pia, ukaguzi ulilenga kubaini kama utekelezaji wa mradi uliendana na andiko la mradi. Zaidi, nilichunguza matumizi ya fedha za programu zilizotolewa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kubaini kama zilitumika kwa mujibu wa Mpango wa KKK ndani ya halmashauri.

**Matokeo ya ukaguzi yaliwasilishwa TAKUKURU na mamlaka nyingine husika kwa hatua zaidi.**

## 18.2 Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji

Mnamo tarehe 27 Oktoba 2023 Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia barua Kumb. Na. CAC.95/389/01/47 iliomba Ukaguzi Maalumu juu ya tuhuma za ubadhirifu wa fecha za bakaa za mwaka wa fedha 2021/22 zilizoombwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji kupitia sekretarieti ya mkoa wa Kigoma.

Ukaguzi huo maalum ulilenga kubaini usahihi wa matumizi ya fedha za bakaa zilizoombwa na jinsi fedha hizo zilivyotumika katika miradi ya maendeleo ya halmashauri ya manispaa ya Kigoma Ujiji.

Mnamo tarehe 09 Novemba 2023 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alianza Ukaguzi Maalumu kuhusiana na fedha zilizohamishwa kutoka Akaunti ya Amana ya OR-TAMISEMI kwenda halmashauri ya manispaa ya Kigoma Ujiji. Ukaguzi ulijikita katika kuhakiki iwapo kiasi cha Sh. milioni 497.75 kilichoombwa kuvuka mwaka wa fedha 2021/22 na kuhamishiwa Halmashauri ni sahihi na kilistahili kwa mujibu wa taratibu na sheria.

Kadhalika nilihakiki uhalali na usahihi wa matumizi ya jumla ya Sh. milioni 463.59 fedha za miradi ya maendeleo zilizohamishiwa Manispaa ya Kigoma Ujiji kutoka OR - TAMISEMI.

**Matokeo ya Ukaguzi yaliwasilishwa kwa Mh. Waziri Mkuu na mamlaka nyingine husika kwa hatua zaidi.**

## 18.3 Halmashauri ya Jiji la Tanga - Chongoleani

Ukaguzi huu maalum ulifanyika kutokana na malalamiko ya wananchi ambao ndio wamiliki wa ardhi juu ya utwaaji wa ardhi, uthaminishaji na mchakato wa fidia uliofanywa na TPDC.

Malalamiko hayo kupitia barua yenye Kumb. Na. FA.94/319/01 ya tarehe 9 Novemba 2022 yalihusu ukiukwaji wa sheria na taratibu za utwaaji,

uthamini na ulipaji fidia ya ardhi katika maeneo yao yaliyopo Kata ya Chongoleani Mkoani Tanga. Walibainisha kuwa ukiukwaji huo ulihusisha ukokotoaji wa fidia kwa kutumia viwango vya chini visivyoendana na bei ya soko la ardhi. Ukaguzi ulihusisha kipindi cha kuanzia Januari 2017 hadi Desemba 2020.

Ili kupata ukweli wa tuhuma hizo, nilipitia mchakato wa utwaaji ardhi katika eneo la Chongoleani Tanga ambapo TPDC walipanga kujenga Miundombinu ya Hifadhi ya Taifa ya Mafuta. Mapitio hayo yalilenga kubainisha iwapo mchakato huo ulizingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utwaaji Ardhi.

Kadhalika nilitathmini viwango vya fidia vinavyotolewa kwa Watu walioathirika na miundombinu ya Hifadhi ya Mafuta ya Akiba ya Taifa ili kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za uthamini wa fidia

Aidha, nilitathmini malipo ya fidia yaliyotolewa kwa wahanga wa Mradi ili kubaini kama walistahili kwa mujibu wa Sheria.

**Matokeo ya Ukaguzi yaliwasilishwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi na mamlaka husika kwa hatua zaidi.**

### 18.4 Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi

Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi kupitia ofisi ya Mbunge, Jimbo la Mbozi waliomba kaguzi maalum kupitia barua ya tarehe 6 Septemba 2021.

Ukaguzi ulijikita katika mapato ya ada ya leseni za biashara kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Juni 2022, na ulilenga kubaini ubadhirifu wa makusanyo ya mapato yatokanayo na vyanzo vya mapato, ujenzi wa shule ya Kisimani na malipo ya posho ya safari kwa wajumbe wa menejimenti ya halmashauri

Nilipitia matumizi ya Sh. milioni 700 zilizotumika katika ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Kismani na kutathmini taratibu za manunuzi katika kumuomba mkandarasi wa ujenzi wa majengo ya shule na kubaini iwapo mkandarasi na mwajiri walitimiza wajibu wao kwa mujibu wa Mkataba na kubaini hasara iliyojitokeza.

Pia, nilihakiki na kubaini upotevu katika makusanyo ya mapato ya Sh. milioni 603.53 kutoka vyanzo vya ndani kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Aidha nilihakiki mashine 142 za PoS za halmashauri ili kubaini kama zilitumika kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa, na pia nilihakiki kama kuna upotevu wa tozo ya mapato ya kahawa katika kiasi cha Sh. milionin 613.03 kilichokusanywa kuanzia Julai 2016 hadi Juni 2021.

Mwisho nilihakiki uhalali wa posho za safari ya wajumbe wa Menejimenti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/21.

**Matokeo ya Ukaguzi yaliwasilishwa kwa Mbunge anayewakilisha Jimbo la Mbozi na mamlaka husika kwa hatua zaidi.**

### 18.5 Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kupitia barua Na. PCCB/SGD/ENQ/23/2022, aliniomba kukagua tuhuma za ubadhirifu wa mapato yatokanayo na mabasi makubwa ya abiria kuingia Stendi Kuu ya Mabasi ya Wilaya ya Manyoni kuanzia tarehe 12 Machi 2020 hadi 31 Mei 2022. Ukaguzi wa kiuchunguzi ulianza rasmi tarehe 20 Septemba 2023 na kukamilika 13 Oktoba 2023.

Ukaguzi huo ulijikita katika kuhakiki taarifa za makusanyo ya mapato ya mabasi makubwa ya abiria yaliyopita katika Stendi Kuu ya Mabasi ya Wilaya ya Manyoni na uwasilishaji wa mapato yaliyokusanywa. Uhakiki uliangazia idadi ya mabasi makubwa yaliyopita katika Stendi Kuu ya Mabasi ya Wilaya ya Manyoni kwa kuzingatia takwimu za mizani ya Tinde, Mwendakutima, na Itigi, na za mabasi yanayoanzia au kuishia mkoani Singida. Nilizingatia kiasi cha fedha kilichopaswa kukusanywa kutokana na idadi ya mabasi hayo.

Pia, nilihakiki kiwango cha fedha kilichokusanywa kutokana na ushuru wa mabasi makubwa yaliyopita katika stendi kuu ya mabasi yaliyooneshwa na yasiyooneshwa katika Mfumo wa LGRCIS.

Aidha, nililenga kubaini kama kuna hasara yoyote kwa Halmashauri kwa kukusanywa ushuru wa mabasi makubwa ya abiria bila kuoneshwa katika Mfumo wa LGRCIS.

**Matokeo ya ukaguzi yaliwasilishwa TAKUKURU na mamlaka zingine husika kwa hatua zaidi.**

# SURA YA KUMI NA TISA



## MAPITIO YA UFANISI WA SEKRETARIETI ZA MIKOA

**19.0 Utangulizi**

Ibara ya 61 (1) na (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaainisha majukumu ya Mkuu wa Mkoa. Aidha, Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Tawala za Mikoa, Sura 97 inaagiza kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Mkoa kama chombo cha serikali katika kila mkoa.

Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) akiwa Afisa Masuuli wa Sekretarieti ya Mkoa, aliyepewa jukumu la kuzisimamia na kuzisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza malengo yao ya maendeleo endelevu kwa kuwezesha na kukuza maendeleo ya Halmashauri kwa kufikia malengo ya Taifa.

Malengo hayo ni pamoja na kukuza utawala bora, kutoa huduma za kiutawala na rasilimali watu, kuimarisha upatikanaji wa miundombinu bora ya kijamii na kiuchumi, na kuimarisha maandalizi ya maafa na usimamizi wa mazingira.

Sura hii inaeleza masuala muhimu yanayohusu taarifa za fedha, ufanisi na utendaji kazi wa bajeti, udhibiti wa matumizi, taratibu za manunuzi na miradi inayotekelezwa kwa njia ya 'force account' katika Sekretarieti 26 za Mikoa ya Tanzania Bara.

**19.1 Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa Sekretarieti za Mikoa kwa Mwaka 2021/22**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 93 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009; kila Afisa Masuuli wa taasisi iliyokaguliwa, anatakiwa kuandaa majibu ya taarifa ya ukaguzi ya taasisi husika ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya kuwasilishwa kwa taarifa ya ukaguzi wa hesabu kwenye Bunge.

Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa miaka ya nyuma kwa Sekretarieti za Mikoa 26, umeoneshwa katika **Jedwali Na. 120** na kufafanuliwa kwa kina katika **Kiambatisho Na. 51**.

**Jedwali Na. 120: Utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi**

| Hali ya utekelezaji | Idadi ya mapendekezo | % |
|---|---|---|
| Yaliyotekelezwa | 332 | 46 |
| Utekelezaji unaendelea | 222 | 31 |
| Yasiyotekelezwa | 75 | 11 |
| Yaliyojirudia | 72 | 10 |
| Yaliyopitwa na wakati kutokana na matukio mbalimbali | 12 | 2 |
| **Jumla** | **713** | **100** |

**Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa kila Sekretarieti ya Mkoa**

Kutokutekeleza mapendekezo yangu kunasababisha kujirudia kwa mapungufu yaliyobainishwa na hivyo kuchangia kukosekana kwa ufanisi katika utendaji na hatimaye kuathiri utoaji wa huduma kwa umma.

**Ninasisitiza maafisa masuuli wa Sekretarieti za Mikoa kuongeza juhudi na kuharakisha hatua muhimu katika kutekeleza mapendekezo yangu ya ukaguzi, ili kuimarisha utendaji na kutoa huduma stahiki kwa umma.**

## 19.2 Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya PAC

Majukumu ya Kamati yameainishwa kwenye Agizo Na.14 la Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la nyongeza la nane (Juni 2020), na hivyo ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni nyenzo muhimu kwa Kamati kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Tathmini yangu ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya PAC kwa Sekretarieti za Mikoa hadi mwaka wa fedha 2022/23 imeoneshwa kwenye **Jedwali 121** na **122**.

**Jedwali Na. 121: Utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya PAC**

| Hali ya utekelezaji | Idadi ya Maagizo | % |
|---|---|---|
| Yaliyotekelezwa | 50 | 72 |
| Utekelezaji unaendelea | 17 | 25 |
| Yasiyotekelezwa | 0 | 0 |
| Yaliyopitwa na wakati kutokana na matukio mbalimbali | 2 | 3 |
| **Jumla** | **69** | **100** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa kila Sekretarieti ya Mkoa*

**Jedwali Na. 122: Taarifa ya utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya PAC**

| Na. | Jinal Sekretarieti ya Mkoa | Yaliyotekelzwa | Utekelezaji unaendelea | Yaliyopitwa na wakati |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kigoma | | 6 | |
| 2 | Arusha | 5 | | 1 |
| 3 | Shinyanga | 6 | | |
| 4 | Singida | 6 | 1 | |
| 5 | Dar Es Salaam | - | 2 | |
| 6 | Manyara | 3 | 2 | |
| 7 | Mbeya | 5 | | |
| 8 | Simiyu | 5 | | |
| 9 | Kagera | 2 | 1 | 1 |
| 10 | Geita | 2 | 2 | |
| 11 | Tanga | 2 | 2 | |
| 12 | Mtwara | 3 | | |
| 13 | Songwe | 3 | 1 | |
| 14 | Ruvuma | 2 | | |
| 15 | Tabora | 1 | | - |
| 16 | Mara | 5 | | |
| | **Jumla** | 50 | 17 | 2 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi kwa kila Sekretarieti ya Mkoa*

Ucheleweshaji wa utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya PAC unaashiria kuwa, kasoro zilizobainika hazijashughulikiwa ipasavyo hivyo kuna uwezekano wa kuendelea kuziweka taasisi husika katika hatari ya kutokea kwa matukio ya ubadhirifu, kukosa ufanisi na, na kushindwa kutoa matokeo yanayotarajiwa.

**Ninazishauri Sekretarieti za Mikoa kutekeleza maagizo ya Kamati yaliyosalia ili kushughulikia visababishi vya mapungufu yaliyobainika na kuzuia kutojirudia kwa mapungufu hayo kwa siku zijazo.**

## 19.3 Usimamizi wa Matumizi

### 19.3.1 Ukiukwaji uliobainika katika usimamizi wa Akaunti ya Amana Sh. milioni 790

Akaunti ya amana huendeshwa hasa ili kuhifadhi fedha kutoka kwa waweka amana tofauti kwa madhumuni yaliyobainishwa awali. Fedha zinazotumiwa kutoka kwenye akaunti za amana zinatarajiwa kuendana na madhumuni ya msingi ya amana hizo.

Kinyume na Kanuni ya 132 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 inayomtaka afisa anayeidhinisha marejesho ya madai ya amana ili kujiridhisha kuwa madhumuni ya kuweka amana yametimia na afisa huyo lazima pia ajiridhishe ikiwezekana kwa kurejea stakabadhi ya awali iliyotolewa, kwamba mtu anayedai amana ndiye mweka amana halisi au vinginevyo ana haki ya kurejeshewa pesa.

i) **Malipo yaliyofanywa kwa shughuli zisizokusudiwa Sh. milioni 441**

Niligundua malipo ya Sh. milioni 441 yalifanyika na Sekretarieti za Mkoa tatu kutoka kwenye akaunti ya amana kufanya shughuli ambazo zilikuwa nje ya malengo ya fedha zilizowekwa bila kurejeshwa kwenye akaunti. Kitendo hiki ni kinyume na Kanunui ya Na. 132 ya Kanuni za Fedha za Umma, ya mwaka 2001.

Kutumia fedha za akaunti ya amana kutekeleza shughuli zisizokusudiwa kuna athiri upatikanaji wa fedha hizo kwa waweka amana na huweza kuharibu sifa ya taasisi. Taarifa ya malipo yaliyofanyika imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 123.**

**Jedwali Na. 123: Malipo kwa shughuli zisizokusudiwa**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Dar es Salaam | 208,102,488 |
| 2 | Geita | 173,066,800 |
| 3 | Lindi | 59,841,000 |
| **Jumla** | | **441,010,288** |

ii) **Malipo ya ziada kutoka kwenye akaunti ya amana Sh. milioni 10**

Tathmini yangu ya usimamizi wa akaunti za amana iligundua kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi ilitoa pesa ambazo zilizidi kiasi kilichowekwa na kufikia Sh. milioni 10.

iii) **Malipo bila stakabadhi sambamba Sh. milioni 339**

Nilibaini kuwa Sh. milioni 339 zililipwa kutoka Akaunti za Amana za Sekretarieti za Mikoa mitano ili kugharamia shughuli mbalimbali bila kunukuu stakabadhi (mamlaka) zilizokiri kupokea amana hizo. Hii ni kinyume na Kanuni Na. 132 ya Kanuni za Fedha za Umma, ya mwaka 2001.

Malipo hayo yanaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa kuwa fedha za amana zinaweza kutumika kwa shughuli zisizokusudiwa. Maelezo yameoneshwa kwenye **Jedwali Na. 124**.

**Jedwali Na. 124: Malipo bila stakabadhi sambamba**

| Na. | Jina la Sekretarieti ya Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Mwanza | 197,869,499 |
| 2 | Kagera | 78,284,554 |
| 3 | Pwani | 28,267,610 |
| 4 | Njombe | 20,719,167 |
| 5 | Ruvuma | 14,762,000 |
| **Jumla** | | 339,902,830 |

**Napendekeza kwa Sekretarieti za Mkoa kuanzisha taratibu za haraka za kurejesha kiasi ziada kilichotolea kwenye akaunti ya amana na kutoa maelezo ya malipo ya shughuli zisizotarajiwa pia kuhakikisha kwamba zinazingatia kanuni ya 132 ya Fedha za Umma.**

### 19.3.2 Malipo yasiyokuwa na stakabadhi za kielektroniki Sh. milioni 964

Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru, Sura ya 438 [R.E. 2019] kinataka mtu, ambaye hutoa bidhaa, kutoa huduma, au kupokea malipo kuhusiana na bidhaa zinazotolewa au huduma zinazotolewa ili kutoa stakabadhi ya fedha au ankara ya fedha kwa kutumia vifaa vya kielektroniki vya kifedha.

Nilibaini Sh. milioni 964 zilizolipwa na Sekretarieti za Mikoa 10, kwa wazabuni, wakandarasi, na watoa huduma wengine bila kudai stakabadhi za kielektroniki. Kushindwa kudai stakabadhi za EFD kunakuza ukwepaji kodi na hatimaye kuinyima Serikali kukusanya mapato kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 125**.

**Jedwali Na. 125: Malipo yasiyokuwa na stakabadhi za kielektroniki**

| Na | Sekretarieti | Kiasi | Na | Sekretarieti | Kiasi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kigoma | 572,584,141 | 6 | Kagera | 19,147,402 |
| 2 | Shinyanga | 152,930,306 | 7 | Simiyu | 15,916,632 |
| 3 | Tabora | 77,072,541 | 8 | Geita | 14,546,772 |
| 4 | Mtwara | 57,433,703 | 9 | Kilimanjaro | 9,795,788 |
| 5 | Mara | 39,549,015 | 10 | Lindi | 5,513,520 |
| | | **Jumla** | | | **964,489,820** |

**Ninapendekeza kwamba menejimenti za Sekretarieti za Mikoa zizingatie matakwa ya Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, [Sura ya 438] kwa kudai stakabadhi za EFD, ili kuepusha ukwepaji kodi. Pia, wanapaswa kutoa taarifa kwa TRA kuhusu wazabuni ambao watashindwa kutoa stakabadhi za EFD kwa hatua zaidi.**

**Aidha, TRA inapaswa kuongeza ufuatiliaji wa kubaini wauzaji wasio waaminifu ambao hawatoi stakabadhi za EFD na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria ya kodi.**

### 19.3.3 Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslimu kiasi cha Sh. milioni 980

Nilibaini kuwa malipo yenye thamani ya Sh milioni 980 yalifanywa na Sekretarieti nne kupitia fedha taslimu, kwa wanufaika mbalimbali wakiwemo wazabuni na wafanyakazi kinyume na Kanuni ya 93 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 zinazotaka malipo yote

yafanywe kwa watu waliotajwa katika vocha pekee au wakala wao aliyeidhinishwa na chochote kinachowezekana lazima kifanywe kwa njia ya uhamisho wa moja kwa moja wa benki au hundi.

Ukiukwaji huu unachangiwa na udhibiti duni wa uidhinishaji wa malipo katika Sekretarieti za Mikoa, pamoja na kukosekana kwa akaunti za benki za baadhi ya mafundi wa ndani. Malipo yaliyofanywa kwa pesa taslimu yamo katika **Jedwali Na. 126.**

**Jedwali Na. 126: Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslimu**

| Na | Jina la Sekretarieti | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Kigoma | 605,001,100 |
| 2 | Singida | 292,390,937 |
| 3 | Tanga | 73,755,615 |
| 4 | Morogoro | 9,349,400 |
| | **Jumla** | **980,497,052** |

Kwa maoni yangu, kufanya malipo ya fedha taslimu kwa wazabuni kunaweza kuvutia matumizi mabaya ya fedha za umma kutokana na wazabuni husika kutolipa kodi stahiki kwa serikali.

**Ninapendekeza Sekretarieti za Mikoa ziongeze usimamizi na zizingatie matakwa ya Kanuni ya 93 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 kwa kuimarisha udhibiti wa ndani dhidi ya malipo.**

### 19.3.4 Mapungufu katika usimamizi wa matumizi ya Sekretariati za Mikoa

Uchambuzi wa malipo ya mwaka wa fedha 2022/23 unaonyesha mapungufu kadhaa ambayo yanaendelea kuongezeka, ikimaanisha kuwa, usimamizi wa Sekretarieti za Mikoa haukuchukua hatua za kurekebisha. Mapungufu hayo ymeorodheshwa hapa chini ni kama ifuatavyo;

Nimebaini Sekretarieti mbili zilikuwa na masurufu ya Sh. milioni 51 ambayo yalikuwa yamelipwa kwa wafanyakazi kwa ajili ya shughuli mbalimbali, lakini hawakurejesha hadi wakati wa ukaguzi kinyume na Kanuni ya 103 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001.

Kutorejeshwa kwa masurufu kunaashiria mapungufu katika ufuatiliaji wa urejeshwaji wa masurufu yaliyotolewa, hivyo inaweza kutoa mianya kwa watumishi wasio waaminifu kufanya matumizi mabaya ya fedha za umma. Tazama **Jedwali Na.127**.

**Jedwali Na. 127: Kutorejeshwa kwa masurufu**

| Na. | Jina la Sekretarieti ya Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Lindi | 31,479,109 |
| 2 | Dar es Salaam | 19,647,646 |
| **Jumla** | | 51,126,755 |

- Nilibaini kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe ilikuwa na kodi ya zuio ya Sh. milion 5 hadi tarehe 30 Juni 2023 iliyoripotiwa chini ya malipo ya taarifa zao za fedha. Kiasi hicho kilikatwa kutoka kwa wauzaji lakini hakijatumwa Mamlaka ya Mapato kinyume na Kifungu cha 83 (A) na Aya ya 4(c) (v) ya Jedwali la Kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332.

- Sekretarieti za Mikoa mitatu zilichelewesha kuwasilisha makato/michango ya kisheria na kuzalisha deni la Sh. milioni 21. Kutowasilisha makato ya kisheria sio tu kunasababisha adhabu za kifedha bali pia kunawanyima watumishi haki za mafao ya hifadhi ya jamii, kama vile mafao ya kustaafu. Tazama **Jedwali Na.128.**

**Jedwali Na. 128: Adhabu ya malimbikizo ya makato ya watumishi**

| Na. | Jina la Sekretarieti ya Mkoa | Kiasi cha Michango (Sh.) | Adhabu (Sh.) | Jumla (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | 2,130,738 | 510,938 | 2,641,676 |
| 2 | Kilimanjaro | 13,857,153 | 809,805 | 14,666,958 |
| 3 | Region | 946,282 | 3,695,454 | 4,641,736 |
| **Jumla** | | 16,934,173 | 5,016,197 | 21,950,370 |

**Ninapendekeza kwa Menejimenti za Sekretarieti za Mikoa husika, zihakikishe zinazingatia sheria na kanuni katika usimamizi wa fedha za umma ili kuepusha mapungufu.**

## 19.4 Usimamizi wa Ununuzi

### 19.4.1 Ununuzi uliofanywa bila idhini ya Bodi za Zabuni na kutoka kwa wazabuni ambao hawajaidhinishwa na GPSA wenye thamani ya Sh. milioni 661

Ukaguzi wangu wa usimamizi wa manunuzi na mikataba ulibaini kuwa Sekretarieti nne zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. milioni 365 kutoka kwa wazabuni ambao hawakuorodheshwa na GPSA huku Sekretarieti ya Mkoa wa Mara ikinunua bidhaa mbalimbali zenye thamani ya Sh. milion 295 bila kupata kibali kutoka kwa Bodi ya Zabuni.

Kinyume na Kanuni ya 19(1) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inazitaka taasisi zinazofanya manunuzi kuandaa tangazo la zabuni za kitaifa na kimataifa na kuziwasilisha kwa Mamlaka ili zichapishwe kwenye Jarida na Tovuti ya Zabuni wakati Kanuni ya 20(1) Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kuwasilisha taarifa za tuzo ya kandarasi kuhusiana na ununuzi wowote uliofanywa bila kuzingatia njia ya manunuzi iliyotumika, kwa PPRA ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya tuzo ya kuchapishwa katika Jarida na Tovuti ya Zabuni. Kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali Na.129.**

**Jedwali Na. 129: Manunuzi bila idhini ya bodi**

| Na | Jina la Sekretarieti | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| | Manunuzi yaliyofantywa na wazabuni ambao haujaidhinishwa na GPSA | |
| 1 | Mara | 198,905,462 |
| 2 | Tabora | 82,975,850 |
| 3 | Songwe | 65,954,500 |
| 4 | Katavi | 17,807,184 |
| | **Jumla ndogo** | **365,642,996** |
| Manunuzi yaliyofanywa bila idhini ya Bodi ya Zabuni | | |
| | Mara | 295,702,340 |
| | **Jumla kuu** | **661,345,336** |

Mapungufu yaliyoonekana yanasababishwa na mifumo ya udhibiti wa ndani isiyojitosheleza pamoja na kutofuata kanuni za manunuzi.

**Ninapendekeza Sekretarieti zichukue hatua zinazofaa ikiwa ni pamoja na kuongeza udhibiti na usimamizi wakati kwa taratibu ya manunuzi.**

### 19.4.2 Manunuzi yaliyofanywa nje ya mfumo wa ununuzi wa kielektroniki Sh. milioni 334

Kanuni ya 342 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 inaeleza kuwa, "Mfumo wa ununuzi wa kielektroniki utatekelezwa na taasisi zote zinazofanya manunuzi kwa ukamilifu au sehemu sambamba na taratibu za kawaida za mwongozo".

Zaidi ya hayo, PPRA ilitoa Tangazo kwa Umma kuarifu umma kwa ujumla na wadau kuhusu ununuzi wa umma kuhusu kuanza kwa utendakazi kamili wa mfumo wa ununuzi wa kielektroniki tarehe 20 Agosti 2019.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Sekretarieti tatu zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. milioni 334 kutoka nje ya Mfumo wa manunuzi wa kielektroniki kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.130.**

**Jedwali Na. 130: Manunuzi nje ya mfumo wa ununuzi wa kielektroniki**

| Na | Jina la Sekretarieti | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Ruvuma | 273,229,101 |
| 2 | Iringa | 40,027,344 |
| 3 | Arusha | 21,725,950 |
| | **Jumla** | **334,982,395** |

Kutoshirikishwa kwa wazabuni na mafunzo duni kwa maofisa manunuzi vinanazuiya matumizi bora ya mfumo wa TANePs, na hivyo kusababisha kutokuwepo kwa msaada wa kutosha kwa taasisi. Hii inasababisha matumizi duni ya uwezo wa mfumo wa ununuzi kielektroniki.

Kwa maoni yangu, lengo la kuongeza ufanisi, kupunguza muda wa manunuzi, kupunguza hatari, na kuimarisha uwazi katika ununuzi wa umma kupitia manunuzi ya kielektroniki linaweza lisifikiwe kutokana na changamoto na vikwazo katika utekelezaji.

**Ninapendekeza kwa Sekretarieti husika kushirikiana na mamlaka zinazohusika kuhamasisha na kupanga mafunzo kwa wadau wote wakiwemo wafanyakazi wa PMU na ICT hasa kuhusu mfumo wa ununuzi wa kielektroniki na jinsi ya kutumia mfumo huo kwa ufanisi.**

### 19.4.3 Manunuzi ya Sh. bilion 4.82 yaliyofanywa bila ushindanishi wa bei

Kanuni ya 76 ya Manunuzi ya Umma, ya mwaka 2013 iliyorekebishwa na Kanuni ya 27 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Marekebisho) ya mwaka 2016 (G.N. Na. 333 ya tarehe 30.12.2016) inazitaka taasisi nunuzi zinazojihusisha na ununuzi wa huduma, bidhaa na kazi. uuzaji wa mali za umma kufanywa kwa njia ya ushindani wa zabuni.

Kinyume chake, mapitio yangu ya ununuzi yaliyofanywa katika Sekretarieti nne yalibainisha kuwa manunuzi yenye thamani ya Sh. milioni 231 yalifanywa bila mwaliko wa nukuu za bei wakati Sekretarieti mbili zilichagua njia moja ya manunuzi yenye thamani ya Sh. bilioni 4.59 kinyume na Kanuni ya 164(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na.131.**

**Jedwali Na. 131: Manunuzi yaliyofanywa bila ushindanishi**

| Na | Jina la Sekretarieti | Kiasi |
|---|---|---|
| | Manunuzi yaliyofanywa pasipo kushindanishwa | |
| 1 | Mwanza | 114,124,879 |
| 2 | Dar es salaam | 65,129,220 |
| 3 | Ruvuma | 33,900,356 |
| 4 | Simiyu | 18,323,800 |

| | | |
|---|---|---|
| | **Jumla ndogo** | **231,478,255** |
| | Manunuzi yaliyofanywa kwa njia moja | |
| 1 | Lindi | 3,340,045,317 |
| 2 | Tabora | 1,247,452,576 |
| | **Jumla ndogo** | **4,587,497,893** |
| | **Jumla kuu** | **4,818,976,148** |

Kutofuatwa ipasavyo kwa sheria na taratibu za manunuzi kwa usimamizi wa taasisi za ununuzi kulisababisha taratibu za manunuzi zisizo na ushindani.

**Ninaishauri Sekretarieti kufuata Sheria na kanuni husika ili kupata thamani ya fedha, pamoja na kutoa fursa za haki kwa wazabuni wengine.**

### 19.4.4 Kuanza kwa utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 3.29 kabla ya kufanya tathmini ya athari za mazingira

Kanuni ya 241(3) ya kanuni za ununuzi wa umma, 2013 inasema kwamba, "taasisi nunuzi itatathmini athari za mazingira kwa kazi yoyote katika hatua ya upangaji wa mradi na kwa vyovyote vile, kabla ya taratibu za manunuzi kuanza."

Pia, Kifungu cha 81(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura. 191 inahitaji utafiti wa tathmini ya athari za mazingira ufanyike kabla ya kuanza au kufadhili mradi.

Nilibaini kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani ilitekeleza miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 3.29 bila kufanya tathmini ya athari za kimazingira kabla ya kuanza kwa miradi hiyo, kinyume na kanuni na vifungu vilivyotajwa.

Kuanzisha miradi bila kufanya tathmini ya athari za mazingira kunaweka taasisi kuwajibika kwa adhabu na faini zinazoepukika kutoka kwa mashirika ya udhibiti.

**Naishauri Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhakikisha kuwa Sekretarieti ya Pwani inafanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza mradi wowote wa ujenzi. Hatua hii ni muhimu ili kuhakikisha mafanikio ya mradi na kuimarisha taasisi nunuzi ili kuzuia athari za mazingira.**

### 19.4.5 Mapungufu yaliyobainika wakati wa kufanya tathmini ya mchakato wa manunuzi

Tathmini yangu ya ununuzi na usimamizi katika Sekretarieti, nilibaini mapungufu kadhaa katika manunuzi yanayohusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:

- Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu ilisaini mikataba yenye thamani ya Sh. milioni 14 kabla ya kuhakikiwa na mwanasheria kinyume na kanuni Na.59(1)na (5) na kanuni Na.60 za Kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 kama zilivyorekebishwa na kanuni Na.2 na 3 ya marekebisho ya Kanuni za ununuzi wa Umma za mwaka 2016 (Tanzazo la serikali Na.121 la tarehe 22.4.2016).

- Kinyume na Kanuni za ununuzi wa Umma Na. 242 (1) na 248 za mwaka 2013, nilibaini Sekretarieti nne zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. milioni 80.48 kabla ya bidhaa kupokelewa licha ya malipo kufanyika kama ilivyofafanuliwa kwenye **Jedwali Na.132**.

- Kinyume na Kanuni za 244(1) na 245 za PPR, 2013, nilibaini kuwa Sekretarieti mbili zilinunua bidhaa zenye thamani ya Sh. milioni 91 kutoka kwa wazabuni bila kukaguliwa na Kamati ya Ukaguzi na Kupokea Bidhaa.

- Nilibaini kuwa Sekretarieti mbili zilinunua na kutumia vifaa vya ujenzi ikiwa ni pamoja na nondo na saruji vyenye thamani ya Sh. milioni 95 katika miradi ya ujenzi bila kupimwa, kinyume na Kanuni ya 244(1) ya ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kama ilivyofafanuliwa katika **Jedwali Na.132.**

**Jedwali Na. 132: Mapungufu katika mchakato wa ununuzi**

| Na. | Sekretarieti ya Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| Malipo ya bidhaa ambazo hazikupokelewa | | |
| 1. | Lindi | 29,835,000 |
| 2. | Mwanza | 26,765,830 |
| 3. | Mtwara | 15,140,000 |
| 4 | Manyara | 8,742,000 |
| | Jumla | 80,482,830 |
| Bidhaa zilizopokelewa bila kukaguliwa | | |
| 1. | Mara | 82,873,688 |
| 2. | Geita | 8,901,130 |
| | Jumla | 91,774,818 |
| Malighafi za ujenzi ambazo havikupimwa | | |
| 1. | Mara | 55,537,128 |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Shinyanga | 39,486,000 |
| | Jumla | 95,023,128 |

Kutofuata sheria na kanuni za manunuzi ya umma kuna athari katika miradi inayotekelezwa kwani bidhaa au huduma zenye ubora duni zinaweza kutolewa wakati wa utekelezaji wa miradi.

**Ninapendekeza kwamba Ofisi ya Rais TAMISEMI ihakikishe Sekretarieti zote zinazingatia kanuni na sheria zinazohitajika wakati manunuzi katika utekelezaji wa miradi.**

## 19.5 Tathmini ya miradi ya maendeleo

### 19.5.1 Mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa miradi katika Sekretarieti

Tathmini niliyofanya katika Sekretarieti wakati wa usimamizi wa utekelezaji miradi ya maendeleo nilibaini mapungufu kadhaa;

- Sekretarieti mbili zilitekeleza miradi yenye thamani ya Sh. milioni 232 ambayo imekamilika lakini haijaanza kutumika kama ilivyokusudiwa. **Rejea Jedwali Na.133**.

- Sekretarieti ya Mwanza imechepusha fedha zilizowekwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo yenye thamani ya Sh. milioni 84 kwenda kugharamia shughuli ambazo hazikupangwa, kinyume na Kifungu cha 27 (4) cha Sheria ya Bajeti, Sura. 439. **Rejea Jedwali Na.133**.

- Wakati wa ukaguzi, nilibaini Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga ilichelewa kwa kiasi kikubwa katika uanzishaji wa mradi wa Nyumba ya mapumziko kwa viongozi yenye thamani ya Sh. milioni 550 kati ya miezi minne hadi 20 baada ya kupokea fedha zilizotengwa.

- Nilipitia vyeti vya malipo na kubaini kuwa, Sekretarieti ya Mkoa wa Mara ililipa jumla ya Sh. milioni 97 kwa kazi zilizotekelezwa lakini kazi hizo hazikujumuishwa katika nyaraka za vipimo kinyume na Kanuni ya 243 (2) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2013.

- Nilibaini Sekretarieti mbili, zilifanya miradi ya ujenzi yenye thamani ya Sh. bilioni 3.95 bila kudai dhamana ya utendaji kutoka

kwa wakandarasi kama inavyotakiwa na Kanuni ya 29 ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013. **Rejea Jedwali Na.133**

- Nilipitia faili la mradi na kubaini Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara ilifanya mabadiliko ya bei ya mikataba ya awali bila kupata kibali kutoka kwa bodi za zabuni husika hadi kufikia Sh. milioni 12 kinyume na Kanuni ya 110(7) Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2013.

- Nilibaini kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe ilishindwa kurejesha malipo ya awali yenye thamani ya Sh. milioni 28 yaliyotolewa kwa wakandarasi baada ya mikataba kusitishwa kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 23.1 cha Mashariti ya Jumla ya Mkataba.

- Sekretarieti mbili zilinunua vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 144 zaidi ya mahitaji kinyume na Aya ya 13 (5) ya Mwongozo wa Kufanya Kazi kwa Kutumia 'Force Account'. Maelezo yameoneshwa katika **Rejea Jedwali Na.133.**

**Jedwali Na. 133: Sekretarieti za Mikoa zenye miradi yenye mapungufu**

| Na. | Sekretarieti za Mikoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| Miradi iliyokamilika lakini haitumiki | | |
| 1. | RS Coast | 182,174,100 |
| 2. | RS Shinyanga | 49,860,000 |
| | **Jumla** | **232,034,100** |
| Miradi iliyotekelezwa bila ya mkandarasi kuwasilisha dhamana ya kazi | | |
| 1. | RS Lindi | 2,819,023,438 |
| 2. | RS Tabora | 1,134,996,190 |
| | **Jumla** | **3,954,019,628** |
| Ununuzi wa vifaa vya ujenzi zaidi mahitaji | | |
| 1. | RS Tabora | 114,762,261 |
| 2. | RS Kagera | 29,664,440 |
| | **Jumla** | **144,426,701** |

Tofauti zilizobainika zilitokana na kutofuatwa kwa sheria na kanuni, uzembe wa mipango na udhaifu katika kufuatilia utekelezaji wa miradi

**Ninashauri wasimamizi wa Sekretarieti kuchukua hatua zinazofaa dhidi ya mapungufu iliyobainishwa hapo juu na kuzingatia sheria ili kufikia lengo lililokusudiwa na kupata thamani ya fedha.**

### 19.5.2 Miradi ambayo haijakamilika yenye thamani ya Sh. bilioni 8.09

Kanuni ya 114 (b) za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inaitaka taasisi nunuzi kuwajibika kwa usimamizi madhubuti wa manunuzi ya bidhaa, huduma au kazi zinazofanywa na kufuatilia maendeleo na ukamilishaji wa kazi kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba.

Katika ukaguzi, nilibaini miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 7.52 katika Sekretarieti nane ambayo haijakamilika. Pia, nilibaini miradi yenye thamani ya Sh. milioni 572 inayotekelezwa na Sekretarieti tatu, ambayo haijakamilika licha ya muda wa kukamilika kuisha. Rejea **Jedwali Na.134** na **135**.

**Jedwali Na. 134: Miradi ambayo haijakamilka**

| Na | Jina la Mkoa | Kiasi | Na | Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Rukwa | 2,808,262,352 | 5 | Singida | 503,113,500 |
| 2 | Tabora | 2,308,495,811 | 6 | Mtwara | 300,000,000 |
| 3 | Pwani | 767,792,805 | 7 | Mara | 242,939,988 |
| 4 | Simiyu | 509,982,295 | 8 | Tanga | 85,000,000 |
| | **Jumla** | | | | **7,525,586,751** |

**Jedwali Na. 135: Miradi kutokamilika licha ya muda kuisha**

| Na | Jina la Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Simiyu | 390,775,478 |
| 2 | Shinyanga | 91,500,000 |
| 3 | Kilimanjaro | 90,000,000 |
| | Jumla | 572,275,478 |

Kwa ujumla, kutokamilika kwa miradi hii kunachangiwa na kuchelewa na kutotolewa kwa fedha za kutosha, ucheleweshaji wa michakato ya manunuzi, usimamizi na ufuatiliaji wa kutosha wa miradi.

Kuchelewa kukamilika kwa miradi hii kunaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama, kutokana na kuongezeka kwa gharama za vifaa kutokana na mfumuko wa bei.

**Ninapendekeza Sekretarieti kwa kushirikiana na Ofisi ya Raisi-TAMISEMI na Wizara ya Fedha, kuhakikisha bajeti iliyoidhinishwa inatoka kwa wakati pia usimamizi na ufuatiliaji wa mradi unaimarishwa kwa kutembelea maeneo ya miradi, kutoa ripoti za maendeleo na tathmini ya utendaji ili kubaini vikwazo mapema na kuchukua hatua za mapema.**

**Pia, naishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Fedha kufanya tathmini ya kina ya miradi inayotekelezwa na Sekretarieti za Mikoa na kutoa fedha kadri ya bajeti iliyoidhinishwa ili kuwezesha utekelezaji wake na kuepusha athari za kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo.**

## 19.6 Utekelezaji wa Miongozo ya Bajeti

### 19.6.1 Upungufu wa mgawo wa bajeti kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni na madai ya wafanyakazi Sh. bilioni 2.79

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 22(1) cha Sheria ya Bajeti, [Sura ya 439], Mashirika ya Umma yatatayarisha makadirio ya bajeti na kuwasilisha kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa uchunguzi na kupitishwa kwa mujibu wa Sheria hii na kupokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa.

Pamoja na jitihada zilizofanywa na Sekretarieti za kutenga bajeti kwa ajili ya kulipa madeni kwa mwaka wa fedha 2022/23, ukomo wa bajeti uliotolewa ulikuwa hautosherezi kulipa madeni yote ikilinganishwa nay ale yaliyooneshwa katika taarifa za fedha za mwaka uliopita wa 2021/22.

Kwa hiyo, kiasi cha Sh. bilioni 2.79 hakikulipwa kwa wazabuni na madai ya wafanyakazi kwa Sekretarieti tano kutokana na ukomo wa bajeti ambao hauendani na deni lililoainishwa katika taarifa ya fedha kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na.136.**

**Jedwali Na. 136: Madeni na madai yasiyolipwa**

| Na | Jina la Mkoa | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Iringa | 216,851,762 |
| 2 | Songwe | 709,247,831 |
| 3 | Ruvuma | 957,691,466 |
| 4 | Kagera | 545,241,620 |
| 5 | Dar es Salaam | 366,002,180 |
| **Jumla** | | **2,795,034,859** |

Bajeti pungufu kwa ajili ya ulipaji wa madeni huibua wasiwasi kuhusu athari zinazoweza kutokea kifedha na uaminifu wa taasisi. Inawezekana kuongezeka kwa madeni kutokana na ufinyu katika bajeti inayopatikana, na hivyo kuzuia uwezo wa taasisi kutenga kiasi kikubwa zaidi cha ulipaji wa deni.

**Nashauri Menejimenti za Sekretarieti kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kufanya tathmini ya kina ya madeni ambayo bado haijalipwa kwa kutoa kipaumbele katika bajeti kwa ajili ya ulipaji wa madeni kwa wakati, hasa kwa kuzingatia madeni yaliyohakikiwa.**

### 19.6.2 Uhamishaji wa fedha kiasi cha Sh. milioni 214 bila kibali kutoka kwenye mamlaka husika

Kifungu cha 41(2) cha Sheria ya Bajeti,[SURA YA 439] kinaelekeza kwamba 'bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha 1, afisa masuhuli hatatenga fedha ambapo: (b) fedha zinafaa kuhamishiwa kwa taasisi nyingine ya serikali au mtu mwingine.

Kinyume na masharti yaliyoainishwa katika Sheria, nilibaini Sekretarieti nne zilihamisha vifungu vya bajeti kwa Sh. milioni 214 bila kupata kibali kutoka kwa Waziri wa Fedha kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali Na.137.**

**Jedwali Na. 137: Uhamishaji wa fedha bila kibali**

| Na | Sekretarieti | Kiasi | Na | Sekretarieti | Kiasi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mtwara | 84,740,000 | 3 | Tanga | 42,762,000 |
| 2 | Manyara | 48,080,000 | 4 | Mara | 38,595,879 |
| | **Jumla** | | | | **214,177,879** |

**Ninawashauri wasimamizi wa Sekretarieti kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha kuimarisha udhibiti wa bajeti kwa kuhakikisha kwamba vibali vyote vinatoka kwa mamlaka husika. Mbinu hii itasaidia kupunguza ugawaji ambao haujaidhinishwa wakati wa utekelezaji wa bajeti, na hivyo kuhakikisha kwamba michakato ya uidhinishaji inafuatwa na kulinda uadilifu wa bajeti.**

### 19.6.3 Fedha za maendeleo kukaa kwenye akaunti ya amana kwa muda mrefu kiasi cha Sh. bilioni 3.11

Kanuni Na 21 (1) na (2) ya Kanuni za Bajeti za mwaka 2015 inawaagiza Maafisa Masuuli kuwasilisha maombi ya kuendelea kwa namna ya taarifa ya ahadi ambazo hazijatekelezwa siku kumi na tano kabla ya tarehe 30 Juni ya kila mwaka wa fedha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na nakala kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akionyesha sababu za matumizi duni, dhamira ambayo fedha iliyopitishwa itatumika; na tathmini ya uwezo wa matumizi kwa kuzingatia mgao mpya wa bajeti; na kwamba ahadi zote ambazo hazijatekelezwa mwishoni mwa mwaka wowote wa fedha zitatumika ndani ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha unaofuata.

Nilibaini kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza ilikuwa na fedha katika Akaunti ya Amana jumla ya Sh. bilioni 3.11 ambazo zilikuwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Kufuatia maagizo ya kukabidhi mradi kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania tarehe 11 Agosti 2022.

Nina shaka kuhusu kuwepo fedha hizo kwa muda mrefu kuanzia tarehe 11 Agosti 2022 hadi wakati huu wa ukaguzi -Oktoba 2023 kwenye akaunti ya Amana kwa kuwa zinaweza kutumika kwa shughuli zisizopangwa.

**Ninashauri Sekretarieti kwa kushirikiana na Ofisi ya Raisi-TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango ichukue hatua za haraka kwa kuhamisha Sh. bilioni 3.11 kwenda Hazina. Hii itawezesha utekelezaji wa mradi unaosubiri.**

## 19.7 Tathmini ya Utendaji

### 19.7.1 Ucheleweshaji wa Ugawaji wa Bakaa ya Fedha Taslimu Sh. bilioni 2.6 kutoka Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam Iliyovunjwa

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam alipokea agizo tarehe 25 Februari, 2021 kupitia barua yenye kumbukumbu CCB.56/98/01/90 kutoka kwa Katibu Mkuu, OR-TAMISEMI.

Agizo hilo liliwapa jukumu la kusimamia na kuratibu uhamisho wa mali na madeni kati ya Halmashauri ya Jiji iliyovunjwa na Jiji la Dar es Salaam, pamoja na Manispaa za mkoa wa Dar es Salaam.

Katika tathmini yangu, nimebaini kwamba, pamoja na maelekezo, kumekuwepo na ucheleweshaji wa kugawa bakaa la Sh. bilioni 2.6 tangu mwaka 2021 kwa mamlaka husika kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na.138.**

**Jedwali Na. 138: Ucheleweshwaji ugawaji wa bakaa**

| Na. | Jina la Akaunti | Bakaa (Sh.) |
|---|---|---|
| A. | Akaunti ya Biashara | |
| 1 | Akauntiy ya Wanawake, Vijana na wenye Ulemavu Na. 0001732800002/1 DCB - Tawi la Uhuru | 1,046,841,783 |
| 2 | Mapato ya Ndani Na. 150211141600 CRDB Premier Branch | 469,172,675 |
| 3 | Akaunti ya Amana Na. 150211142000 CRDB Premier Branch | 259,975,933 |

| Na. | Jina la Akaunti | Bakaa (Sh.) |
|---|---|---|
| 4 | Akaunti ya Masurufu Na. 0150211846200 CRDB Premier Branch | 135,048,425 |
| **Jumla Ndogo (A)** | | **1,911,038,816** |
| B. | Akaunti za Benki Kuu | |
| 5 | Akaunti ya Maendeleo No 9921210301 BOT | 259,593,512 |
| 6 | Akaunti ya Mishahara Na 9921210801 BOT | 135,237,100 |
| 7 | Akaunti ya Hazina ya Maendeleo Na. 9921211001 BOT | 112,213,191 |
| 8 | Akaunti ya Mfuko Mkuu Na 9921210101 BOT | 101,718,009 |
| 9 | Akaunti ya Amana Na 9921169787 BOT | 68,225,358 |
| 10 | Malipo Mengine Na 9921210901 BOT | 12,771,800 |
| 11 | Akauntiy ya Wanawake, Vijana na wenye Ulemavu Na. 9921211101 BOT | 6,000,000 |
| **Jumla Ndogo (B)** | | **695,758,971** |
| **Jumla Kuu** | | **2,606,797,887** |

**Ninapendekeza Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam afanye mawasiliano ya haraka na Katibu Mkuu (Ofisi ya Rais TAMISEMI) na Wizara zinazohusika kuhusu mgawanyo wa bakaa ya fedha za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam lililovunjwa na kuunda Halmashauri mpya ya Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri za Manispaa ya Dar es Salaam. Mkoa wa Dar es Salaam na Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam.**

# SURA YA ISHIRINI

## OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**20.0 Utangulizi**

Sura hii inazungumzia matokeo ya ukaguzi yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa Fungu 56 – Ofisi ya Rais - Tawala wa Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na taasisi washirika (affiliate institutions).

Wizara ilianzishwa chini ya Ibara za 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikiwa na jukumu la kusimamia maendeleo ya mikoa na utawala kwa kuratibu sera na mikakati ya maendeleo ya mijini na vijijini na shughuli za Sekretarieti za Mikoa.

Taasisi washirika ni pamoja na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA), Wakala la Mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam (DART Agency), Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB), Mfuko wa Barabara ulio chini ya OR-TAMISEMI, Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) - Hombolo, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), na Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT).

Nilifanya ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na taasisi zake washirika, na kubaini masuala yafuatayo: -

**20.1 Fungu 56: Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI)**

Wakati wa ukaguzi wa Fungu 56, niliona masuala mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na Menejimenti kama ifuatavyo: -

**20.1.1 Kukosekana kwa kanzidata na taarifa za fedha za kampuni za mawasiliano kwa ajili ya ukokotoaji wa ushuru wa huduma**

OR-TAMISEMI haikuwa na kanzidata ya kampuni zilizopewa leseni za kutoa huduma ya mawasiliano pamoja na mawanda ya shughuli zao, wala kampuni husika hazikuwisilisha taarifa za hesabu, hali inayoleta ugumu katika ukokotoaji wa ushuru wa huduma.

Kutokuwa na kanzidata ni kinyume na Kanuni ya 3(2)(b) ya Kanuni za Fedha za Serikali za Mitaa (Ukusanyaji na Usimamizi Ushuru wa Huduma kutoka Sekta ya Mawasiliano) za mwaka 2021, ambayo inaipa Wizara mamlaka ya kuanzisha na kutunza kanzidata ya kampuni zilizopewa leseni na mawanda ya shughuli zao. Aidha, Kanuni ya 6(2) ya Kanuni hizo inaelekeza kampuni husika kuwasilisha taarifa za hesabu za mwaka ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya mwaka wa fedha wa Kampuni husika kumalizika.

Kwa mwaka wa fedha 2022/23, OR-TAMISEMI ilikusanya jumla ya Sh. bilioni 12.18 kama ushuru wa huduma pasipo kuwa na taarifa za hesabu za kampuni, ikiwa ndicho kigezo muhimu cha kutambua kiasi cha ushuru wa huduma kinachopaswa kulipwa.

Kukosekana kwa kanzidata, mawanda ya shughuli za kampuni, na taarifa za hesabu za kampuni husika vinasababisha OR – TAMISEMI kutotambua kwa usahihi kiasi halisi cha ushuru wa huduma kinachopaswa kukusanywa, hali inayoweza kusababisha upotevu wa mapato kwa mamlaka za serikali za mitaa.

**Ninapendekeza OR – TAMISEMI kuanzisha kanzidata ya kampuni zote zilizopewa leseni za mawasiliano pamoja na mawanda ya shughuli za kampuni hizo kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika ufuatialiaji na ukusanyaji wa ushuru wa huduma. Pia, wakati utaratibu ukiwekwa wa kuhakikisha kampuni zenye leseni zinawasilisha taarifa za hesabu ndani ya muda unaotakiwa, Menejimenti ya OR – TAMISEMI inashauriwa kushirikiana taasisi zingine kama Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kupata taarifa za mauzo za kampuni hizo ili kurahisisha ukokotoaji wa ushuru wa huduma unaopaswa kulipwa.**

### 20.1.2 Kutokukusanya ushuru wa maegesho Sh. bilioni 9.98

Ukaguzi wangu wa mfumo wa ukusanyaji wa ushuru wa maegesho ulibaini kwamba, kuanzia Aprili 2021 hadi Juni 2023 wamiliki wa vyombo vya usafiri vilivyoegeshwa kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara hawakulipa kiasi cha jumla ya Sh. bilioni 9.98 kama ushuru wa maegesho na OR – TAMISEMI haikuchukua hatua zozote thabiti kuhakikisha ukusanyaji wa kiasi hicho cha fedha.

Hii ni kinyume na Kanuni ya 9(1) ya Kanuni za Serikali za Mitaa juu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Maegesho ya Vyombo vya Usafiri katika

Hifadhi za Barabara, za mwaka 2021, kila mmiliki wa chombo cha usafiri kinachoegeshwa katika maegesho atakuwa na wajibu wa kulipa ushuru wa maegesho. Maelezo yapo katika **Jedwali Na.139**.

**Jedwali Na. 139: Ushuru wa maegesho ambao haukukusanywa**

| Mwaka | Miezi ya Madai | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 2021 | Aprili - Desemba | 1,161,568,000 |
| 2022 | Januari - Desemba | 6,807,617,100 |
| 2023 | Januari - Juni | 2,011,381,400 |
| **Jumla** | | **9,980,566,500** |

**Chanzo:** *Mfumo wa ukusanyaji ushuru wa maegesho*

Kutokukusanya ushuru wa maegesho Sh. 9,980,566,500 kunazuia utekelezaji wa shughuli mbalimbali zenye thamani hiyo.

**Ninapendekeza OR- TAMISEMI, kuimarisha udhibiti katika usimamizi na ufuatiliaji katika ukusanyaji wa ushuru katika Serikali za Mitaa ili kuhakikisha ushuru wa maegesho kwenye hifadhi za barabara unakusanywa kwa ufanisi hivyo kuongeza makusanyo ya serikali.**

### 20.1.3 Kukosekana ufanisi katika ukusanyaji wa ada ya maegesho baada ya jukumu hilo kuhamishiwa Halmashauri kutoka TARURA

Nilipitia mwenendo wa ukusanyaji wa ushuru wa maegesho, hasa baada ya jukumu la ukusanyaji kuhama kutoka TARURA kwenda OR-TAMISEMI kuanzia Julai 2022, na kubaini kupungua kwa ukusanyaji wa ada ya maegesho.

OR-TAMISEMI kupitia mamlaka za serikali za mitaa ilikusanya Sh. bilioni 12.78 katika mwaka wa fedha 2022/23 sawa na 56% ya lengo lililowekwa na TARURA la Sh. bilioni 23.02. Kiasi kilichokusanywa kimepungua kwa Sh. bilioni 7.73 (38%) ikilinganishwa na Sh. bilioni 20.51 zilizokusanywa na TARURA mwaka 2021/22 na pungufu kwa Sh. bilioni 2.58 (17%) ya makusanyo yaliyokusanywa na TARURA mwaka 2020/21 ambayo yalikuwa Sh. bilioni 15.37.

Takwimu hizi zinaonesha kutokuwapo na ufanisi kwenye makusanyo ya ushuru katika serikali za mitaa ikilinganishwa na wakati ushuru huo unakusanywa na TARURA.

**Naishauri OR-TAMISEMIkuangalia uwezekano wa kuunganisha mfumo wa kukusanya ushuru wa maegesho na mfumo wa usimamizi wa**

**usalama barabani ili kushirikiana na Jeshi la Polisi katika ufuatiliaji na ukusanyaji wa ada ya maegesho ya magari kutoka kwa wasiolipa.**

### 20.1.4 Kuchelewa kufanyiwa kazi kwa maombi ya vibali vya maegesho kumesababisha kutokusanywa kwa Sh. milioni 141.47 kwa mita moja ya mraba

Kanuni ya 12 ya Kanuni za Serikali za Mitaa juu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Maegesho ya Vyombo vya Usafiri katika Hifadhi za Barabara, za mwaka 2021, inampa mtu au taasisi yeyote, haki ya kuomba kibali cha maegesho maalumu ya chombo cha usafiri kwa kujaza fomu maalumu ya maombi.

Nilipitia maombi ya nafasi za maegesho zilizowekwa akiba katika Halmashauri za Majiji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza, na Manispaa ya Kinondoni, na kubaini ucheleweshaji katika kufanyia kazi jumla ya maombi 252 ya nafasi 922 za maegesho zilizowekwa akiba, kwa kipindi cha kati ya siku 16 hadi 855. Maelezo yameoneshwa katika **Jedwali Na.140.**

**Jedwali Na. 140: Maombi ya maegesho maalumu yaliyocheleshwa**

| Halmashauri | Idadi ya maombi | Idadi ya maegesho | Idadi ya siku zilizocheleshwa | Kiasi kwa mita moja ya mraba (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| H/Jiji la Arusha | 20 | 71 | 23 to 344 | 1,167,733 |
| H/Jiji la Dar es salaam | 126 | 309 | 17 to 801 | 74,898,667 |
| H/ Jiji la Dodoma | 5 | 17 | 259 to 792 | 1,258,133 |
| H/M Kinondoni | 29 | 181 | 325 to 799 | 29,251,999 |
| H/Jiji Mwanza | 72 | 344 | 16 to 855 | 34,894,133 |
| **Jumla** | **252** | **922** | | **141,470,665** |

**Chanzo**: *Mfumo wa ukusanyahi ushuru wa maegesho*

Huenda maombi yalicheleweshwa kwa makusudi kwa manufaa ya watu wachache wanaoweza kuwa wananufaika na ukusanyaji wa ushuru wa maegesho nje ya mifumo ya kifedha ya Halmashauri husika.

Ucheleweshaji huo umesababisha kutokusanywa kwa jumla ya Sh. milioni 141.47 kwa mita moja ya mraba kwa maegesho yote 922 yaliyoombewa vibali.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI kufuatilia na kuchunguza juu ya ucheleweshaji wa kufanyia kazi maombi ya vibali vya magesho**

**maalumu katika mamlaka za serikali za mitaa na kuchukua hatua zinazostahili, na kuhakikisha maombi hayo na mengine mapya yanashughulikiwa haraka bila kucheleweshwa.**

### 20.1.5 Bajeti ya miradi ya maendelo katika MTEF kutoendana na utekelezaji halisi wa miradi husika

Wakati wa mapatio ya Muundo wa Mapato na Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) kwa mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini kuwa, OR-TAMISEMI ilitenga bajeti ya jumla ya Sh. milioni 71.42 kwa miradi sita kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.141.**

Hata hivyo, bajeti halisi na taarifa za hesabu zinazoonesha mapato na matumizi halisi kwa miradi hiyo yalikuwa makubwa zaidi kuliko kiasi kilichooneshwa katika MTEF.

Hali hii inaonesha kuwa bajeti katika MTEF haiwiani na bajeti halisi na utekelezaji wa miradi husika.

**Jedwali Na. 141: Kutowiana kwa bajeti ya miradi na MTEF**

| Mradi | Bajeti kwa mujibu wa MTEF (Sh.) | Bajeti kwa mujibu wa Nyaraka za Mradi na taarifa za hesabu (Sh.) | Jumla ya fedha iliyopokelewa (Ikijumuisha salio anzia) (Sh.) | Kiasi kilichotumika (Sh.) | Salio (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| RISE | 6,000,000,000 | 19,733,899,049 | 19,733,899,049 | 2,975,205,555 | 16,758,693,494 |
| TACTIC | 16,800,000,200 | 56,394,427,600 | 56,394,427,600 | 32,650,778,284 | 23,743,649,316 |
| HSPS | 822,145,374 | 2,258,540,374 | 3,931,086,295 | 3,759,811,812 | 171,274,483 |
| BOOST | 6,748,000,000 | 266,495,505,277 | 263,289,107,765 | 246,463,892,106 | 16,825,215,660 |
| SEQUIP | 15,293,750,000 | 295,072,208,814 | 301,376,987,844 | 218,044,419,909 | 82,944,304,475 |
| DMDP | 25,760,000,000 | 84,978,921,073 | 86,675,835,723 | 86,662,933,495 | 12,902,228 |
| Jumla | **71,423,895,574** | **724,933,502,187** | **731,401,344,276** | **590,557,041,161** | **140,456,039,656** |

***Chanzo:*** *MTEF, Nyaraka za Mradi na Taarifa za Hesabu 2022/23*

Upungufu katika maandalizi ya bajeti ya miradi yanaelezwa kutokana na ukomo wa bajeti unaotolewa na Wizara ya Fedha.

Kutowiana kwa bajeti za miradi na taarifa za fedha za MTEF husababisha mapato na matumizi ya miradi husika kutojumuishwa katika taarifa za hesabu za OR – TAMISEMI.

Kutofautiana huko kunahatarisha usahihi na kuaminika kwa mchakato wa kupanga bajeti na utoaji taarifa za hesabu kulingana na mwongozo wa maandalizi ya mipango ya Serikali na bajeti.

**Ninashauri OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kuhakikisha mipango kazi wa mwaka na bajeti za miradi zinajumuishwa kikamilifu katika Mapato na Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) kwa lengo la kuonesha shughuli zote zilizopangwa kutekelezwa ili kuimarisha udhibiti wa matumizi na ufanisi katika utoaji wa taarifa za hesabu.**

### 20.1.6 Upungufu katika maombi, utolewaji na uhamishaji wa fedha zilizovuka mwaka kutoka Hazina kwenda Halmashauri Sh. bilioni 45.54

Mnamo tarehe 23 Agosti 2023, OR-TAMISEMI iliiomba Wizara ya Fedha kutolewa kwa kiasi cha jumla ya Sh. bilioni 45.54 kwenda Akaunti ya Amana ya OR – TAMISEMI (LGAs Miscellaneous Deposit Account) Na. 9921169787, ambazo ni fedha za mamlaka za serikali za mitaa zilizovuka mwaka (2021/22) na tarehe 30 Juni 2023 kuhamishiwa katika Akaunti ya Amana ya Hazina (Treasury Deposit Account) Na. 9921169777.

Hata hivyo, mnamo tarehe 26 Septemba 2023 Wizara ya Fedha ilitoa kiasi cha jumla ya Sh. bilioni 42.78, kwenda Akaunti Na. 9921169787 ikiwa ni pungufu kwa Sh. bilioni 2.76 ikilinganishwa na fedha zilizoombwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, OR-TAMISEMI ilihamisha kiasi cha jumla ya Sh. bilioni 37.92 kwenda mamlaka za serikali za mitaa na kusalia na bakaa ya Sh. bilioni 4.87.

Uchambuzi wa fedha zilizoombwa na kupokelewa kutoka Hazina na baadae kuhamishwa kwenda mamlaka za serikali za mitaa, uilibaini upungufu ufuatao: -

(a) Fedha za maendeleo kiasi cha Sh. bilioni 3.15 ziliombwa Hazina kwa ajili ya Halmashauri 22 lakini ni kiasi cha Sh. bilioni 2.35 pekee ndicho kilichotolewa na Hazina na Sh. milioni 799 hazikutolewa na Hazina kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.52;**

(b) Fedha za maendeleo Sh. bilioni 5.49 zilitolewa na Hazina kwa Halmashuri 12 lakini ni Sh. bilioni 3.79 pekee zilizotolewa na OR

– TAMISEMI kwenda Halmashauri na kusalia na bakaa ya Sh. bilioni 1.69 kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.53;**

(c) Fedha za maendeleo kiasi cha Sh. bilioni 2.86 zilipokelewa na OR-TAMISEMI kutoka Hazina kwa ajili ya Halmashauri 24 lakini ni Sh. bilioni 3.52 zilizotolewa na OR – TAMISEMI kwenda Halmashauri na kusalia na bakaa ya Sh. milioni 663 kama zinavyoonekana katika **Kiambatisho Na.54;**

(d) Fedha za maendeleo kiasi cha Sh. bilioni 6.21 ziliombwa kwa ajili ya Serikali 18 za Mitaa; ambapo kiasi cha Sh. bilioni 5.98 zilipokelewa na OR-TAMISEMI kutoka Hazina. Hata hivyo, ni kiasi cha Sh. bilioni 4.29 pekee ndicho OR – TAMISEMI ilihamisha kwenda Serikali za Mitaa hii inaonesha kuwa OR – TAMISEMI iliomba Sh. bilioni 1.93 zilizosemekana kuwa za Serikali za Mitaa lakini zilipopokelewa hazikuhamishwa kwenda Serikali za Mitaa. Maelezo yameoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.55;**

(e) Fedha za maendeleo kiasi cha Sh. bilioni 1.65 ziliombwa kwa ajili ya Serikali za Mitaa 11; ambapo Sh. bilioni 1.75 ilipokelewa OR – TAMISEMI na Sh. bilioni 1.75 zilipelekwa Serikali za Mitaa ikimaanisha kuwa Sh. milioni 96.57 zilitolewa zadi ya kiasi kilichoombwa na OR-TAMISEMI kwa ajili ya halmashauri. Maelezo yameoneshwa katika **Kiambatisho Na.56**.

Hadi tarehe 19 Desemba 2023, kiasi cha jumla ya Sh. bilioni 4.87 kinachojumuisha fedha za maendeleo Sh. milioni 761.67 na fedha za matumizi ya kawaida Sh. bilioni 4.11 kilikuwa bado kipo kwenye Akaunti ya Amana ya OR-TAMISEMI (LGAs Miscellaneous Deposit Account) pasipo kuhamishiwa kwenye Halmashauri au kurudishwa Hazina.

Upungufu huo yanadaiwa kusababishwa na baadhi ya miamala ya marekebisho kwenye daftari la fedha (cash book) inayofanyika moja kwa moja ndani ya mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) (auto dummy transactions) ambayo haikufanyika na kusababisha baadhi ya Halmashauri kuhamisha salio linaloonekana (ambalo halikupaswa kuonekana) kwenye daftari la fedha kwenda akaunti ya amana hali iliyosababisha baadhi ya fedha kutumika kufuta salio hilo hasi kwenye daftari la fedha.

Upungufu huo unaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha kwa Halmashauri zilizopelekewa fedha zaidi ya ilivyostahili.

**Ninashauri Menejimenti ya OR - TAMISEMI kuhakikisha inafanya usuluhishi stahiki na kuhakikisha uhamishaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwenda Serikali za Mitaa baada ya kufanya usuluhishi wa kina wa bakaa, na kiasi chochote kitakachokuwa kimetolewa zaidi kinapaswa kurejeshwa Hazina. Pia, OR -TAMISEMI inashauriwa kuimarisha na kufuatilia kitengo kinachofanya usuluhishi ili kufanya uhakiki wa kina wa salio kabla ya kuomba fedha hazina.**

## 20.2 Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)

TARURA ilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali, [SURA YA 245], na kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali Na. 211 la tarehe 12 Mei 2017, lengo kuu likiwa ni kukuza viwango vya matengenezo na uendelezaji wa barabara za vijijini na mijini, ukitilia mkazo ubora, ufanisi, na gharama nafuu.

Aidha, uanzishwaji wa TARURA ulilenga kushughulikia vikwazo katika sekta ya usafirishaji wa barabarani nchini Tanzania, ambavyo kwa muda mrefu vimetatiza usimamizi mzuri na wenye ufanisi wa barabara. TARURA inahusika na kupanga, kubuni, kujenga, na kutunza barabara za mijini na vijijini nchini Tanzania.

Wakati wa ukaguzi wa hesabu za TARURA, nilibaini upungufu ufuatao:

### 20.2.1 Uharibifu na vizuizi barabarani kutokana mamlaka za huduma za maji na umeme kuingilia mtandao wa barabara za TARURA

Kwa mujibu wa Agizo Na. 2 la Uanzishwaji wa Wakala za Serikali (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania) la mwaka 2017, TARURA inawajibika na ujenzi na matengenezo ya barabara za vijijini na mijini nchini Tanzania.

Kwa upande mwingine, Kanuni ya 10 na 16(3) ya Kanuni za Usimamizi wa Barabara za mwaka 2009 inahitaji mtu yeyote anayeweka kizuizi katika eneo la barabara kukiondoa ndani ya siku 14 na kutafuta idhini ya awali kutoka kwa Wakala kuhusu shughuli ambazo zitaweka kizuizi katika eneo la barabara.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini shughuli za baadhi ya Mamlaka za Maji na TANESCO zilisababisha uharibufu na vizuizi kwenye mtandao wa barabara kama ifuatavyo: -

(a) Katika matengenezo ya sehemu korofi na ya kawaida ya barabara za Esso - Longdong (3.25km), Lolovono - Safina, na Muriet – Sojema katika Mkoa wa Arusha kwa gharama Sh. milioni 194.53.

Nilibaini uharibifu wa barabara baada ya kuzikagua mnamo tarehe 17 Novemba 2023. Sehemu ya barabara iliharibiwa kutokana na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira - Arusha kuchimba barabara kwa ajili ya kuweka bomba za maji taka na kusababisha uharibifu mkubwa hasa baada ya mvua kunyesha.

(b) Kadhalika, katika mkoa wa Morogoro, TARURA ilikuwa na wakandarasi wanne kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Ngerengere - Kidunda 75km kwa jumla ya gharama ya Sh. bilioni 1.91 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.142**.

**Jedwali Na. 142: Matengezo ya barabara ya Ngerengere - Kidunda**

| Na | Maelezo ya mktaba | Tarehe ya kuanza na kumaliza kazi | Kiasi cha Mkataba (Sh) | Kiasi kilicholipwa (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kuongeza hadhi ya barabara ya Ngerengere-Kidunda 8km | 10/08/2022 to 30/05/2023 | 499,791,620 | 496,885,740 |
| 2. | Kuongeza hadhi ya barabara ya Ngerengere-Mkulazi-Kidunda 10km | 24/08/2022 to 12/09/2023 | 492,488,000 | 430,952,140 |
| 3. | Kuongeza hadhi ya barabara ya Ngerengere-Mkulazi-Kidunda 6km | 06/02/2023 to 07/01/2024 | 425,647,000 | 17,300,000 |
| 4. | Ukarabati wa barabara ya Ngerengere-Kidunda 10km | 26/10/2021 to 26/01/2022 | 489,820,000 | 489,203,710 |
| Jumla | | | 1,907,746,620 | 1,434,341,590 |

**Chanzo**: Majalada ya mikataba

Nilibaini kuwa tarehe 16 Februari 2023, DAWASA iliifahamisha TARURA juu ya mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ambapo mkataba ulisainiwa

tarehe 31 Oktoba 2022. Mradi huo unajumuisha kuboresha barabara ya Ngerengere - Kidunda 75km kwa kiwango cha changarawe.

Wakati TARURA inajulishwa juu ya mradi huu, ilikuwa imeshawalipa Wakandarasi wake jumla ya kiasi cha Sh. bilioni 1.43 kwa matengenezo ya barabara hiyo, ambapo Wakandarasi wawili walikuwa hawajakamilisha kazi zao.

TARURA ililazimika kutoa amri ya kusimamisha kazi kwa Wakandarasi hao ili kuruhusu DAWASA kuendelea na uboreshaji barabara hiyo uliokusudiwa.

Kwa mujibu wa taarifa ya usanifu (design report) ya mradi huo iliyowasilishwa na DAWASA kwa TARURA kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Ngerengere - Bwawa Kidunda, jumla ya upana wa barabara ni 10m wakati upana wa wakati huo ulikuwa 7m.

Pia, Aya 4.4.2 ya taarifa hiyo, inaonesha uwepo wa miundombinu mikubwa 10 sehemu ambapo maji hukatisha, na mitaro inayohitaji kalvati za zege 22 zenye kipenyo cha kati ya 1200mm hadi 600mm.

Kwa kuzingatia mapendekezo ya Mshauri Mwelekezi, miundombinu yote iliyokuwa kwenye barabara ilistahili kubadilishwa. Hadi tarehe 2 Novemba 2023, mkandarasi aliyeajiriwa na DAWASA alikuwa akiendelea na kazi.

(c) Vizuizi kutokana na usimikaji wa nguzo za umeme barabarani:-

- Ukaguzi wa mkataba Na. AE/092/2022/2023/DSM/W/27 wa Sh. milioni 363.70 kwa ajili ya barabara ya Zomboko – Kingugi katika Manispaa ya Temeke na eneo la mradi uliofanyika tarehe 4 Oktoba 2023, ulibaini kusimikwa kwa nguzo ya umeme barabarani. Katika barua yenye Kumb. Na. CA.225/366/01/11 ya tarehe 17 Agosti 2022, TARURA iliitoa notisi (notice) kwa TANESCO kuhamisha nguzo hiyo. Hata hivyo, hadi tarehe ya ukaguzi wa mradi huo, ikiwa ni miezi 14 tangu kutolewa kwa notisi hiyo, nguzo hiyo haikuwa imehamishwa;

- Vilevile, katika mikataba Na. AE/092/2022/2023/TAG/W/72 na Na. AE/092/2022/2023/TAG/W/65 yenye thamani ya Sh. milioni

554.65 na Sh. milioni 499.68 mtawalia, kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Mji wa Mombo katika Wilaya ya Korogwe, na kuboresha barabara za Mji wa Pangani kwa kiwango cha lami (bitumen) kulikuwa na tatizo la usimikaji nguzo za umeme barabarani.

TARURA iliiandikia TANESCO kupitia barua Kumb. Na. CA.274/339/01/33 ya tarehe 14 Aprili 2023 na Na. AE/092/2022/2023/TAG/W/65 ya tarehe 23 Januari 2023 kuondoa nguzo barabarani.

Hata hivyo, TANESCO haikuondoa nguzo hizo zilizosimikwa katika barabara ya Market- Community Centre Road na kwenye barabara ya Jamhuri katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, na kusababisha vizuizi barabarani.

Kukwamisha kazi na kuingilia mtandao wa barabara kunahusiana na upangaji duni wa miradi, ushirikiano hafifu baina ya taasisi za Serikali katika utekelezaji wa miradi, hali ambayo inasababisha upotevu wa fedha za umma.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya TARURA kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI kuimarisha ushirikiano na taasisi zingine za Serikali katika kuhakikisha ushiriki wao katika kubuni na kutekeleza miradi, ili kuzuia uharibifu, mwingiliano, na uwezekano wa kutokea matumizi mabaya ya fedha za umma na kuepuka hasara inayoweza kujitokeza.**

### 20.2.2 Ucheleweshaji na kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 65.55

Kanuni ya 114 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013, inaitaka taasisi nunuzi kuwa na usimamizi bora wa ununuzi wowote wa kazi inazofanya na kufuatilia maendeleo na ukamilishaji wa kazi kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba. Taasisi nunuzi inatakiwa kuchukua au kuanzisha hatua za kurekebisha au za kisheria juu ya ukiukwaji wa masharti ya mkataba; na kuhakikisha kwamba majukumu yaliyowekwa kimkataba yanatekelezwa kikamilifu.

Mapitio yangu ya mafaili ya mikataba na ukaguzi wa miradi uliofanyika kati ya Septemba 2023 hadi Novemba 2023, yalibaini ucheleweshaji katika kukamilisha miradi 59 ya thamani ya Sh. bilioni 44.82. Japokuwa,

baadhi ya wakandarasi, waliongezewa muda mara kadhaa kazi zao hazikukamilika ndani ya muda ulioongezwa kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na.57**.

Kadhalika, nilibaini kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi 29 yenye thamani ya Sh. bilioni 20.73 hali iliyosabababisha wakandarasi kuongezewa muda. Licha ya ongezeko hilo la muda, kutokana na kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi husika, huenda miradi hiyo haitakamilishwa ndani ya wakati kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na.58**.

Kasi ndogo katika utekelezaji wa miradi inachangiwa na sababu kadhaa ikiwamo, uwezo mdogo wa baadhi ya wakandarasi wanaotekeleza miradi mingi ndani ya kipindi kimoja, kuchelewa kuanza kwa miradi na mtiririko hafifu wa fedha kwa upande wa mwajiri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi husika.

Kucheleweshwa kwa utekelezaji wa miradi ndani ya kipindi cha mkataba kunaweza kusababisha kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Pia, inaweza kusababisha gharama za ziada na ubora hafifu wa mradi.

**Ninapendekeza Menejimenti ya TARURA kuimarisha mifumo yake ya udhibiti na usimamizi wa mikataba ili kuhakikisha wakandarasi wanaanza utekelezaji wa miradi kwa wakati, na kuboresha ufuatiliaji ili kuhakikisha miradi husika inakamilika ndani ya muda uliokubaliwa.**

### 20.2.3 Upungufu katika usanifu wa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 27.75

Aya 3.7.1 ya Mwongozo wa Usanifu wa Barabara wa Wizara ya Ujenzi wa mwaka, 2011 unaelekeza kwamba mradi wa njia kuu unaweza kujumuisha ujenzi wa barabara mpya au kuboresha barabara iliyopo. Katika hali zote mbili, michoro huandaliwa baada ya upimaji wa kina, usanifu na uchunguzi.

Njia inayotumika kufanya upimaji ina athari muhimu kwenye usanifu, uzalishaji wa vipimo na makadirio ya gharama na hatimaye kwenye utekelezaji wa kazi.

Pia, Aya ya 5.7 ya Mwongozo wa Usanifu wa Barabara wa Wizara ya Ujenzi wa mwaka, 2011 unaeleza kuwa, usanifu sahihi wa michoro ihusuyo maji ni sifa muhimu katika mipango na usanifu wa barabara kwa ujumla. Katika

uchoraji wa mifereji, vipengele vya haidrolojia kama mvua, kiasi cha mtiriko na asili ya mkondo wa maji ni muhimu.

Katika ukaguzi wa mikataba minne yenye thamani ya Sh. bilioni 27.75, nilibaini upungufu katika usanifu wa miradi hiyo, ambayo yanaweza kuathiri ubora wa mradi, gharama na ucheleweshaji utekelezaji wa miradi husika kama ilivyobainishwa katika **Kiambatisho Na.59.**

Udhaifu katika usanifu wa miradi unatokana na kutokutumia taarifa halisi zilizokusanywa kutoka eneo la mradi, ambayo inaweza kusababishwa na uchunguzi hafifu au usio sahihi wa haidrolojia na haidroliki, upimaji na uchunguzi wa miamba wakati wa hatua ya usanifu na uwezekano wa kukosea au kutojumuisha katika taarifa ya usanifu.

**Ninashauri Menejimenti ya TARURA katika utekelezaji wa miradi ijayo: - a), kufanya uchunguzi kikamilifu wa kihaidrojia na kihaidroliki na kutumia taarifa halisi zinazokusanywa eneo la mradi katika kufanya usanifu, (b) Kufanya mapitio ya maandalizi na hatua za upimaji eneo la mradi, na taarifa ya usanifu ili kupunguza upungufu katika utekelezaji wa miradi, (c) Kuhakikisha miradi itakayotekelezwa inajumuisha upimaji na uchunguzi wa kina kabla ya usanifu wa barabara, kuwianisha usanifu uliofanyika na bajeti ya utekelezaji wa mradi husika.**

### 20.2.4 Mikataba iliyotolewa kwa wazabuni ambao hawakukidhi vigezo vya zabuni husika Sh. bilioni 1.99

Kwa mujibu wa Kanuni 206 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, GN.446, zabuni ambayo haikuikidhi (responsiveness) vigezo vya zabuni, itakataliwa na taasisi nunuzi, na haiwezi kufanywa kuwa na sifa kwa kuifanyia marekebisho, au kuondoa kipengele au nyaraka ambayo haikukidhi vigezo vya zabuni.

Miongoni mwa vigezo vya tathmini katika Sehemu ya IV ya Nyaraka za Zabuni, sehemu ndogo ya 2.5 ilimtaka mzabuni kuwasilisha cheti cha uthibitisho wa kutodaiwa kodi (Tax clearance certificate) kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Januari 2019 hadi Mei 2022; na sehemu ndogo ya 3.1(iii) ilimtaka mzabuni kuwasilisha taarifa za fedha zilizokaguliwa na zinazokubalika kwa mwajiri zinazothibitisha hali ya kifedha ya wakati huo na matarajio ya kipindi cha miaka miwili (kuanzia 2019 hadi 2021).

Katika ukaguzi wa mchakato wa tathimni ya zabuni 25 zilizotolewa na TARURA kwa wakandarasi 14 katika mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini kuwa mikataba sita yenye thamani ya Sh. bilioni 1.99 ilitolewa kwa zabuni ambazo hazikukidhi vigezo kwa mujibu wa nyaraka za zabuni. **Jedwali Na.143** linaonesha wilaya na mikataba husika.

**Jedwali Na. 143: Zabuni ambazo hazikukidhi vigezo**

| Na | Jina la Wilaya | Namba ya Zabuni/mkataba | Kiasi cha Mkataba (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Kalambo | AE/092/2022 - 2023/RKW/W/27 | 251,563,000 | Mzabuni hakuwasilisha cheti cha uthibitisho wa kutodaiwa kodi |
| 2 | H/W Nkasi | AE/092/2022 - 2023/RKW/W/07 | 313,667,000 | |
| 3 | H/M Sumbawanga | AE/092/2022 - 2023/RKW/W/32 | 421,196,399 | Mzabuni aliwasilisha cheti cha uthibitisho wa kutodaiwa kodi kichokwisha muda wake |
| 4 | H/W Nkasi | AE/092/2022 - 2023/RKW/W/28 | 500,000,000 | |
| 5 | H/W Sumbawanga | AE/092/2022 - 2023/RKW/W/30 | 385,099,800 | Mzabuni aliwasilisha taarifa za fedha za mwaka 2020 tu. |
| 6 | H/M Sumbawanga | AE/092/2022 - 2023/RKW/W/44 | 117,651,372 | Mzabuni aliwasilisha taarifa za fedha za mwaka 2021 tu. |
| **Jumla** | | | **1,989,177,571** | |

**Chanzo:** TANEPS, mikataba

Vilevile, nilibaini kuwa Mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/10 wenye thamani ya Sh. bilioni 16.79 kwa ajili ya kuboresha barabara ya Kasulu – Kabanga – Kasumo - Muyama (12.5 Km) kwa kiwango cha lami - Awamu I, alipewa mzabuni ambaye hakukidhi kigezo kutokana na kutokufanyika uchunguzi wa kiutendaji wa mzabuni na Kamati ya Tathmin.

Kipengele cha 3.3 katika Sehemu ya IV ya Vigezo na Mahitaji (Qualification criteria and Requirements) kilimtaka mzabuni kutoa taarifa juu ya mikataba anayotekeleza au ambayo amekabidhiwa kutekeleza.

Baada ya kupitia taarifa za zabuni fomu FIN-3.4 katika mfumo wa TANEPS, mzabuni alionesha kuwa na kazi zinazoendelea za thamani ya Sh. milioni 50 katika mkoa wa Tabora. Hata hivyo, nilibaini kuwa ndani ya kipindi hicho, mzabuni huyo alikuwa na mikataba 13 na TARURA inayoendelea yenye thamani ya Sh. 7.8 bilioni. Mkandarasi alitoa taarifa isiyo sahihi kuhusu mikataba inayoendelea pengine kwa lengo la kuishawishi timu ya tathmini kumpatia zabuni hiyo.

Kumpitisha mzabuni asiyekidhi vigezo vya zabuni kwenda hatua ya tathmini ya kina na hatimaye kupewa zabuni husika kunawanyima fursa ya ushindani wazabuni wengine wanaokidhi vigezo; hivyo, kuhatarisha usawa na ushindani katika mchakato wa uteuzi. Pia, kutokana na kazi nyingi za mkandarasi, kuna hatari ya kuchelewesha utekelezaji wa miradi hiyo.

Utoaji wa mikataba kwa wazabuni wasiokidhi vigezo unahusishwa na kushindwa kwa kamati ya tathmini kuchunguza kukubaliana (compliance) kwa zabuni zilizowasilishwa na vigezo vya tathmini vilivyowekwa katika nyaraka za zabuni.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya TARURA kuhakikisha wajumbe wa kamati za tathmini wanakumbushwa mara kwa mara kufanya tathmini kwa ufasaha kulingana na vigezo vilivyobainishwa katika nyaraka za zabuni, na Bodi ya Zabuni inapaswa kuhakikisha inafanya mapitio ya mchakato na taarifa za tathmini kwa umakini.**

### 20.2.5 Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara kwa teknolojia mpya kabla ya kumaliza majaribio na kuridhika na utendaji wake Sh. bilioni 9.02

TARURA imeanzisha mpango wa majaribio ya teknolojia tatu mbadala katika ujenzi wa barabara ambazo ni ECOROADS, Plymer na Ecozyme katika mikoa minane kwa kutumia kemikali maalumu ya kuimarisha udongo (soil stabilising agent) kwa gharama ya Sh. bilioni 27.

Mnamo tarehe 11 Aprili 2023, TARURA iliingia Mkataba Na. AE/092/2022/23/HQ/W/19 wa thamani ya Sh. bilioni 9.02 kwa ajili ya kuboresha sehemu ya barabara ya Sawala – Mkonge – Iyegeya - Lulanda (10.4 km) kwa kuweka tabaka mbili (double surface dressing) kama sehemu ya majaribio ya teknolojia ya ECOROADS.

Hata hivyo, katika ukaguzi wa utekelezaji wa mradi huo wa majaribio nilibaini upungufu kama vile; kukosekana kwa kanuni na miongozo ya ndani katika ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia mpya, matumizi ya bidhaa za teknolojia hiyo pasipo na ithibati na maelezo (specifications) na kuanza kutekeleza mradi (a full-scale project) kabla ya kukamilisha majaribio na kuridhika na utendaji wa teknolojia husika.

Utaratibu unaotumika katika majaribio ya teknolojia mpya ni kuwa; mzabuni alpaswa kujenga sehemu ya barabara isiyopungua kilometa moja kwa gharama zake mwenyewe ili kudhihirisha utendaji wake ambapo sehemu hiyo ingeangaliwa (monitored) kwa kipindi kisichopungua miaka miwili, na huo ungekuwa msingi wa kukubalika kwa teknolojia hiyo kutumika nchini.

Katika mwaka wa fedha 2020/21, ECOROAD Tanzania Ltd, ambayo ni kampuni tanzu ya ASZ Africa Ltd, ilifanyia majaribio teknolojia ya ECOROADS kwa kilometa moja kwenye barabara ya Nala-Lugala-Mbalawala-Veyula kwa gharama yao wenyewe.

Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi kwamba TARURA ilifuatilia na kutathmini sehemu ya barabara hiyo kwa miaka miwili na kuridhika na utendaji wa teknolojia hiyo kabla ya kusaini mkataba wa utekelezaji wa mradi kamili.

Kwa maoni yangu, kutumia teknolojia mbadala mpya kutekeleza mradi kamili bila ya ithibati, miongozo au kanuni za ndani za utekelezaji na pasipo kujiridhisha na utendaji wa teknolojia husika, inaiweka TARURA katika hatari ya matumizi ya fedha yasiyo na tija iwapo mradi hautakidhi viwango vinavyohitajika vya ubora, hali itakayosababisha kuongezeka kwa gharama za matengenezo na kupungua kwa muda wa maisha ya barabara.

**Ninapendekeza kwamba, Menejimenti ya TARURA kwa kushirikiana na Wizara inayohusika na ujenzi: - (a) Kuanzisha miongozo mbadala, sera, na kanuni kwa ajili ya kuongoza utekelezaji wa miradi kwa kutumia teknolojia mpya; (b) Kusaini mikataba ya utekelezaji miradi kwa teknolojia mbadala baada ya majaribio kuhitimishwa na kuridhika na utendaji wa teknolojia; na kufuatilia na kutathmini utendaji na uimara wa barabara zilizojengwa kwa kutumia teknolojia husika.**

### 20.2.6 Kazi za matengenezo ya barabara zinazoingiliana zilizotumia kiasi cha Sh. milioni 62.31

(a) Katika Mkataba Na. AE/092/2021/2022/MAR/W/68 wa thamani ya Sh. milioni 318.27 ulioanza tarehe 25 Oktoba 2021 hadi 27 Juni 2022 na kipindi cha matazimio kilichomalizika tarehe 27 Desemba 2022, TARURA katika mkoa wa Mara ilimlipa mzabuni kiasi cha Sh.

milioni 46.82 kupitia Cheti (IPC) Na. 2 kwa ajili ya kuondoa tabaka bovu la changarawe na kurudishia tabaka zuri barabara ya Bwaikutururu - Bwaikumsoma kwenye kilomita 0+000 hadi 3+400.

Hata hivyo, katika Mkataba mwingine Na. AE/092/2022/2023/11 wa thamani ya Sh. milioni 223.02 ulioanza tarehe 10 Desemba 2022 na kumalizika tarehe 23 Machi 2023, nilibaini malipo ya Sh. milioni 44.81 kwa mkandarasi mwingine kupitia Vyeti (IPCs) Na. 1 & 2 kwa ajili ya kuondoa tabaka bovu la changarawe na kurudishia tabaka zuri barabara ya Bwaikutururu - Bwaikumsoma kwenye kilomita 0+000 hadi 3+200. Kipande hiki cha barabara kilikuwa kiko kwenye mkataba wa awali, na wakati wa kuingia mkataba wa pili Na. AE/092/2022/2023/11, barabara husika ilikuwa kwenye kipindi cha matazimio. Hivyo, kiasi kilicholipwa kwenye mkataba wa pili cha Sh. milioni 44.81 kingeweza kuepukika.

(b) Vivyo hivyo, katika mkataba Na. AE/092/2021/2022/MAR/W/73 wenye thamani ya Sh. milioni 224.91 kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara kwenye barabara ya Nyamaguku - Kirogo, ulioanza tarehe 6 Januari 2022 na kumalizika tarehe 27 Oktoba 2022 huku kipindi cha matazamio kikiisha tarehe 24 Aprili 2023. Katika mkataba huu, TARURA ilimlipa mkandarasi kiasi cha Sh. milioni 26.4 kupitia vyeti IPC 1 na 2 kwa kazi ya kuchonga barabara ya Nyamaguku - Kirogo kwenye kilometa 0+000 hadi 13+000.

Hata hivyo, katika mkataba mwingine Na. AE/092/2022/2023/50 wa thamani ya Sh. milioni 474.33 uliojumuisha kazi ya matengenezo sehemu korofi barabara ya Nyamaguku – Kirogo, ambao thamani ya mkataba ilirekebishwa kuwa Sh. milioni 509.46, ukianza na kumalizika tarehe 24 Oktoba 2022 na 30 Aprili 2023 mtawalia, nilibaini kuwa wigo wa kazi ulijumuisha kipande cha barabara kwenye kilomita 8+000 hadi 15+000 ambacho kinaingiliana na kipande cha barabara cha mkataba Na. AE/092/2021/2022/MAR/W/73 kwenye kilomita 8+000 hadi 13+000. Hii inaonesha kuwa wakandarasi wawili walifanya kazi kwenye kipande hicho cha barabara kwa wakati mmoja.

Nilibaini malipo ya Sh. milioni 158.58 kwa mkandarasi kupitia Cheti (IPC) Na. 2 na Hati ya Malipo. Na. 0S100077V230176 ya 6 Aprili 2023 yaliyojumuisha Sh. milioni 17.5 kwa kazi ya kuchonga barabara ya Nyamaguku – Kirogo kwenye kilomita 8+000 -15+000.

Katika uchunguzi wa awali uliofanywa na TARURA, ilibainika kukosekana kwa utaalamu katika usimamizi wa kazi na upungufu kwenye taarifa za mikataba; ambapo tayari hatua za kinidhamu zimechukuliwa kwa waliohusika.

Upungufu huo umesababisha malipo yasiyo na tija ya kiasi cha jumla ya Sh. milioni 62.31 (Sh. 44.81 + Sh. 17.5) kwa kazi zinazoingiliana.

**Ninapendekeza kwamba Menejimenti ya TARURA; (a) Kuboresha maelezo (specifications) na uwazi kwenye mikataba ili kuhakikisha wigo wa kazi ni sahihi na kuimarisha ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa ili kuongeza udhibiti wa ubora; na (b) Kufanya uchunguzi zaidi kuhusu suala hilo na kuchukua hatua stahiki ikiwamo kurejeshwa kwa Sh. milioni 62.31 zilizolipwa isivyostahili.**

### 20.2.7 Malipo kwa kazi ambazo hazikufanyika kiasi cha Sh. milioni 98.91

Kanuni ya 243 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013, inazitaka taasisi nunuzi kuidhinisha malipo kulingana na vipimo na uthibitisho, katika vipindi au hatua zilizooneshwa katika mikataba na kwamba asilimia kadhaa ya thamani ya kazi zilizotekelezwa kutoka kila cheti cha malipo kinaweza kukatwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya matazamio endapo mkataba utaweka takwa hilo.

Katika mwaka 2022/23, TARURA iliingia mikataba na wakandarasi kwa kazi mbalimbali za barabara zinazojumuisha kusafisha eneo la mradi, uwekaji tabaka la changarawe, kuchonga barabara na uwekaji kalvati, ambapo kiasi cha Sh. milioni 312.16 kililipwa kwa kazi hizo (kwa mikataba mitatu).

Hata hivyo, baada ya kukagua eneo la mradi mnamo tarehe 26 Oktoba 2023 na kupima upya kazi zilizofanyika, ilibainika kuwa zilikuwa na thamani ya Sh. milioni 213.25 pekee na siyo Sh. milioni 312.16 zilizolipwa. Hivyo, TARURA ililipa kiasi cha Sh. milioni 98.91 zaidi isivyostahili. Maelezo yapo **Jedwali Na.144.**

**Jedwali Na. 144: Malipo kwa kazi ambazo hazikufanyika**

| Mkataba Na. | Maelezo ya kazi zilizolipiwa zaidi | Kiasi kilicholipwa (Sh.) | Thamani ya kazi iliyoteklezwa baada ya kupima upya (Sh.) | Kiasi kilicholipwa zaidi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| AE/092/2022/2023/MAR/W/38 | Kusafisha eneo la mradi, uwekaji wa tabaka la changarawe na ujenzi wa kalvati. | 122,484,310 | 74,800,810 | 47,683,500 |
| AE/092/2022/2023/MAR/W/53 | Uwekaji wa tabaka la changarawe kwenye maeneo korofi. | 155,925,000 | 126,967,500 | 28,957,500 |
| AE/092/2021-2022/MAR/W/01 | Kuchonga barabara na uwekaji wa tabaka la changarawe wakati wa matengezo ya mara kwa mara. | 33,750,000 | 11,485,500 | 22,264,500 |
| **Jumla** | | **312,159,310** | **213,253,810** | **98,905,500** |

**Chanzo**: Vyeti vya kazi, hati za malipo na upimaji

Malipo kwa kazi zisizotekelezwa yanahusishwa na udhaifu katika upimaji na uthibitisho katika utekelezaji wa mkataba; hali ambayo imesababisha matumizi yasiyo na tija.

Menejimenti ya TARURA inahusisha udhaifu huu na mwenendo mbaya (misconduct) wa Ofisi ya Mkoa wa Mara, na hatua za kinidhamu zimechukuliwa dhidi ya maofisa waliohusika. Hadi Desemba 2023, uchunguzi wa ndani ulikuwa unaendelea.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya TARURA: - (a) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa ubora katika utekelezaji wa miradi kulingana na masharti ya mkataba ikiwamo kuhakikisha malipo yanafanyika kwa kazi zilizopimwa na kuthibitika kufanyika; na (b) Kuchukua hatua stahiki dhidi ya wale waliohusika ikiwamo kurejesha kiasi kilicholipwa zaidi cha Sh. milioni 98.91.**

### 20.2.8 Ununuzi yaliyofanyika bila kutumia njia ya ushindani wa bei - Sh. bilioni 14.81

Kanuni ya 152 ya Kanuni za ununuzi wa Umma za mwaka 2013, taasisi nunuzi inatakiwa kutoa nyaraka za zabuni iliyofungwa kwa wazabuni wachache ikiwa: kuna hitaji la dharura kwa bidhaa, kazi au huduma kama taasisi haitakuwa na muda wa kutosha kufanya ushindanishi wa bei, na kama kuna uharaka ambao haukutarajiwa na taasisi na haukusababishwa na matendo ya upande wake au haja ya kufikia lengo la kijamii kwa kuyaita makampuni ya ndani au jamii zishiriki.

Kadhalika, Kanuni ya 161 (1) ya Kanuni hizo inaelekeza mazingira ambapo taasisi nunuzi inaweza kupata nukuu za bei kutoka kwa mzabuni mmoja, kujadili na kuingia katika mkataba moja kwa moja.

Kinyume na Kanuni hizo, katika ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 14.81 nilibaini TARURA ilitumia njia ya ununuzi kutoka chanzo kimoja (single source) na mchakato wa zabuni iliyofungwa kwa wazabuni wachache, badala ya zabuni za ushindani bila sababu za msingi za kukidhi masharti ya Kanuni ya 161 (1) na 152 (1) za Kanuni za Ununuzi za Umma, 2013. Zabuni husika zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na.60**.

Utumiaji wa njia ya ununuzi ya chanzo kimoja na mchakato wa zabuni zilizofungwa kwa wazabuni wachache inapunguza uwazi na fursa sawa kwa wazabuni wengine wanaostahiki kushindana; hivyo, kuzuia matumizi bora ya fedha za umma.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya TARURA kuhakikisha inatoa kipaumbele matumizi ya njia za ushindanishi wa bei katika ununuzi ili kuhakikisha uwazi, na ushindani katika ununuzi, isipokuwa pale ambapo kuna sababu za msingi za kutumia njia ya ununuzi kutoka chanzo kimoja au zabuni zilizofungwa kwa wazabuni wachache.**

## 20.3 Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka - Dar es Salaam (DART)

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ni taasisi inayofanya kazi chini ya OR-TAMISEMI. DART ilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali, Sura Na. 30, iliyotangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali Na. 120 la tarehe 25 Mei 2007.

Majukumu ya Wakala ni pamoja na kuanzisha na kuendesha mfumo wa Usafiri wa Kasi wa Mabasi (BRT) ndani ya Dar es Salaam, kuhakikisha

mzunguko wa utaratibu wa magari katika mitaa na barabara za mjini, na kuhakikisha usimamizi wenye ufanisi wa wakala.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kasoro zifuatazo ambazo zinahitaji kushughulikiwa: -

### 20.3.1 Miundombinu ya BRT - awamu ya pili kukamilika lakini ununuzi wa watoahuduma za mabasi haujafanyika

Aya ya 4.1.1 ya Taarifa ya Tathmini ya Mradi kuhusu Mradi wa Mabasi yaendayo haraka (BRT) – Awamu ya II, inaelekeza kuwa TANROADS itakuwa Wakala anayetekeleza mradi ambaye atafanya ununuzi na usimamizi wa mikataba ya miundombinu ya BRT. DART itakuwa na jukumu la kufanya ununuzi wa watoahuduma/waendeshaji wa mabasi, mfumo wa ukusanyaji wa nauli na mifumo ya kiteknolojia pamoja na kusimamia shughuli zote za mfumo wa BRT.

Hadi Agosti 2023, TANROADS ilkuwa imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya BRT Awamu ya II kwa 98.86%. Hii ni pamoja na ujenzi wa barabara unaofikia urefu wa kilomita 20.3, madaraja mawili ya juu, na vituo 29 vya mabasi katika ya njia ya kutoka Mbagala hadi katikati ya Jiji (CBD) kwa jumla ya Sh. bilioni 217.48; ambapo mradi ulitarajiwa kukamilika tarehe 25 Septemba 2023.

Hata hivyo, nimebaini kuwa, licha ya kukamilika kwa miundombinu na huduma za ujenzi, DART haikuwa imeanza mchakato wa ununuzi wa huduma za waendeshaji wa mabasi.

Kuchelewesha mchakato wa ununuzi wa huduma za waendeshaji wa mabasi kunaathiri uwezekano wa kufikia malengo ya mradi wa BRT Awamu ya II kwa wakati; hivyo, kuathiri maboresho yanayotarajiwa katika usafiri wa umma. Pia, thamani ya fedha inakosekana kutokana na kukamilika kwa matengenezo na hatari ya usalama wa miundombinu iliyokamilika bila kutumika.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya DART kuanzisha na kuharakisha mchakato wa ununuzi wa waendeshaji wa mabasi wanaohitajika kwa uendeshaji wa BRT Awamu ya II; na kuandaa mpango kamili wa uendeshaji kwa ajili ya kuunganisha mabasi katika mfumo wa BRT, ikiwamo ratiba na mikataba na watoahuduma.**

**20.3.2 Bidhaa za gharama ya Sh. bilioni 3.43 zilizonunuliwa kwa ajili ya kufunga mfumo wa kielektroniki wa kukusanya nauli za mabasi kutokutumika**

DART ilinunua kadi janja (smart cards) na SAMs kwa Mkataba Na. AE/053/TZ/-DART-P/262569/2021/2022/G/14, zenye thamani ya Dola za Marekani 400,960, sawa na Sh. bilioni 1; ambapo, mnamo tarehe 19 Juni 2023, kadi janja 200,000 na SAMs 1,200 ziliwasilishwa. Bidhaa hizi zilinunuliwa kwa lengo la kufunga mfumo wa malipo ya kielektroni, kurahisisha malipo ya nauli na ufuatiliaji wa mapato. Licha ya bidhaa hizo kuletwa, hazijaanza kutumika na hadi Oktoba 2023 zilikuwa zimehifadhiwa.

Vilevile, katika mkataba Na.AE/053/TZ/TZ-DART-P/150937/262569/2021/2022/G/13, vifaa vya TEHAMA vyenye thamani ya Sh. bilioni 2.43 kwa ajili ya kufunga mfumo wa kielektroni wa kukusanya nauli vilivyowasilishwa kati ya tarehe 30 Desemba 2022 na 10 Mei 2023 vilikuwa havijaanza kutumika hadi mwezi Oktoba 2023.

Kwa pamoja, bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 3.43 kwa mikataba yote miwili zilinunuliwa kwa ajili ya ufungaji wa mfumo wa kielektroni wa nauli za basi lakini hazijatumika; hivyo, kutopata thamani ya fedha iliyokusudiwa.

Kushindwa kutumia bidhaa zilizonunuliwa kunahusishwa na kuchelewa kufunga mageti yanayohitajika kwenye vituo vya mabasi ambapo, mfumo wa malipo ya kielektroni na kadi janja, SAMs ulipaswa kufungwa na kutumika.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya DART kutoa kipaumbele na kuharakisha ufungaji wa mageti yanayohitajika kwenye vituo vya mabasi ambapo mfumo wa malipo ya kielektroni, kadi janja, na SAMs, unakusudiwa kufungwa na kutumika. Hii itawezesha kutumia kikamilifu bidhaa zilizonunuliwa na kupata faida zilizokusudiwa za mfumo wa malipo ya kielektroni hivyo kupata thamani ya fedha.**

**20.3.3 Tuzo ya zabuni ya Sh. milioni 274.77 ilitolewa kwa mzabuni aliyeghushi cheti cha uthibitisho wa kutodaiwa kodi**

Kifungu cha 11.1h cha Mwaliko wa Zabuni Na. AE/053/2022/2023/NC/08 kwa ajili ya utoaji huduma za usafi kwa vituo vikuu, vituo vidogo vya

mabasi, na ofisi za DART kwa Awamu ya 1 na 2, kilielekeza kuwasilishwa kwa cheti cha uthibitisho wa kutodaiwa kodi (Tax clearance certificate) na cheti cha VAT kama sehemu ya mahitaji ya wasilisho la zabuni.

Baada ya kufanya ukaguzi wa vyeti vilivyowasilishwa kwa zabuni yenye thamani ya Sh. milioni 274.77 ilibainika kuwa mzabuni aliwasilisha cheti cha uthibitisho wa kutodaiwa kodi, kinachoonekana kutolewa na kuidhinishwa tarehe 4 Januari 2023 na kumalizika muda wake tarehe 30 Juni 2023. Hata hivyo, nilibaini kuwa cheti hicho hakikuwa kimepatikana kupitia mifumo rasmi ya TRA, hali inayoonesha kuwa cheti hicho kimeghushiwa.

Kuwasilisha nyaraka iliyoghushiwa kunazua wasiwasi kwamba mzabuni huenda hakutekeleza wajibu wake wa kulipa kodi ipasavyo. Pia, kutoa mkataba kwa mzabuni aliyewasilisha nyaraka ya kughushi kunadhoofisha uadilifu wa mchakato wa ununuzi na uteuzi wa mzabuni.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya DART kuanzisha utaratibu imara wa uhakiki wa nyaraka wakati wa tathmini ya zabuni na mchakato wa kutoa tuzo ya zabuni. Hii itajumuisha uchunguzi wa kina wakati wa mchakato wa tathmini ambao unahusisha mawasiliano ya moja kwa moja na mamlaka husika kwa ajili ya kuthibitisha uhalali wa nyaraka zilizowasilishwa. Pia, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya mzabuni aliyewasilisha nyaraka iliyoghushiwa.**

### 20.3.4 Huduma ya usafirishaji abiria isiyoridhisha inayotolewa na mtoa huduma wa mpito (UDART)

Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Mtoaji wa Huduma ya Mpito (TSP) - Awamu ya 1 kati ya DART na UDA Rapid Transit (UDART) PLC ambao ulisainiwa tarehe 16 Agosti 2019, kinamtaka UDART kuwa na jumla ya mabasi 140.

Vilevile, kulingana na Kifungu cha 2.1 cha marekebisho ya 4 ya mkataba ambao ulisainiwa tarehe 5 Agosti 2021, ilikubaliwa kurekebisha mkataba wa TSP kwa kuongeza magari 70 ya mita 18 aina ya "articulated", na kufanya jumla ya mabasi kuwa 210. Hii ingemuwezesha mtoa huduma kuhakikisha kuwa 90% ya magari yote yanafanya kazi kwenye njia kuu na ndogo wakati wa nyakati zenye abiria wengi na 10% iliyobaki itatumika kama akiba kwa ajili ya kubadilisha mabasi yanapoharibika.

Baada ya uchambuzi wa hali ya uendeshaji, nilibaini kwamba hadi Novemba 2023, mabasi 132 sawa na 63% hayakuwa yanatumika na yalihitaji ukarabati na matengenezo. DART iliihusisha NIT katika kufanya ukaguzi na majaribio ya mabasi, na kubaini jumla ya Sh. bilioni 2.1 kuhitajika ili kukarabati na kutengeneza mabasi hayo.

Kuwapo kwa idadi kubwa ya mabasi yanayohitaji ukarabati na matengenezo kunavuruga huduma za usafiri wa umma na kusababisha usumbufu kwa abiria na kutopata thamani ya fedha kutokana na kutotumika kikamilifu kwa miundombinu ya BRT.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya DART kuchukua hatua za haraka kupata fedha ili kufanikisha ukarabati na matengenezo ya mabasi, na kuhakikisha upatikanaji wa vipuri vya kubadilisha na kuwa na ratiba ya matengenezo ya mara kwa mara.**

### 20.4 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB) iliundwa chini ya Kifungu cha 56 ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290. Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ina jukumu la kutoa mikopo kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya kufadhili miradi ya maendeleo ya kiuchumi; hivyo, kusaidia juhudi za Serikali katika kuboresha ustawi wa kijamii na kiuchumi wa wakazi katika mamlaka za serikali za mitaa husika.

LGLB inajiendesha chini ya uangalizi wa OR – TAMISEMI. Nilifanya ukaguzi wa hesabu za LGLB na kubaini upungufu ufuatao:

#### 20.4.1 Mikopo ya Sh. bilioni 2.17 kutofanyiwa marejesho kwa kipindi cha zaidi ya miezi 18

Kifungu Na. 2 cha makubaliano ya mkopo kati ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB) na mamlaka za serikali za mitaa kinaelekeza kufanyika kwa marejesho kila mwezi kulingana na ratiba ya marejesho iliyokubaliwa.

Hata hivyo, nilibaini kuwa mamlaka sita za serikali za mitaa zilisimamisha malipo ya salio la mikopo yao kiasi cha Sh. bilioni 2.17 kwa kipindi kinachotofautiana kati ya miezi 18 hadi 79 kufikia Novemba 2023 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.145**. Halmashauri moja haijawahi kurejesha hata mara moja mkopo wake wa Sh. milioni 465.09 tangu kutolewa kwake tarehe 27 Julai 2017.

**Jedwali Na. 145: Halmashauri zilizochelewesha marejesho**

| Jina la Halmashauri | Tarehe ya kutolewa mkopo | Tarehe ya rejesho la mwisho | Miezi bila kufanya marejesho | Salio la Mkopo hadi 30 Juni 2023 (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| H/Wilaya ya Tunduru | 29/03/2019 | 22/04/2021 | 31 | 3,976,168 |
| H/Wilaya ya Bukombe | 01/12/2016 | 31/05/2022 | 18 | 1,063,236,490 |
| H/Wilaya ya Ruangwa | 25/7/2019 | 02/04/2021 | 31 | 591,137,446 |
| H/Wilaya ya Namtumbo | 27/04/2017 | Haijawahi kurejesha | 79 | 465,097,500 |
| H/Manispaa ya Singida | 12/12/2003 | 06/08/2018 | 63 | 29,878,540 |
| H/Wilaya ya Pangani | 05/01/2006 | 30/04/2019 | 55 | 14,043,799 |
| **Jumla** | | | | **2,167,369,943** |

**Chanzo**: Daftari la mikopo

Kutokurejeshwa kwa mikopo kunatokana na LGLB kushindwa kusimamia makubaliano ya dhamana; hivyo, kuiweka katika hatari ya matatizo ya kifedha, ikiwemo kuhatarisha uwezo wake wa kutoa mikopo na kuendelea kufanya kazi kama taasisi endelevu.

**Ninapendekeza kwamba LGLB kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI kufanya mapitio ya sheria na kanuni ili ziendane vizuri na mazingira ya uendeshaji katika kusimamia dhamana za mikopo. Marekebisho haya yatasaidia kuhakikisha mikopo inarejeshwa kwa wakati, kwa kuzingatia kwamba usimamizi mzuri wa fedha ni muhimu katika kuimarisha uendeshaji wa shughuli za Bodi na kusaidia utekelezaji wa mipango ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.**

## 20.5 Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) - Hombolo

Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) kilianzishwa chini ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa, Sura ya 396. Madhumuni ya kuanzishwa kwa chuo hiki ni kuboresha utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa na wadau wengine kupitia utoaji wa mafunzo, utafiti, na huduma za ushauri.

Jukumu lake kuu ni kurahisisha mchakato wa ugatuzi wa madaraka, utawala bora, utoaji wa huduma bora, kupunguza umaskini, na kukuza ustawi wa kijamii na kiuchumi wa wananchi kote nchini.

Wakati wa ukaguzi wa LGTI, nilibaini udhaifu ufuatao: -

### 20.5.1 Ujenzi wa Jengo la Utawala uliotekelezwa

Kwa mujibu wa andiko la Mradi wa ujenzi wa Jengo la Utawala lililotolewa mwaka wa 2021, gharama za mradi zilikadiriwa kuwa Sh. bilioni 4.94 chini ya ufadhili wa vyanzo vya ndani ya taasisi. Ujenzi wa mradi huu kwa njia ya "Force account " ulitarajiwa kuanza mwaka 2021/22 na kukamilika katika robo ya nne ya mwaka wa fedha wa 2025/26.

Hata hivyo, ukaguzi wa eneo la mradi uliofanyika tarehe 22 Desemba 2023 ulibaini uwapo wa ofisi ya muda iliyojengwa, ghala, na vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 453.77 vilivyonunuliwa kwa mkopo na kuletwa tangu Julai 2022 lakini bado havijatumika. Hakukuwa na shughuli yoyote ya ujenzi inayoendelea katika eneo hilo.

Pia, nilibaini kwamba, Chuo hakikuwa na kibali cha ujenzi, michoro ya mradi, maelezo ya kiufundi (specifications), makadirio ya gharama na mchanganuo wa vifaa vya ujenzi haikuwa umeandaliwa kabla ya ununuzi wa vifaa hivyo kufanyika.

Udhaifu huu unaweza kuwa unatokana na upungufu katika mpango wa mradi na kutowajibika ipasavyo kwa menejimenti katika usimamizi na utekelezaji wa mradi. Pia, ukosefu wa fedha za kutekeleza mradi.

Kwa maoni yangu, ununuzi wa vifaa vya ujenzi bila michoro ya mradi, maelezo ya kiufundi, mchanganuo wa mahitaji ya vifaa, makadirio ya gharama, na kibali cha ujenzi, kunaashiria uwepo wa maslahi yaliyojificha katika ununuzi na utekelezaji wa mradi. Kuna hatari kubwa ya hasara ya kifedha kutokana na kununua vifaa pasipo kuvitumia, na kuongezeka kwa gharama za ujenzi kadri mradi unavyoendelea kutelekezwa.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya Chuo kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI kuhakikisha upangaji thabiti wa mradi kama njia mojawapo bora ya kuhakikisha mafanikio ya mradi. Hii itahusisha kupata nyaraka muhimu za mradi, na kuandaa mpango wa utekelezaji wa mradi.**

**Pia, wanapaswa kuhakikisha ujenzi wa mradi unaanza ili kuepuka upotevu au uharibifu wa vifaa vya ujenzi vilivyohifadhiwa. Aidha,**

**ufuatiliaji wa mara kwa mara wa maendeleo ya mradi ni muhimu kuhakikisha mradi unatekelezwa kwa wakati na ndani ya bajeti.**

### 20.5.2 Nyaraka za zabuni na ununuzi wa Sh. milioni 997.83 kutokuidhinishwa na Bodi ya Zabuni

Kanuni ya 185 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 (iliyofanyiwa marekebisho 2016), inataka nyaraka za zabuni kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni kabla ya zabuni kutangazwa. Pia, Kanuni za 55 (2), 163 (4), na 185 (1) za Kanuni hizo zinazuia taasisi kutoa tuzo ya zabuni isipokuwa utoaji huo umeidhinishwa na Bodi ya Zabuni.

Hata hivyo, nilibaini kuwa, LGTI ilinunua bidhaa zenye thamani ya Sh. milioni 997.83 kutoka kwa wazabuni mbalimbali, lakini nyaraka za zabuni wala ununuzi husika haukuidhinishwa na Bodi ya Zabuni. Maelezo yameoneshwa katika **Jedwali Na.146.**

**Jedwali Na. 146: Ununuzi bila ya idhini ya Bodi ya Zabuni**

| Mkataba Na. | Maelezo ya Mkataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| **PA/080/2021/2022/G/04/14** | Ununuzi na usambazji wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya ujezi wa jengo la utawala | 591,390,040 |
| **PA/080/2021/2022/G/04/13** | Kuleta na kufunga samani katika madarasa na ofisi | 347,112,340 |
| **AE/092/2022-2023/MZA/W/03** | Kuleta na kusimika mfumo wa mtandao (network system) | 59,330,006 |
| **Jumla** | | 997,832,386 |

**Chanzo**: Daftari la mikataba

Ununuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni unadhoofisha uadilifu, usawa, na uwazi wa maamuzi katika ununuzi na kuweka taasisi katika hatari ya kushindwa kupata thamani ya pesa zilizotumika katika ununuzi uliofanywa.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya Chuo kuimarisha mifumo ya ndani ili kuzuia kutokufuata misingi na taratibu za ununuzi zilizowekwa ili kuimarisha kufuata sheria za ununuzi.**

## 20.6 Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ilianzishwa chini ya Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Sura ya 448. Tume hiyo ilianzishwa kuleta mageuzi ya msingi katika usimamizi, utawala na uendeshaji wa utumishi wa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wanaofanya kazi katika Utumishi wa Umma.

Nimebaini mapungufu ambayo yanahitaji kurekebishwa ili kuhakikisha Tume inafikia malengo yaliyo kusudiwa na secta ya elimu kufikia viwango vinavyo kubalika.

### 20.6.1 Kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi Sh. bilioni 6.49

Mnamo tarehe 29 Juni 2021, TSC ilisaini Mkataba Na. IE/047/2020/2021/HQ/W/01 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi katika Kiwanja Na. 939 Kitalu AA kilichopo Chinyoyo - Dodoma, ambapo mradi ulipangwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 18. Hata hivyo, nilibaini kuwa mradi haukuanza hadi Desemba 2022 kutokana na mzozo wa umiliki wa ardhi uliotatuliwa kwa TSC kuhamishiwa Kiwanja Na. 77 Kitalu BB kilichopo Ndejengwa.

Pia, nilibaini kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi wa thamani ya Sh. bilioni 6.49. Mradi ulitarajiwa kukamilika tarehe 5 Juni 2024, lakini hadi Oktoba 2023, ujenzi ulikuwa umefikia wastani wa 30% tu.

Kasi ndogo na uchelewaji katika kutekeleza mradi kulisababishwa na kuchelewa kuanza ujenzi kutokana na mzozo wa umiliki wa ardhi uliosababisha mabadiliko ya kiwanja na mahali pa mradi, kuongezeka kwa bei ya mkataba kutokana na kucheleweshwa kwa kuanza kwa mradi na mabadiliko katika wigo wa kazi yanayohitaji nyongeza ya fedha.

Kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi inazuia kufikia kwa wakati malengo yaliyokusudiwa, na inaweza kusababisha gharama za mradi kuongezeka.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya TSC kuimarisha usimamizi wa mradi na kuhakikisha kwamba mradi unakamilika kwa wakati.**

## 20.7 Mfuko wa Barabara (Sehemu iliyochini ya OR-TAMISEMI)

Mfuko wa Barabara ulianzishwa chini ya Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tozo za Barabara, na Mafuta, Sura ya 220, maalumu kwa ajili ya kuweka fedha zote zilizokusanywa kama ada za barabara na mafuta zilizotozwa kwenye dizeli na petroli, ada za usafirishaji, leseni za magari mazito, ada za uzito kupita kiasi, au kutoka vyanzo vingine vyovyote kwa kiwango au viwango vitakavyoamuliwa na Bunge wakati wowote.

Tangu mwaka 2000/01, Wizara ya Ujenzi na OR TAMISEMI wamefanya shughuli za Mfuko wa Barabara kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara. Mpango wa kazi unategemea Mkataba wa Utendaji uliosainiwa kati ya

Bodi ya Mfuko wa Barabara na OR-TAMISEMI, ambao lengo lake ni kusaidia Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Wilaya, na taasisi zingine zinazohusika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kwamba bado kuna fedha kiasi cha Sh. bilioni 1.26 ambazo hazijarejeshwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Jumla ya mkopo wote ilikuwa Sh. bilioni 2.52 na ulitolewa mwaka wa fedha 2017/18 na ulipaswa kulipwa kwa awamu nne, ambapo awamu ya mwisho ilitakiwa kulipwa tarehe 30 Septemba 2018.

Mkopo ambao haujarejeshwa kwa muda mrefu unahatarisha uimara wa kifedha wa Mfuko, hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya Mfuko wa Barabara chini ya OR-TAMISEMI kuanzisha na kujadiliana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni mpango mpya wa kulipa deni, iwapo Halmashauri hiyo inakabiliwa na changamoto za kifedha ambazo zinazuia kulipa mkopo huo. Hii itajumuisha kurekebisha ratiba ya marejesho au kukubaliana juu ya mipango mbadala inayokubalika kwa pande zote.**

## 20.8 Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT)

Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) ni taasisi ya wanachama ililoanzishwa mwaka 1984 baada ya kuanzishwa upya kwa mfumo wa Serikali za Mitaa nchini Tanzania. Wanachama wake ni mamlaka zote za serikali za mitaa katika Tanzania Bara.

Lengo kuu la ALAT ni kulinda haki na maslahi ya mamlaka za serikali za mitaa kwa kuziwakilisha katika ngazi za Kitaifa na kimataifa, kushawishi na kudai mabadiliko ya sera ili kuboresha utendaji wa Mamlaka hizo. Pia, inawajibika kutoa huduma za kiufundi na kitaalam kwa wanachama wake, na kurahisisha programu za ushirikiano na Mamlaka zingine za Serikali za mitaa katika ngazi ya kimataifa.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kwamba ALAT imeendelea kukabiliwa na changamoto ambazo zimekuwapo kwa miaka kadhaa. Changamoto hizi ni pamoja na; michango isiyolipwa kutoka kwa wanachama wake yenye thamani ya Sh. bilioni 5.16 ambayo haijalipwa hadi 2021/22 na kutofanyika tathmini ya shughuli zake za uendeshaji kutokana na kutokuwapo kwa kitengo cha ukaguzi wa ndani.

Changamoto hizi zinahitaji hatua za haraka za marekebisho kwani zinaathiri ufanisi wa Jumuiya katika kutimiza jukumu lake.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya ALAT kuangalia upya muundo wake wa utawala na usimamizi ili kutambua udhaifu au mapengo yoyote yanayochangia uwepo wa changamoto zilizopo. Hii inaweza kuhusisha marekebisho ya sera, taratibu, na muundo wa taasisi ili kuboresha uwajibikaji, uwazi, na ufanisi katika maamuzi na usimamizi wa rasilimali.**



# MAPENDEKEZO YA JUMLA

Serikali imeonesha juhudi za kupongezwa katika kuongeza uwazi na ufanisi katika usimamizi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ikidhihirishwa na mipango kama vile kuanzishwa kwa MUSE na TAUSI ili kuimarisha udhibiti wa ndani.

Kufuatia ripoti zangu zilizopita, Serikali imechukua hatua mbalimbali ambazo zinastahili pongezi, ikiwamo uhamisho wa watumishi ndani ya idara za uhasibu na hatua za kinidhamu kwa wale wanaohusishwa na ubadhirifu wa fedha. Ninapongeza hatua hizi, haswa katika kuweka kipaumbele na kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ili kupunguza hatari za usimamizi mbaya wa kifedha na upungufu katika udhibiti.

Hata hivyo, taarifa hii inabainisha dosari kadhaa zilizosalia ambazo zinahitaji hatua zaidi kutoka kwa Serikali, hivyo, naiomba sana OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuandaa mpango kazi wa kina wa utekelezaji wa haraka wa mapendekezo ya mara kwa mara na kurekebisha kasoro zilizobainika katika mifumo iliyoboreshwa.

Aidha, hatua kali lazima ziendelee kuchukuliwa dhidi ya watumishi watakaobainika kukiuka sheria, hasa katika masuala ya ununuzi na ukusanyaji wa mapato.

## Kiambatisho 1: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

| Na. | Halmashauri | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Arusha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha |
| 2 | H/W Arusha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 3 | H/W Babati | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 4 | H/Mji Babati | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha |
| 5 | H/W Bagamoyo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 6 | H/W Bahi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha |
| 7 | H/W Bariadi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 8 | H/Mji Bariadi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 9 | H/W Biharamulo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 10 | H/W Buchosa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 11 | H/W Buhigwe | Inayoridhisha | Yenye shaka | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 12 | H/W Bukoba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 13 | H/M Bukoba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 14 | H/W Bukombe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 15 | H/W Bumbuli | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 16 | H/W Bunda | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 17 | H/Mji Bunda | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 18 | H/W Busega | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 19 | H/W Busokelo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 20 | H/W Butiama | Inayoridhisha | Yenye shaka | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 21 | H/W Chalinze | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 22 | H/W Chamwino | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 23 | H/W Chato | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 24 | H/W Chemba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 25 | H/W Chunya | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 26 | H/Jiji Dar es Salaam (Zamani Ilala) | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 27 | H/Jiji Dodoma | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 28 | H/W Gairo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 29 | H/W Geita | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha |
| 30 | H/Mji Geita | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha |
| 31 | H/W Hai | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 32 | H/W Hanang | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 33 | H/W Handeni | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |

| Na. | Halmashauri | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 34 | H/Mji Handeni | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 35 | H/Mji Ifakara | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 36 | H/W Igunga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 37 | H/W Ikungi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 38 | H/W Ileje | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 39 | H/M Ilemela | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 40 | H/W Iramba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 41 | H/W Iringa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 42 | H/M Iringa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 43 | H/W Itigi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 44 | H/W Itilima | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 45 | H/M Kahama | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 46 | H/W Kakonko | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 47 | H/W Kalambo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 48 | H/W Kaliua | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 49 | H/W Karagwe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 50 | H/W Karatu | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 51 | H/W Kasulu | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 52 | H/Mji Kasulu | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 53 | H/W Kibaha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 54 | H/Mji Kibaha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 55 | H/W Kibiti | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 56 | H/W Kibondo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 57 | H/M Kigamboni | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 58 | H/W Kigoma | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 59 | H/M Kigoma/Ujiji | Mbaya | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 60 | H/W Kilindi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye shaka | Inayoridhisha | Yenye shaka | Yenye shaka |
